

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 3 Juni, 2022

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae.

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

MHE. AGNES M. MARWA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Cosato David Chumi.

Na. 325

Serikali Kutenga Fedha za Dharura kwa Ajili ya Barabara

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutenga fedha za dharura kwa ajili ya barabara?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TARURA* imekuwa ikitenga fedha za dharura sawa na asilimia tano ya bajeti ya fedha za Mfuko wa Barabara. Katika mwaka wa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi bilioni 11.45 kwa ajili ya fedha za dharura za matengenezo ya barabara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha ya dharura kwa ajili ya kufanya matengenezo na ujenzi wa miundombinu ya barabara kulingana na upatikanaji wa fedha. Lengo ni kuboresha mtandao wa barabara unaohudumiwa na *TARURA*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini pia napenda kuipongeza Serikali kwamba sasa imeanza kutenga fedha za dharura kwa ajili ya barabara zetu za *TARURA*, naipongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, barabara ya kutoka Changarawe kwenda Kisada ambayo inapita maeneo ya Matanana na Bumilayinga kutokana na miti ambayo wananchi walipanda kwa wingi na sasa imekomaa, inatumika sasa na malori makubwa.

Je, Serikali iko tayari kuitazama barabara hii kwa macho mawili kwa sababu inaharibika mara kwa mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tunafahamu kwamba na wewe Naibu Spika ni mmoja wa wanufaika wa Mradi wa *DMDP* kama utakuja kukamilika, na sisi watu wa miji 45 tuna Mradi wa *TACTIC*. Mimi na wananchi wa Mafinga tunapenda kufahamu, je, katika huu Mradi wa *TACTIC* ambao utanufaisha kata nyingi za pale Mjini Mafinga, Upendo, Isalavanu, Kinyanambo na kadhalika, je, unaanza lini kwa sisi wa tu wa Mafinga? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ya nyongeza ya Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Jimbo la Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari kuiangalia kwa umakini barabara ya Changarawe – Kisada ambayo Mheshimiwa Mbunge ameianisha hapa ili tuhakikishe kwamba inafanyiwa matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lini Mradi wa *TACTIC* utanza. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kuwa Halmashauri ya Mji wa Mafinga Mjini ipo katika awamu ya tatu ya utekelezaji wa mradi huo ambao utanza katika mwaka wa fedha unaokuja wa 2022/2023. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mafuwe.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata tatizo la mafuriko, madaraja mengi ndani ya Wilaya ya Hai yalielezuliwa yakiwemo Madaraja ya Marire na Kikafu. Daraja hili limekuwa kero kubwa kwa wananchi jambo linalomlazimu Mheshimiwa Diwani Martin Munisi kila siku asubuhi kuamka kwenda kuwavusha watoto wa shule kwenye daraja hili. Je, Serikali ni lini itakarabati madaraja haya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa daraja hili lina changamoto nyingi, niwaagize *TARURA* Mkoa wa Kilimanjaro wafike eneo la tukio wafanye tathmini na kuchukua hatua za haraka ikiwemo kujenga daraja dogo la dharura ili eneo hilo liweze kupitika, ahsante sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, Manispaa ya Mpanda nayo ni kati ya Manispaa ambazo zipo kwenye Mradi wa *TACTIC*. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie na sisi Mpanda ni lini tutaanza Mradi huu wa *TACTIC*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Mpanda ipo katika Awamu ya Tatu ya Utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC* ambao utanza mwaka wa fedha 2022/2023, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, swali namba 327 ambalo linahusiana na barabara linajibiwa na Waziri huyu huyu. Kwa bahati mbaya limepangwa baada ya swali namba 326, kwa hiyo tutauliza swali namba 327 halafu tutarudi 326; Mheshimiwa Nicodemus Maganga.

Na. 327

**Mradi wa Barabara Unaofadhiliwa na
World Bank – Mbogwe**

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA aliuliza: -

Je, ni lini mradi wa barabara wa kilometa 96 unaofadhiliwa na Benki ya Dunia utafika Mbogwe?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Nicodemus Maganga, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Tanzania, kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) na Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*), inatekeleza Mradi wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji Jamii na Ufunguaji Fursa za Kijamii na Kiuchumi Vijijini (*Roads to Inclusion and Socioeconomic Opportunities - RISE*). Mradi huu utagharimu kiasi cha dola za Marekani milioni 350, ambapo, kiasi cha milioni 300 ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia na milioni 50 ni mchango wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe ni miongoni mwa Halmashauri zitakazonufaika na Mradi wa *RISE* ambapo jumla ya kilometa 96 zinaratajiwa kujengwa. Kwa sasa *TARURA* ipo kwenye hatua ya manunuzi ya Mtaalamu Mshauri wa kufanya usanifu wa kina (*detailed engineering design*) wa barabara zilizopendekezwa. Ujenzi unatarajiwa kuanza ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023 baada ya usanifu kukamilika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maganga.

MHE. NICODEMAS H. MAGANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ya Serikali, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbogwe ina barabara nyingi, ukizijumlisha upana wake ni zaidi ya kilometa 3,000, hivyo basi barabara nyingi mpaka sasa hazipitiki Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe ni shahidi, tulishawahi kwenda pamoja kwenye hilo jimbo.

Je, ni lini sasa hizi barabara nyingine ambazo haziko kwenye mpango utanipa bajeti ili *TARURA* ya Mbogwe iweze kuzitengeneza?

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wilaya ya Mbogwe ina madaraja manne na mpaka sasa hivi madaraja hayo hayapitiki, likiwemo Daraja na mpaka wa Bukombe, Kata ya Masumbwe ambalo linaunganishwa na Kata ya Bugerenga.

Naomba kujua sasa Mheshimiwa Naibu Waziri umejipangaje ili kuweza kunisaidia wananchi wangu waendeleo kufaidika na Serikali hii? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajenga barabara hatua kwa hatua na ndiyo maana hatua ya kwanza Mji wa Mbogwe umeingizwa katika Mpango wa *RISE*. Hatua nyingine Mheshimiwa Rais alifanikisha kuongeza bajeti ya *TARURA* ambapo tunafika maeneo mengi.

Kwa hiyo, hata hizo barabara ambazo zimebakia tutaendelea kuzijenga kwa kutenga fedha za bajeti katika kila mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madaraja ambayo Mheshimiwa Mbunge ameanisha hapa vilevile lengo la Serikali kupitia *TARURA* ni kufungua barabara hususani katika yale madaraja mabovu yakiwemo hayo aliyoyataja.

Kwa hiyo, tutaendelea kufanya tathmini na tutatenga fedha ili kuhakikisha kwamba yanajengwa kwa wakati, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali namba 326, Mheshimiwa Stella Alex Ikupa.

Na. 326

Ugawaji wa Mafuta ya Ngozi kwa Watu Wenye Ulemavu

MHE. STELLA I. ALEX aliuliza: -

Je, ni Halmashauri na Manispaa ngapi nchini zinatekeleza ununuzi na ugawaji wa mafuta ya ngozi kwa watu wenye ulemavu wa ngozi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma kwa watu wenye ulemavu zimeendelea kuboreshwa kote nchini, ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya watu wenye ulemavu 138,468 kati yao wanawake 68,401 na wanaume 70,067 wametambuliwa. Aidha, katika kipindi hicho, watu wenye ulemavu wapatao 15,596 wamehudumiwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwakinga watu wenye ualbino dhidi ya maradhi ya ngozi kutokana na jua, kati ya mwaka 2020 hadi 2022 jumla ya Halmashauri 102 kwenye mikoa 20 imetekeleza ununuzi na ugawaji wa mafuta ya ngozi (*sun-screen cream*) kwa kushirikiana na wadau. Jumla ya wanufaika 3,389 walipata huduma hiyo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ikupa.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 tuna idadi ya watu wenye ualbino

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wapatao 16,000 lakini kutokana na jibu la Serikali inaonesha kwamba watu wenye ualbino ambao wamenufaika na mafuta haya ni 3,389 kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukumbuke kwamba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alishotoa maelekezo kwa Halmashauri hizi kwamba zihakikishe zinanunua na kugawa mafuta haya ya watu wenye ualbino.

Nini kauli ya Serikali kwa Halmashauri ambazo hazitatekeleza takwa hili, na hasa ikizingatiwa kwamba maelekezo yameshatolewa mara nyingi, lakini pia miongozo ipo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili la nyongeza; kwa kuwa sasa hivi tunakwenda kuwa na zoezi hili la sensa, hivyo tunategemea kwamba tutapata idadi halisi ya watu wenye ulemavu, aina za ulemavu na mahali wanapatikana ama mahali walipo.

Serikali inaonaje sasa ikianza kuyanunua mafuta haya ikawa inayashusha moja kwa moja kwenye vituo vya afya na zahanati, tofauti na utaratibu uliopo sasa ambapo mafuta haya kwa maeneo ambayo yalikuwa yakinunuliwa yalikuwa yakipatikana kwenye Hospitali za Mikoa na Wilaya? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Stella Alex Ikupa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Stella Ikupa amekuwa mstari wa mbele sana kuhakikisha anawasemea watu wenye ulemavu wakiwemo wenye ulemavu wa ngozi na Serikali ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, inawajali na kuwathamini sana watu wote wenye ulemavu na ndiyo maana katika mipango yetu tumekubaliana

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kwamba kwanza ni maelekezo ya Serikali kwamba Halmashauri zetu zote zinapotenga fedha kwa ajili ya dawa lazima zitenge fedha kwa ajili ya mafuta haya kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kurudia tena kauli hiyo ya Serikali ambayo ilikwishatolewa kwamba Halmashauri zote zihakikishe zinatenga fedha, miongoni mwa bajeti ya dawa lazima mafuta haya ya watu wenye ualbino yaweze kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 Halmashauri zote zimefanya utambuzi na kufanya maoteo ya mahitaji ya mafuta hayo na katika mwaka huu tutakuwa na mafuta hayo kwa kiasi kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusiana na kusogeza huduma hizi karibu zaidi na watu wenye ulemavu, ni kweli tutakuwa na Sensa ya Watu na Makazi tarehe 23 Agosti, 2022. Niwaombe watu wote wenye ulemavu, pamoja na Watanzania wote, tujitokeze wote ili tuhesabiwe, na hii itasaidia sana Serikali kuwatambua watu wenye ulemavu na kujua mahali walipo na mafuta haya sasa yatasogezwa kwenye vituo vile kwa idadi kulingana na watu wenye ulemavu walipo katika maeneo hayo, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; kwa kuwa watu wengi wenye ulemavu wa ngozi hawako kwenye vituo, wengine wako vijijini; je, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba hata wale ambao hawko kwenye vituo vya Watoto walio na *albinism*.

Je, nini mkakati wa Serikali kuwafikia kule waliko kuwapa mafuta?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba siyo wote wenye ulemavu wa ngozi (ualbino) wapo kwenye vituo vya huduma, kwa maana ya watoto, lakini hapa tunaongelea watoto na watu wazima kupata huduma hii. Sasa utaratibu ambao tutauweka, kwanza tukisogeza huduma hizi za mafuta karibu na zahanati na vituo maana yake wale watu wenye ualbino watajua kwamba mafuta yakiisha watakwenda kwenye zahanati ya karibu zaidi au kwenye kituo cha afya au hospitali ya karibu zaidi. Kwa hiyo, mpango wa Serikali ni kusogeza zaidi upatikanaji wa huduma hii kwenye vituo katika jamii zetu, ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

Na. 328

Kufungua Ubalozi wa Tanzania nchini Pakisatan

MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua Ubalozi wa Tanzania nchini Pakistan?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kufanya utafiti wa kuangalia uwezekano wa kufungua Ubalozi nchini Pakistan. Utafiti huo unahusisha kuangalia faida za kiuchumi zilizopo nchini humo ambazo Tanzania inaweza kunufaika nazo ikiwa ni pamoja na kuainisha gharama za ufunguzi wa Ubalozi huo na uendeshaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa nchi yetu imefaidika sana kutokana na balozi mbalimbali ambazo tumefungua nchi mbalimbali na hasa kwenye uwekezaji, biashara, pamoja na utalii na hasa kwenye biashara ya mazao ya kilimo.

Je, nchi hii ya Pakistan kwa sababu wana ubalozi wao hapa nchini tunashirikianaje pamoja na nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa nchi ya Pakistan haina Ubalozi hapa; je, kuna nchi ngapi za namna hii ambazo zina balozi zao hapa nchini na sisi hatuna balozi zao kwenye nchi zao? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Hilo swali la pili rudia tena.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza la pili?

SPIKA: Swali la pili rudia tena.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivi, kuna nchi mbalimbali ambazo zina balozi zao hapa nchini, lakini sisi hatuna balozi kwenye nchi zao; je, nchi zipi hizo nchi?

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri jibu la kwanza la pili usijibu kwa sababu linahitaji takwimu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa Tanzania haina ubalozi nchini Pakistan lakini tunawakilishwa na ubalozi wetu ambao upo Abu Dhabi UAE. Kwa hiyo, mahusiano ya nchi zetu mbili hizi ni makubwa na tumekuwa tukishirikiana katika masuala mbalimbali hasa ya kibiashara ambapo nchi yetu imekuwa ikisafirisha kwenda Pakistan bidhaa kama pamba, chai na madini ya vito kama vile *Tanzanite* pamoja na nafaka kama vile maharage. Lakini pia kutoka Pakistan tumekuwa pia tukishirikiana nao na tumekuwa tuki-*import* bidhaa za dawa za binadamu pamoja na dawa za viwanda vya nguo na nafaka. Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani.

Na. 329

**Serikali kukamilisha majadiliano na Kampuni
ya *Tanzania Leaf Tobacco* ili
kununua Tumbaku**

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha majadiliano na Kampuni ya *Tanzania Leaf Tobacco* ili iweze kurudi nchini kuendelea kununua tumbaku?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu na wakulima wa tumbaku nchini kuwa mwekezaji mpya ambaye ni mzawa Kampuni ya *Amy Holdings Limited* imekamilisha taratibu za kuchukua shughuli zilizokuwa zinafanywa na Kampuni ya *TLTC* na ameshapewa leseni. Aidha, Kampuni ya *Amy Holdings Limited* imeanza kununua tumbaku ambapo inatarajiwa kununua tani 10,000 za tumbaku katika msimu wa mwaka 2022/2023 ambazo itazichakata katika kiwanda kilichopo Morogoro ifikapo mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wakulima wote nchini, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufungua milango ya wawekezaji ambayo matokeo yake ni pamoja na kupatikana kwa mwekezaji huyu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cherehani.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, niendeleo kumshukuru sana Rais na nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hawa wa tumbaku wamekuwa wakipangiwa uzalishaji na makampuni na mwisho wa siku wanachozalisha kinakuwa kidogo tofauti na matarajio yao na hasa wakulima hawa wadogo; na wanachozalisha cha ziada mwisho wa siku kinashindwa kununuliwa na mwisho wake kinaitwa jina la makinikia; nini kauli ya Serikali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali langu la pili, kumekuwa na makato makubwa sana ya upandaji wa miti kwa wakulima hawa wa tumbaku. Fedha nyingi zinaishia kwa makampuni hayo na nyingine zinaishia benki na mkulima anaondoka bila fedha na mfano tu tosha mwaka jana

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wakulima hawa wa tumbaku wameweza kukatwa zaidi ya dola milioni tatu za miti ambapo ni zaidi ya bilioni sita. Nini kauli ya Serikali ili hao wakulima sasa tuwawekee mazingira mazuri waweze kuzalisha kwa wingi na weweze kupata faida kubwa na Serikali yetu iweze kupata fedha za kigeni? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la kwanza ni kweli imekuwepo hiyo changamoto na ndiyo maana Serikali tumeendelea kuhakikisha kwamba tunafungua milango kuwaleta nchini wawekezaji wengi zaidi ili kupata soko la uhakika la tumbaku yetu. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Serikali itaendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba zao hili la tumbaku linapata soko la uhakika na wakulima mwisho wa siku tumbaku yao inanunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la kuhusu makato, hii ni *concern* ambayo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiisema mara kwa mara na tumeshamuelekeza Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku, kukaa na wadau wote kuona namna bora ya uendeshaji wa shughuli ya biashara ya tumbaku ili mkulima anufaike na kila ambacho anakilima shambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili tunalichukua kwa umakini mkubwa na tunaendelea kulifanyia kazi ili mwisho wa siku mkulima aweze kunufaika na tumbaku yake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakoso.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa *Bulamata AMCOS* wa eneo la Mishamo walilima tumbaku zao na kuwauzia Kampuni ya *Naile Leaf Limited* wanaidai kampuni hiyo dola za Kimarekani 600,000. Ni lini Serikali itawasaidia hawa wakulima wadogo ambao wamedhulumiwa haki zao za kimsingi na walipewa leseni na Serikali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Moshi Kakoso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna madai ya wakulima dhidi ya hii kampuni, Mheshimiwa Waziri aliwaita makampuni yote yanayodaiwa na akatoa mwongozo wa malipo; moja kati ya kazi ambayo Mkurugenzi wa Bodi anaendelea kuifuatilia ni kuhakikisha kwamba wakulima hao wanalipwa lakini pia tumewapa sharti kwamba hatuta-*renew* leseni yao mpaka pale watakapokamilisha malipo ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Kilimo tunahakikisha kwamba tunasimamia kwa dhati ili wakulima hawa waweze kulipwa na jambo hili lipo ndani ya meza ya Mheshimiwa Waziri, kazi inaendelea kuhakikisha kwamba malipo haya yanafanyika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Emmanuel Mageni Kasalali, Mbunge wa Sumve.

Na. 330

**Kuondolewa kwa mazao ya Choroko na
Dengu kwenye utaratibu wa Stakabadhi za Ghala**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA K.n.y. MHE. KASALALI E.
MAGENI** aliuliza:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Je, ni kwa nini Serikali isiyaondoe mazao ya choroko na dengi kwenye utaratibu wa stakabadhi ghalani kwani utaratibu huo umekuwa kero kwa wakulima na wanunuzi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Mageni Kasalali, Mbunge wa Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unawezesha uuzaji wa mazao kwa ubora na bei ya ushindani, kupata takwimu sahihi za uzalishaji za mauzo na kuchochea uzalishaji. Mathalani, katika msimu wa mwaka 2020/2021 jumla ya kilo 14,394,077 za choroko zenye thamani ya shilingi bilioni 18.7 ziliuzwa kwa mfumo wa Stakabadhi za Ghala ikilinganishwa na kilo 1,130,453 zilouzwa katika msimu wa mwaka 2019/2020 katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Tabora na Singida.

Mheshimiwa Spika, zao la choroko, dengi na mazao mengine yataingizwa kwenye mfumo wa stakabadhi kwa kuzingatia vigezo muhimu vya uwepo wa ghala, waendesha ghala, elimu kwa wadau wa mfumo na mazingira ya soko kwa wakati husika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chaya.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya yongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa kumekuwa na changamoto nyingi sana kwenye huu mfumo wa stakabadhi ghalani; je, nini mpango wa Serikali sasa kutoa elimu kwa wakulima wa choroko na dengi kabla ya mfumo haujaanza?

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, mfumo wa stakabadhi ghalani unahitaji uwepo wa *warehouse* (maghala); nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wanaanzisha maghala katika halmashauri zote ambazo huu mfumo unakwenda kufanyakazi? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la kwanza la kuhusu elimu, Wizara tumejipanga kutoa mwongozo ambao ndani yake pia unajumuisha masuala ya elimu na masuala yote ya muhimu kabla ya kuingia katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Lengo letu ni kutatua changamoto ambazo zimekuwepo na hivyo kupitia mwongozo huu utakuwa umetibu tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu maghala, tunafahamu kwamba moja kati ya *requirement* kubwa ya stakabadhi za ghala lazima kuwepo na maghala. Katika bajeti yetu ambayo tumeisoma kupitia Wizara ni kwamba katika mwaka wa fedha unaokuja tunakwenda kujenga maghala mengi katika maeneo ya uzailishaji, lengo letu ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na maghala kuanzia katika ngazi za vijiji ambapo wanazalisha kwenda juu. Kwa hiyo katika eneo hilo, Serikali imeona imeona umuhimu na tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa maghala.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Butondo.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, msimu wa kilimo cha mazao ya choroko pamoja na dengi wa mwaka 2021/2022 katika Mkoa wa Shinyanga wakulima wa dengi walipata changamoto kubwa ya kupatiwa fedha kwa wakati; na hii ni kutokana na mfumo mzima kutokuwa na maandalizi mazuri ya ulipaji wa fedha katika Vyama vya Msingi ambavyo

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

vilinunua mazao haya kupitia Vyama hivyo vya Msingi; je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba fedha ziwe zinafika kwa wakati kupitia Vyama vya Msingi vilivyopo katika ngazi hiyo ya ushirika ili mradi kuondoa hata na changamoto hii ya wakulima wa dengu na choroko katika maeneo hayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Butondo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya awali, kwa kutambua changamoto hizi tumeamua kuja na mwongozo maalum ambao utawajumuisha wadau wote. Lengo la mwisho ni kuhakikisha ya kwamba mkulima anafaidika na mazao yake na tunaondoa changamoto hasa za ucheleweshaji wa malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba ndani mwongozo huu tutakwenda kutatua changamoto zote zilizopo katika mfumo wa stakabadhi za ghala.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka.

Na. 331

Ujenzi wa Barabara zilizofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina nchini

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara nyingi nchini zilizokwisha kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara zote zilizokwishafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Mpango huo unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa barabara nyingi hapa nchini zimeshafanyiwa upembuzi yakinifu kwa muda mrefu sasa na hizo barabara zimeshakuwa ni nyingi sana; na bado ukiuliza unaambiwa tunatafuta fedha kwa ajili ujenzi.

Je, Serikali haioni kwamba imefika wakati sasa tusitische kwanza kuendelea kufanyia upembuzi yakinifu tumalize hizi barabara ambazo tayari zimeshajengwa ili *resource* tulizonazo tumalizie hizi zilizojengwa ndipo tuendee kufanya upembuzi yakinifu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, iko barabara inayotoka Masasi kwenda Nachingwea mpaka Liwale zaidi ya kilometa 158, barabara hii imeshafanyiwa upembuzi yakinifu zaidi ya miaka minane sasa.

Je, ni lini Serikali watajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuzifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ambazo tunaendelea nazo. Lakini pia naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya mahitaji ili barabara ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami ni kujua gharama zake ili hata wakati Serikali inatafuta fedha inakuwa inafahamu gharama ya zile barabara, inakuwa inafahamu ni wananchi gani ambao watapisha ujenzi, lakini pia inasadia kuzuia wananchi wasijenge maeneo ambako barabara itapita.

Kwa hiyo, tutaendelea kufanya usanifu ili kuwa tayari tunapopata fedha tuanze kujenga badala ya kusubiri kuanza usanifu pale tunapokuwa tumepata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, barabara aliyoitaja ya Masasi – Nachingwea hadi Liwale, katika bajeti hii tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza kuijenga barabara kuanzia Masasi kwenda Nachingwea na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili kipande cha Nachingwea kwenda Liwale, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiswaga.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan ameshasaini mkopo wa trilioni 1.2 ambao unahusisha ujenzi wa barabara kadhaa, viwanja kadhaa pamoja na barabara ya kwenda *Ruaha National Park* inayopita Jimboni Kalenga.

Je, ni lini sasa Serikali tutegemee kuona kazi zinaanza kutekelezeka? Ahsante sana.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; napenda kujibu swali la nyongeza la Kiswaga, Mbunge wa Kalenga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *World Bank* wameshakubali kujenga barabara ya kutoka Iringa kwenye *Ruaha National Park* na ni kati ya hizo fedha ambazo ni *1.7 trillion*. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo sasa kinachosubiriwa tu nikuanza taratibu za manunuzi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sillo.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa barabara ya Dareda - Dongobesh usanifu wa kina umeshakamilika; je, ni lini zabuni zitatangazwa ili ujenzi huu uanze mara moja?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara ya Dareda - Dongobesh imeshakamilika kwa kufanyiwa usanifu wa kina. Kwa hiyo, kwa sasa Serikali ipo kwenye hatua za kutafuta fedha ili barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kisangi.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi kubwa za Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutujengea barabara ya mwendokasi kutoka Bendera Tatu mpaka Mbagala Rangitatu, lakini bado kuna changamoto kubwa katika maeneo ya Rangitatu.

Je, Serikali lini itakamilisha kujenga tena upya na vizuri kwa kiwango cha lami barabara kutoka Mbagala Kokoto - Rangitatu kwenda Kongowe - Mwandege? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii imekuwa na changamoto kubwa hasa ya foleni na Serikali sasa imeiweka kwenye mpango barabara hii ili iweze kujengwa upya na kupunguza foleni kubwa ambayo ni adha kubwa sana kwa wakazi wa Mbagala kwenda Kongowe, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kabati.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa barabara inayopitiwa na Mlima Kitonga ni barabara ambayo imekuwa ikipata ajali nyingi na imekuwa ikipitisha mpaka wagonjwa wanaopelekwa hospitali ya Muhimbili.

Je, Serikali sasa iko tayari kujenga kwa kiwango cha lami barabara mbadala ili kama magari yakichelewa kupita pale kwa siku mbili au siku tatu; barabara ya Mahenge - Udekwa inayokwenda kutokezea Ilula ili wananchi waweze

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kupita kama magari yamekwamwa muda mrefu? Ahsante.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjulishe Mheshimiwa Mbunge, kwanza kumpongeza kwa kutoa hilo wazo na sisi kama Serikali tumelichukua ili kweli kwamba kunapotokea changamoto basi tuwe na *alternative* ya kuweza kupitisha hasa kama kutatokea suala la wagonjwa kama alivyosema. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kassinge.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza katika Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kiranjeranje – Nanjilnji mpaka Ruangwa ni barabara ambayo imenadiwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 mpaka 2025, lakini pia imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Je, lini Serikali itatenga fedha au kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa, kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, azma ya Serikali ni kuzijenga barabara zote kwa kiwango cha lami na ndio maana tumeshaanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa tayari tumeshaanza hiyo ni hatua na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili tuweze kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Ardhi. Mheshimiwa Kakunda.

Na. 332

Viwango vya Nyumba Bora ya Kuishi Kitaifa

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA aliliza:-

Je, nyumba bora ya kuishi inatakiwa kuwa na sifa zipi na ni kwa nini Serikali haiweki ruzuku kwenye vifaa vya ujenzi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi naomba kumjibu Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge na Chifu wa Wakonongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba ni mojawapo ya mahitaji muhimu ya mwanadamu. Nyumba bora ni ile yenye huduma bora kwa usalama na afya kwa wakazi wake. Jitihada za Serikali kuhakikisha nyumba bora zinajengwa kwa gharama nafuu ni pamoja na kuweka mazingira wezeshi ya uanzishwaji wa viwanda vya kuzalisha vifaa vya ujenzi, kufanya utafiti na kuwezesha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kazi za ujenzi na kuhamasisha taasisi za fedha

kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na ununuzi wa nyumba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kabisa ambayo yamekwenda shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya sensa ya mwaka 2012 nchi yetu ina jumla ya nyumba 11,873,1950; kati ya hizo, nyumba bora ni 3,444,519 sawasawa na asilimia 37.1 maana yake tuna nyumba 8,429,431 ambazo ni sawa na asilimia 62.9 nyumba hizi sio bora, lakini kati ya hizo nyumba 2,359,906 sawasawa na asilimia 25.4 ni nyumba zimezekwa kwa nyasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu; nyumba ya kawaida ya vyumba viwili inahitaji shilingi 400,000 kwa maana ya kununua *bundle* mbili za mabati. Je, kwa nini Serikali isiweke pale shilingi 200,000 kwa mtu ili na yeye achange shilingi 200,000 ili hatimaye Serikali itumie kama shilingi bilioni 432 kuondoa kabisa nyumba za nyasi katika nchi hii? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; ni kwa nini Serikali isiweke viwango vya nyumba bora, ili kila mwananchi awe anazingatia ujenzi wa nyumba bora? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Joseph George Kakunda, maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

tutakapokuwa tumekamilisha sera ya nyumba na makazi jibu lako litakuwepo ndani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye swali la pili; ni kwamba Wizara imeendelea kuandaa rasimu ya Taifa ya Nyumba ambayo pamoja na mambo mengine itatoa mwongozo wa viwango vya nyumba bora vinavyotakiwa kuzingatiwa na wadau wote. Aidha, sera hiyo itaweka uratibu rahisi wa upatikanaji wa vifaa vya ujenzi vya gharama nafuu, upatikanaji wa mikopo ya nyumba, mfumo wa uratibu wa wadau wa sekta ya nyumba na hivyo kuwezesha upatikanaji wa nyumba bora kuwa za gharama nafuu, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mayenga.

MHE. LUCY T. MAYENGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sababu kubwa ambayo inasababisha wananchi waweze kushindwa kujenga nyumba bora ni gharama kubwa ya vifaa vya ujenzi, lakini vifaa hivi ni suala ambalo haliko Wizara ya Ardhi, liko Wizara ya Viwanda na Biashara.

Je, Wizara hii iko tayari sasa kukaa na Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuangalia zile sababu zote zinazofanya vifaa kuwa bei kubwa ikiwemo matamko ya viongozi, gharama kubwa za kodi na changamoto nyingine? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa mawazo yake mazuri, lakini nataka nimhakikishie tu kwamba yako maelekezo toka kwa Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla kukaa na Wizara zote zinazohusika katika eneo hili la ujenzi wa nyumba ikiwemo Wizara ya Ujenzi, ili kuhakikisha kwamba gharama zinakuwa

nafuu katika ujenzi, lakini pia katika vifaa na kuhakikisha mazingira yanakuwa mazuri ya upatikanaji wa nyumba zilizo bora na salama.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Paresso. Ahsante Mheshimiwa Ridhiwani kwa majibu mazuri.

Na. 333

**Umuhimu wa kuipatia ruzuku Bodi ya Maji ya
KAVIWASU – Karatu**

MHE. CECILIA D. PARESSO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaipatia ruzuku Bodi ya Maji ya *KAVIWASU* kwa kuwa imekuwa ikiendeshwa kwa gharama za wananchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Maji Namba 5 ya mwaka 2019 ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira kupitia kifungu cha 13(1)(b) vyombo vya watumia maji vinaruhusiwa kutoa huduma za maji kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini ambapo chombo cha watumia maji cha *KAVIWASU* kinatoa huduma kwenye baadhi ya maeneo ya mji wa Karatu. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha hakuna changamoto katika utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa mji wa Karatu unapata huduma ya maji inayotolewa na kusimamiwa na taasisi mbili za *KARUWASU* na *KAVIWASU*. Hivyo, Serikali inao

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

mpango wa kuanzisha taasisi moja na imara itakayotoa huduma ya maji kwa ufanisi kwa eneo lote la mji wa Karatu. Taasisi hiyo itapata ruzuku kwa kuzingatia miongozo iliyopo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini dhamira au msukumo wa Serikali wa kufikiria kuanzisha taasisi moja badala ya kuimarisha taasisi zilizopo na hususan hii taasisi ya *KAVIWASU* kwa sababu imekuwa ikifanya vizuri zaidi kulinganisha na ile taasisi ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; utozaji wa bei kati ya taasisi hizi mbili hutofautiana na ni ukweli kwamba hiyo taasisi ya Serikali inapata unafuu na bei yake inakuwa nafuu kwa sababu, inapata ruzuku kutoka Serikalini, ilhali ile taasisi iliyoanzishwa na wananchi haipati unafuu wowote na gharama zinabaki palepale. Serikali kwa mara nyingine mpo tayari kuipa ruzuku taasisi hii ya wananchi ili kuunga mkono jitihada za wananchi katika kupata maji katika Mji Mdogo wa Karatu? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lini tutaweka hizi taasisi kuwa moja; mara baada ya taratibu zote za Kiserikali kukamilika tutahakikisha tunafanya hizi taasisi mbili inakuwa moja kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utozaji wa bei unatofautiana, chombo ambacho kinasimamiwa na Serikali kinapewa ruzuku na kile cha wananchi hakipewi ruzuku;

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kitakachofanyika ni kitakuwa chombo kimoja kwa hiyo, ruzuku ya Serikali itaingia na lengo la Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama mpendwa anayetaka akinamama tuwatue ndoo kichwani, tuhakikishe huduma zinakuwa chini, tutahakikisha bei zinakuwa rafiki kwa wananchi na ruzuku pale inapobidi itakuwa inafika kwa wakati.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Rweikiza.

Na. 334

Ujenzi wa Chuo cha VETA Burugo - Nyakato

MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Chuo cha VETA Burugo – Nyakato katika Jimbo la Bukoba Vijijini utakamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera ambacho ujenzi wake ulianza mwaka 2019. Utekelezaji wa mradi huo unafanywa kupitia ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China wenye thamani ya shilingi bilioni 22.4 na mradi umefikia asilimia 96 na unategemea kukamilika mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi huo kutatoa fursa ya utoaji wa mafunzo kwa wananchi wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Mkoa wa Kagera kwa ujumla. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rweikiza.

MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Awali napenda niipongeze na kuishukuru Serikali kwa hatua iliyofikia ya ujenzi wa Chuo cha *VETA*, kizuri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Je, mara tutakapoanza kuchukua wanafunzi na kuwaingiza kwenye masomo, wanafunzi hawa wa chuo hiki watapatiwa mikopo ya Serikali ili masomo yaweze kutolewa vizuri? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa bado Serikali hatujaanza utaratibu wa kutoa mikopo kwa wanafunzi hawa wa *VETA* na vyuo vingine vya kati. Kwa hiyo, tunachofanya ni nini sasa kama Serikali? Tunachofanya kama Serikali kwa vyuo hivi vya kati pamoja na *VETA*, tumejaribu kupeleka ruzuku kwenye maeneo hayo na ndio maana utaona hata ada zake tofauti na vile vyuo vingine vya juu. Ada kwa wanafunzi hawa wa *VETA* kwa wale wa bweni ni shilingi 120,000 na wale wa kutwa ni shilingi 60,000 ambayo sio thamani halisi ya mafunzo hayo pale, lakini baada ya Serikali kuona umuhimu wa mafunzo haya imeamua kutoa ruzuku.

Kwa hiyo, kwa hivi sasa bado hatujaanza kutoa mikopo. Tunalibeba kama ushauri tuweze kuangalia katika kipindi kijacho kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha kama tunaweza tukatoa mikopo katika maeneo haya. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bupe.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwanza kabisa tunapenda kuishukuru Serikali kwa kutujengea Chuo cha *VETA* Mkoa wa Rukwa, chuo cha kisasa, chuo kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali langu ni lini sasa chuo hicho kitafunguliwa na wanafunzi waweze kupata mafunzo? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kulikuwa na mikoa ambayo vyuo vya *VETA* vya mikoa bado havijakamilika, miongoni mwa mikoa hiyo ni pamoja na Mkoa wa Rukwa na mwingine ni Mkoa wa Njombe, Geita pamoja na Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ukamilishaji wa majengo yale sasa unakamilika. Katika fedha zile za Uviko-19 tulizopata mwaka uliopita tumeweza kupeleka pale zaidi ya bilioni nne kwa ajili ya ukamilishaji wa chuo kile na tunataraji ujenzi ule unaweza ukakamilika katika kipindi hiki kifupi cha mwezi huu wa Juni na mwezi wa Julai, ili basi ifikapo mwezi wa kumi au mwezi Januari mwakani mafunzo pale yaweze kuanza. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Furaha.

MHE. FURAHA N. MATONDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Jinbo la Buchosa lina watu wanaozidi laki nne, lakini hawana Chuo cha *VETA*; je, ni lini Serikali itajenga chuo cha *VETA* katika Halmashauri

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ya Buchosa ili wananchi wale waweze kupata elimu, lakini pia waweze kujajiri? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Furaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sera yetu ya elimu na hata katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inazungumza ujenzi wa Chuo cha VETA katika kila Wilaya nchini. Kwa hiyo, nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeanza. Tulianza na Wilaya 25, lakini Wilaya nne nazo vilevile zilikuwa tayari zimeshajengewa katika mwaka ule uliopita wa fedha na sasa hivi Serikali tuko mbioni katika utafutaji wa fedha, ili basi Wilaya zilizobaki karibu Wilaya 70 tuweze kukamilisha ujenzi huu wa vyuo vya VETA katika Wilaya zote nchini. Nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa maswali yetu yamekwisha na ukiona maswali ya nyongeza ni machache na mengine hakuna ujue Serikali iko *site* na inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Orodha ya majina ya wageni ndio kwanza imeingia, kwa hiyo, wageni waliopo Bungeni leo hii, wageni waliopo Jukwaa la Spika, wageni wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana - Waziri wa Maliasili na Utalii ambao ni viongozi, watendaji, Wenyeviti wa Bodi na wadau wa maendeleo ya sekta ya utalii na taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Dkt. Francis Michael - Katibu Mkuu, Ndugu Juma Mkomi - Naibu Katibu Mkuu, ahsanteni sana, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wanafamilia wa Dkt. Pindi Chana na Mheshimiwa Mary Masanja, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, msimame kwa pamoja. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Bunge, wasimame kwa pamoja. Wageni wote wa Waheshimiwa Wabunge simameni kwa pamoja, ahsanteni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 42 na walimu kumi kutoka *American and British English Centre* ya Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 86 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya *John Merlin* ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 114 kutoka shule ya Mtakatifu Theresa wa Avila iliyopo Same, Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

NAIBU SPIKA: Waziri wa Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ...

NAIBU SPIKA: Haya, kwa hiyo kwa makofi haya nategemea, kwa makofi haya tunategemea hakuna masuala ya tembo leo humu. *(Makofi/Kicheko)*

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha, ninaomba Bunge lako lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kujenga uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Aidha, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniadini na kunipa dhamana ya kusimamia Wizara hii yenye umuhimu mkubwa kwa Taifa na jamii kwa ujumla. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kumuomba kwa Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na afya njema ili aendelee kuwatumikia Watanzania. *(Makoff)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao thabiti katika kusimamia maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Kupitia miongozo na maelekezo yao mazuri na yenye tija Wizara imeendelea kutimiza wajibu wake wa kuimarisha uhifadhi na kuendeleza utalii na hivyo kuchangia katika juhudi za kukuza uchumi na ustawi wa wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha nikupongeze wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, nimpongeze pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge letu tukufu imani hiyo imejengeka kutokana na umahiri na weledi mkubwa mliouonesha katika kuliongoza Bunge hili. Vilevile

niwapongeze Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha shughuli za Bunge letu kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mbunge wa Kondoa Mjini kwa kujadili, kushauri na kupitisha mapendekezo ya makadirio na mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa namna ya kipekee niseme kwa uwazi kuwa Kamati hii imekuwa na mchango mkubwa katika kuishauri Wizara kupitia maoni na maelekezo yake, tunasema ahsante sana. Wizara itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati na Bunge lako tukufu ili kufanikisha malengo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninaomba nitumie fursa hii adhimu kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa juhudi kubwa wanazozifanya katika kusimamia na kuhifadhi maliasili na kuendeleza utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninawashukuru wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa kuendelea kuniunga mkono kwa dhati katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii. Ninapenda kuwahimiza wote kushiriki katika uhifadhi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wenzangu wa Wizara akiwemo Mheshimiwa Mary Francis Masanja, Naibu Waziri; Dkt. Francis Kasabubu Michael, Katibu Mkuu na Ndugu Selemani Juma Mkomi, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nimpongeze mtangulizi

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wangu pia Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria kwa mchango wake aliutoa katika kufanikisha majukumu mbalimbali ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninawashukuru watendaji wakuu na watumishi wa Wizara na wadau wote wa sekta ya maliasili na utalii kwa ushirikiano wanaoendelea kutupa katika kuiongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi wote wa Serikali wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri, Wabunge na Wakuu wa Taasisi pamaja na watumishi, ndugu, jamaa na marafiki kwa jinsi walivyojitoa katika kutufariji na kufanikisha mazishi ya mama yetu mpendwa Regina Mpetro Mlowe. Kwa kweli Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kutoa pole kwako, Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako tukufu, ndugu, jamaa na marafiki na Watanzania wenzangu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Elias Kwandikwa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa William Tate Olenasha aliyekuwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; Mheshimiwa Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar; na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa.

Aidha, natoa pole kwa ndugu, marafiki na watumishi wote wa Wizara kutokana na watumishi kumi waliopoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu yao. Kwa hakika, watumishi hawa ni mashujaa ambao wamepoteza maisha wakitetea rasilimali za nchi yetu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

Pia nitumie fursa hii kutoa pole kwa watumishi waliojeruhiwa wakati wa kutekeleza majukumu yao. Sambamba na hilo, ninatoa pole za dhati kwa wananchi

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ambao wamepata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu na hivyo kujeruhiwa, kupoteza ndugu na kuharibiwa mali zao kwa kweli tunasema pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo imejikita katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali za maliasili na malikale zenye mchango mkubwa katika kuendeleza utalii, ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi. Aidha, maeneo ya hifadhi ndiyo vyanzo vikuu vya maji, nishati, makazi ya wanyamapori na viumbe wengine, uhifadhi wa udongo na ufyonzaji wa hewa ukaa, hali inayopunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Vilevile malikale zinatumiwa kuhifadhi historia na tamaduni zetu. Hivyo, ninaomba nitumie fursa hii kutoa rai kwa Watanzania wote na wadau wa sekta ya maliasili na utalii nchini, kuendelea kushirikiana na Wizara kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii, kwa maendeleo ya Taifa letu na dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija katika eneo la ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022; Wizara iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 689.35 kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 478.01 zinakusanywa na Wizara kupitia mfumo wa *TRA* kutoka vyanzo vya *TANAPA*, *NCAA* na *TAWA* na shilingi bilioni 211.33 zinakusanywa moja kwa moja na Wizara kupitia mfumo wa *MNRT Portal* kutoka Idara, mifuko na taasisi nyingine za Wizara. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022 Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 396.27 sawa na asilimia 57 ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 249.83 zimekusanywa kupitia *TRA* na shilingi bilioni 146.44 zimekusanywa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

571.63 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 418.86 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 152.77 ni miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022 Wizara na Taasisi zake ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 474.35 sawa na asilimia 83 ya bajeti iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 357.75 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 116.61 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuzungumzie mafanikio katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara imepata mafanikio mbalimbali na naomba tuanze na utangazaji utalii na kuvutia uwekezaji kupitia Programu Maalum ya *Tanzania The Royal Tour*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa napenda kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake kwa kweli kubwa za kuitangaza nchi yetu kimataifa kupitia programu ya *Tanzania The Royal Tour*. Programu hiyo imewezesha kuitambulisha Tanzania kimataifa kwa kutangaza vivutio vya utalii vya kipekee vya nchi yetu; kuonesha fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye sekta ya maliasili na utalii pamoja na kuimarisha nafasi ya nchi katika jumuiya za kimataifa. Programu hii *Tanzania The Royal Tour* ilizinduliwa mwezi Aprili, 2022 katika Jiji la New York na Jiji la Los Angeles mjini Marekani na kuendelea katika Jiji la Arusha, Dar es Salaam, Zanzibar na Dodoma. (makofi)

Katika uzinduzi nchini Marekani zaidi ya watu 6,000 walishiriki wakiwemo viongozi wa kitaifa, viongozi wa majiji husika na watu maarufu, wawekezaji, wadau wa utalii na uhifadhi na wafanyabiashara mbalimbali. Uzinduzi huo pia ulishirikisha vyombo mbalimbali vya habari vya kimataifa vikiwemo vituo vya televisheni na redio vya *CBS, Fox News, NBC, YouTube* na *PBS - Amazon Prime Video*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, programu ya *Tanzania The Royal Tour* imeanza kuleta matunda kwa kuvutia watalii na

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wawekezaji mbalimbali kutembelea nchini. Mathalani wakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka katika masoko ya utalii wakiwemo Marekani, Ufaransa na Lithuania wamehamasika kutembelea nchini ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao. Aidha, wawekezaji kutoka Taifa la Bulgaria wameonesha nia ya kuwekeza nchini kwa kujenga hoteli nne zenye hadhi ya nyota tano katika Hifadhi za Taifa Serengeti, Ziwa Manyara na Tarangire; na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine, Serikali imesaini mkataba wa ushirikiano katika masuala ya utalii, biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Jiji la Dallas Marekani. Hatua hiyo itafungua fursa za usafiri wa anga kwa kuwezesha safari za moja kwa moja za ndege kutoka Tanzania hadi Dallas, Marekani na hivyo kuongeza idadi ya wageni nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kuendelea kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kutangaza utalii na kuvutia uwekezaji kwa maslahi mapana ya Taifa na ustawi wa jamii kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kuendelea kutambulika Kimataifa katika masuala ya utalii na uhifadhi; kimsingi Tanzania imeendelea kutambulika kimataifa na kupata tuzo mbalimbali zikiwemo Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa hifadhi inayoongoza kwa ubora Barani Afrika kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2021; na Tanzania kuwa nchi inayoongoza kwa shughuli za utalii Barani Afrika. Kimsingi tuzo hizi zilitolewa na *World Travel Award*. (*Makofi*)

Tuzo nyingine ni pamoja na *Travellers' Choice Destination – National Parks of the World* iliyotolewa na *Tripadvisor* ambapo Tanzania imeingiza hifadhi nne katika orodha ya hifadhi 25 bora duniani zikiongozwa na Hifadhi ya Taifa Serengeti. Hifadhi nyingine ni Hifadhi za Taifa Kilimanjaro na Tarangire; Eneo lingine ni Hifadhi za Taifa Kilimanjaro na

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Tarangire na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Aidha, Zanzibar na Jiji la Arusha zimeorodheshwa na *Tripadvisor* kupitia *Travellers' Choice Destination Africa* kuwa ni miongoni mwa maeneo kumi bora ya shughuli za utalii Barani Afrika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa malighafi ya mazao ya misitu kwa ajili ya viwanda; Wizara imefanikiwa kuongeza upatikanaji wa malighafi ya mazao ya misitu katika mashamba ya miti ya Serikali kutoka mita za ujazo 729,000 kwa mwaka 2020/2021 hadi wastani wa mita za ujazo 1,000,000 kwa mwaka 2021/2022. Mafanikio haya yametokana na juhudi mbalimbali zikiwemo: kuendeleza mashamba ya miti kwa kupanda miche zaidi ya milioni 29 na kuanzisha shamba jipya la miti la Makere, Mkoa wa Kigoma lenye ukubwa wa hekta 29,827.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika uendeshaji wa minada ya mazao ya misitu na wanyamapori; Wizara imeongeza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kuendesha minada ya mazao ya misitu na wanyamapori. Mathalani Wizara imefanikiwa kuendesha jumla ya minada saba ya kielektroniki iliyojumuisha vitalu 100 vya uwindaji wa kitalii, kati ya vitalu hivyo vitalu 64 vimeuzwa na kufanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 18.1 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 5.0 ambacho kingekusanywa kwa njia ya kiutawala (*administrative*) bila kutumia elektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kuendeleza utalii ikolojia katika hifadhi za misitu za mazingira asilia; katika kupanua wigo wa mazao ya utalii nchini, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya utalii ikolojia katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia zikiwemo Hifadhi za Amani, Pugu Kazimzumbwi, Magamba na Ziwa Duluti. Baadhi ya juhudi zilizofanyika ni ukarabati wa barabara zenye urefu wa kilometa 66.7, kwa njia za watembea kwa miguu kilometa 163.2 na ujenzi wa kambi tano za kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto ya uwepo wa janga la UVIKO-19, sekta ya utalii nchini

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

imeendelea kuwa stahimilivu ambapo idadi ya watalii na mapato yameendelea kuongezeka. MATHALANI katika mwaka 2021 Tanzania imefanikiwa kupokea jumla ya watalii wa kimataifa 922,692 ikiwa ni ongezeko la asilimia 48.6 kutoka watalii 620,867 kwa mwaka 2020 wakati wa UVIKO sasa tumekuwa tunazidi kuongeza watalii.

Aidha, mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa pia yameongezeka kutoka dola za Marekani milioni 714.59 mwaka 2020 hadi dola za Kimarekani bilioni 1.3 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 83. Mafanikio haya yamechochewa na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Wizara na Mheshimiwa Rais Mama yetu mpendwa Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukua kwa utalii wa ndani; Wizara imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani kupitia kampeni na programu mbalimbali. Hatua hizi zimeongeza idadi ya watalii wa ndani waliotembelea maeneo ya hifadhi, vituo vya malikale na makumbusho kutoka watalii 562,549 mwaka 2020 hadi 788,933 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 40.2. Ongezeko la idadi ya watalii limechangwiwa na juhudi mbalimbali zikiwemo kampeni za kutangaza utalii, maadhimisho na maonesho mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupungua kwa ujangili na uvunaji haramu wa maliasili; Wizara imeendelea kuongeza jitihada za kuimairisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Jitihada hizo za kudhibiti zinadhihirishwa na matokeo ya sensa ya wanyamapori iliyofanyika mwaka 2021 ambapo idadi ya tembo imeongezeka kwa asilimia 30 katika Mfumo Ikolojia Ziwa Natron - *West Kilimanjaro*.

Aidha, katika Mfumo Ikolojia Ruaha - Rungwa idadi ya nyati imeongezeka kwa asilimia 80, pundamilia asilimia 36 na palahala asilimia 65 ikilinganishwa na sensa iliyofanyika mwaka 2018. Pia idadi ya faru weusi ambao wako hatarini kutoweka imeongezeka kwa asilimia 27.5 ikilinganishwa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

idadi yao kwa mwaka 2018. Ongezeko la Wanyamapori hao ni kiashiria cha kuimarika kwa ulinzi na maeneo ya hifadhi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarika kwa utalii wa urithi wa utamaduni na malikale; Wizara imefanikiwa kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vituo vya malikale na makumbusho kutoka 349,264 mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia 582,080 mwezi Aprili 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 167. Ongezeko hilo limechochewa na juhudi mbalimbali zikiwemo kuanzisha programu maalum za kuhamasisha makundi katika jamii kutembelea vivutio vya malikale na makumbusho, kufanya matamasha ya utamaduni katika maeneo mbalimbali nchini, kuanzisha jarida maalum la makumbusho, kufanya mikutano maalum na wahariri wa vyombo vya habari na kuimarisha miundombinu katika maeneo ya malikale na makumbusho. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija katika eneo la utekelezaji wa majukumu ya Wizara; sekta ya wanyamapori ina jukumu la kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo na kufanya tafiti za wanyamapori ndani na nje ya maeneo ya hifadhi. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara imetekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutoa elimu kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya hifadhi. Aidha, Wizara imetumia teknolojia ya kufuatilia nyendo za wanyamapori hao kwa kuwafunga vifaa maalum vya kusukuma mawimbi ili kurahisisha ufuatiliaji. Katika kufanikisha zoezi hilo, jumla ya tembo 107, mbwa mwitu saba, faru 64, nyumbu kumi na simba 21 kwa kweli waliofungwa mikanda ya mawasiliano *GPS collar* ili kuwezesha kufuatiliwa mienendo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara imetenga fedha kiasi cha shilingi 1,230,000,000 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa vituo 11 vya askari wa kuzuia wanyamapori wakali na waharibifu

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

katika maeneo korofi nchini. Tayari fedha hizo zimetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango na sasa ujenzi wa vituo hivyo 11 unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha Kanuni na Amri za Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu, aidha imefanya mapitio ya Kanuni za Utalii wa Picha za mwaka 2016, Kanuni za Uwekezaji Mahiri ya mwaka 2021, Kanuni ya Mashamba ya Wanyamapori ya mwaka 2020 na Kanuni za Biashara ya Nyara ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, taratibu za usajili wa magari ya Jeshi la Uhifadhi kutoka namba za kiraia kwenda namba za kijeshi zimekamilika ambapo magari 1,338 kati ya 1,699 yamepata usajili huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (*TANAPA*); katika kuboresha mahusiano kati ya hifadhi na jamii shirika limetoa elimu ya uhifadhi kwa vijiji 477 vinavyopakana na hifadhi za Taifa. Aidha, shirika kwa kushirikana na wadau mbalimbali limetoa chanjo 63,005 dhidi ya magonjwa wa mapafu kwa ng'ombe, kondoo na mbuzi katika vijiji 12 vinavyopakana na Hifadhi za Taifa Mkomazi na Tarangire. Hatua hii inalenga kuzuia milipuko na kusambaa kwa magonjwa yanayoweza kuathiri wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (*TAWA*); mamlaka imetoa jumla ya leseni 36 za ufugaji wa wanyamapori na kwa wawekezaji wa bustani, mashamba na ranchi za wanyamapori, na leseni 34 kwa ajili ya kuendesha biashara ya wanyamapori. Aidha, mamlaka imetoa maeneo saba kwa wawekezaji nchini chini ya utaratibu wa uwekezaji mahiri katika mapori ya akiba na tengefu. Uwekezaji huo umeiwezesha mamlaka kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za uwindaji wa kitalii kutoka shilingi bilioni 4.2 kwa mwaka wa fedha 2021 hadi shilingi bilioni 22.1 mwezi Aprili, 2022 sawa na asilimia 426.2. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko; katika hatua nyingine mamlaka imefungua na kujenga barabara zenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

urefu wa kilometa 321.5 kwa kiwango cha changarawe na madaraja mawili katika mapori ya akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro; mamlaka imekarabati vituo sita vya askari katika maeneo ya Lemala, Makhoromba, Ndotu, Kakesio, Endamagha na Masamburai na ujenzi wa vituo vipya vya askari katika maeneo ya Lositete na Lemala kimsingi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mamlaka imekamilisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 4.2 inayoshuka *Crater* ya Ngorongoro kwa kiwango cha tabaka gumu la mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutafuta suluhu ya kudumu ya changamoto za matumizi mseto ya ardhi ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, mamlaka imefanya uhamasishaji kupitia vikao na mikutano ya majadiliano baina ya Serikali na wadau mbalimbali wakiwemo wenyeji waishio ndani ya eneo hilo. Kupitia jitihada hizo, jumla ya kaya 278 zenye wakazi 1,439 wamejiandikisha kuhama kwa hiari kutoka hifadhini. *(Makoff)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara imebainisha maeneo mbadala ya yaliyopo Handeni, Tanga na Kitwai, Manyara kwa ajili ya makazi kwa wananchi watakaohama kutoka eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Kwa upande wa Handeni, mamlaka imebainisha eneo lenye ukubwa wa hekta 112,239 kwa ajili ya matumizi ya makazi na huduma za jamii. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 Wizara ilifanikiwa kupima eneo lenye ukubwa wa hekta 73,528.73 lililogawanywa kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo makazi hekta 10,000 kilimo hekta 13,628.48, malisho hekta 22,176.06, ujenzi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo hekta 1,329.35, ushoroba wa wanyamapori hekta 26,314.42 na hifadhi ya misitu hekta 6,082.72 zoezi la upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi katika eneo lililobaki pamoja na eneo la Kitwai lenye ukubwa wa hekta 409,416 kimsingi linaendelea.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (*TAWIRI*); Taasisi imeidadi wanyamapori katika mifumo ikolojia ya Ruaha, Rungwa na Katavi, Rukwa, maeneo ya mtawanyiko na shoroba zilizomo katika mifumo ikolojia hiyo. Mathalani matokeo ya sensa katika mfumo ikolojia wa Ruaha, Rungwa yanaonesha kuwa kuna tembo 15,608, nyati 20,911, swalapala 8,646, pundamilia 10,552, palahala 6,636 na kongoni 4,017. Aidha, matokeo hayo yakilinganishwa na yale ya mwaka 2018 yanaonesha kuimarika kwa idadi ya tembo sambamba na ongezeko la nyati kwa asilimia 80, pundamilia asilimia 36 na palahala asilimia 65. Kwa ujumla takwimu zinaonesha maeneo yaliyohifadhiwa yamezidi kuimarika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori (Mweka); chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 834 katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Aidha, chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 22 juu ya mbinu ya kukamata na kuhamasisha nyoka katika eneo ya Bulyanhulu, Mkoa wa Shinyanga na mafunzo kwa waongoza utalii wapatao 1060 kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Vilevile chuo kimejenga kumbi mbili ma mihadhara katika *campus* kuu ya Mweka na eneo la mafunzo kwa vitendo kwa kuchinja lililopo Wilayani Babati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie kituo cha mafunzo ya uhifadhi ya maliasili na jamii, Likuyu Sekamaganga; kituo kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 204 ambapo askari wanyamapori wa vijiji 20 wamepata mafunzo ya usimamizi wa rasilimali za maliasili na askari 150 wa *TAWA* wamepata mafunzo ya utayari wa Jeshi la Uhifadhi na Wanyamapori na Misitu, katika hatua nyingine kituo kimeandaa mitaa mipya ya kozi za Astashahada na Stashahada ya Utalii na Waongoza Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania; mfuko huu umeendelea kuwezesha *operation* maalum za kuzuia ujangili, utekelezaji wa kazi za kikosi kazi cha Taifa cha kupambana na ujangili na jeshi la

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

uhifadhi wa wanyamapori na misitu. Aidha, mfuko umewezesha kufanyika kwa uhakiki wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya 36 zilizoathiriwa pamoja na kufanya malipo ya shilingi milioni 790.7 kwa wahanga 3,598 walioathiriwa na wanyamapori hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia sekta ya misitu na nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara imetekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Mazao ya Mbao yanayohandisiwa *National Engineered Wood Sector Development Framework 2021/2030* pamoja na mpango kazi wa utekelezaji wake utakaowezesha uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vya mazao ya misitu hapa nchini. Pia Wizara imefanya maboresho ya Kanuni ya Tozo za Mazao ya Misitu ya mwaka 2020 na kuandaa Kanuni Mpya Toleo Na. 59 la mwaka 2022. Vilevile Wizara imekamilisha ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki vitano na ukarabati wa viwanda katika Wilaya za Kibondo, Nzega, Sikonge, Bukombe, Mlele na Tabora Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (*TFS*); wakala umehakiki mipaka ya misitu 120 yenye urefu wa kilometa 160, kuweka vigingi 589 na mabango 204, kujenga barabara zenye urefu wa kilometa 49, kalavati nane na daraja moja katika mashamba ya miti 14 ya Buhindi, Kiwira, Longuza, Meru, *North Kilimanjaro*, Rondo, Rubare, *Sao Hill*, Shume, Mpepo, Ukaguru, *West Kilimanjaro*, Wino na *North Ruvu*. Aidha, wakala umeandaa mipango 48 ya usimamizi na uendelezaji wa misitu yenye ukubwa wa hekta zaidi ya milioni 1.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija upande wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (*TAFORI*); taasisi imefanya utafiti kuhusu moto wa misituni na kubaini kuwa takribani eneo la kilometa za mraba 95,793 liliungua na moto kwa kipindi cha

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

mwaka 2021/2022. Aidha, maeneo ambayo yameathirika zaidi na moto ni Mikoa ya Lindi, Morogoro na Katavi. Pia utafiti umebaini uwepo wa maeneo yaliyoathirika na matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi kama vile Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Hifadhi za Misitu na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vikuu vya moto ni pamoja na ufunguaji mashamba kwa ajili ya kilimo, uvunaji asali usiotumia zana za kisasa, majangili na moto mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija upande wa vyuo vya taaluma ya misitu na ufugaji nyuki vinajumuisha Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (*BTI*), Chuo cha Viwanda vya Misitu (*FITI*) na Chuo cha Misitu Olmotonyi (*FTI*); katika mwaka wa fedha 2021/2022 Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wanafunzi 378 pamoja na kutoa elimu ya ufugaji nyuki wenye tija kwa wafugaji nyuki 130 katika Wilaya za Sikonge, Mlele na Mpanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie Mfuko wa Misitu Tanzania; mfuko kimsingi umegharamia ununuzi wa mashine za kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki kwa ajili ya viwanda vinne katika Halmashauri za Wilaya ya Kibondo, Bukombe, Sikonge na Mlele.

Aidha, mfuko umetoa ruzuku kwa miradi 60 inayoendelea na miradi mipya 63 ya uanzishaji wa vitalu vya miti na upandaji miti shuleni katika Wilaya 36 za mikoa nane inayopatikana katika maeneo ya nyanda kame ikiwemo hapa tulipo Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii nchini. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ilitekeleza majukumu yake katika sekta ya utalii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki iliandaa Onesho la Kwanza la Kimataifa la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani *East*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

African Regional Tourism Expo lililofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 9 hadi 16 Oktoba, 2021.

Katika hatua nyingine Wizara ilishiriki Mkutano wa 64 wa Shirika la Utalii Duniani, Kamisheni ya Kanda ya Afrika yaani the 64th *UNWTO Commission for Africa* uliofanyika kuanzia tarehe 2 hadi 4 Septemba, 2021 katika Kisiwa cha Cabo Verde ambapo Tanzania ilichaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa mwenyeji wa Mkutano ujao wa 65 wa *UNWTO* ambao utafanyika mnamo mwezi wa kumi Jijini Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie Bodi ya Utalii Tanzania; bodi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeratibu ushiriki wa Tanzania katika maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Maonesho hayo ni pamoja na maonesho ya *FITUR 2022* na *InvesTour* ya nchini Uhispania, *National Tour Association Annual Convention*, nchini Marekani, *road show* iliyohusisha nchi za Ujerumani, Austria, Switzerland, Sweden na Denmark na *Africa Tourism Leadership Forum 2021*, nchini Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, bodi iliratibu ushiriki wa Wizara katika onesho la dunia la *Expo 2020 Dubai*, Umoja wa Falme za Kiarabu na uzinduzi wa Programu ya *Royal Tour*. Katika onesho hilo, nchi yetu ilipewa heshima ya pekee ya kuwa na siku maalum ambapo mnara maarufu duniani wa *Burj Khalifa* ulipambwa kwa rangi za bendera ya Tanzania na vivutio vya utalii vilivyopo nchini vilioneshwa mubashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie Chuo cha Taifa cha Utalii (*NCT*); kimsingi chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,127 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, chuo kimekarabati miundombinu ya kutolea mafunzo katika *campus* za Bustani, Arusha na Temeke na kununua na kusimika mifumo ya TEHAMA, vitendea kazi na vifaa mbalimbali vya kutolea mafunzo na kujifunzia katika *campus* za Mwanza, Temeke, Bustani na Arusha. Vilevile chuo kimenunua eneo lenye jumla ya ekari 32.2 kwa ajili ya ujenzi wa *campus* ya Mwanza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye sekta ya mambo ya kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za malikale na urithi wa utamaduni. Katika mwaka wa fedha 2021 Wizara imetekeleza shughuli mbalimali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea kuenzi falsafa za Baba wa Taifa Wizara imezindua mpango wa miaka 10 wa kuhifadhi kumbukumbu, kuenzi na kusherehekea urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Katika kutekeleza mpango huo Wizara imeratibu Adhimisho la Kumbukizi ya miaka 100 tangu kuzaliwa kwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo taasisi za elimu, makundi ya vijana, asasi za kijamii na wananchi kwa ujumla. Kilele cha maadhimisho hayo kilifanyika tarehe 13 Aprili, 2022 Mwitongo, Butiama, Mkoani Mara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie sasa Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania; kwa kweli Shirika limekusanya mikusanyo 54 kutoka kwa jamii ya watu wa Songea na mikusanyo 25 kutoka kwa jamii ya watu wa Rukwa. Sambamba na hilo, ukusanyaji wa kumbukumbu za Marais wastaafu nchini umefanyika ikiwemo hotuba 79 zinazohusu ukombozi, maendeleo, uchumi utamaduni na siasa. Aidha, mikusanyo 1,290 ya akiolojia imekusanywa kutokana na utafiti uliofanyika eneo la Laetoli lenye nyayo za zamadamu. Ili kuendelea kutunza kumbukumbu hizi, Shirika limeandaa mfumo wa kidigitali wa kusajili na kuhifadhi mikusanyo na limejiunga na *data saver* ya *National Internet Data center*. Katika hatua nyingine Shirika limeweka onesho la kudumu la tembo katika Makumbusho ya Elimu Viumbe -Arusha na usimikaji wa taswira za wanyamapori wakiwemo nyati, tembo, twiga, faru na kiboko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie sasa Mfuko wa Mambo Kale; mfuko umewezesha maandalizi ya mpango wa miaka 10 wa kuenzi na kusherehekea urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere; ukarabati wa jengo alilofikia Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati wa kudai

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

uhuru lililopo Manispaa ya Mikindani, Mtwara, kufanya tathmini ya Sera ya Malikale ya 2008 na kuwezesha uandaaji wa rasimu ya uwekezaji katika maeneo ya malikale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa miradi ya maendeleo; mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara imeendelea kutekeleza miradi mitano ya maendeleo ambayo ni Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Nyanda za Juu Kusini Mradi huu unaitwa *REGROW*; Mradi wa Kuzuia na Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara; Mradi wa Panda Miti Kibiashara; Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu (*FORVAC*) na Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (*BEVAC*). Kwa upande mwingine Wizara ilitekeleza Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Athari za UVIKO-19 ambapo iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 90.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2021/2022 yamefafanuliwa kuanzia ukurasa wa 32 hadi ukurasa wa 104 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya zipo changamoto; Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo pamoja na uwepo wa ugonjwa wa UVIKO-19 duniani ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa sekta ya utalii; ongezeko la migogoro kati ya binadamu na wanyamapori ambao umesababisha uharibifu wa mali, vifo na mlipuko wa magonjwa kati ya binadamu na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni uwepo wa matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi na uvamizi wa maeneo ya hifadhi kwa shughuli za kibinadamu; utegemezi mkubwa wa misitu kwa ajili ya nishati; na uwepo wa mimea vamizi katika baadhi ya maeneo ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hizi, Wizara imeweka mikakati mbalimbali ikiwemo kutoa elimu kwa wadau wa utalii juu ya namna bora

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ya kutumia mwongozo wa uendeshaji wa shughuli za sekta ya utalii; kujenga vituo vya askari katika maeneo yenye changamoto kubwa ya matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu; kutumia mbinu za kielektroniki za kufuatilia mienendo ya makundi ya wanyamapori wakali na waharibifu; kutoa elimu ya namna ya kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu; kuimarisha doria za kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara; kuendelea kutoa elimu ya namna ya kuzuia na kukabiliana na moto kichaa katika maeneo ya hifadhi; kuweka alama na mabango katika maeneo ya mipaka ya hifadhi; kuwezesha jamii inayopakana na maeneo ya hifadhi kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo yao; na kuwezesha miradi mbalimbali ya jamii ikiwemo ufugaji nyuki kwa lengo la kuwapatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija upande wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023; Wizara imeandaa mpango na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/2023 kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 hadi 2025/2026; na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 – 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya mpango huo ni pamoja na ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2022/2023 makadirio ya maduhuli yatakusanywa kutokana na sekta ya maliasili na utalii ni jumla ya shilingi bilioni 670.86. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 469.36 zitakusanywa na Wizara kupitia mfumo wa *TRA* kutoka vyanzo vya *TANAPA*, *NCAA* na *TAWA* na shilingi bilioni 201.49 zitakusanywa moja kwa moja na Wizara kupitia mfumo wa *MNRT Portal* kutoka Idara, Mifuko na Taasisi nyingine za Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa mwaka 2022/2023 inakadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 624.14; kati ya fedha hizo shilingi bilioni 443.70 zitagharamia matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 180.44 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Makadirio ya matumizi ya kawaida yanajumuisha makadirio ya mishahara shilingi bilioni 175.88

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

na makadirio ya matumizi mengineyo shilingi bilioni 267.82. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi bilioni 109.88 fedha za ndani na shilingi bilioni 70.56 fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuangalie kazi zitakazotekelezwa na Wizara na taasisi na taarifa hii ipo ukurasa 112 hadi 139.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza na eneo la Wanyama Pori; Wizara itajenga barabara mpya zenye urefu wa kilometa 2,500 katika Hifadhi za Taifa za Arusha, Burigi - Chato, Gombe, Katavi, Kilimanjaro, Kitulo, Mahale, Udzungwa, Manyara, Rubondo, Rumanyika - Karagwe, Ruaha, Mikumi, Nyerere na Serengeti. Aidha, Wizara itajenga njia za utalii zenye urefu wa kilometa 251 na barabara za kutembea kwa miguu zenye urefu wa kilometa 342.5. Vilevile itakarabati barabara zenye urefu wa kilometa 6,500 na viwanja vya ndege 17 katika Hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi, Nyerere, Saadani, Tarangire, Mkomazi na Serengeti.

Aidha, itawezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 30 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Nyerere na vijiji 18 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Serengeti; kuchimba mabwawa nane na kukarabati mabwawa matano kwa matumizi ya wanyamapori katika hifadhi za Taifa za Mkomazi, Tarangire, Mikumi, Katavi, Ruaha, Saadani na Serengeti. Pia Wizara itaboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori kwa kudhibiti mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 30,331 katika Hifadhi za Taifa Nyerere, Saadani, Serengeti, Arusha, Ibanda-Kyerwa, Mto Ugalla, Mikumi, Mkomazi na Katavi. Vilevile Wizara itaotesha miti ya asili 100,000 katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya misitu na nyuki; Wizara itaandaa mipango ya kazi ya utekelezaji mikakati na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu na Ufugaji Nyuki, mathalani kuandaa Mkakati wa Taifa wa Miti ya Mianzi; Kilimo-Mseto na Mkaa. Aidha, kuandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Usimamizi wa Nyuki wasiouma. Pia Wizara itaandaa Mipango ya Usimamizi wa Misitu 57 yenye

ukubwa wa hekta 1,703,202 na kufanya mapitio ya Mipango ya Usimamizi wa Misitu ya Hifadhi 111.

Vilevile kuweka vigingi 1,369 na mabango 2,133; na kujenga minara miwili mipya ya kubaini matukio ya moto na kukarabati mingine 11. Kwa upande mwingine, Wizara itaanzisha shamba jipya moja la ufugaji nyuki; kuzalisha tani 49 za asali, tani 2.9 za nta na kilo 50 za chavua na kuchonga mizinga ya nyuki 1,200.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija upande wa sekta ya utalii; Wizara itakamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999; na kuandaa Programu ya Maendeleo ya Utalii nchini. Aidha, itabainisha maeneo ya fukwe katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kwa ajili ya uwekezaji na uendelezaji wa shughuli za utalii. Katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kupanga huduma za malazi katika daraja na ubora katika Mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya na Mwanza. Sambamba na hilo, Wizara itabaini vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji wa shughuli za utalii nchini katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Morogoro na Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mambo ya kale; Wizara itafanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Malikale ya mwaka 2008 na kuandaa mkakati wa utekelezaji na kufanya mapitio ya Sheria ya Mambo Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281. Aidha, Wizara itaandaa kanuni na miongozo ya uhifadhi na utafiti wa maeneo ya malikale; vigezo vya kutambua rasilimali za urithi wa utamaduni kuwa urithi wa Taifa; na mpango wa kitaifa wa usimamizi wa uendelezaji wa rasilimali za urithi wa utamaduni. Katika hatua nyingine Wizara itapima maeneo saba ya malikale na kutengeneza mfumo wa maombi ya vibali vya utafiti. Sambamba na hilo Wizara itafanya ukarabati wa majenzi ya kale 22; kufanya tafiti nne na kukusanya na kuhifadhi mikusanyo ya asili na kiutamaduni 220.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu shughuli na miradi itakayotekelezwa katika mpango na bajeti

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ya Wizara kwa mwaka 2022/2023 yamefafanuliwa kuanzia ukurasa 106 hadi ukurasa 141 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichukue nafasi hii kutoa shukrani kwa mashirika na taasisi za Kimataifa ambazo tumekuwa tukishirikiana nazo. Naomba kutoa shukrani kwa *AfDB, AWF, AWHF, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IMF, ITC, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, WTTTC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF*. Aidha, ninapenda kuwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende sasa kwenye maombi ya fedha; kwa heshima na taadhima ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishhe jumla ya shilingi 624,142,732,000 kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023; kati ya fedha hizo, shilingi 443,706,567,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 180,436,165,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi 175,884,707,000 za mishahara; na shilingi 267,821,860,000 za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi 109,879,563,000 fedha za ndani; na shilingi 70,556,572,000 fedha za nje.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa hebu fedha za ndani soma tena.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za ndani; fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha shilingi 175,884,707,000 za mishahara; na shilingi 267,821,860,000 za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi 109,879,593,000 fedha za ndani; na shilingi 70,556,572,000 fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, www.maliasili.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* za Bunge kwa ajili ya kumbukumbu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHESHIMIWA BALOZI, DKT. PINDI H. CHANA (MB.) WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, ninaomba Bunge lako lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

2. *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kujenga uchumi na maendeleo endelevu ya nchi yetu. Aidha, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa dhati kabisa, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Wizara hii yenye umuhimu

mkubwa kwa Taifa na jamii kwa ujumla. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu kumuomba kwa Mwenyezi Mungu azidi kumpa nguvu na afya njema ili aendelee kuwatumikia Watanzania.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati Mheshimiwa *Dkt. Philip Isdori Mpango*, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa *Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)*, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao thabiti katika kusimamia maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Kupitia miongozo na maelekezo yao mazuri na yenye tija, Wizara imeendelea kutimiza wajibu wake kwa kuimarisha uhifadhi na kuendeleza utalii na hivyo kuchangia katika juhudi za kukuza uchumi na ustawi wa wananchi kwa ujumla. Aidha, nikupongeze wewe binafsi, Mheshimiwa *Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)*, Spika wa Bunge na Mheshimiwa *Mussa Azzan Zungu (Mb.)*, Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge letu Tukufu. Imani hiyo imejengeka kutokana na umahiri na weledi mkubwa mliouonesha katika kuliongoza Bunge hili. Vilevile, niwapongeze Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha shughuli za Bunge letu kwa weledi mkubwa.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa dhati, ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa *Ally Juma Makoja (Mb.)*, Mbunge wa Kondoja Mjini kwa kujadili, kushauri na kupitisha mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa namna ya kipekee, niseme kuwa Kamati hii imekuwa na mchango mkubwa katika kuishauri Wizara kupitia maoni na maelekezo yake. Wizara itaendelea kuzingatia maoni na ushauri wa Kamati na Bunge lako Tukufu ili kufanikisha malengo yake.

5. **Mheshimiwa Spika**, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walionitangulia kumpongeza Mheshimiwa *Emmanuel Lekishon Shangai* kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Mheshimiwa *Shamsi Vuai Nahodha* kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninaomba nitumie fursa hii adhimu kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa juhudi kubwa wanazozifanya katika kusimamia na kuhifadhi maliasili; na kuendeleza utalii. Vilevile, ninawashukuru wananchi wa Mkoa wa Njombe kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu kama Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii. Ninapenda kuwahimiza wote kushiriki katika uhifadhi wa maliasili, malikale na kuendeleza utalii kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika**, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wenzangu wa Wizara akiwemo Mheshimiwa Mary Francis Masanja (Mb.), Naibu Waziri; *Dkt.* Francis Kasabubu Michael, Katibu Mkuu; na Ndugu Juma Selemani Mkomi, Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nimpongeze mtangulizi wangu Mheshimiwa *Dkt.* Damas Daniel Ndumbaro (Mb.), Waziri wa Katiba na Sheria kwa mchango wake aliutoa katika kufanikisha majukumu mbalimbali ya Wizara. Vilevile, ninawashukuru Watendaji Wakuu na Watumishi wa Wizara; na wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika kuiongoza sekta hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

7. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi wote wa Serikali wakiwemo waheshimiwa mawaziri, wabunge na wakuu wa taasisi; pamoja na watumishi, ndugu, jamaa na marafiki kwa jinsi walivyojitua katika kutufaraji na kufanikisha mazishi ya marehemu mama yetu mpendwa Regina Mlowe. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

8. **Mheshimiwa Spika**, nitumie nafasi hii kutoa pole kwako, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania wenzangu kwa kuondokewa na wapendwa wetu: Mheshimiwa Elias Kwandikwa, aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga

Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa William Tate Olenasha aliyekuwa Naibu Waziri wa Uwekezaji (Ofisi ya Waziri Mkuu) na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; Mheshimiwa Khatibu Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar; na Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa. Aidha, natoa pole kwa ndugu, marafiki na watumishi wote wa Wizara kutokana na watumishi 10 waliopoteza maisha wakati wakitekeleza majukumu yao. Kwa hakika, watumishi hawa ni mashujaa ambao wamepoteza maisha wakitetea rasilimali za nchi yetu. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina. Pia, nitumie fursa hii kutoa pole kwa watumishi waliojeruhiwa wakati wanatekeleza majukumu yao. Sambamba na hilo, ninatoa pole za dhiti kwa wananchi ambao wamepata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu na hivyo kujeruhiwa, kupoteza ndugu na kuharibiwa mali zao.

9. Mheshimiwa Spika, hotuba hii inajumuisha sehemu kuu tano (5) ambazo ni: Utangulizi; Mchango wa Maliasili na Utalii katika kukuza Uchumi na Maendeleo Endelevu; Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

2.0 MCHANGO WA MALIASILI NA UTALII KATIKA KUKUZA UCHUMI NA MAENDELEO ENDELEVU

10. Mheshimiwa Spika, Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali za maliasili na malikale zenye mchango mkubwa katika uendelezaji utalii, ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi. Aidha, maeneo ya hifadhi ndiyo vyanzo vikuu vya maji, nishati, makazi ya wanyamapori na viumbe wengine. Pia, maeneo hayo ni muhimu katika uhifadhi wa udongo na ufyonzaji wa hewa ukaa, hali inayopunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, malikale zinatumika kuhifadhi historia na tamaduni zetu.

11. **Mheshimiwa Spika**, maliasili zimeendelea kuchangia katika Pato la Taifa (GDP) na ustawi wa jamii kupitia shughuli za kiuchumi ikiwemo utalii na uuzaji wa mazao ya misitu na nyuki. Mathalan, misitu huchangia asilimia 85 ya nishati yote inayotumika nchini kutokana na matumizi ya miti (mkaa na kuni); na asilimia 90 ya vifaa vya ujenzi na samani zinazotumika majumbani. Kwa upande mwingine, rasilimali za misitu na nyuki huchangia asilimia 3.3 ya Pato la Taifa; asilimia 5.9 ya mapato yatoakanayo na biashara ya nje; na ajira takriban milioni 4 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Katika hatua nyingine, asilimia 90 ya umeme unaozalishwa kwa nguvu ya maji unatokana na vyanzo vya maji ambavyo vingi viko katika maeneo yaliyohifadhiwa. Hata hivyo, mchango huo katika GDP haujumuishi thamani ya kifedha na faida nyingine kama vile huduma za kiikolojia na faida nyingine za misitu. Aidha, utalii huchangia asilimia 25 ya fedha za kigeni na huzalisha ajira takriban milioni 1.6 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Kwa upande mwingine, ustawi wa utalii unategemea pamoja na masuala mengine, miundombinu iliyo bora pamoja na uhifadhi wa maliasili, malikale, historia na utamaduni.

12. **Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa hali ya uhifadhi unaonesha kuongezeka kwa uharibifu wa maliasili na mazingira katika maeneo mengi nchini. Kiwango cha kutoweka kwa misitu kwa mwaka kimeongezeka kutoka hekta 372,800 kwa makadirio ya mwaka 2015 hadi hekta 469,420 kwa makadirio ya mwaka 2018. Uharibifu huo unasababishwa na ongezeko la idadi ya watu, usafishaji wa mashamba kwa ajili ya kilimo, uchomaji moto holela na matumizi mengine yasiyo endelevu ya rasilimali za misitu. Hali hiyo inachangia kuleta mabadiliko ya tabianchi na athari zake kama vile ukame, kuongezeka kwa joto, mafuriko na mabadiliko ya misimu ya mvua.

13. **Mheshimiwa Spika**, uhusiano bora kati ya uhifadhi na maendeleo una mchango mkubwa katika ustawi na matumizi endelevu ya maliasili, ukuaji wa uchumi, ustawi wa wananchi na usalama wa Taifa. Ninaomba nitumie fursa hii kutoa rai kwa Watanzania wote na wadau wa sekta ya

maliasili na utalii nchini, kuendelea kushirikiana na Wizara kuhifadhi maliasili, malikale na kuendeleza utalii, kwa maendeleo ya Taifa letu na dunia kwa ujumla.

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII

14. **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 04 hadi 05 Mei 2021, Wizara iliwasilisha katika Bunge lako Tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na kupokea maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge, kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, Wizara imepokea maoni ya Kamati wakati ikiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

15. **Mheshimiwa Spika**, ushauri na maoni ya Kamati yalikuwa ni pamoja na: kutambua, kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii; usimamizi wa maliasili; kujenga na kuimarisha miundombinu iliyomo ndani ya hifadhi; kudhibiti uvamizi katika maeneo ya hifadhi; na kutatua migogoro. Ushauri mwingine ulikuwa kushirikisha Sekta Binafsi; elimu na uhamasishaji; usimamizi na ukusanyaji wa mapato; kuongeza bajeti ya miradi ya maendeleo ya Wizara; kuandaa Mpango kazi mahsusni wa kunufaika na Mjusi dinosaria aliyepo Ujerumani; na kuvuna mamba kwenye mikoa ambayo imekumbwa na matukio mengi ya wananchi kushambuliwa na wanyama hao.

16. **Mheshimiwa Spika**, pia, Kamati ilishauri kuimarishwa kwa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) nchini kwa kuanzisha kampasi kikanda, kupandisha hadhi Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) kuwa mamlaka, kufanya utafiti na tathmini ya aina ya miti inayofaa na idadi inayotakiwa kupandwa katika mikoa yote nchini, kuongeza kasi ya kupanda miti kibiashara katika maeneo mengine nchini, na kuanzisha Kampasi ya Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) katika mikoa ya kanda ya kusini mwa nchi.

17. **Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imezingatia maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

4.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022

18. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maliasili na Utalii ina jukumu la kusimamia uhifadhi wa maliasili, malikale na maendeleo ya utalii. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara inasimamia maeneo yaliyohifadhiwa kisheria yenye ukubwa wa kilomita za mraba 307,800 sawa na asilimia 32.5 ya eneo lote la nchi. Maeneo hayo yanajumuisha hifadhi za Taifa 22, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, mapori ya akiba 27, mapori tengefu 26, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi za Wanyamapori (WMAs) 21, maeneo matatu (3) ya ardhioevu chini ya mkataba wa *Ramsar*, hifadhi za misitu ya asili 419, hifadhi za misitu ya mazingira asilia 20, mashamba ya miti ya Serikali 24, hifadhi za nyuki 12, maeneo ya malikale 132 na vituo saba (7) vya Makumbusho ya Taifa.

19. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/2022 - 2023/2024, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025, Sera na Sheria mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), maagizo mbalimbali ya viongozi wa Serikali na mikataba ya kikanda na kimataifa.

20. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

4.1 Ukusanyaji Maduhuli

21. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi 689,345,854,249.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 478,014,580,522.00** zinakusanywa na Wizara kupitia mfumo wa TRA kutoka vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA na **Shilingi 211,331,273,727.00** zinakusanywa moja kwa moja na Wizara kupitia mfumo wa *MNRT Portal*/kutoka Idara, Mifuko na Taasisi nyingine za Wizara. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 397,428,671,967.86** sawa na **asilimia 58** ya lengo la makusanyo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 250,985,216,073.86** zimekusanywa kupitia TRA na **Shilingi 146,443,455,894.00** zimekusanywa na Wizara kupitia mfumo wa *MNRT Portal*.

4.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

22. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 571,632,424,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 418,859,544,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 152,772,880,000.00** ni miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara na Taasisi zake ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 416,601,358,591.55** sawa na **asilimia 73** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 357,120,042,324.35** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 59,481,316,267.20** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

4.3 Mafanikio

23. *Mheshimiwa Spika*, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo:

4.3.1 Utangazaji Utalii na Kuvutia Uwekezaji kupitia Programu Maalum ya *Tanzania - The Royal Tour*

24. *Mheshimiwa Spika*, kipekee kabisa, napenda kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Samia

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa juhudi zake kubwa za kuitangaza nchi yetu kimataifa kupitia programu ya *Tanzania – The Royal Tour*. Programu hiyo imewezesha kuitambulisha Tanzania kimataifa kwa kutangaza vivutio vya utalii vya kipekee vya nchi yetu; kuonesha fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye sekta ya maliasili na utalii pamoja na kuimarisha nafasi ya nchi katika Jumuiya za kimataifa. Kimsingi, programu hii imehusisha uandaaji wa filamu inayoonesha vivutio na fursa za uwekezaji zilizopo nchini. Pamoja na maeneo mengine, filamu hiyo inaonesha pia vivutio mbalimbali vya utalii katika hifadhi za Taifa, Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, maeneo ya malikale, tamaduni zetu na visiwa vya Zanzibar.

25. **Mheshimiwa Spika**, programu hii ilizinduliwa mwezi Aprili, 2022 katika Jiji la New York na Jiji la Los Angeles nchini Marekani; na kuendelea katika Jiji la Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar. Katika uzinduzi uliofanyika nchini Marekani, zaidi ya watu 6,000 walishiriki wakiwemo: viongozi wa kitaifa, viongozi wa majiji husika, watu maarufu, wadau wa utalii na uhifadhi, wawekezaji na wafanyabiashara mbalimbali. Uzinduzi huo pia ulishirikisha vyombo mbalimbali vya habari vya kimataifa vikiwemo: vituo vya televisheni na redio vya *CBS, Fox News, NBC, YouTube* na *PBS - Amazon Prime video*.

26. **Mheshimiwa Spika**, programu ya *Tanzania – The Royal Tour* imeanza kuleta matunda kwa kuvutia watalii na wawekezaji mbalimbali kutembelea nchini. Mathalan, wakala wa utalii zaidi ya 30 kutoka katika masoko ya utalii yakiwemo Marekani, Ufaransa na Lithuania wamehamasika kutembelea nchini ili kujifunza na kujionea vivutio mbalimbali vya utalii kwa lengo la kuvitangaza katika nchi zao. Aidha, wawekezaji kutoka Taifa la Bulgaria wameonesha nia ya kuwekeza nchini kwa kujenga hoteli nne (4) zenye hadhi ya nyota tano (5) katika hifadhi za Taifa Serengeti, Ziwa Manyara na Tarangire; na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

27. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Serikali imesaini mkataba wa ushirikiano katika masuala ya utalii, biashara na uwekezaji baina ya Tanzania na Jiji la Dallas Marekani, mwezi Aprili, 2022. Hatua hiyo itafungua fursa za usafiri wa anga kwa kuwezesha safari za moja kwa moja za ndege kutoka Tanzania hadi Dallas, Marekani na hivyo kuongeza idadi ya wageni nchini. Sambamba na hilo, mtandao maarufu wa habari nchini Marekani ujulikanao kama *theGrio* umetambua juhudi za Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuiongoza vyema sekta ya utalii na uhifadhi nchini, hivyo kuifanya Tanzania kuwa kivutio cha kwanza cha utalii katika Bara la Afrika kwa mwaka 2022. Kwa ujumla, jitihada hizi zitaleta matokeo chanya katika kuongeza idadi ya watalii na hivyo kufikia lengo la watalii milioni 5 na mapato Dola za Marekani bilioni 6 ifikapo mwaka 2025, kama ilivyoelekezwa katika Ibara 67(a) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025.

28. **Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza programu hiyo, Wizara itaendelea kuimarisha miundombinu mbalimbali ya utalii ikiwemo barabara, viwanja vya ndege na mawasiliano katika maeneo ya hifadhi ili kuhakikisha vivutio vilivyomo vinafikika kwa urahisi. Aidha, Wizara itaboresha huduma za malazi kwa kuongeza idadi ya vitanda na kuvutia uwekezaji; kutangaza vivutio vya utalii; kuibua mazao mapya ya utalii; kuimarisha utoaji mafunzo ya huduma katika sekta ya utalii na ukarimu; kuimarisha ulinzi na usalama wa wageni wanaotembelea maeneo ya hifadhi; na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi.

29. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kuendelea kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kutangaza utalii na kuvutia uwekezaji kwa maslahi mapana ya Taifa na ustawi wa jamii kwa ujumla.

4.3.2 Tanzania kuendelea Kutambulika Kimataifa katika Masuala ya Utalii na Uhifadhi

30. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia jitihada za Wizara za kutangaza vivutio kwenye masoko mbalimbali na kuboresha huduma za utalii na uhifadhi, Tanzania imeendelea kutambulika kimataifa na kupata tuzo mbalimbali zikiwemo: Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa hifadhi inayoongoza kwa ubora Barani Afrika (Africa's Leading National Park Attraction) kwa miaka mitatu (3) mfululizo kuanzia mwaka 2019 hadi 2021; na Tanzania kuwa nchi inayoongoza kwa shughuli za utalii Barani Afrika (Africa's Leading Destination for the Year 2021), tuzo hizi zilitolewa na *World Travel Award*. Tuzo nyingine ni pamoja na *Travellers' Choice Destination – National Parks of the World*, iliyotolewa na *Tripadvisor* ambapo Tanzania imeingiza hifadhi nne (4) katika orodha ya hifadhi 25 bora duniani zikiongozwa na Hifadhi ya Taifa Serengeti. Hifadhi nyingine ni Hifadhi za Taifa Kilimanjaro na Tarangire; na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Vilevile, Shirika la Hifadhi za Taifa limetunukiwa Cheti cha Ubora wa Huduma za Kiwango cha Kimataifa cha *ISO 9001:2015* kutokana na kuimarishwa kwa utoaji wa huduma bora za utalii.

31. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo, TANAPA imepata tuzo ya utoaji wa huduma zenye viwango (*European Awards for Quality Achievement - Platinum*) iliyotolewa na *European Society for Quality Research - ESQR*. Aidha, Zanzibar na Jiji la Arusha zimeorodheshwa na *Tripadvisor* kupitia *Travellers' Choice Destination – Afrika* kuwa miongoni mwa maeneo 10 bora ya shughuli za utalii Barani Afrika. Katika hatua nyingine, Hifadhi ya Taifa Serengeti imebuka kinara kati ya vivutio 10 bora vilivyoorodheshwa na mtandao wa *safaribookings.com* ulio maarufu duniani kama kivutio kinachofaa kutembelewa katika Bara la Afrika. Aidha, Tanzania imepewa tuzo ya kutambulika kwa ufanisi katika uhifadhi na utalii. Tuzo hii imetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Sudan Kusini wakati wa Onesho la Kwanza la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki (East Africa Regional Tourism Expo - *EARTE*) lililofanyika Jijini Arusha mwezi Oktoba, 2021. Kwa ujumla, tuzo hizi zimekua chachu ya kuvutia na kuwajengea imani watalii

kutoka masoko mbalimbali ya utalii duniani hasa katika kipindi hiki cha janga la UVIKO-19.

4.3.3 Kuongezeka kwa Malighafi ya Mazao ya Misitu kwa ajili ya Viwanda

32. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikiwa kuongeza upatikanaji wa malighafi ya mazao ya misitu katika mashamba ya miti ya Serikali mita za ujazo 729,000 kwa mwaka 2020/2021 hadi wastani wa mita za ujazo 1,000,000 kwa mwaka 2021/2022. Ongezeko hili la malighafi limeiwezesha Wizara kuingia mikataba 561 ya uvunaji wa mazao ya misitu katika mashamba ya miti ya Serikali na wafanyabiashara wa mazao hayo. Mafanikio haya yametokana na juhudi mbalimbali zikiwemo: kuendeleza mashamba ya miti kwa kupanda miche 29,670,223; na kuanzisha Shamba jipya la Miti la Makere, Mkoa wa Kigoma lenye ukubwa wa hekta 29,827. Juhudi nyingine ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu uhifadhi na uanzishwaji wa mashamba ya miti ya taasisi na watu binafsi.

4.3.4 Kuongezeka kwa Matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika Uendeshaji wa Minada ya Mazao ya Misitu na Wanyamapori

33. Mheshimiwa Spika, Wizara imeongeza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kuendesha minada ya mazao ya misitu na wanyamapori. Katika kufanikisha hili, Wizara imeendesha kwa mara ya kwanza minada miwili ya kielektroniki ya kuuza mazao ya misitu. Hatua hii imeongeza uwazi na ushindani ambao umesababisha kuongezeka kwa mapato ya mauzo yatokanayo na minada ya kielektroniki ya misaji na mkurungu kwa asilimia 15 ikilinganishwa na ambavyo ingeuzwa kwa njia ya kiutawala. Aidha, Wizara imefanikiwa kuuza kwa njia ya mnada jumla ya mita za ujazo 989.99 za magogo ya miti aina ya mkurungu ambapo kiasi cha Shilingi 1,686,300,000.00 kimepatikana.

34. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara imefanikiwa kuendesha jumla ya minada saba (7) ya

kielektroniki iliyojumuisha vitalu 100 vya uwindaji wa kitalii. Kati ya vitalu hivyo, 64 vimeuzwa na kufanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi 18,078,000,000.00 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 5,023,200,000 ambacho kingekusanywa kwa njia ya kiutawala (administrative allocation). Kwa muhtadha huo, mauzo kwa njia ya mnada wa kielektroniki yamewezesha soko kuamua thamani halisi ya vitalu vya uwindaji wa kitalii. Mathalan, kitalu cha daraja la tatu (3) kilichokuwa kinauzwa kwa Dola za Marekani 18,000 kupitia njia ya kiutawala, kimenunuliwa kwa Dola za Marekani 255,000 ikiwa ni ongezeko la asilimia 1,317. Pamoja na ongezeko la mapato, matumizi ya mifumo hii imeendelea kuongeza uwazi na kurahisisha ufanyaji biashara katika mazao ya misitu na wanyamapori.

4.3.5 Kushiriki kikamilifu katika Miradi ya Kimkakati

35. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imefanikiwa kukamilisha kazi ya kusafisha eneo la ekari 274,608 kwa ajili ya Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo la mradi. Sambamba na hatua hiyo, Wizara imeshiriki katika zoezi la kufanya tathmini ya athari za kimazingira katika eneo la Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani Tanga, Tanzania lenye urefu wa kilomita 1,443. Lengo la tathmini hiyo ni kuhakikisha kuwa maliasili na malikale zilizopo katika eneo la mradi zinaendelea kuhifadhiwa. Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza tija katika kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Maliasili na Utalii na sekta nyingine za kiuchumi.

4.3.6 Kuendeleza Utalii Ikolojia katika Hifadhi za Misitu za Mazingira Asilia

36. *Mheshimiwa Spika*, katika kupanua wigo wa mazao ya utalii nchini, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya utalii ikolojia katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia zikiwemo hifadhi za Amani, Pugu Kazimzumbwi, Kalambo, Rungwe, Magamba na Ziwa Duluti. Baadhi ya juhudi zilizofanyika ni ukarabati wa barabara zenye urefu wa kilomita

66.7, njia za watembea kwa miguu kilomita 163.2 na ujenzi wa kambi tano (5) za kitalii. Sambamba na hilo, Wizara imeandaa na kurusha vipindi 105 vya redio, 48 vya televisheni, makala 72, *video clips* 87 na vipeperushi 21,200 vya kutangaza vivutio vilivyopo katika maeneo hayo; na kuendesha programu mbalimbali za uhifadhi na utalii wa ndani.

4.3.7 Sekta ya Utalii Kuendelea kuwa Stahimilivu (Resilient) katika kipindi cha UVIKO-19

37. Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto ya uwepo wa janga la UVIKO-19, sekta ya utalii nchini imeendelea kuwa stahimilivu ambapo idadi ya watalii na mapato yameendelea kuongezeka. Mathalan, katika mwaka 2021, Tanzania imefanikiwa kupokea jumla ya watalii wa kimataifa 922,692 ikiwa ni ongezeko la asilimia 48.6 kutoka watalii 620,867 kwa mwaka 2020. Aidha, mapato yatokanayo na watalii wa kimataifa yameongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 714.59 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani milioni 1,310.34 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 82. Mafanikio hayo yamechochewa na juhudi mbalimbali zilizofanywa na Wizara zikiwemo: kufanikisha Onesho la Kwanza la Kimataifa la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki; na uzinduzi wa programu maalum ya *Tanzania - The Royal Tour*. Juhudi nyingine ni pamoja na kutumia mabalozi wa hiari wa utalii, ziara za mafunzo (FAM - trips) na utekelezaji wa Mwongozo wa Kuendesha Shughuli za utalii katika kipindi cha kukabiliana na janga la UVIKO - 19.

4.3.8 Kukua kwa Utalii wa Ndani

38. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani kupitia kampeni na programu mbalimbali. Hatua hizi zimeongeza idadi ya watalii wa ndani waliotembelea maeneo ya hifadhi, vituo vya malikale na makumbusho kutoka watalii 562,549 mwaka 2020 hadi 788,933 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 40.2. Ongezeko la idadi ya watalii limechangiwa na juhudi mbalimbali zikiwemo: Kampeni ya kutangaza utalii wa faru katika Hifadhi ya Taifa Mkomazi; programu maalum ya Onesho la Mchango wa

Mwanamke katika Kuhifadhi Mila na Utamaduni wa Mtanzania; Kampeni Maalum ya Uhamasishaji wa Kupanda Mlima Kilimanjaro kupitia maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru; matukio mbalimbali ya utalii wa michezo; maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani; na maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani 2022 ambapo takriban wanawake 680 walitembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kushirikiana na vyombo vya habari kutangaza na kuhamasisha utalii wa ndani.

4.3.9 Kupungua kwa Ujangili na Uvunaji Haramu wa Maliasili

39. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuongeza jitihada za kuimairisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na nyuki na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Jitihada hizo zinadhihirishwa na matokeo ya sensa ya wanyamapori iliyofanyika mwaka 2021 ambapo idadi ya tembo imeongezeka kwa asilimia 30 katika Mfumo lkolojia Ziwa Natron - West Kilimanjaro. Aidha, katika Mfumo lkolojia Ruaha - Rungwa, idadi ya nyati imeongezeka kwa asilimia 80; pundamilia asilimia 36; na palahala asilimia 65 ikilinganishwa na sensa iliyofanyika mwaka 2018. Pia, idadi ya faru weusi ambao wako hatarini kutoweka imeongezeka kwa asilimia 27.5 ikilinganishwa na idadi yao kwa mwaka 2018. Ongezeko la wanyamapori hao ni kiashiria cha kuimarika kwa ulinzi na usimamizi wa maeneo ya hifadhi.

40. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio hayo yamechangiwa na juhudi za Serikali ikiwa ni pamoja na kufanya doria ambapo jumla ya siku doria 434,371 zimefanyika na kuwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 7,719 pamoja na nyara za Serikali na magogo yenye ujazo wa mita 1,218. Juhudi nyingine ni kufanya operesheni maalum za kiintelijensia zilizowezesha kuzuiwa kwa matukio 66 ya ujangili; kukamatwa kwa silaha mbalimbali zikiwemo bunduki 135 na kuvunjwa kwa mitandao ya ujangili; na kuimarisha Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu kwa kutoa mafunzo ya kijeshi, upelelezi, uchunguzi na usimamizi wa kesi kwa watumishi mbalimbali. Pamoja na juhudi hizi natoa wito kwa wananchi

kuendelea kushirikiana na Wizara kulinda na kutunza rasilimali zilizopo kwa maslahi ya kizazi cha sasa na vijavyo.

4.3.10 Kupandishwa Hadhi Maeneo ya Hifadhi

41. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikiwa kupandisha hadhi mapori tengefu matatu (3) na WMA moja (1) kuwa mapori ya akiba Luganzo - Tongwe, Msima, Igombe na Wami - Mbiki. Hatua hii imeongeza idadi ya Mapori ya Akiba kutoka 22 hadi 27. Lengo la jitihada hizi ni kuimarisha ulinzi na matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo katika maeneo hayo. Aidha, upandishwaji hadhi wa maeneo hayo unalenga kuchochea uhifadhi na uwekezaji katika shughuli za utalii wa picha na uwindaji.

4.3.11 Kuimarika kwa Utalii wa Urithi wa Utamaduni na Malikale

42. Mheshimiwa Spika, Wizara imefanikiwa kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea vituo vya malikale na makumbusho kutoka 349,264 mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia 582,080 mwezi Machi 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 167. Ongezeko hilo limechochewa na juhudi mbalimbali zikiwemo: kuanzisha programu maalum za kuhamasisha makundi mbalimbali katika jamii kutembelea vivutio vya malikale na makumbusho; kufanya matamasha ya utamaduni katika maeneo mbalimbali nchini; kuanzisha jarida maalum la makumbusho; na kufanya mikutano maalum na wahariri wa vyombo vya habari. Katika hatua nyingine, Wizara imeimarisha miundombinu katika maeneo ya malikale na makumbusho kwa kujenga nyumba 12 zinazoonesha tamaduni za jamii ya Wangoni, Wakinga, Wasafwa na Wasukuma kwa kufuata ramani ya Tanzania katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam; kukarabati jengo la kihistoria la Soko la Watumwa; na jengo alilokuwa anafikia Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere - Mikindani, Mtwara katika kipindi cha harakati za uhuru.

4.4 Utekelezaji wa Masuala Mtambuka

4.4.1 Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Katika Maeneo Yaliyohifadhiwa

43. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kutatua migogoro ya ardhi baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa. Baadhi ya kazi zilizofanyika ni pamoja na kuhakiki mipaka ya hifadhi yenye urefu wa kilomita 33,107; kusafisha kilomita 5,743; na kuweka vigingi 1,219 na mabango 1,096 katika maeneo ya hifadhi za misitu na wanyamapori. Katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kushiriki na kutoa ushirikiano kwa Kamati ya Kitaifa ya Mawaziri nane (8) yenye lengo la kutatua migogoro ya ardhi nchini. Pia, Wizara imeendelea na zoezi la uhakiki wa mipaka ya maeneo ya malikale na urithi wa utamaduni kwa kupima maeneo ya vituo vya Kalenga, Tembe la Kwihara, Ujiji Kigoma, Tongoni, Amboni na Kunduchi; na kuendelea na taratibu za kupata hati za umiliki za maeneo hayo. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wananchi pamoja na kamati mbalimbali katika ngazi za mkoa na wilaya kuhusu umuhimu wa kulinda maeneo yaliyohifadhiwa.

4.4.2 Ushirikishaji wa Wadau katika Uhifadhi na Uendelezaji Utalii

44. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kushirikiana na wananchi, sekta binafsi, washirika wa maendeleo na wadau wengine katika kutekeleza majukumu yake. Katika kufanikisha hilo, Wizara imepanda miti 13,000,000 katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo mashambani, maeneo yaliyoathiriwa na uharibifu wa mazingira pamoja na kandokando ya vyanzo vya maji. Kati ya miche hiyo, miche 690,000 ilipandwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma kama jitihada za kuendeleza kampeni ya Dodoma ya Kijani. Aidha, katika kuendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika uhifadhi na kunufaika na rasilimali za maliasili, Wizara imegawa mizinga ya nyuki 2,133; madawati 111; na kugawa vifaa vya ujenzi kama vile saruji mifuko 305, mbao 2,423 na vifaa mbalimbali vya michezo. Kwa upande mwingine,

Wizara imejenga soko la samaki, Kilombero; jengo la utawala na maktaba katika Shule ya Sekondari ya Mwambesi, Pwani; ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi ya Ihefu, Mufindi; na ukarabati wa soko katika Kijiji cha Sange, Ileje.

45. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa jamii na wadau wengine wanapata elimu kuhusu uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za maliasili na shughuli za Utalii, Wizara imeendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa rasilimali za wanyamapori, misitu na nyuki kwa viongozi wa Wilaya, Kata, vijiji, kamati za maliasili za vijiji, madiwani, wanafunzi na vikundi vya ufugaji nyuki kwa kufanya mikutano 16,046 katika vijiji 2,107. Aidha, elimu ya uhifadhi wa malikale imetolewa katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Mwanza na Tabora. Vilevile, Wizara imewezesha jamii kuanzisha na kutangaza hifadhi za misitu na nyuki za vijiji zenye ukubwa wa hekta 541,562.97 katika wilaya za Liwale, Handeni, Tunduru, Kilwa, Mpwapwa na Kilosa. Pia, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau katika kuwaelimisha kuhusu miongozo ya uendeshaji wa biashara za utalii nchini, uendelezaji wa mazao ya utalii ikiwemo utalii wa utamaduni na fukwe. Kwa upande mwingine, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

46. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuhamasisha jamii katika masuala ya uhifadhi wa mila na utamaduni wa mtanzania, jamii ya wenyeji wa mikoa ya Njombe (Wakinga) na Mbeya (Wasafwa) zimefanikiwa kujenga kaya zenye jumla ya nyumba saba (7) katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam. Aidha, Wizara imewezesha uanzishaji wa Makumbusho ya Wairaq katika Wilaya ya Karatu; Makumbusho ya Benki ya CRDB, Dar es Salaam; na uboreshaji wa Makumbusho ya Bujora na kituo cha Utamaduni Dofa, Karatu. Vilevile, Katika jitihada za kukabiliana na moto kichaa, Wizara kwa kushirikiana na wadau imetoa elimu kwa wananchi 1,731 kutoka katika vijiji 333 vinavyopakana na hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Burigi - Chato, Udzungwa na Mto Ugalla; na maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki.

4.4.3 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

47. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania ilipewa heshima ya kuwa nchi pekee ya Kanda ya Afrika kushiriki mdahalo maalum wa mawaziri kuhusu masuala ya kisera ya uendelezaji utalii katika maeneo ya vijijini yaani *Ministerial Debate on Policies to Foster Tourism for Rural Development*. Mdahalo huo ulifanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa 24 wa Shirika la Utalii Duniani Jijini Madrid, Uhispania mwezi Desemba, 2021 ambapo Tanzania ilishiriki na ilisisitiza uimarishaji wa uhifadhi na utalii endelevu. Aidha, Tanzania ilipongezwa kwa mkakati wake wa kuendeleza utalii wa utamaduni na vyakula kupitia zao jipya la *Swahili Tourism*. Katika hatua nyingine, Wizara ilishiriki Mkutano wa 64 wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Utalii Kamisheni ya Afrika uliofanyika nchini Cabo Verde mwezi Septemba, 2021; na maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani yaliyofanyika Jijini Abidjan, Ivory Coast mwezi Septemba, 2021.

48. **Mheshimiwa Spika**, katika hatua nyingine, Wizara imeshiriki mikutano mbalimbali katika Sekta ya Maliasili na Utalii ikiwemo: Mkutano wa 13 wa Kamati ya Uongozi wa Mkataba wa Lusaka katika kukabiliana na ujangili na usafirishaji haramu wa mazao ya wanyamapori na mimea uliofanyika Jijini Livingstone, Zambia mwezi Machi 2022; Mkutano wa 23 wa nchi wanachama wa Mkataba wa UNESCO wa mwaka 1972 unaohusu ulinzi na uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Dunia uliofanyika Paris, Ufaransa mwezi Novemba, 2021; na Mkutano wa Umoja wa Afrika kuhusu urejeshwaji wa urithi wa utamaduni ulio nje ya Bara la Afrika uliofanyika Dakar Senegal mwezi Novemba, 2021. Vilevile, Wizara ilishiriki Jukwaa la Uhifadhi wa Wanyamapori Afrika uliofanyika Gaborone, Botswana mwezi Novemba, 2022; Mkutano wa masuala ya uwindaji wa kitalii uliofanyika Las Vegas, Marekani mwezi Januari, 2022; na Mikutano ya Mkataba wa Kimataifa Unaosimamia Biashara ya Wanyamapori na Mimea iliyo hatarini kutoweka (CITES) iliyofanyika Mwezi Machi, 2022 nchini Ufaransa.

49. **Mheshimiwa Spika**, Sambamba na hilo, Wizara imeshiriki Mkutano wa Nne (4) wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Kenya uliofanyika Jijini Nairobi nchini Kenya mwezi Agosti, 2021. Aidha, Wizara imeshiriki mkutano wa ushirikiano baina ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika sekta za maliasili, malikale na utalii uliofanyika Zanzibar mwezi Septemba, 2021 ili kuboresha ushirikiano katika uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji wa utalii. Vilevile, Wizara imeendesha mafunzo ya kujengea uwezo wataalam wa Afrika ili kuwawezesha kuandaa maeneo ya kuingizwa katika Orodha ya Urithi wa Dunia. Mafunzo hayo yalifanyika Jijini Dar es Salaam mwezi Desemba, 2021 na yalishirikisha nchi 10 ambazo ni Msumbiji, Zimbabwe, Ethiopia, Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Zambia, Rwanda, Algeria na Mwenyeji Tanzania. Katika hatua nyingine, Wizara imeratibu na kushiriki mikutano mingine ya kikanda na kimataifa ikiwemo SADC, EAC, IORA, UAE, Tripartite ya AU - SADC - EAC pamoja na mikutano ya Tume za Ushirikiano kati ya Tanzania na nchi mbalimbali.

4.4.4 Utawala na Uendelezaji Rasilimaliwatu

50. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utendaji kazi, Wizara imehuisha muundo wake ambapo majukumu ya kiutendaji ya Idara ya Utalii yamehamishiwa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na majukumu ya kiutendaji ya Idara ya Mambo ya Kale kwenda Shirika la Makumbusho ya Taifa (NMT). Aidha, muundo mpya wa Wizara umejumuisha Kitengo cha Uratibu wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misisitu. Katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kazi ambapo nyumba na ofisi 25 zimejengwa pamoja na ununuzi wa mitambo 43, magari 74, pikipiki 33, samani na vitendea kazi vya ofisi. Sambamba na hilo, watumishi 144 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na 630 ya muda mfupi ili kuwajengea uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Vilevile, Wizara imeajiri watumishi 389 wa kada mbalimbali na kupandisha vyeo watumishi 1,343. Pia, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuanza ujenzi wa jengo la makao makuu ya Wizara katika eneo la Mji wa Serikali - Mtumba, Jijini Dodoma.

51. **Mheshimiwa Spika**, ili kuimairisha afya za watumishi na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, Wizara imeendelea kuhamasisha na kuwezesha watumishi kushiriki mazoezi mbalimbali baada ya saa za kazi na siku za mapumziko ya wiki. Aidha, Wizara kupitia taasisi zake imeshiriki mashindano ya SHIMUTA na SHIMIWI yaliyofanyika Mjini Morogoro mwezi Oktoba na Novemba, 2021 mtawalia, na maadhimisho ya Mei Mosi yaliyofanyika Jijini Dodoma mwezi Mei, 2022 na kufanikiwa kupata tuzo mbalimbali. Kwa upande mwingine, Wizara imeendelea kusimamia maslahi, maadili, ustawi na afya za watumishi ikiwa ni pamoja na kuwawezesha watumishi waliojitokeza wanaoishi na VVU na Ukimwi kupata lishe bora. Vilevile, katika kuendelea na juhudi za kupambana na janga la UVIKO-19, Wizara imetoa vifaa kinga kwa watumishi.

4.5 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara

4.5.1 Sekta ya Wanyamapori

52. **Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Wanyamapori ina jukumu la kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo na kufanya tafiti za wanyamapori ndani na nje ya maeneo ya hifadhi. Utekelezaji wa majukumu hayo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Wanyamapori ya mwaka 2007 na kusimamiwa na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Sura 283, Sheria ya Hifadhi za Taifa Sura 282, Sheria ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro Sura 284 na Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania Sura 260. Aidha, majukumu haya yanatekelezwa kupitia Idara ya Wanyamapori, TANAPA, NCAA, TAWA, TAWIRI, TWPF, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori – Mweka (CAWM), Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori - Pasiansi (PWTI) na Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii - Likuyu Sekamaganga (CBCTC).

4.5.1.1 Masuala Mahsusi ya Sekta ya Wanyamapori

(i) Utatuzi wa Migogoro baina ya Binadamu na Wanyamapori Wakali na Waharibifu

53. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu,

Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Utatuzi wa Migogoro baina ya Wanyamapori na Binadamu (2020 - 2024). Mkakati huu unalenga kuweka njia bora na endelevu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu, kupunguza madhara ya wanyamapori kwa jamii na kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo ya hifadhi wanapata elimu ya namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

54. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imeendelea kutoa elimu ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya hifadhi na kutumia teknolojia ya kufuatilia nyendo za wanyamapori hao kwa kuwafunga vifaa maalum vya kusukuma mawimbi ili kurahisisha ufuatiliaji. Katika kufanikisha zoezi hilo, jumla ya tembo 107 (Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, mfumo ikolojia Tarangire – Manyara na Selous - Mikumi; mapori ya akiba Maswa na Ikorongo - Grumeti; na Pori Tengefu Longido); mbwa mwitu saba (7) na faru 64 (Mfumo ikolojia Serengeti); nyumbu 10 (mifumo ikolojia ya Tarangire na Serengeti) na simba 21 (Mifumo ikolojia ya Serengeti na Ruaha - Rungwa) waliofungwa mikanda ya mawasiliano (GPS collar) wameendelea kufuatiliwa mienendo yao.

55. *Mheshimiwa Spika*, hata hivyo Wizara imetoa mafunzo ya mbinu za kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu hususan tembo katika wilaya 21 na kujenga vizimba viwili (2) vya mamba Ziwa Rukwa katika Wilaya ya Songwe kwa ajili ya kuwakinga wananchi na madhara ya mamba. Katika hatua nyingine, Wizara imeanzisha utaratibu wa mawasiliano wa namba za simu za kiganjani za bure kwenye kanda ili kuwezesha wananchi kutoa taarifa za wanyamapori wakali na waharibifu kwa ajili ya kupata msaada wa haraka inapotokea matukio. Vilevile, Wizara imeanzisha vikosi maalum vya mwitikio wa haraka vinavyojumuisha askari wahifadhi na askari wa vijiji hususan katika maeneo yenye matukio mengi ya wanyamapori wakali na waharibifu katika wilaya za Lindi Mjini, Tunduru, Bunda, Manyoni, Meatu, Itilima, Bariadi na Ngorongoro. Aidha,

mamba waliokuwa wanatishia uhai wa watu katika Mto Ruvu na Ziwa Victoria wamevunwa.

56. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha jitihada za kupunguza madhara yatokanayo na wanyamapori wakali na waharibu kwa wananchi. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara imetenga fedha kiasi cha Shilingi 1,230,000,000 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa vituo 11 vya askari wa kuzuia wanyamapori wakali na waharibifu katika wilaya 11 nchini. Vituo hivyo vinaendelea kujengwa katika Kijiji cha Malwilo Wilaya ya Meatu; Kijiji cha Kijereshi Wilaya ya Busega; Kijiji cha Milola Wilaya ya Mchinga; Kijiji cha Milonde Wilaya ya Tunduru; Kijiji cha Kwakoa Wilaya ya Mwangi; Kijiji cha Itunundu Wilaya ya Iringa; Kijiji cha Udinde Wilaya ya Songwe; Kijiji cha Ndala Wilaya ya Nzega; Kijiji cha Lubungo Wilaya ya Mvomelo; Kijiji cha Ilangali Wilaya ya Chamwino; na Kijiji cha Mtera Wilaya ya Mwapwa.

57. Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na Wizara ni pamoja na kuendelea kulipa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, jumla ya Shilingi 790,721,500.00 zimetolewa kwa wahanga 3,598 walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu katika wilaya 36. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali katika jitihada za kukabiliana na wanyamapori hao.

(ii) Udhhibiti wa Mimea Vamizi katika Maeneo ya Hifadhi

58. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya tafiti na kutumia mbinu mbalimbali za kukabiliana na mimea vamizi katika maeneo ya hifadhi. Katika kutekeleza hili, Wizara imefanya tathmini katika hifadhi za Taifa nane (8) ambazo ni Serengeti, Arusha, Saadani, Mkomazi, Mikumi, Katavi, Nyerere na Ibanda - Kyerwa; na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Tathmini imebaini uwepo wa spishi 33 za mimea vamizi ikiwemo *Bidens schimperi*, *Gutenbergia cordifolia* na *Tagetes minuta* kwenye eneo la ukubwa wa hekta 35,331. Wizara imeendelea kudhibiti mimea hiyo kwa kutumia mbinu

mbalimbali ikiwemo matumizi ya moto mpango, kung'oa na kufyeka ambapo jumla ya hekta 10,668.88 imedhibitiwa.

4.5.1.2 Idara ya Wanyamapori

59. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, Wizara imekamilisha Kanuni na Amri za Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu. Kukamilika kwa kanuni hizi kumwezesha utekelezaji wa mfumo na majukumu ya jeshi hilo katika kulinda rasilimali za maliasili. Sambamba na hilo, Wizara imefanya mapitio ya Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori (2014 - 2019) na rasimu ya Mkakati mpya wa miaka 10 (2022 - 2032) iko katika hatua ya kupata maoni ya wadau kwa hatua zaidi. Aidha, ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na utoaji huduma kwa wateja, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za Utalii wa Picha za mwaka 2016; Kanuni za Uwekezaji Mahiri ya mwaka 2021; Kanuni ya Mashamba ya Wanyamapori ya mwaka 2020; na Kanuni za Biashara ya Nyara ya mwaka 2010. Vilevile, taratibu za usajili wa magari ya Jeshi la Uhifadhi kutoka namba za kiraia kwenda namba za kijeshi zimekamilika ambapo magari 1,338 kati ya 1,699 yamepata usajili huo.

60. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuimarisha uhifadhi wa wanyamapori nchini, Wizara imefanya tathmini ya mapori tengefu 18 na kuandaa mpango na vipaumbele vya maeneo matano (5) yatakayopandishwa hadhi kuwa mapori ya akiba na kukamilisha Mtaala wa mafunzo ya kijeshi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI pamoja na wadau wengine imeendelea na zoezi la uhakiki wa shoroba za Kwakuchinja, Selous - Niassa na Upper - Kitete kwa lengo la kuweka alama ili kuzihifadhi. Kwa upande mwingine, Wizara inakamilisha taratibu za kuingiza nchini faru weupe 30 kutoka Afrika Kusini kwa lengo la kuboresha uhifadhi na utalii katika Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro; na hifadhi za Taifa Burigi - Chato na Mikumi.

4.5.1.3 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania - TANAPA

61. *Mheshimiwa Spika*, Shirika lina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji utalii kwenye hifadhi za Taifa 22. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika limeendelea kuboresha mahusiano kati ya hifadhi na jamii ambapo elimu ya uhifadhi imetolewa kwa vijiji 477 vinavyopakana na hifadhi za Taifa. Aidha, Shirika limeongeza wigo wa kutoa elimu ya uhifadhi katika shule za msingi na sekondari kwa kuanzisha programu maalum za elimu ya uhifadhi katika shule 147 zinazopakana na Hifadhi za Taifa za Saadani, Mikumi, Udzungwa, Kitulo, Katavi, Gombe, Mahale, Rubondo, Ibanda-Kyerwa na Rumanyika – Karagwe. Vilevile, Shirika limetoa mafunzo ya kuanzisha benki za kijamii za shughuli za uhifadhi (COCOBA) kwa wanachama 649 wa vikundi 43 ili kujikwamua kiuchumi na kupunguza utegemezi wa mazao ya maliasili.

62. *Mheshimiwa Spika*, ili kuimarisha mifumo ya kiikolojia, Shirika limeendelea kudhibiti maambukizi ya magonjwa kati ya wanyamapori na mifugo. Katika kutekeleza hili, Shirika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali limetoa chanjo 63,005 dhidi ya ugonjwa wa mapafu kwa ng'ombe, kondoo na mbuzi. Chanjo hii imetolewa katika vijiji 12 vinavyopakana na hifadhi za Taifa Mkomazi na Tarangire. Aidha, chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa imetolewa kwa mbwa 2,683 na paka 55 katika vijiji 12 vinavyopakana na hifadhi za Taifa Mkomazi na Tarangire. Hatua hii inalenga kuzuia milipuko na kusambaa kwa magonjwa yanayoweza kuathiri wanyamapori ambao kutokana na mienendo yao kwa nyakati tofauti hufika katika maeneo yaliyo nje ya hifadhi.

63. *Mheshimiwa Spika*, ili kuboresha nyanda za malisho, kudhibiti magonjwa na moto kichaa pamoja na kuongeza mawanda ya shughuli za utalii, Shirika limeendelea kutekeleza programu za moto mpango katika hifadhi za Taifa 11 ambapo jumla ya hekta 1,935,621 zimechomwa moto. Aidha, barabara za kuinga moto zenye urefu wa kilomita 162.9 zimetengenezwa ili kuzuia moto kuunguza maeneo ya hifadhi. Katika hatua nyingine, Shirika limeendelea kuboresha miundombinu ya utalii kwa kujenga madaraja mawili (2)

katika hifadhi ya Taifa Tarangire na Ruaha; kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 3,157 katika hifadhi 16; na kutengeneza mwongozo wa uendelezaji na usimamizi wa viwanja vya ndege katika hifadhi za Taifa. Vilevile, Shirika limekarabati viwanja vya ndege 12 katika hifadhi za Taifa za Ruaha, Serengeti, Nyerere, Tarangire, Saadani, Mikumi na Mkomazi.

64. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendelea kuimarisha huduma za malazi na kuvutia uwekezaji wa utalii, Shirika limetoa maeneo 41 yenye uwezo wa kubeba vitanda 2,250 kwa wawekezaji kwa ajili ya kujenga miundombinu ya huduma za malazi kwa watalii. Aidha, jumla ya maeneo mapya 103 yenye uwezo wa vitanda 5,500 yameainishwa katika hifadhi za Taifa Nyerere, Mto Ugalla, Burigi - Chato, Rubondo, Ruaha, Serengeti, Tarangire, Ziwa Manyara, Mikumi, Saadani, Mkomazi na Arusha. Aidha, Shirika limeainisha maeneo maalum 11 ya uwekezaji katika hifadhi za Taifa Nyerere, Burigi - Chato, Katavi, Mto Ugalla na Ruaha; na kujenga "cottages" 13 zenye jumla ya vitanda 79 katika hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Burigi - Chato, Rubondo, Saanane, Mikumi na Mkomazi ili kuwezesha huduma ya malazi kwa watalii wa ndani na nje ya nchi.

65. *Mheshimiwa Spika*, katika kuongeza mazao mapya ya utalii na wigo wa ukusanyaji mapato, Shirika limeanzisha utalii wa faru katika hifadhi za Taifa Mkomazi na Serengeti. Aidha, Shirika limeendelea kukamilisha taratibu za awali za uanzishwaji wa mazao ya utalii wa uvuvi wa samaki na uendeshaji baiskeli katika Hifadhi ya Taifa Katavi, utalii wa boti katika Hifadhi ya Taifa Ruaha na utalii wa kupiga kasia (canoeing) katika hifadhi za Taifa Tarangire na Ziwa Manyara. Aidha, Shirika limejenga viwanja vya michezo vya mpira wa miguu, mpira wa wavu na mchezo wa *tennis* katika Hifadhi ya Taifa Mikumi kwa lengo la kuchochea utalii wa michezo.

66. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua ya kutangaza utalii kidijitali, Shirika limeandaa na kusambaza video fupi 83 na mabango ya kielektroniki 139 yenye jumbe mbalimbali kuhusu vivutio vya utalii vinyavyopatikana katika hifadhi za Taifa.

Aidha, Shirika limeendelea kuhamasisha utalii kupitia michezo ikiwemo michezo ya Wabunge wa mabunge ya Afrika Mashariki, mashindano ya mbio na matamasha yaliyoanzishwa katika hifadhi na mikoa mbalimbali nchini. Vilevile, Shirika limeendelea kutangaza vivutio vyake katika vyombo vya habari vya ndani na vya kimataifa vikiwemo BBC, CCTV na CGTN. Sambamba na hilo, Shirika limeendelea kupanua wigo wa matumizi ya teknolojia kutangaza na kuhamasisha utalii kwa kutengeneza *QR codes* za vipeperushi vya lugha za Kifaransa, Kiingereza na Kihispaniola ambavyo vimesambazwa katika Ofisi 44 za Balozi za Tanzania nje ya nchi. Pia, Shirika limewezesha kufanyika kwa ziara tisa (9) za mafunzo kwa makundi mbalimbali ya kimkakati wakiwemo: wakala wa biashara za utalii, wahariri wa vyombo vya habari, wawekezaji na watu mashuhuri kutoka ndani na nje ya nchi. Pia, Shirika limeendelea kushiriki maonesho mbalimbali ya utalii ndani na nje ya nchi.

67. Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha mazingira ya kufanya biashara na utoaji wa huduma katika maeneo ya hifadhi za Taifa, Shirika limeboresha miundombinu ya TEHAMA kwa kutengeneza mfumo endeshi utakaowezesha kampuni za utalii kuwasilisha maombi ya awali ya nafasi za maeneo ya kupiga kambi za kitalii kwa wageni. Aidha, Shirika limeanzisha dawati mtandao la kutolea msaada na usajili wa matukio mbalimbali. Vilevile, mifumo ya teknolojia na mawasiliano ya huduma ya mtandao imeboreshwa ili kupanua huduma katika malango mapya matatu (3) yaliyofunguliwa katika hifadhi za Taifa Ziwa Manyara, Rubondo na Mkomazi.

68. Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa kukamilisha ujenzi wa nyumba za watumishi 28 katika hifadhi za Taifa Ruaha (10), Serengeti (2), Burigi - Chato (6), Mto Ugalla (5), Mahale (2) na Ibanda - Kyerwa (3). Aidha, Shirika linaendelea kukamilisha ujenzi wa nyumba 17 katika hifadhi za Taifa Nyerere (7) na Ruaha (10). Vilevile, Shirika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali limenunua boti moja (1) kwa ajili ya kuimarisha doria katika Hifadhi ya Taifa Ziwa Manyara; na magari sita (6) kwa ajili ya kuimarisha shughuli za utalii na uhifadhi.

69. **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha ulinzi na usalama wa hifadhi, Shirika limeendelea kutumia vifaa mbalimbali vya kiteknolojia vikiwemo vifaa vya mawasiliano ya mtandao mpana (LoRa Transmitters), *trimble GPS*, vifaa vya kuwezesha kuona usiku pamoja na kamera maalum (hand held thermal image camera) ili kufuatilia usalama wa wanyamapori. Sambamba na hilo, Shirika limeendelea kujiimarisha katika kutumia mbinu za kisasa za kufanya doria zinazoongozwa na taarifa za kiintellijensia. Kwa kutumia mbinu hizo, Shirika limeweza kufanyika kwa jumla ya siku doria 216,663 zilizowezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 4,217 waliochukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Aidha, nyara za Serikali pamoja na silaha zikiwemo bunduki aina ya *shortgun (7)*, *rifle (2)* na magobore (33) zilikamatwa. Jitihada hizi zimewezesha kudhibiti ujangili, hususan wa tembo na faru katika maeneo ya hifadhi za Taifa.

4.5.1.4 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA

70. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ina jukumu la kusimamia uhifadhi na kuendeleza utalii katika mapori ya akiba 27, maeneo ya mifumo ya ikolojia manne (4), mapori tengefu 26 na maeneo matatu (3) ya ardhioevu. Aidha, Mamlaka ni mwangalizi na mshauri wa shughuli za uhifadhi katika maeneo 21 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori, mashamba 34, bustani 30, ranchi sita (6) na Kituo kimoja (1) cha kulelea wanyamapori wenye matatizo mbalimbali.

71. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu hayo, Mamlaka imetoa jumla ya leseni 36 za ufugaji wa wanyamapori kwa wawekezaji wa bustani, mashamba na ranchi za wanyamapori; na leseni 34 kwa ajili ya kuendesha biashara ya nyamapori. Aidha, Mamlaka imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ambapo jumla ya maeneo saba (7) yametolewa kwa wawekezaji chini ya utaratibu wa uwekezaji mahiri katika mapori ya akiba na tengefu. Maeneo hayo ni mapori ya akiba Ikorongo (1), Grumeti (1), Maswa (3) na Selous (1); na Pori Tengefu la Ziwa Natron (1). Uwekezaji huo umeiwezesha Mamlaka kuongeza mapato yatokanayo

na shughuli za uwindaji wa kitalii kutoka Shilingi 4,294,512,390.00 kwa mwaka 2021 hadi Shilingi 22,109,585,590.00 mwezi Aprili, 2022.

72. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za wanyamapori kwenye mapori ya akiba na tengefu, ardhioevu na maeneo ya wazi, Mamlaka imefanya jumla ya siku doria 104,678 zilizowezesha kukamatwa kwa nyara mbalimbali za Serikali, majangili 2,389, bunduki 102 na mitego ya nyaya 1,314. Jitihada hizo zimechangia kupunguza idadi ya mifugo inayovamia maeneo ya vitalu vya uwindaji kutoka mifugo 9,248 mwaka wa fedha 2020/2021 hadi mifugo 7,267 mwaka wa fedha 2021/2022. Kupungua kwa mifugo, kumewezesha kuongezeka kwa umiliki wa vitalu kutoka asilimia 63 hadi asilimia 70.4. Aidha, Mamlaka imetoa mafunzo kwa watumishi 1,863 kuhusu Kanuni na Amri za Jumla za Jeshi la Uhifadhi. Vilevile, Mamlaka imetoa mafunzo ya utayari ya Jeshi la Uhifadhi la Wanyamapori na Misitu kwa watumishi 150 kwa lengo la kuimarisha nidhamu na ufanisi wa utendaji kazi.

73. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kuboresha miundombinu ya utalii kwa kujenga lango la wageni, vituo saba (7) vya kukusanya mapato, kambi nne (4) za wageni, kituo kimoja (1) cha kutolea taarifa kwa wageni, jengo moja (1) la kupumzikia wageni, ofisi tano (5), karakana mbili (2) na vituo viwili (2) vya askari katika mapori ya akiba ya Maswa, Pande, Rukwa, Wami - Mbiki, Kijereshi, Mkungunero, Lukwika/Lumesule, Swagaswaga na Moyowosi; mapori tengefu ya Kilombero na Ziwa Natron; Kituo cha Urithi wa Dunia cha Kilwa Kisiwani na Songo Mnara; Eneo la Bustani ya Wanyamapori Tabora; na Ofisi ya Kanda ya Kati na Magharibi. Katika hatua nyingine, Mamlaka imefungua na kujenga barabara zenye urefu wa kilomita 321.5 kwa kiwango cha changarawe na madaraja mawili (2) katika mapori ya akiba 11 ya: Wami - Mbiki (km 25), Mpanga/Kipengele (km 16), Mkungunero (km 89.5), Swagaswaga (km 20), Liparamba (km 20), Maswa (km 40), Pande (km 12), Igombe (km 37), Kijereshi (km 22) na Lukwika/Lumesule (km 40) na madaraja

makubwa (2) katika Pori la Akiba Liparamba na Mpanga/ Kipengele.

74. *Mheshimiwa Spika*, katika kupanua wigo wa masoko ya uwindaji wa kitalii, Mamlaka imeshiriki maonesho mbalimbali ya biashara ya kimataifa ikiwemo *Safari Club International Convention*, Marekani. Kupitia maonesho hayo, Mamlaka iliweza kutangaza fursa za uwekezaji na kuhamasisha wafanyabiashara kuwekeza katika shughuli za utalii na uwindaji. Aidha, Mamlaka imeandaa mfumo wa kidijitali unaotoa taarifa kwa wageni kuhusu vivutio vya utalii vilivyopo katika maeneo yanayosimamiwa na TAWA. Aidha, Mamlaka imeanzisha ranchi sita (6) katika mikoa ya Manyara (2), Kilimanjaro (1), Pwani (2) na Simiyu (1); mashamba ya wanyamapori 27; na bustani za wanyamapori 24 ili kurahisisha upatikanaji wa nyamapori kwa wananchi.

4.5.1.5 Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro - NCAA

75. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka ina jukumu la kusimamia shughuli za uhifadhi wa maliasili na malikale, uendelezaji wa utalii na ustawi wa jamii zinazoishi ndani ya eneo la hifadhi. Katika utekelezaji wa jukumu hilo, Mamlaka imeendelea kuimarisha ulinzi wa maliasili na malikale zilizopo ndani ya Hifadhi kwa kufanya siku doria 28,980 zilizofanikisha kukamatwa kwa watuhumiwa 44 wa makosa ya ujangili wa wanyamapori. Aidha, Mamlaka imeboresha ulinzi wa faru kwa kuwawekea alama maalum za utambuzi na mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya ufuatiliaji. Vilevile, Mamlaka imeboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kukarabati vituo sita (6) vya askari katika maeneo ya Lemala, Makhoromba, Ndotu, Kakesio, Endamagha na Masamburai. Pia, ujenzi wa vituo vipya vya askari katika maeneo ya Lositete na Lemala unaendelea. Sambamba na hatua hizo, Mamlaka imeendelea kutoa mafunzo ya amri za jumla na kanuni za kudumu za Jeshi la Uhifadhi kwa watumishi 718 na semina kuhusu maadili kwa watumishi 136. Mafunzo haya yamesaidia kuimarisha nidhamu na utendaji kazi wa watumishi katika ulinzi na uhifadhi wa maliasili na malikale zilizopo hifadhini.

76. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeimarisha miundombinu ya utalii ndani ya hifadhi kwa kukamilisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 4.2 inayoshuka kreta ya Ngorongoro kwa kiwango cha tabaka gumu la mawe; na ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 15 kutoka Ndotu hadi Kakesio kwa kiwango cha changarawe. Sambamba na hilo, Mamlaka imekarabati barabara zenye urefu wa kilomita 472 ndani ya Hifadhi; na miundombinu ya viwanja vya ndege vya Ndotu na Ngorongoro. Aidha, katika kuhamasisha uwekezaji wa shughuli za utalii, Mamlaka imefungua barabara zenye urefu wa jumla ya kilomita 19 kuelekea maeneo ya uwekezaji yaliyo jirani na Kreta ya Empakai. Vilevile, Mamlaka imeendelea kukarabati miundombinu ya umeme, vyoo na mifumo ya maji ndani ya Hifadhi ili kuboresha huduma za utalii na kuvutia uwekezaji. Sambamba na hilo, Mamlaka imenunua mitambo mizito mitano (5) na malori matano (5) kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara ndani ya hifadhi. Pia, upembuzi yakinifu wa ujenzi wa barabara kuu yenye kilomita 83 kutoka lango kuu la Loduare hadi Golini kwa kiwango cha tabaka gumu umekamilika.

77. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuongeza mapato na muda wa mtalii kukaa hifadhini, Mamlaka imeendelea kuibua mazao mapya ya utalii ikiwemo utalii wa usiku (night game drive), utalii wa kutembea kwenye miti (canopy walkways), utalii wa kutembea na farasi, utalii wa baiskeli na utalii wa puto ndani ya hifadhi. Katika hatua nyingine, Mamlaka imeendelea kushiriki maonesho ya utalii ndani na nje ya nchi. Vilevile, Mamlaka imeendelea kutangaza mubashara vivutio vya utalii katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Mathalan, kupitia onesho la *Dubai Expo 2020*, washiriki kutoka mataifa mbalimbali waliweza kuona mubashara vivutio vilivyopo hifadhini.

78. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha uwepo wa maji safi na salama, Mamlaka imekamilisha kwa asilimia 65 ujenzi wa mradi wa maji ujulikanao kama *Mama Hhawu Water Treatment Plant* wenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 1,500,000 kwa siku. Mradi huo unahusisha ujenzi wa mtambo

wa kuchuja maji, ukarabati wa banio na matanki mawili (2) yenye uwezo wa lita 105,000 kwa ajili ya kuhifadhi maji na ujenzi wa kituo cha uendeshaji wa mtambo. Mradi huu pamoja na kuwanufaisha wageni wanaoingia Hifadhini, pia utawanufaisha wananchi 5,000 wanaopakana na Hifadhi ikiwa ni pamoja na hospitali teule ya Wilaya ya Karatu.

79. Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea na jukumu la kuendeleza jamii ya wenyeji waishio ndani ya Hifadhi. Katika kutekeleza jukumu hili, Mamlaka imetoa ufadhili kwa wanafunzi 2,163 wa jamii ya wenyeji katika ngazi ya shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu. Aidha, Mamlaka imegawa mizinga 1,878 kwa vikundi 94 vya wafugaji nyuki katika wilaya za Ngorongoro, Karatu, Monduli na Meatu. Vilevile, Mamlaka imewezesha utoaji wa huduma za afya kwa wenyeji katika Zahanati ya Ngorongoro; kuwapatia wenyeji 1,300 kadi za bima ya afya ya jamii iliyoboreshwa (iCHF); na kutoa chanjo kwa jumla ya mifugo 2040. Sambamba na hatua hizo, Mamlaka imefanya mikutano 183 yenye jumla ya washiriki 34,803 kwa lengo la kutoa elimu ya uhifadhi na namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

80. Mheshimiwa Spika, ili kutafuta suluhu ya kudumu ya changamoto za matumizi mseto ya ardhi ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Mamlaka imefanya uhamasishaji kupitia vikao na mikutano ya majadiliano baina ya Serikali na wadau mbalimbali wakiwemo wenyeji waishio ndani ya eneo la Hifadhi. Kupitia jitihada hizo, jumla ya kaya 278 zenye wakazi 1,439 walikua wamejiandikisha kuhama kwa hiari kutoka hifadhini. Pia, Wizara imebainisha maeneo mbadala ya Handeni, Tanga na Kitwai, Manyara kwa ajili ya makazi kwa wananchi watakaohama kutoka Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro. Kwa upande wa Handeni, Mamlaka imebainisha eneo lenye ukubwa wa hekta 112,239 kwa ajili ya matumizi ya makazi na huduma za jamii. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara ilifanikiwa kupima eneo lenye ukubwa wa hekta 73,528.73 lililogawanywa kwa ajili ya matumizi mbalimbali yakiwemo: makazi (hekta 10,080.4), kilimo (hekta 13,628.48), malisho (hekta 22,176.06), ujenzi wa taasisi za elimu ya juu na vyuo (hekta 1,329.37), ushoroba wa wanyamapori

(hekta 26,314.42) na hifadhi ya misitu (hekta 6,082.72). Zoezi la upimaji na upangaji wa matumizi ya ardhi katika eneo lililobaki pamoja na eneo la Kitwai lenye ukubwa wa hekta 409,416 linaendelea.

81. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara kwa kushirikiana na Uongozi wa mikoa ya Arusha na Tanga imekamilisha ujenzi wa nyumba 103 katika eneo la Handeni ambazo ni awamu ya kwanza ya ujenzi wa nyumba 500 kwa ajili ya wananchi wenyeji waishio ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro ambao wameridhia kuhama kwa hiari. Sambamba na ujenzi wa nyumba hizi, maeneo haya yatakuwa na miundombinu muhimu ya kijamii ikiwemo barabara zenye urefu wa kilomita 2,880, umeme, maji, zahanati 25, vituo vya afya vitatu (3), shule za msingi 25, shule za sekondari nne (4), ofisi nne (4) za vijiji, ofisi 11 za kata, ofisi moja (1) ya tarafa, ofisi moja (1) ya mahakama na kituo kimoja (1) cha polisi na mahakama. Wizara inaendelea na juhudi za kukamilisha miundombinu muhimu pamoja na kuhamasisha na kuelimisha jamii ili waweze kuhama kwa hiari kwa manufaa ya uhifadhi na maendeleo ya jamii.

82. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha nyanda za malisho na kudhibiti mimea vamizi, jumla ya ekari 7,000 zimechomwa kwa kutumia njia ya moto mpango. Aidha zoezi la kung'oa/kufyeka magugu vamizi limefanyika katika eneo lenye jumla ya ekari 2,500. Jitihada hizi zimesaidia kuboresha nyanda za malisho na makazi ya wanyamapori sambamba na kupunguza mgongano baina ya wanyamapori na mifugo. Katika hatua nyingine, Mamlaka imeotesha jumla ya miche ya miti 460,000 ambapo miche 54,460 imegawiwa kwa jamii zinazozunguka eneo la Hifadhi.

83. Mheshimiwa Spika, Katika kuimarisha uwekezaji wa kitalii ndani ya Hifadhi, Mamlaka imetenga jumla ya maeneo mapya sita (6) kwa ajili ya uwekezaji wa kimkakati yenye uwezo wa jumla ya vitanda 480. Maeneo haya yatatolewa kwa wawekezaji wa kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya huduma za malazi ya hadhi ya juu ili kuvutia wageni wenye hadhi kutembelea Hifadhi. Aidha Mamlaka

imetenga maeneo mawili (2) katika eneo lililokuwa likitumika kama makao makuu kwa ajili ya kujenga hosteli ili kutoa huduma za malazi ya gharama nafuu mahsusi kwa watalii wa ndani.

4.5.1.6 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori - TAWIRI

84. Mheshimiwa Spika, Taasisi ina jukumu la kuratibu na kufanya tafiti za wanyamapori nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Taasisi imeidadi wanyamapori katika mifumo ikolojia ya Ruaha – Rungwa na Katavi – Rukwa; maeneo ya mtawanyiko; na shoroba zilizomo katika mifumo ikolojia hiyo. Matokeo ya sensa katika mfumo ikolojia wa Ruaha - Rungwa yanaonesha kuwa kuna tembo 15,608, nyati 20,911, swala pala 8,643, pundamilia 10,552, palahala 6,636 na kongoni 4,017. Aidha matokeo hayo yakilinganishwa na yale ya mwaka 2018 yanaonesha kuimarika kwa idadi ya tembo sambamba na ongezeko la nyati kwa asilimia 80, pundamilia asilimia 36, na palahala asilimia 65.

85. Mheshimiwa Spika, matokeo ya sensa katika Mfumo Ikolojia wa Katavi - Rukwa yameonyesha kuwa kuna tembo 3,089, nyati 24,405, pundamilia 3,339, kongoni 3,356 na twiga 1,295. Matokeo haya yakilinganishwa na sensa iliyofanyika mwaka 2018 yanaonyesha ongezeko la asilimia mbili (2) kwa tembo; na idadi ya wanyamapori wengine wakiwemo nyati, pundamilia, kongoni na twiga haikubadilika kwa kiwango kikubwa. Matokeo hayo pia yanaonesha kupungua kwa shughuli za kibinadamu katika mifumo ikolojia hiyo. Aidha, matokeo ya sensa katika Mfumo Ikolojia Ziwa Natron - West Kilimanjaro yameonesha kuwa kuna ongezeko la idadi ya tembo kutoka 169 mwaka 2018 hadi 219 mwaka 2021; na ongezeko la wanyamapori wengine wakiwemo pundamilia na nyumbu. Vilevile, matokeo ya sensa katika eneo la West Kilimanjaro ni pundamilia 3,651, swala granti 1,284, nyati 18, swala thomi 553 na twiga 1,030. Hata hivyo, idadi ya nyati imepungua kwa asilimia 19 na swala thomi kwa asilimia 16. Matokeo hayo yanasababishwa na ongezeko la mifugo hususan ng'ombe ambao wameongezeka kwa asilimia 337 kutoka 80,344 mwaka 2018 hadi 350,881 mwaka 2021. Kwa

ujumla, takwimu zinaonesha maoneo yaliyohifadhiwa yamezidi kuimarika.

86. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutatua migongano baina ya binadamu na wanyamapori, Taasisi ilihamisha wanyamapori 278 (nyumbu 180 na pundamilia 98) kutoka maeneo ya Mto wa Mbu kwenda Hifadhi ya Taifa Tarangire; na simba 13 waliokuwa wanahatarisha maisha ya binadamu katika wilaya za Bunda na Serengeti kwenda Hifadhi ya Taifa Burigi - Chato. Aidha, katika kutatua migogoro baina ya binadamu na wanyamapori, Taasisi imefunga mikanda ya mawasiliano kwa ajili ya kufuatilia mienendo ya wanyamapori. Jumla ya makundi ya tembo 107 katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; Pori la Akiba Maswa na mapori tengefu ya Longido na Ziwa Natron; makundi ya Mbwa mwitu 7 katika Mfumo Ikolojia Serengeti; na makundi ya simba 21 katika mifumo ikolojia Serengeti na Ruaha - Rungwa wamefungwa mikanda ya mawasiliano kwa ajili ya ufuatiliaji wa nyendo zao. Kwa upande mwingine, Taasisi ilitoa mafunzo ya mbinu za kukabiliana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori (simba na tembo) kwa waelimishaji 610 katika wilaya 21 watakaotoa mafunzo kwa jamii ya namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. Katika hatua nyingine, Taasisi iliandaa Kongamano la 13 la Kisayansi la Kimataifa lililofanyika Jijini Arusha, mwezi Desemba 2021 kwa lengo la kutoa matokeo ya tafiti mbalimbali kuhusu uhifadhi. Washiriki katika Kongamano hilo walikuwa 436 toka nchi 18 duniani na mada 177 ziliwasilishwa.

4.5.1.7 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - CAWM Mweka

87. Mheshimiwa Spika, Chuo kina jukumu la kutoa mafunzo katika ngazi za Cheti cha Msingi, Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kinafanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uhifadhi wa wanyamapori na uendeshaji utalii. Katika kutekeleza hili, mwaka 2021/2022, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 834 katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Aidha, jumla ya wanafunzi 433

walihitimu na kutunukiwa vyeti katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki 22 juu ya mbinu ya kukamata na kuhamisha nyoka katika eneo la Bulyankulu, Mkoa wa Shinyanga na mafunzo kwa waongoza watalii wapatao 1,060 kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar.

88. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kupitia mitaala 10 iliyopo; kuandaa mitaala nane (8) mipya; na kuboresha Kitengo cha TEHAMA kwa kununua vitendea kazi mbalimbali vya kuimarisha utendaji kazi. Aidha, ili kuboresha utoaji wa mafunzo, Chuo kimejenga kumbi mbili (2) za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250 kila moja katika kampasi kuu ya Mweka (1) na eneo la Mafunzo kwa Vitendo Kwakuchinja (1). Vilevile, Chuo kimekamilisha ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 294 katika kampasi kuu ya Mweka na kununua magari mawili (2) kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

4.5.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi

89. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi ina jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori na himasheria katika ngazi ya Astashahada. Katika kutekeleza jukumu hilo, Taasisi imedahili wanafunzi 410 katika fani za uhifadhi wanyamapori na himasheria, uongozaji watalii na usalama kwa ngazi ya Astashahada na Astashahada ya awali. Aidha, Taasisi imetoa mafunzo ya utayari wa Jeshi la Uhifadhi kwa watumishi wapya 43 wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania. Katika hatua nyingine, Taasisi imetoa mafunzo ya muda mfupi kuhusu usimamizi wa rasilimali za wanyamapori kwa wanavijiji 140 kutoka wilaya za Tanganyika, Mpanda, Nsimbo, Serengeti, Uvinza, Kigoma, Simanjiro na Karatu. Vilevile, Taasisi inaendelea kuboresha mitaala yake ili kuendana na mahitaji ya kila siku katika uhifadhi wa wanyamapori na utalii. Pia, Taasisi ipo katika hatua za mwisho za ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kubeba watu 400 kwa wakati mmoja

pamoja na uchimbaji wa kisima kirefu cha maji safi katika eneo la mafunzo Forti Ikoma.

4.5.1.9 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu- Sekamaganga

90. Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu - Sekamaganga kina jukumu la kuzijengea uwezo jamii zinazoishi jirani na maeneo yaliyohifadhiwa ili zishiriki katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kituo kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 204 ambapo Askari Wanyamapori wa Vijiji 20 wamepata mafunzo ya usimamizi wa rasilimasili za maliasili; askari 34 wamepata mafunzo ya kuongoza watalii; na askari 150 wa TAWA wamepata mafunzo ya utayari wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misit. Vilevile, Kituo kimetoa ushauri wa kitaalam kwa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori tano (5) za Mbarang'andu, Kimbanda na Kisungule (Namtumbo); na Chingoli na Nalika (Tunduru). Katika hatua nyingine, Chuo kimefanya mapitio ya mitaala ya kozi za Astashahada ya Awali ya Utalii na Waongoza watalii, Askari Wanyamapori wa Vijiji, Viongozi wa Wajumbe wa Kamati za Maliasili za Vijiji pamoja na kuandaa mitaala mipya ya kozi za Astashahada na Stashahada ya utalii na waongoza watalii.

4.5.1.10 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - TWPF

91. Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania una jukumu la kuwezesha uhifadhi wa wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mfuko umeendelea kuwezesha operesheni maalum za kuzuia ujangili; utekelezaji wa kazi za Kikosi Kazi cha Taifa cha kupambana na ujangili (NTAP); na Jeshi la Uhifadhi. Aidha, Mfuko umewezesha kufanyika kwa uhakiki wa matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu katika wilaya 36 zilizoathirika pamoja na kufanya malipo ya Shilingi 790,721,500.00 kwa wahanga 3,598 walioathiriwa na wanyamapori hao. Kwa upande mwingine, Mfuko

umewezesha zoezi la kupandisha hadhi mapori tengefu matatu (3) kuwa mapori ya akiba. Vilevile, Mfuko umewezesha kufanyika kwa mapitio ya Kanuni mbalimbali za Sekta ya Wanyamapori; kufanya tathmini ya utendaji wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori; kuandaa mpango mkakati wa kuongoa shoroba; na kuwezesha upatikanaji wa silaha za Jeshi la Uhifadhi.

4.5.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

92. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Misitu (1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998). Aidha, utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika sekta hizi unasimamiwa na Sheria ya Misitu Sura 323, Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224 na Sheria ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania Sura 277. Vilevile, jukumu la uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki hutekelezwa kupitia Idara ya Misitu na Nyuki, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), Chuo cha Misitu Olmotonyi (FTI), Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) Moshi, Chuo cha Ufugaji Nyuki (BTI) Tabora na Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF).

4.5.2.1 Masuala Mahsusi ya Sekta ya Misitu na Nyuki

(i) Kuongeza Thamani ya Mazao ya Misitu na Nyuki

93. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha kuwa mazao ya misitu na nyuki yanayozalishwa hapa nchini yanaongezwa thamani, Wizara imeendelea kutoa elimu, kuhamasisha na kuwezesha wadau mbalimbali kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya misitu na nyuki. Juhudi hizi zinalenga kuhakikisha viwanda vilivyopo na vitakavyojengwa vinazalisha bidhaa mbalimbali zitokanazo na mbao pamoja na mazao ya nyuki ili kuongeza thamani na mapato yatokanayo na bidhaa hizo. Pamoja na juhudi hizo, Wizara imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Mazao ya Mbao Yaliyohandisiwa (National Engineered Wood Sector

Development Framework 2021 - 2031) pamoja na Mpango kazi wa utekelezaji wake utakaowezesha uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vya mazao ya misitu. Pia, Wizara imekamilisha ujenzi wa viwanda vitano (5) na ukarabati wa kiwanda kimoja (1) cha kuchakata mazao ya nyuki katika wilaya za Kibondo, Nzega, Sikonge, Bukombe, Mlele na Tabora Mjini.

(ii) Kuboresha Mazingira ya Kibiashara katika Sekta za Misitu na Nyuki

94. *Mheshimiwa Spika*, ili kuboresha mazingira ya kibiashara na kuendelea kuvutia wawekezaji katika sekta za Misitu na Nyuki, Wizara imeendelea kufanya maboresho ya tozo mbalimbali na kuandaa miongozo ya kuratibu biashara ya mazao na huduma za misitu na nyuki. Wizara imefanya maboresho ya Kanuni ya Tozo za Misitu Na. 627 ya mwaka 2020 na kuandaa Kanuni mpya iliyotolewa katika Tangazo la Serikali Na. 59 la mwaka 2022. Katika hatua nyingine, Wizara imeandaa Mwongozo na kanuni za kuratibu biashara ya hewa ukaa (carbon trading) na mwongozo wa kutumia makundi ya nyuki kwa ajili ya kutoa huduma ya uchavushaji wa mimea. Maboresho hayo yamechochea uwekezaji na ukuaji wa biashara ya mazao na huduma katika sekta za misitu na nyuki.

4.5.2.2 Idara ya Misitu na Nyuki

95. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imekamilisha maandalizi ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Misitu 2021 - 2031; Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki 2021 - 2031; Mkakati wa Kitaifa wa Mazao ya Mbao Yaliyohandisiwa wa mwaka 2021 - 2031; Taarifa ya Misitu ya Jamii (PFM Facts and Figures) ya mwaka 2022; na Mpango kazi wa Usimamizi wa Misitu ya Jamii wa mwaka 2022. Aidha, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uanzishwaji na Usimamizi wa Hifadhi za Nyuki na Manzuki wa mwaka 2021; Mwongozo wa Usimamizi na Matumizi Endelevu ya Misitu ya Mikoko wa mwaka 2021; Taratibu za Kitaifa za Mafunzo na Elimu ya Ugani

ya Ufugaji Nyuki za mwaka 2021; Mwongozo wa kufanya utafiti wa misitu na nyuki nchini wa mwaka 2022; Mwongozo wa kutumia makundi ya nyuki kwa ajili ya kutoa huduma ya uchavushaji wa mimea wa mwaka 2022; na Agizo la Kiufundi Na. 1 (*Technical Order No. 1*) la mwaka 2021 kuhusu uzalishaji, ubora na tija ya mazao ya misitu. Katika hatua nyingine, Wizara imefanya tathmini ya Sheria na Kanuni ya Misitu ili kuboresha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi. Miongozo hii inalenga kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki pamoja na kuongeza mapato ya Serikali.

96. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imekamilisha kazi ya tathmini ya mchango wa sekta ya misitu na nyuki katika pato la Taifa. Tathmini hiyo imebaini kuwa sekta ya misitu na nyuki kwa sasa inachangia asilimia 3.3 ya pato ghafi la Taifa. Aidha, tathmini imebainisha maeneo yenye mchango mkubwa katika kuongeza mapato na maeneo mengine mapya ambayo yanahitaji msukumo ili kuweza kuongeza uchangiaji wa sekta ya misitu na nyuki katika uchumi wa Taifa.

97. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu na nyuki, Wizara imekamilisha Andiko la Kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Misitu na Nyuki Tanzania na hatua inayofuata ni kupitisha katika mamlaka mbalimbali za maamuzi. Katika hatua nyingine, Wizara imeratibu mikutano miwili (2) ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Misitu - NAFAC; mikutano mitatu (3) ya Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki - NABAC; na vikao vitatu (3) vya wadau wa misitu kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki. Sambamba na hilo, Wizara imeanza utekelezaji wa mradi wa kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya ufugaji nyuki (BEVAC). Mradi huu pamoja na manufaa mengine utaimarisha usimamizi wa manzuki na hifadhi za nyuki, kuunganisha wazalishaji wa mazao ya nyuki na masoko, kuimarisha uwezo wa taasisi zilizo kwenye mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki ili ziweze kutoa huduma stahiki katika ukuzaji wa sekta ya ufugaji nyuki nchini, pamoja na

kuwajengea uwezo makundi mbalimbali wakiwemo wanawake kushiriki shughuli mbalimbali za ufugaji nyuki.

98. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa jamii inaendelea kuelimishwa na kuhamasishwa kushiriki katika uhifadhi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara imeratibu maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani yaliyofanyika Mkoa wa Ruvuma tarehe 29 Julai, 2021; na maadhimisho ya siku ya misitu Duniani na upandaji miti Kitaifa yaliyofanyika Mkoa wa Mwanza tarehe 23 Machi, 2022. Aidha, Wizara imesajili na kuingiza taarifa za wafugaji nyuki 1,026 kwenye kanzidata ya Misitu na Nyuki iliyounganishwa na Mfumo wa *MNRT - Portal*. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani imeratibu Mkutano wa Pili wa Kimataifa wa Kikundi kazi cha Misitu ya Nyanda Kame uliofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 17 hadi 18 Novemba, 2021.

4.5.2.3 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS

99. Mheshimiwa Spika, Wakala umepewa jukumu la kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki zilizo chini ya Serikali Kuu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wakala unasimamia misitu 463 iliyohifadhiwa kisheria. Misitu hiyo inajumuisha: mashamba ya miti 24, misitu ya mazingira asilia 20, misitu ya hifadhi ya asili 419 na hifadhi za nyuki 12. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wakala umehakiki mipaka ya misitu 120 yenye urefu wa kilomita 160; kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 1,112; kuweka vigingi 589 na mabango 204; na kuchimba mashimo 48 yanayoonesha uelekeo wa mpaka. Aidha, Wakala umejenga barabara zenye urefu wa kilomita 49, kalavati nane (8) na daraja moja (1) katika mashamba ya miti 14 ya Buhindi, Kiwira, Longuza, Meru, North Kilimanjaro, Rondo, Rubare, Sao Hill, Shume, Mpepo, Ukaguru, West Kilimanjaro, Wino na North Ruvu. Vilevile, Wakala umekarabati kilomita 906 za barabara, kalvati 18 na madaraja nane (8) katika misitu ya mazingira asilia ya Amani, Pugu – Kazimzumbwi, Magamba na Mlima Rungwe; na mashamba ya miti 24. Katika hatua nyingine, mipango 48 ya usimamizi na uendelezaji wa misitu yenye ukubwa wa hekta 1,157,134 imeandaliwa.

100. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wakala umeendesha jumla ya siku doria 84,050 ambazo zimewezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 726. Aidha, doria zimewezesha kukamatwa kwa mazao mbalimbali ya misitu ikiwemo magunia 19,934 ya mkaa, magogo yenye ujazo wa mita 1,218.19, kuni zenye mita za ujazo 180, nguzo 5,239, mbao 3,761 pamoja na fremu za milango na madirisha 802. Kwa upande mwingine, mafunzo kuhusu usimamizi shirikishi wa misitu; athari na namna ya kukabiliana na moto kichaa; na upandaji na utunzaji wa miti yametolewa kupitia mikutano 297 katika vijiji 236. Pia, Wakala umetoa elimu ya biashara ya mazao ya misitu na nyuki kwa wadau 532.

101. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kuendeleza mashamba 24 ya Serikali yenye ukubwa wa hekta 510,000 Wakala umetekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuzalisha tani 11.35 za mbegu bora za miti; kupanda miche 9,795,687 katika eneo lenye ukubwa wa hekta 7,833; kupalilia hekta 19,601; kupogoa miti hekta 10,137; na kupunguza miti katika eneo la hekta 1,559. Aidha, misitu yenye ukubwa wa hekta 121,100 imehifadhiwa kisheria. Kadhalika, ili kuendeleza ulinzi wa mashamba ya miti; kilomita 596 za njia za kuzuia moto zilisafishwa, kukarabati minara 16 ya kubaini matukio ya moto pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi 236 wanaofanya kazi ya kukabiliana na moto kwenye mashamba. Katika hatua nyingine, Wakala umeandaa Mpango Mkakati wa miaka 30 wa kusimamia na kuendeleza mashamba ya miti ambao utawezesha kuanzishwa na kuongeza wigo wa mashamba ya miti ya kibiashara kama vile mianzi, utomvu, mpira na miti ya dawa kama vile *Prunus africana* inayotumika kutengeneza madawa ya kutibu saratani.

102. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuimarisha shughuli za utalii ikolojia na malikale, Wakala umekarabati kilomita 66.7 za barabara za ndani ya hifadhi za misitu asilia, kilomita 163.2 za njia za kutembea watalii na kambi tano (5) za kupumzikia. Aidha, Wakala umeandaa na kurusha vipindi 173 vya *Tanzania ya Kijani* katika televisheni na redio vyenye maudhui ya uendelezaji wa utalii; uhifadhi wa misitu na ufugaji

nyuki; matumizi ya nishati mbadala; na kukabiliana na matukio ya moto. Vilevile, Wakala umeandaa na kusambaza vipeperushi 20,622 na makala moja (1) ya vivutio vya utalii ilirushwa kwenye televisheni na programu sita (6) zilizorushwa kupitia redio mbalimbali nchini. Kwa upande mwingine, Wakala umeendelea kuelimisha Umma kuhusu uhifadhi na huduma mbalimbali zinazotolewa na Wakala kupitia matamasha na maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi. Pia, katika kuendeleza utalii wa malikale, Wakala umefanya ukarabati wa ofisi, ujenzi wa banda la utalii, ujenzi wa *camping - site* yenye uwezo wa kubeba wageni 20 na ukarabati kituo cha kutolea taarifa katika Kituo cha Malikale cha Kolo (Kondoa)". Vilevile, Wakala umejenga banda la kupumzikia wageni katika kituo cha malikale cha Kaole. Ili kuongeza ufanisi katika uhifadhi na ukusanyaji wa maduhuli, Wakala umeboresha mfumo wa *Forest Resources Management Information System* (FREMIS) na kuunda mfumo fungamanishi mpya ujulikanao kama *TFS Intergrated Information Management System* (TFS - IIMS). Vilevile, mafunzo maalum yametolewa kwa wataalam watano (5) wanaotoa huduma za kiufundi kuhusu mfumo huo.

103. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kusimamia na kuendeleza ufugaji nyuki, Wakala umezalisha tani 12.4 za asali na tani 0.3 za nta kutoka kwenye manzuki 182. Aidha, Wakala umeanzisha mashamba mawili (2) maalum ya kufuga nyuki (*bee farm*) ya Kondoa - Manyoni na Mwambao - Handeni. Wakala umetengeneza mizinga 2,500 na kuongeza mashine za kutengeneza mizinga katika kiwanda cha Wakala kilichopo Kondoa. Vilevile, ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya nyuki kwa jamii, Wakala umetoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ya nyuki kwa vikundi 49 vyenye wafugaji 896 na kugawa mizinga 416 kwa jamii katika wilaya za Mvomero, Lindi, Nyasa na Songea. Kwa upande mwingine, Wakala umekusanya sampuli 70 za asali kutoka katika wilaya 29 na kuzipeleka kwenye maabara ya kimataifa iliyopo nchini Ujerumani kwa lengo la kupima ubora wa asali inayozalishwa hapa nchini. Matokeo yanaonesha kuwa asilimia 99 ya sampuli hizo zimekidhi viwango vya ubora wa

kimataifa na hivyo kutoa fursa kwa asali ya Tanzania kuendelea kuuzwa katika masoko mbalimbali duniani.

104. Mheshimiwa Spika, Wakala umeendelea kuboresha ustawi wa watumishi kwa kuweka mazingira wezeshi ya kufanyia kazi. Katika kutekeleza hilo, Wakala umejenga ofisi 12 na kukarabati majengo 46 katika Ofisi za Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kasikazini, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kusini, Kanda Mashariki na mashamba ya miti ya West Kilimanjaro, Ukaguru, Sao Hill, Rubare, Rondo, Kawetire na Buhindi. Aidha, Wakala umenunua magari 26 na pikipiki 33 ili kuwezesha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za uhifadhi wa misitu na nyuki. Vilevile, Wakala umetoa mafunzo ya utayari ya kijeshi kwa watumishi 498 na mafunzo ya Kanuni na Amri za Jeshi la Uhifadhi kwa watumishi 161. Mafunzo haya yamesaidia kuimarisha nidhamu na utendaji kazi kwa watumishi katika kulinda na kusimamia rasilimali za misitu, nyuki na malikale.

4.5.2.4 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI

105. Mheshimiwa Spika, Taasisi ina jukumu la kufanya na kuratibu utafiti wa misitu na ufugaji nyuki na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za misitu na ufugaji nyuki. Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu imefanya utafiti kuhusu moto wa misituni kwa kutumia *Satellite* na kubaini kuwa eneo la kilomita za mraba 95,793 liliungua na moto kwa kipindi cha mwaka 2021/2022. Aidha, maeneo ambayo yameathirika zaidi na moto ni mikoa ya Lindi (kilomita za mraba 13,066), Morogoro (kilomita za mraba 11,539) na Katavi (kilomita za mraba 10,878). Pia, utafiti umebaini uwepo wa maeneo yaliyoathirika na matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi kama vile Hifadhi za Taifa (kilomita za mraba 32,652), mapori ya Akiba (kilomita za mraba 26,733), Hifadhi za Misitu (kilomita za mraba 11,725) na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (kilomita za mraba 267). Vyanzo vikuu vya moto huo ni pamoja na ufunguaji mashamba kwa ajili ya kilimo, uvunaji asali usiotumia zana za kisasa, majangili na moto mpango. Ili kupambana na moto kichaa Wizara itaendelea kushirikiana na wadau kutoa elimu kwa jamii kuhusu vyanzo, athari na mbinu za

kukabiliana na moto katika maeneo ya hifadhi. Sambamba na hilo, TAFORI kwa kushirikiana na Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki (EAMCEF) imetengeneza mfumo wa utoaji wa taarifa za uhalifu ikiwemo moto ili kuwezesha jamii kukabiliana na matukio ya moto kwa wakati.

106. Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) katika kufanya utafiti juu ya uvunaji wa utomvu kwenye miti ya misindano ili kubaini umri sahihi wa kuvuna utomvu, madhara yake kwenye ukuaji wa miti na ubora wa mbao. Matokeo ya awali ya utafiti yanaonesha kuwa ugemaji wa utomvu unaathiri miti yenye umri wa kati ya miaka mitano (5) hadi 20. Wastani wa ukuaji wa kipenyo cha mti unaogemwa hupungua kwa asilimia 16 ukilinganisha na mti usiogemwa. Hivyo, ili kupunguza athari ya ukuaji wa miti inashauriwa kuwa uvunaji wa utomvu ufanyike kwa miti yenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.

107. Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kubaini mchango wa rasilimali za misitu kwa jamii, Taasisi imefanya utafiti wa uzalishaji na biashara ya mazao yatokanayo na mti wa Mlonge. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mti wa mlonge hupandwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo mikoa ya Iringa, Pwani, Morogoro, Tanga, Dar es Salaam na Dodoma. Mti huu hutumika kuzalisha bidhaa mbalimbali ikiwemo dawa, lishe na mafuta. Aidha, utafiti unaonesha kuwa kwa mwaka mkulima hupata wastani wa Shilingi 2,054,944.41 kupitia uuzaji wa mbegu za mlonge na Shilingi 572,365.00 kupitia uuzaji wa majani ya mlonge. Kutokana na fursa hiyo, inashauriwa kuwa jamii iendelee kutunza na kupanda miti ya milonge ili kuweza kuongeza kipato cha kaya na Taifa kwa ujumla.

108. Mheshimiwa Spika, Katika hatua nyingine, Taasisi imefanya utambuzi na utafiti wa miti iliyopandwa katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Morogoro na Ruvuma. Lengo la utafiti huu ni kutambua aina na kiwango cha miti iliyopo katika mikoa hiyo kwa lengo la kutoa taarifa kwa wawekezaji. Matokeo ya utafiti yamebaini uwepo wa spishi

kuu tatu (3) ambazo ni misindano, mikaratusi na miwato. Aidha, spishi hizo zipo katika eneo la ukubwa wa hekta 203,172.35 ambapo kwa mikoa ya Iringa na Morogoro ni hekta 72,347; Mkoa wa Njombe hekta 115,391.04; Mkoa wa Mbeya hekta 14,140.21; na Mkoa wa Ruvuma hekta 1,294.10. Matokeo hayo yanaonesha kuwa rasilimali za misitu zilizopo katika maeneo hayo ni toshelevu kwa wawekezaji kuwekeza viwanda vya kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya misitu. Hata hivyo, ili kuwa na uwekezaji endelevu katika sekta ya misitu, inashauriwa kuendelea na usimamizi na kuongeza mashamba mapya ya miti katika mikoa hiyo.

109. Mheshimiwa Spika, Taasisi imefanya utafiti wa kutambua aina na kiwango cha miti inayotumika kama miti dawa kwa mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mwanza, Mara na Kagera. Matokeo ya utafiti yamebainisha uwepo wa aina (spishi) tano (5) za miti inayotumika kama miti dawa katika mikoa hiyo. Aina ya miti hiyo ni Nengonengo (*Securidaca longipenduculata*), Ng'watya (*Zahna africana*), Msana (*Combretum zeyheri*), Mlungulungu (*Zantoxylum chalybeum*) na Mzima (*Terminalia sericea*). Spishi hizi za miti hutumika kutibu magonjwa mbalimbali yakiwemo athma, homa kali, magonjwa ya zinaa, matatizo ya tumbo, matatizo ya kibofu cha mkojo, upungufu wa damu na matatizo ya njia ya mfumo wa upumuaji. Hata hivyo, uwepo na mtawanyiko wa spishi hizi hutofautiana kati ya spishi moja (1) na nyingine. Aidha, TAFORI kwa kushirikiana na wadau wengine wa sekta ya misitu imetengeneza teknolojia ya kuoanisha aina za miti na maeneo ya kupanda (Site - Species Matching Tool, SSMT) kwa ajili ya kurahisisha upandaji wa miti nchini ikiwa ni njia ya kusaidia mkulima kutambua aina ya miti na mahali inapostahili kupandwa. Ili kuhakikisha uwepo endelevu wa aina ya miti hii muhimu, Wizara itaendelea kuelimisha jamii na kuanzisha programu maalum ya kutunza na kuendeleza miti dawa.

4.5.2.5 Vyuvo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki

110. Mheshimiwa Spika, Vyuvo vya taaluma ya misitu na ufugaji nyuki vinajumuisha Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki (BTI); Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI) na Chuo cha Misitu

Olmotonyi (FTI). Vyuo hivi vimepewa jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wanafunzi 378 pamoja na kutoa elimu ya ufugaji nyuki wenye tija kwa wafugaji nyuki 130 katika wilaya za Sikonge, Mlele na Mpanda. Aidha, Chuo kimeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia kwa kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki, kukarabati jengo la utawala na kuanza ujenzi wa karakana ya kufundishia. Vilevile, Chuo cha Viwanda vya Misitu kimedahili wanafunzi 286, kuendesha programu ya mafunzo kazini kwa wahitimu 20 katika viwanda vitano (5) vya kuchakata magogo katika mikoa ya Iringa na Njombe; na kukarabati bwalo la chakula la wanafunzi. Katika hatua ya kuendelea kusogeza huduma kwa jamii, Chuo kimepata eneo lenye ukubwa wa hekta 150 katika eneo la Shamba la Miti Sao Hill kwa ajili ya kuanzisha Kampasi. Pia, Chuo cha Misitu Olmotonyi kimedahili wanafunzi 892 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Sambamba na hilo, Chuo kimeanza zoezi la mapitio ya mitaala ya kozi tano (5) ambapo kazi hii itakamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2022.

4.5.2.6 Mfuko wa Misitu Tanzania - TaFF

111. *Mheshimiwa Spika*, Mfuko una jukumu la kuwezesha shughuli za uhifadhi, usimamizi na uendelezaji rasilimali za misitu. Katika kuendeleza jitihada za kuongoa maeneo yaliyoharibiwa, Mfuko umetoa ruzuku kwa miradi 60 inayoendelea na miradi mipya 63 ya uanzishaji wa vitalu vya miti na upandaji miti shuleni katika wilaya 36 za mikoa nane (8) inayopatikana katika maeneo ya Nyanda Kame ikiwemo Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu na Manyara. Pia, Mfuko umetoa ruzuku maalum kwa miradi minne (4) inayotekelezwa na Taasisi za Serikali ambapo miradi mitatu (3) inahusu uanzishaji na uendelezaji wa mashamba ya miti ya kupandwa katika mikoa ya Kigoma na Morogoro; na mradi mmoja (1) ni ujenzi wa kituo cha kukusanya mazao ya nyuki katika Wilaya ya Mlele. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mfuko umegharamia ununuzi wa mashine za kuchakata na

kufungasha mazao ya nyuki kwa ajili ya viwanda vinne (4) katika Halmashauri za Wilaya ya Kibondo, Bukombe, Sikonge na Mlele. Vilevile, Mfuko umetoa ruzuku kwa miradi 12 ya uhifadhi na uendelezaji misitu na miradi 92 ya ufugaji nyuki inayoendelea kutekelezwa na wadau.

112. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande mwingine, Mfuko umetoa ruzuku kwa miradi 11 ya ufugaji nyuki kwa vikundi 40 vya vijana na wanawake katika mkoa ya Kigoma, Tabora, Songwe, Lindi, Katavi, Mbeya na Morogoro. Aidha, Mfuko umewezesha Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa masuala ya Misitu na Kamati ya Kitaifa ya Ushauri ya Ufugaji Nyuki kutekeleza majukumu yake. Kwa kuzingatia jitihada hizo, Mfuko uliweza kupata tuzo ya Taifa ya utendaji bora ya mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa kuwa mshindi wa pili kitaifa kati ya mifuko 21 iliyoshindanishwa.

4.5.3 Sekta ya Utalii

113. *Mheshimiwa Spika*, Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii nchini. Utekelezaji wa jukumu hilo unaongozwa na Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999, usimamiaji wa Sheria ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008 na Sheria ya Bodi ya Utalii Tanzania Sura 364. Vilevile, jukumu hilo hutekelezwa kupitia Idara ya Utalii, Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT).

4.5.3.1 Suala Mahsus katika Sekta ya Utalii

(i) Kukuza Utalii wa Mikutano na Matukio

114. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendeleza juhudi za kukuza utalii na kuimarisha uhifadhi, Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki iliandaa Onesho la Kwanza la Kimataifa la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki lililofanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 09 hadi 16 Oktoba, 2021. Onesho hilo lilijumuisha waoneshaji 185 kutoka nchi mbalimbali na wanunuzi wa kimataifa 41 kutoka nchi 22 ndani na nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, pamoja na onesho hilo kufanyika katika kipindi cha UVIKO-19, jumla ya wageni 2,733

walishiriki na wadau kutoka maeneo mbalimbali duniani walipata fursa ya kufuatilia makongamano ya kitaalamu kwa njia ya mtandao.

115. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara ilishiriki Mkutano wa 64 wa Shirika la Utalii Duniani - Kamisheni ya Kanda ya Afrika (64th UNWTO Commission For Africa - CAF) uliofanyika kuanzia tarehe 02 hadi 04 Septemba, 2021 katika Kisiwa cha Cabo Verde, ambapo Tanzania ilichaguliwa kwa mara ya kwanza kuwa Mwenyeji wa Mkutano ujao wa 65 wa UNWTO - CAF. Mkutano huo utafanyika Jijini Arusha tarehe 05 hadi 07 Oktoba, 2022 na maudhui yake ni kujenga upya utalii stahimilivu wa Afrika kwa maendeleo jumishi ya kijamii na kiuchumi yaani *Rebuilding Africa's Tourism Resilience for Inclusive Socio-Economic Development*.

4.5.3.2 Idara ya Utalii

116. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya biashara ya utalii nchini, Wizara imefanya mapitio ya Sheria ya Utalii Sura 365 na kutangaza maboresho kupitia Tangazo la Serikali Na. 41 la mwaka 2021. Maboresho hayo yamewezesha kuondoa mamlaka ya Bodi ya Leseni katika kutoa leseni za wakala wa biashara za utalii nchini ambazo kwa sasa zinatolewa kupitia mfumo wa kielektroniki wa *MNRT Portal*. Hatua hiyo imeongeza tija katika utoaji huduma ikiwemo kurahisisha mchakato wa utoaji wa leseni za biashara za utalii na hivyo kupunguza gharama, muda na kuongeza wigo wa ushiriki wa wananchi na wawekezaji mbalimbali katika biashara hizo.

117. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli, Wizara imefanya kaguzi za biashara za utalii katika maeneo mbalimbali nchini. Maeneo hayo ni pamoja na: malango ya kuingilia wageni katika hifadhi za Taifa za Tarangire, Ruaha, Mikumi na Ziwa Manyara; na Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ambapo jumla ya Shilingi 994,593,250.00 zimekusanywa kutokana na kaguzi hizo. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi - Dawati la Utalii na Diplomasia kubaini na kuwachukuliwa hatua

wafanyabiashara wa utalii wasiofuata sheria, kanuni na taratibu za kuendesha shughuli hizo.

118. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusajili wakala wapya wa biashara za utalii nchini ambapo hadi kufikia Aprili, 2022 jumla ya wakala wapya 252 wamesajiliwa. Aidha, Wizara imetambua na kuhakiki huduma za malazi katika mikoa 26 Tanzania bara ambapo imeongeza idadi ya huduma zilizopaswa kukusanya tozo ya kitanda siku kutoka 1,815 mwaka 2020 hadi 8,681 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 378. Sambamba na hilo, Wizara imepanga huduma za malazi nne (4) katika daraja za ubora wa nyota zilizopo katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Pwani na Kigoma. Vilevile, Wizara imeimarisha mfumo wa kielektroniki wa kupanga huduma za malazi katika viwango vya ubora wa nyota - *AserT* unaowezesha watoahuduma za malazi kujitathmini wenyewe kabla ya huduma zao kupangwa katika daraja za ubora. Lengo ni kuhakikisha huduma hizo zinakuwa na ubora unaostahili pamoja na kukidhi mahitaji ya soko la utalii.

119. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati, Wizara imepata eneo lenye ukubwa wa ekari 22.44 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Utalii wa Mikutano na Matukio katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, Jijini Dar es Salaam. Aidha, Wizara imepokea nyaraka za umiliki pamoja na ramani za eneo hilo. Hatua inayoendelea ni kumpata Mtaalam Elekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa mradi. Katika kuendeleza zao la utalii wa fukwe nchini, Wizara imebaini maeneo yenye fursa za uwekezaji wa shughuli za utalii pembezoni mwa Bahari ya Hindi katika mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Lindi na Mtwara. Lengo ni kuyasajili maeneo hayo kama Kanda Maalum za Kiuchumi za Utalii kupitia Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje - EPZA. Aidha, Wizara ilifanya mkutano na wadau Jijini Dar es Salaam mwezi Februari, 2022 kwa lengo la kujadili uendelezaji wa maeneo hayo. Hatua hii itachochea ukuaji na uendelezaji wa shughuli za utalii wa fukwe, meli na michezo ya kwenye maji katika maeneo ya fukwe nchini.

120. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau wa utalii nchini ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilifanya jumla ya vikao sita (6) Jijini Arusha. Vikao hivyo vilihusisha vyama mbalimbali vya wadau katika sekta ikiwemo TATO, TLTO, TCT, TTGA, HAT na TPSF. Miongoni mwa masuala muhimu yaliyojadiliwa kupitia vikao hivyo ni pamoja na fursa za uwekezaji, utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta na uendelezaji na utangazaji wa mazao ya utalii nchini.

4.5.3.3 Bodi ya Utalii Tanzania - TTB

121. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Utalii ina jukumu la kutangaza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Bodi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeratibu ushiriki wa Tanzania katika maonesho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Maonesho hayo ni pamoja na *FITUR 2022 na InvesTour* ya nchini Uhispania; *National Tour Association Annual Convention (NTA Travel/Exchange)*, nchini Marekani; *road show* iliyohusisha nchi za Ujerumani, Austria, Switzerland, Sweden na Denmark; na *Africa Tourism Leadership Forum 2021*, nchini Rwanda. Aidha, Bodi iliratibu ushiriki wa Wizara katika onesho la dunia la *Expo 2020 Dubai*, Umoja wa Falme za Kiarabu, na uzinduzi wa Programu ya *The Royal Tour*. Katika onesho hilo, nchi yetu ilipewa heshima ya pekee ya kuwa na siku maalum ambapo mnara maarufu duniani wa *Burj Khalifa* ulipambwa kwa rangi za bendera ya Tanzania; na vivutio vya utalii vilivyopo nchini vilioneshwa mubashara.

122. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza jitihada za kutangaza vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji nchini, Bodi iliandaa ziara za mafunzo (FAM - trips) tisa (9) zenye jumla ya washiriki 66 kutoka makundi ya wakala wa biashara za utalii, wawekezaji, waandishi wa habari na watu mashuhuri. Wageni hao walitoka katika nchi 23 zikiwemo Algeria (4), Marekani (24), Poland (3), Georgia (8), Canada (5), Nigeria (1), Macedonia (3) na Qatar (18) na kutembelea vivutio mbalimbali nchini ikiwemo hifadhi za Taifa Serengeti na Ziwa Manyara; Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; na Zanzibar. Aidha,

Bodi imeendelea kusambaza nyenzo za kutangaza utalii na kufanya vikao na wakala wa biashara za utalii pamoja na mabalozi wa nchi mbalimbali zikiwemo Marekani, China, Urusi, Ufaransa, Uingereza, Ubelgiji, Israel, Qatar, Kuwait, Sweden, India, Japan, Afrika Kusini, Nigeria, Namibia, Algeria na Rwanda. Juhudi hizo zinalenga kuvutia makundi mbalimbali ya watalii na wawekezaji kutembelea nchini. Mathalan, Tanzania imepokea makundi sita (6) yenye jumla ya watalii 1,924 kwa pamoja kutoka nchi ya Israel.

123. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua fursa mbalimbali za kuwatumia mabalozi wa hiari wa utalii, Bodi imekamilisha mwongozo wa vigezo vya kuchagua na kuainisha majukumu ya mabalozi. Aidha, Wizara imefanya uteuzi wa mabalozi mbalimbali wa hiari akiwemo Bwana Mamadou Sakho, Raia wa Ufaransa ambaye ni mchezaji wa mpira wa miguu wa kimataifa wa Ufaransa; Bi. Rawan Dakik, aliyeweka rekodi ya kuwa mwanamke Mtanzania wa kwanza kupanda na kufika kwenye kilele cha Milima Everest, ambao ni mrefu zaidi duniani; Mtoto Sharon Ringo ambaye pia amepewa heshima ya kuwa Balozi wa Utalii katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; na Bi. Isabella Mwampamba ambaye amekuwa akifanya shughuli mbalimbali za kuhamasisha na kutangaza utalii.

124. Mheshimiwa Spika, Bodi imeendelea kutumia teknolojia mbalimbali katika kutangaza utalii ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza hilo, Bodi inatumia Kituo cha Kielektroniki cha Kutoa Habari (*Digital Command Centre*) ambacho hutangaza na kufuatilia mwenendo wa masuala ya utalii wa Tanzania katika mitandao ya kijamii ya *Facebook*, *Twitter*, *Instagram* na *YouTube*, *Search Engine Optimization (SEO)*, *Email marketing*, *Affiliate Marketing*, *Online Reputation Management (ORM)* na *WebPR*. Katika hatua nyingine, Wizara imeendelea kuhamasisha utalii wa ndani kupitia matamasha na matukio mbalimbali yakiwemo: *Kili Marathon 2022*; *Rock City Marathon*; *Serengeti Marathon*; *Burigi-Chato Marathon*; *Tabora Marathon*; *Majimaji Serebuka*; *Majimaji Festival*; *Bagamoyo Cultural Festival – TaSuBa*; *Dodoma Wine Festival*; *Maonesho ya Utalii Mkoani Tanga*; *Senene Festival*; *Arusha Marathon*; *Zinj Day*; *East Africa Trade Fair*; *Siku ya Utalii*

Duniani 2022; Maonesho ya Biashara - Chato; Mbeya Tulia Marathon 2022; Karibu Dodoma Festival; Karibu Kilifair Summit; na Maonesho ya Biashara na Utalii ya Afrika Mashariki - Mwanza. Matamasha na maonesho hayo yametoa fursa mbalimbali za kutangaza utalii na kuendeleza wigo wa mazao ya utalii nchini.

125. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kutangaza mazao la utalii, Bodi imeratibu ushiriki wa Wizara katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba) ambapo vivutio vya utalii vimetangazwa na elimu ya uhifadhi imetolewa. Kwa upande mwingine, Bodi imeendelea kuimarisha vituo vya kutolea taarifa za utalii katika Kanda kwa kuwapatia nyenzo za kutangaza utalii. Vilevile, Bodi imeendelea kushirikiana na vyombo mbalimbali vya habari kwa ajili ya kutangaza utalii.

4.5.3.4 Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT

126. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Utalii kimepewa jukumu la kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada katika fani ya utalii, ukarimu na uratibu wa matukio. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,127 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimekarabati miundombinu ya kutolea mafunzo katika kampasi za Bustani, Arusha na Temeke; na kununua na kusimika mifumo ya TEHAMA, vitendea kazi na vifaa mbalimbali vya kutolea mafunzo na kujifunzia katika kampasi za Mwanza, Temeke, Bustani na Arusha. Vilevile, Chuo kimenunua eneo lenye jumla ya ekari 32.2 kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mwanza. Katika kuboresha mafunzo ili kuendana na mahitaji ya soko, Chuo kimefanya mapitio ya mitaala tisa (9) na kuandaa mitaala mipya minne (4) katika fani za ukarimu na utalii. Katika hatua nyingine, Chuo kimeanza kuongezeka majengo ya mafunzo katika Kampasi ya Arusha. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kufanya Tathmini ya Mazingira na Athari za Kijamii, kuandaa michoro ya majengo yanayotarajiwa kujengwa kwa kushirikiana na Chuo cha Ufundi - Arusha.

127. Mheshimiwa Spika, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo kwa kutekeleza programu za kimkakati za kukuza ujuzi ikijumuisha Uanagenzi na Utarajali. Katika kutekeleza hilo, mafunzo ya uanagenzi yametolewa kwa washiriki 216; na mafunzo ya Utarajali (Internship Program) kwa wahitimu 135. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau 220 katika mnyororo wa utalii. Vilevile, Chuo kimefanya utafiti na kutoa ushauri kuhusu namna ya uendeshaji wa hoteli zinazomilikiwa na Mfuko wa Taifa la Hifadhi za Jamii (NSSF). Katika hatua nyingine, Chuo kimetoa mafunzo kwa wataalam 44 wa Sekta ya Umma na Binafsi ya kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora wa nyota (hotel assessors). Vilevile, Chuo kimetoa mafunzo maalum kwa watoa huduma 1,072 kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya, Mwanza na Mara ili kuwajengea uwezo na kuimarisha ubunifu wa huduma.

4.5.4 Sekta ya Mambo ya Kale

128. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za malikale na urithi wa utamaduni. Sekta hii inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera ya Malikale ya mwaka 2008; Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281. Sekta ya malikale inajumuisha Idara ya Mambo ya Kale na Shirika la Makumbusho ya Taifa (NMT).

4.5.4.1 Suala Mahsusi katika Sekta ya Mambo Kale

Kuenzi falsafa za Baba wa Taifa Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere

129. Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuenzi falsafa za Baba wa Taifa, Wizara imezindua Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mpango huu unalenga kuweka utaratibu endelevu utakaohakikisha kuwa urithi na falsafa za Mwalimu Nyerere zinaenziwa, kuhifadhiwa na kuendelezwa. Katika kutekeleza mpango huo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeratibu Adhimisho la Kumbukizi ya miaka 100 tangu

kuzaliwa kwa Mwl. Nyerere lililofanyika Mwitongo, Butiama – Mkoa wa Mara tarehe 13 Aprili, 2022. Tamasha hilo lilihusisha matukio mbalimbali yakiwemo msafara wa mbio za baiskeli za *Twende Butiama* kutoka Msasani, Dar es Salaam hadi Mwitongo, Butiama; programu za kielimu kuhusu Urithi wa Mwalimu Nyerere kwa wanafunzi wa sekondari na shule za msingi; midahalo na makongamano, maonesho maalum ya sekta mbalimbali kuhusu mchango wa Mwalimu Nyerere, uzinduzi wa nembo maalum ya miaka 100 ya Mwalimu Nyerere; matembezi ya miguu kwa vijana kutoka Mwanza hadi Butiama pamoja na sanaa za jukwaani. Pia, jamii ilishiriki katika kuenzi falsafa za Mwl. Nyerere kwa kupanda miti na kushiriki katika maonesho ya bidhaa za utalii na utamaduni.

4.5.4.2 Idara ya Mambo ya Kale

130. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha malikale na urithi wa utamaduni vinalindwa, Wizara imekamilisha rasimu ya marekebisho madogo ya Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho Sura 281 na kuwasilisha kwenye Mamlaka husika kwa hatua zaidi. Aidha, Wizara imekamilisha zoezi la kutafsiri Sheria hizo kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kutoa uelewa kwa Umma.

131. *Mheshimiwa Spika*, ili kuimarisha uhifadhi katika maeneo ya malikale, Wizara imehakiki na kupima mipaka katika vituo vya: Magofu ya Kunduchi, Dar es Salaam; Mapango ya Amboni na Magofu ya Tongoni, Tanga; Tembe la Kwihara, Tabora; Makumbusho ya Kumbukizi ya Mkwawa - Kalenga, Iringa; Makumbusho ya Kumbukizi ya Dkt. Livingstone Ujiji, Kigoma; na Makumbusho ya *Dkt. Rashid Mfaume Kawawa*, Songea. Kufuatia hatua hiyo, Makumbusho ya Mkwawa Kalenga, Iringa imepata hati miliki ya ardhi. Aidha, taratibu za upatikanaji wa hati kwa maeneo mengine zinaendelea.

132. *Mheshimiwa Spika*, katika kuendelea kuhifadhi urithi wa historia ya nchi na kutangaza utalii, Wizara imekusanya taarifa ya maeneo mbalimbali ya kihistoria ikiwemo: jengo la iliyokuwa Kamati ya Ukombozi ya Bara la Afrika lililopo Dar

es Salaam; makambi ya wapigania uhuru ya Masonya Ruvuma, Dakawa na Mazimbu Morogoro na Kongwa Dodoma; kituo cha redio Tanzania (RTD) kilichotumika kurusha matangazo wakati wa harakati za ukombozi wa nchi za kusini mwa Bara la Afrika; na Chuo cha Diplomasia Dar es Salaam kilichotumika kutoa mafunzo ya wapigania uhuru. Maeneo mengine ni pamoja na eneo lenye asili ya Mkoa wa Dodoma lililopo Kikuyu, Mapango ya Nang'oma ya Kipatimo Lindi na Mji wa Kihistoria Pangani. Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kutoa vibali 10 kwa watafiti wa ndani na nje kwa ajili ya kufanya utafiti wa malikale katika maeneo mbalimbali yakiwemo Tendaguru, Bonde la Olduvai, Ziwa Eyasi, Kilwa na Isimila. Tafiti hizi zinasaidia kubaini maeneo ya malikale yenye sifa za kutangazwa kuwa Urithi wa Taifa.

4.5.4.3 Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania – NMT

133. *Mheshimiwa Spika*, katika kuimarisha utekelezaji wa shughuli za Makumbusho, Shirika limeandaa sera ya ndani inayotoa mwongozo wa utafiti, ukusanyaji, uhifadhi na utoaji elimu kwa wadau juu ya urithi wa Taifa. Aidha, katika kuhakikisha mila na tamaduni za Watanzania zinaendelea kuhifadhiwa, Shirika limekusanya mikusanyo 54 kutoka kwa jamii ya watu wa Songea na mikusanyo 25 kutoka kwa jamii ya watu wa Rukwa. Vilevile, Shirika limekusanya mikusanyo na taarifa kutoka taasisi mbalimbali ikiwemo Idara ya Maelezo na Shirika la Habari Tanzania (TBC). Pia, zoezi la ukusanyaji wa taarifa za kumbukumbu za Marais wastaafu linaendelea ambapo Hotuba 79 zinazohusu ukombozi, maendeleo, uchumi, utamaduni na siasa zimekusanywa. Aidha, Kitabu cha wasifu wa Hayati Benjamini Mkapa; picha za Marais; na vifaa mbalimbali vimekusanywa na kuhifadhiwa. Kwa upande mwingine, Shirika limetengeneza mfumo wa kidigitali wa kusajili na kuhifadhi mikusanyo na limejiunga na *Datasaver* ya *National Internet Data Center* (NIDC) ili kuhifadhi taarifa za mikusanyo kwa usalama zaidi. Katika hatua nyingine, Shirika kwa kushirikiana na *Goethe Institut* limewajengea uwezo watumishi 24 kuhusu uhifadhi wa mikusanyo kidijitali. Aidha, Shirika limeweka onesho la kudumu la tembo katika Makumbusho ya Elimu Viumbe – Arusha; na

usimikaji wa taswira za wanyamapori wakiwemo nyati, tembo, twiga, faru na kiboko. Kwa upande mwingine, Shirika limefanikiwa kupata Kiwanja hekari 19 katika eneo la Mkonze, Dodoma ambapo jengo la Makumbusho ya Marais litajengwa.

134. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utendaji kazi kwenye vituo vya malikale na makumbusho, Shirika limefanya ukarabati wa jengo la kihistoria la soko la watumwa na kufungua ofisi katika Mji Mkongwe Mikindani. Aidha, Shirika limeanza kusimamia na kuendesha Kituo cha Makumbusho ya *Dkt. Rashid Mfaume Kawawa*. Sambamba na hatua hizi, Shirika limeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu makumbusho na urithi wa utamaduni kwa kuandaa na kurusha vipindi 24 vya redio, 52 vya televisheni na matangazo 40 kwenye mitandao ya kijamii. Vilevile, Shirika limeendelea na kampeni ya *Twenzetu Makumbusho* na programu za *KijijiSoko*, *Museum Art Explosion* na *Mkole* kwa lengo la kuendelea kuhamasisha jamii kuhifadhi na kuendeleza tamaduni zetu. Pia, Shirika limefanya warsha iliyowahusisha wahariri 20 kutoka vyombo vya habari 10 na ya wadau wa elimu ya sekondari jijini Dar es Salaam. Aidha, Shirika limeendesha programu 40 za uelimishaji katika maeneo ya Madaba, Tunduru na Songea; na kuanzisha klabu 35 za historia na uzalendo katika mikoja ya Tanga na Morogoro.

135. Mheshimiwa Spika, Shirika limefanya utafiti wa tafsiri ya malikale zinazohusiana na biashara ya utumwa huko Mikindani (Mtwara) na Pangani (Tanga) na utafiti wa masoko ya utalii wa Makumbusho Tanzania. Aidha, mikusanyo 1,290 ya akiolojia imekusanywa kutokana na utafiti uliofanyika eneo la Laetoli lenye nyayo za Zamadamu. Kupitia tafiti hizo, jumla ya machapisho sita (6) yamezalishwa ikiwemo kitabu kinachoainisha na kuchambua Makumbusho zilizopo nchini. Machapisho hayo yametoa ushauri na mapendekezo ya namna ya kuhifadhi mikusanyo na maeneo ya malikale. Sambamba na hilo, Shirika limefanya utafiti kwa kukusanya vipepeo 5,361 katika eneo la Usambara Mashariki kwa lengo la kubaini umuhimu wake na namna ya kuhifadhi. Matokeo yanaonesha uwepo wa familia nne (4) zenye jumla ya spishi

110 ambazo zinachangia katika uchavushaji wa mimea na utunzaji wa mazingira. Kupitia matokeo hayo, Shirika limeanzisha bustani za vipepeo kwa ajili ya kuhifadhi na kutoa elimu kwa jamii. Aidha, tafiti kuhusu masalia ya mji wa dinosaria katika eneo la Tendaguru zimeendelea kufanyika kwa kushirikiana na chuo kikuu cha Dar es Salaam na Makumbusho ya Elimu Viumbe ya Ujerumani, ambapo masalia ya mji huyu yameendelea kupatikana. Sambamba na hilo, utafiti umefanyika wa kuainisha thamani ya kiutamaduni ya eneo hilo kwa lengo la kuandaa mpango wa usimamizi na uhifadhi.

4.5.4.4 Mfuko wa Mambo ya Kale

136. *Mheshimiwa Spika*, Mfuko huu ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 kwa lengo la kutekeleza majukumu ya uhifadhi na utafiti wa malikale. Katika mwaka 2021/2022, Mfuko umewezesha maandalizi ya Mpango wa miaka 10 wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Vilevile, Mfuko umewezesha ukarabati wa jengo alilofikia Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wakati wa kudai uhuru lililopo Manispaa ya Mikindani, Mtwara; kuandaa mpango mkakati wa miaka mitano (2021/2022 hadi 2025/2026) wa Mfuko wa Mambo ya Kale; kufanya tathmini ya Sera ya Malikale ya 2008; na kuwezesha uandaji wa rasimu ya uwekezaji katika maeneo ya malikale.

4.6 Miradi ya Maendeleo

137. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka 2021/2022, Wizara ilitengewa jumla ya **Shilingi 152,772,880,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara na Taasisi. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi 113,893,184,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 38,879,696,000.00** fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2022 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 59,481,316,267.20** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **Shilingi 33,567,915,783.20** ni fedha za ndani na **Shilingi 25,913,400,484.00** ni fedha za nje. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Idara za Wizara ni kama ifuatavyo:-

(i) **Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth - REGROW)**

138. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, **Shilingi 33,701,696,000.00** ziliidhinishwa. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa mitambo nane (8) kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Hifadhi ya Taifa Nyerere na kukamilisha taratibu za ununuzi wa malori 17, boti za upepo (airboat) mbili (2) na magari mawili (2) ya kuoneshea sinema. Kazi nyingine ni kufanya usanifu na tathmini ya athari za kimazingira kwa ajili ya ujenzi wa barabara (km 2,051); njia za utalii wa miguu (km 132.5) majengo (80); madaraja na viwanja vya ndege 14 katika hifadhi za Taifa Mikumi, Ruaha, Nyerere na Udzungwa; na Hifadhi ya Msitu wa Mazingira Asilia Kilombero.

139. **Mheshimiwa Spika**, katika kutangaza utalii, Wizara imeandaa mkakati wa kutangaza utalii kusini, mwongozo wa mafunzo ya utalii wa nyuki (Api-tourism) na kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha Utafiti wa Wanyamapori, Iringa. Aidha, Wizara imefanya utafiti wa wanyamapori na kukusanya takwimu za mtawanyiko wa wanyamapori katika hifadhi za Taifa Nyerere na Ruaha. Vilevile, miongozo ya kushughulikia migogoro baina ya wanyamapori na binadamu imefanyiwa mapitio; mafunzo ya utalii wa nyuki na matumizi bora ya ardhi yametolewa katika hifadhi za Taifa Nyerere na Ruaha.

140. **Mheshimiwa Spika**, shughuli nyingine zilizofanyika ni uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi kwa jamii zinazopatikana katika eneo la mradi kwa lengo la kuimarisha uhifadhi na kuwaongezea kipato. Aidha, Wizara imetoa mafunzo ya maendeleo ya jamii na usimamizi wa ushirika kwa watumishi 18 wa mradi, wawezeshaji wa jamii 15, maafisa watendaji wa vijiji 15 na wasimamizi saba (7) wa wilaya za Chamwino, Iringa, Kilolo, Morogoro, Mvomero, Kilosa na Ifakara zinazotekeleza mradi. Kwa upande mwingine, skimu ya umwagiliaji ya majaribio ya Madibira imeendelea

kuboreshwa; na ujenzi na ufungaji wa miundombinu ya kupimia maji na utandazaji wa mifereji unaendelea.

(ii) Mradi wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (Support to Combating Wildlife Crime and Advancing Conservation)

141. Mheshimiwa Spika, Mradi unatekelezwa na Wizara kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira wa Kimataifa (Global Environmental Facility - GEF) na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (United Nations Development Programme - UNDP). Kwa mwaka 2021/2022, Mradi uliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 2,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali zikiwemo: kutoa mafunzo ya mbinu za kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya nyara kwa watumishi 110 kutoka Kikosi Kazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili (NTAP) na Kanda 10 za Kiikolojia za Kupambana na Ujangili (TCG); na kuandaa Mwongozo wa Utendaji wa Kikosi Kazi cha Taifa Dhidi ya Ujangili. Kazi nyingine ni kufanya tathmini ya uwezo na mahitaji ya NTAP na TCG; kuondoa vifaa vya mawasiliano (GPS Collars) kwa tembo 16 katika ikolojia ya Ruaha - Rungwa; kuwezesha doria za kiintelijinsia katika ikolojia ya Ruaha – Rungwa; kuhuisha Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara; na ununuzi wa magari 10 kwa ajili ya TCGs.

(iii) Mradi wa Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania)

142. Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatekelezwa kwa ubia baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Ufini. Kwa mwaka 2021/2022, Mradi uliidhinishiwa **Shilingi 328,000,000.00**. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kuwezesha vikundi 64 vya wakulima wa miti wapatao 3,995 kusajiliwa katika ngazi ya wilaya na kuwezesha mikutano 26 katika ngazi ya kijiji na kuvijengea uwezo; kutoa huduma za ugani kwa vikundi 80 vya wakulima wa miti ili kuviimarisha viweze kutoa huduma kwa wanachama wake wapatao 9,662; na kuwezesha utunzaji wa mashamba 15 ya mbegu bora za miti. Sambamba na hilo, viongozi wa vikundi vya wapanda miti na wakulima wa miti 327 wamepatiwa

mafunzo ya uanzishaji, upandaji na utunzaji wa miche katika vitalu vya miti.

143. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika ni kukusanya taarifa za mashamba ya miti 1,557 yenye jumla ya eneo la hekta 1,188.98 yanayomilikiwa na wakulima 1,324; na kuandaa mipango 1,206 ya namna ya kutunza mashamba ya miti. Aidha, mashamba darasa 56 yameanzishwa; kuwezesha utoaji wa hati miliki za kimila za mashamba ya miti 869 katika kijiji cha Ibaga; na kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi 12 katika vijiji 12 katika wilaya za Njombe (2), Ludewa (4), Mufindi (4) na kilolo (2). Katika hatua nyingine, mafunzo ya kupambana na moto kichaa yametolewa kwa wasimamizi 42; kuwezesha ununuzi wa pikipiki 19 kwa ajili ya maafisa ugani wa halmashauri; na kuwezesha wajasiriamali 674 wadogo na wakati kushiriki katika mafunzo ya uchakataji magogo na wajasiriamali zaidi ya 180 kuhusu namna ya kuandaa mipango ya biashara.

144. Mheshimiwa Spika, Wizara imenunua mashine na vifaa maalum kwa ajili ya kutoa elimu kwa vitendo kwa mfumo wa darasa linalotembea (mobile training unit); na kuboresha miundombinu ya kufundishia katika Kituo cha Mafunzo ya Misitu na Viwanda vya Misitu (FWITC), Mjini Mafinga. Kwa upande mwingine, Wizara imewezesha uandaaji wa maandiko ya mradi pamoja na kuchapisha nakala 9,000 za Mwongozo kuhusu usimamizi na utunzaji wa mashamba ya miti. Vilevile, Wizara imewezesha utafiti wa uzalishaji wa mkaa mbadala; kuwezesha maonesho ya uwekezaji katika sekta ya Misitu yaliyofanyika Mkoa wa Iringa, mwezi Novemba 2021; na kuwezesha uandaaji wa andiko la kuimarisha vituo vya mafunzo vya FITI, FTI na FWITC.

(iv) Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu (Forestry and Value Chain Development Programme (FORVAC))

145. Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Tanzania na Ufini. Katika mwaka 2021/2022, jumla ya **Shilingi 2,000,000,000.00**

ziliidhinishwa. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuandaa na kuidhinisha mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 29; na kutenga eneo lenye jumla ya hekta 123,462 za misitu. Aidha, Wizara imenunua sare 432 na pikipiki 20 kwa ajili ya wanakamati wa maliasili wa vijiji katika vijiji 25 viliyoko katika kongani za Tanga, Lindi na Ruvuma; na ununuzi wa pikipiki 16 kwa Halmashauri za wilaya kwa ajili ya maafisa misitu na maafisa nyuki wilaya. Katika hatua nyingine, Wizara imeandaa Mipango ya Usimamizi ya misitu ya vijiji 30 katika eneo la misitu ya vijiji la hekta 269,024; kutangaza kisheria Misitu ya Hifadhi ya vijiji 16 yenye hekta 146,064 katika Tangazo la Serikali Na. 454 la mwaka 2021; na kuandaa mipango ya uvunaji endelevu wa misitu 40 ya vijiji. Sambamba na hilo, Wizara imeanzisha viwanda vinavyotembea vya kuchakata magogo (mobile sawmills) katika wilaya za Ruangwa na Songea; kununua mitambo ya kukausha mbao kwa kutumia nishati ya jua kwa wilaya za Liwale na Ruangwa; kufadhili miradi ya biashara 60 za wajasiriamali wadogo wadogo 630; na kutoa mizinga 1,592 katika wilaya za Handeni, Mbinga na Liwale.

146. Mheshimiwa Spika, Wizara imeanzisha vikundi 19 vya kukopeshana na kuweka akiba vyenye wanachama 801 katika kongani za Tanga, Lindi na Ruvuma; na kupanda miche ya miti 553,620 kwenye hekta 470 katika vijiji vya Mkali A, Mkali B, Liuli na Lipingo katika Wilaya ya Nyasa. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kuhusu dhima na majukumu ya Serikali za Vijiji na Kamati za Maliasili, ufugaji na uchakataji wa mazao ya nyuki kwa viongozi, wataalam wa ngazi ya wilaya na vijiji katika mikoa ya Lindi, Ruvuma na Tanga. Vilevile, vijiji vitano (5) vya Chiseyo, Ikuyu na Litemo (Mpwapwa), Mnkonde (Kilindi) na kwamwande (Handeni) vimewezeshwa kutenga hifadhi za nyuki za vijiji zenye jumla ya hekta 5,069.73. Katika hatua nyingine, Wizara imewezesha uchapishaji wa nyaraka mbalimbali zikiwemo: mikakati ya utekelezaji wa Sera za Taifa za Misitu na Nyuki, Mkakati wa Mazao ya Mbao Yaliyohandisiwa (2021 - 2031) na Mpango kazi wake, Mwongozo wa Takwimu za uhalisia wa Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa misitu na Mwongozo wa Uanzishaji na Usimamizi wa Hifadhi za Nyuki na Manzuki Tanzania.

(v) **Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki – BEVAC**

147. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Jumuiya ya Umoja wa Ulaya. Katika mwaka 2021/2022, jumla ya **Shilingi 1,000,000,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali ikiwemo: kukamilisha taratibu za tathmini kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Maabara ya Utafiti wa Ufugaji Nyuki katika Kituo cha Utafiti wa Ufugaji Nyuki, Njiro - Arusha; na kukamilisha taratibu za ujenzi na maboresho ya miundombinu ya chuo hicho ikihusisha bweni, maktaba na maabara ya mafunzo. Kazi nyingine ni kufanyika kwa tathmini kuhusu mahitaji ya soko na mtazamo wa wanunuzi wa bidhaa za nyuki katika masoko ya kikanda ya Ulaya, Uingereza na Mashariki ya Kati. Aidha, tathmini imefanyika katika maeneo machache ya mradi kwa ajili ya kuelewa uwezo uliopo na kutambua wadau tarajali katika mnyororo wa thamani.

148. *Mheshimiwa Spika*, katika hatua nyingine, ukarabati wa ofisi kuu ya mradi iliyopo Tabora umefanyika; na kununua magari matatu (3), pikipiki 20, samani na vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya ofisi kuu ya uratibu wa mradi Tabora. Sambamba na hilo, vikao vitano (5) vya uratibu vilifanyika Tanzania bara (3) na Zanzibar (2); na warsha ya uzinduzi wa mradi ilifanyika. Kwa upande mwingine, mafunzo yametolewa kwa mashirika mawili (2) ya *Api – Support* na *Honey Exporters Association* yanayojihusisha na biashara ya mazao ya nyuki. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uwezo wa mashirika kwa ajili ya kuanzisha kamati ya utetezi wa maslahi ya biashara na sera za biashara katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

4.7 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Athari za UVIKO-19

149. *Mheshimiwa Spika*, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19. Katika kutekeleza mpango huo, Wizara ya Maliasili na Utalii iliidhinishwa jumla ya **Shilingi 90,202,345,530.00** Hadi kufikia

mwezi Aprili, 2022, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 83,037,216,335.51** sawa na **asilimia 92.1** ya fedha zilizoidhinishwa. Mpango huo unatekelezwa na Idara ya Utalii, Kitengo cha Utafiti na Mafunzo, Kitengo cha TEHAMA na taasisi za TANAPA, TAWA, NCAA, TFS, NMT, TTB, CAWM - MWEKA na NCT.

150. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango huu, Wizara inaendelea na ukarabati wa barabara ambapo jumla ya kilometa 1,164.3 kati ya kilometa 2,383.12 za barabara na vivuko viwili (2) vimekamilika katika maeneo yaliyohifadhiwa, ujenzi wa viwanja vya ndege (airstrips) vitano (5) na njia za kutembea kwa miguu zenye urefu wa kilomita 110. Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa madaraja matano (5), malango 12, vituo vya kutolea taarifa vitano (5), *campsite* nne (4), *picnic site* sita (6), ujenzi wa vyoo sita (6), vituo vitano (5) vya kukusanyia mapato na maeneo ya kutua helikopta (helipads) matano (5). Shughuli hizo zinatekelezwa katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; hifadhi za Taifa tisa (9), mapori ya akiba 10, mapori tengefu mawili (2), hifadhi za misitu ya mazingira asilia 11 na bustani ya wanyamapori moja (1). Maeneo hayo ni pamoja na: hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Gombe, Serengeti, Tarangire, Saadani, Mkomazi, Mahale, Nyerere na Katavi; mapori ya akiba Rungwa, Swagaswaga, Mkungunero, Kijereshi, Wami - Mbiki, Liparamba, Lukwika/Lumesule, Mpanga Kipengere, Igombe na Maswa; mapori tengefu Ziwa Natron na Kilombero; Bustani ya Wanyamapori ya Ruhila; na hifadhi za misitu ya mazingira asilia za Magamba, Pugu - Kazimzumbwi, Nilo, Chome, Essimingor, Mlima Hanang, Mlima Rungwe, Kalambo Falls, Uluguru, Amani na Matogoro.

151. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara inaendelea na ujenzi wa vituo vya taarifa vitatu (3) katika maeneo ya Tendaguru - Lindi, Lindi Manispaa na Kigamboni - Dar es Salaam. Aidha, Wizara imefanya ukarabati wa Jengo la Kihistoria la Watumwa, Mikindani; na magofu ya Kimbiji na Mbua Maji, Kigamboni - Dar es Salaam na Kua - Mafia. Vilevile, Wizara inaendelea na ujenzi wa onesho la tembo katika Kituo cha Elimu Viumbe, Arusha; na nyumba za asili za kaya tatu

(3) za jamii ya Wairaq, Wasukuma na Wazanaki katika Kijiji cha Makumbusho - Dar es Salaam. Vilevile, Wizara inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya vyoo katika Kituo cha Majimaji, Songea; na mfumo wa ulinzi katika makumbusho za Mwalimu Nyerere, Butiama na Elimu ya Viumbe, Arusha. Kwa upande mwingine, Wizara imekamilisha taratibu za manunuzi kwa ajili ya vitendea kazi mbalimbali vikiwemo: magari 10, malori 19, *wheel excavator* tano (5), *motor graders* sita (6), *water bowsers* sita (6), *compactors* tano (5), *low bed* nne (4), *back hoe loader* moja (1), *concrete mixer* moja (1), mahema 529, mtambo mmoja (1) maalum kwa ajili ya kuchimba visima vya maji na boti tatu (3).

152. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za utalii na kukabiliana na janga la UVIKO-19, Wizara imetoa mafunzo kwa wadau wa utalii 4,698 katika mikoa 26 nchini kuhusu miongozo ya kukabiliana na janga la UVIKO-19 pamoja na kutoa chanjo kwa hiari kwa wadau 354. Aidha, mafunzo kwa wataalam wa ndani ya kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora wa nyota (hotel assessors) yametolewa kwa wataalam 43 wa Serikali na Sekta Binafsi. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo maalum kwa watoa huduma 1,072 kutoka mikoa nane (8) ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya, Mwanza na Mara ili kuwajengea uwezo na kuimarisha ubunifu wa huduma. Katika hatua nyingine, Wizara imetoa mafunzo kwa waongoza watalii 1,060 ikijumuisha mafunzo maalum kwa wanawake 89. Mafunzo haya yalikusishwa waongoza watalii kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, Wizara imenunua vifaa kinga vya kukabiliana na UVIKO-19 ikiwemo vitakasa mikono 14,285 vyenye ujazo wa mililita 500 kila moja na barakoa makasha 50 yenye jumla ya barakoa 2,800 kwa ajili ya wadau wa utalii kupitia vyama vyao.

153. Mheshimiwa Spika, katika hatua za kutangaza utalii hasa katika masoko ya kimkakati, Wizara imeshiriki maonesho mawili (2) ya kimataifa ambayo ni *FITUR 2022 na Investour* nchini Uhispania na *Expo 2020 Dubai* katika Umoja wa Falme za Kiarabu. Aidha, programu endeshi (software) kwa ajili ya mfumo wa ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za utangazaji utalii

katika mitandao ya kijamii kupitia *Digital Command Centre* imenunuliwa. Katika hatua nyingine, Wizara kwa mara ya kwanza inaendelea na utafiti wa watalii wa ndani (stand - alone domestic tourism survey) kwa ajili ya kupata mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa. Sambamba na hilo, Wizara imeandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi; na kuboresha mfumo wa *MNRT Portal*; na Mfumo wa kielektroniki wa tathmini ya upangaji wa huduma za malazi na chakula katika daraja za ubora - *AserT*.

4.8 Changamoto na Utatuji

4.8.1 Changamoto

154. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwepo wa ugonjwa wa UVIKO-19 duniani ambao umeathiri kwa kiasi kikubwa sekta ya utalii na hivyo kupungua kwa mapato yanayotokana na sekta hiyo. Aidha, kumekuwa na ongezeko la migogoro kati ya binadamu na wanyamapori ambao umesababisha uharibifu wa mali na vifo. Changamoto nyingine ni; uwepo wa matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi; uvamizi wa hifadhi za wanyamapori, misitu na malikale kwa shughuli za kibinadamu; utegemezi mkubwa wa misitu kwa ajili ya nishati; na uwepo wa mimea vamizi katika baadhi ya maeneo ya hifadhi hali inayosababisha kuathirika kwa uoto wa asili na kupungua kwa malisho ya wanyamapori.

4.8.2 Utatuji wa Changamoto

155. *Mheshimiwa Spika*, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara imeweka mikakati mbalimbali ikiwemo: kutoa elimu kwa wadau wa utalii juu ya namna bora ya kutumia Mwongozo wa Uendeshaji wa Shughuli za Sekta ya Utalii - SOPs; na kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuirejesha Sekta ya Utalii nchini katika hali ya awali kabla ya kuathiriwa na UVIKO-19 ambao umeweka mkazo katika njia mbadala za utangazaji utalii, kuboresha miundombinu ya utalii, kuimarisha

mazao ya utalii na kuhamasisha utalii wa ndani. Mikakati mingine ni kujenga vituo vya askari katika maeneo yenye changamoto kubwa ya matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu; kutumia mbinu za kielektroniki za kufuatilia mienendo ya makundi ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kuwafunga vifaa maalum hususan katika maeneo yenye matukio mengi; kutoa elimu ya namna ya kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutumia mbinu mbalimbali za kitaalamu na asili; na kuimarisha doria za kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu ya namna ya kuzuia na kukabiliana na moto kichaa katika maeneo ya hifadhi; kuweka alama na mabango katika maeneo ya mipaka ya hifadhi; kuwezesha jamii inayopakana na maeneo ya hifadhi kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo yao; kuhimiza wananchi kupanda miti katika maeneo yao kwa ajili ya kupata nishati na matumizi mbalimbali; na kuwezesha miradi mbalimbali ya jamii ikiwemo ufugaji nyuki kwa lengo la kuwapatia kipato. Kwa upande mwingine, Wizara itaendelea kufanya tafiti za namna bora ya kukabiliana na mimea vamizi pamoja na kuendeleza operesheni za kung'oa na kuteketeza mimea hiyo.

5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

156. Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023 umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/2023 - 2024/2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 - 2025, Sera mbalimbali, Mpango Mkakati wa Wizara (2021/2022 - 2025/2026), maagizo mbalimbali ya viongozi wa Serikali na mikataba ya kikanda na kimataifa.

157. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele mbalimbali vya sekta ambavyo ni pamoja na: kukuza utalii wa ndani, kuongeza kasi ya utangazaji utalii kitaifa na kimataifa kwa kuendeleza programu ya *The Royal*

Tour, na kuibua masoko mapya ya utalii; kukarabati na kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi; na kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe, mikutano na matukio, meli za kitalii, michezo na utamaduni. Vipaumbele vingine ni: kuendelea kuishirikisha jamii katika mbinu za kujikinga dhidi ya wanyamapori hatarishi; kuimarisha shughuli za upandaji miti, ufugaji nyuki na mnyororo wa thamani wa mazao yake; kuimarisha mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu; kuimarisha mfumo wa utoaji huduma za utalii ili kukidhi viwango vya kimataifa; kuboresha ulinzi na usalama wa rasilimali za maliasili na malikale; kuendelea kuimarisha tafiti pamoja na mifumo ya takwimu na ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Maliasili na Utalii; na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kuendeleza rasilimaliwatu.

5.1 Ukusanyaji Maduhuli

158. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, makadirio ya maduhuli yatakayokusanywa kutokana na sekta ya maliasili na utalii ni jumla ya **Shilingi 670,856,583,921.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 469,364,418,596.00** zitakusanywa na Wizara kupitia mfumo wa TRA kutoka vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA. Aidha, **Shilingi 201,492,165,325.00** zitakusanywa moja kwa moja na Wizara kupitia mfumo wa *MNRT Portal* kutoka Idara, Mifuko na Taasisi nyingine za Wizara.

5.2 Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

159. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa mwaka 2022/2023 inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 624,142,732,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 443,706,567,000.00** zitagharamia Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 180,436,165,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Makadirio ya Matumizi ya Kawaida yanajumuisha makadirio ya Mishahara **Shilingi 175,884,707,000.00** na makadirio ya Matumizi Mengineyo **Shilingi 267,821,860,000.00**. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha **Shilingi 109,879,593,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 70,556,572,000.00** fedha za nje.

160. *Mheshimiwa Spika*, Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 22,974,824,000.00** kwa ajili ya Wizara na **Shilingi 420,731,743,000.00** kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Kati ya fedha za Wizara, **Shilingi 7,537,783,000.00** ni Mishahara na **Shilingi 15,437,041,000.00** ni matumizi mengineyo. Fedha za taasisi zinajumuisha **Shilingi 168,346,924,000.00** za mishahara na **Shilingi 252,384,819,000.00** fedha matumizi mengineyo.

5.3 Kazi Zitakazotekelezwa na Wizara na Taasisi zake

5.3.1 Sekta ya Wanyamapori

5.3.1.1 Idara ya Wanyamapori

161. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inatarajia kupandisha hadhi mapori tengefu Lake Natron, Kilombero, Loliondo, Lolkisale, Longido, Muhuwesi, Umba River, Mto wa Mbu, Simanjiro, Ruvu Masai, Ruvu Same na Kalimawe; na misitu ya Litumbandyosi na Gesimazoa kuwa mapori ya akiba. Aidha, Wizara itatenga na kurasimisha maeneo ya shoroba za wanyamapori na kuimarisha usimamizi wa maeneo ya mifumo ikolojia inayovuka mipaka ya nchi. Sambamba na hilo, Wizara itaendelea kutoa elimu ya mbinu za kukabilliana na wanyamapori wakali na waharibifu na kutoa kifuta jasho na kifuta machozi kwa waathirika wa matukio ya wanyamapori hao. Vilevile, Wizara itaandaa mkakati wa kutekeleza Sera ya Wanyamapori na kufanya Mapitio ya Sheria na Kanuni mbalimbali zinazosimamia sekta ndogo ya Wanyamapori. Kwa upande mwingine, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mikataba ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa; na kuimarisha mikakati ya kupambana na ujangili na Jeshi la Uhifadhi.

162. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea kuratibu utatuzi wa migogoro ya ardhi baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi. Sambamba na hilo, Wizara itatoa mafunzo ya uongozi na upandishwaji vyeo kwa watumishi wanaounda mfumo wa kijeshi na itaendelea kutoa elimu kwa wananchi na vyombo

vingine vya ulinzi na usalama kuhusu uwepo wa Jeshi la Uhifadhi Wanyamapori na Misit.

5.3.1.2 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania - TANAPA

163. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Shirika litaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuwezesha uandaaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji 30 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Nyerere na vijiji 18 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Serengeti. Shirika pia litachimba mabwawa mapya nane (8); na kukarabati mabwawa matano (5) kwa matumizi ya wanyamapori katika hifadhi za Taifa za Mkomazi, Tarangire, Mikumi, Katavi, Ruaha, Saadani, na Serengeti; kuandaa na kufanya mapitio ya mipango ya ujumla ya usimamizi minne (4) ya hifadhi za Burigi - Chato, Tarangire, Saadani na Kitulo; na kutengeneza mipango sita (6) ya usimamizi wa moto katika hifadhi za Taifa Nyerere, Burigi-Chato, Ibanda-Kyerwa, Mto Ugalla, Rumanyika-Karagwe na Kigosi. Pia, Shirika litaboresha maeneo ya malisho ya wanyamapori kwa kudhibiti mimea vamizi katika eneo lenye ukubwa wa hekta 30,331 katika hifadhi za Taifa Nyerere, Saadani, Serengeti, Arusha, Ibanda - Kyerwa, Mto Ugalla, Mikumi, Mkomazi na Katavi. Vilevile, Shirika litaotesha miti ya asili 100,000 katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro.

164. *Mheshimiwa Spika*, Shirika litaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa hifadhi kwa kuboresha matumizi ya sayansi na teknolojia kwa kununua vifaa 20 vya mawasiliano ya mtandao mpana (LoRa Transmitters), ndege tatu (3) zisizo na rubani na kuweka mfumo wa redio za kidijitali katika vituo vitano (5) katika Kanda ya Magharibi; na hifadhi za Taifa za Nyerere, Ruaha, Udzungwa na Mikumi. Pia, Shirika litanunua vitendea kazi mbalimbali ili kuwezesha operesheni za doria kufanyika kwa tija na ufanisi zaidi.

165. *Mheshimiwa Spika*, Shirika litaendelea kushirikisha jamii zinazoishi jirani na hifadhi katika shughuli za uhifadhi kwa kuimarisha vikundi 28 vya ulinzi shirikishi, vikundi 12 vya COCOBA na vikundi vitatu (3) vya klabu za mazingira. Vilevile,

elimu ya uhifadhi itaendelea kutolewa katika vijiji 864 vinavyozunguka hifadhi zote za Taifa na kuwezesha vijiji 11 kunufaika na miradi 11 ya ujirani mwema. Pia, Shirika litawezesha ununuzi wa mizinga ya nyuki 800 kwa vikundi 24 vya jamii katika vijiji 24. Katika hatua nyingine, Shirika litaendelea kudhibiti majanga ya moto kwenye hifadhi kwa kutengeneza mipango sita (6) ya usimamizi wa moto kichaa katika hifadhi za Taifa Nyerere, Kigosi, Mto Ugalla, Burigi - Chato, Ibanda - Kyerwa na Rumanyika - Karagwe. Sambamba na hilo, Shirika litatekeleza Mipango ya Usimamizi wa Moto na kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi jirani na hifadhi kwa ajili ya kukabiliana na moto kichaa.

166. Mheshimiwa Spika, Shirika litaendelea kupanua wigo wa uwekezaji kwenye hifadhi za Taifa kwa kutenga maeneo mapya 58 ya ujenzi wa loji na kambi za kitalii kwa ajili ya huduma za malazi zenye vitanda 3,330 katika hifadhi za Taifa Nyerere, Mto Ugalla, Burigi - Chato, Rubondo, Ruaha, Serengeti, Tarangire, Ziwa Manyara, Mikumi, Saadani, Mkomazi na Arusha. Pia, Shirika litajenga malazi ya gharama nafuu yenye jumla ya vitanda 308 kwa ajili ya watalii wa ndani katika hifadhi za Taifa Mikumi, Kilimanjaro, Mkomazi, Rubondo na Nyerere.

167. Mheshimiwa Spika, katika kupanua wigo wa utalii na mapato, Shirika litaanzisha utalii wa faru weupe katika hifadhi za Taifa Burigi - Chato na Mikumi. Aidha, Shirika litawezesha kuanza rasmi kwa uwekezaji katika maeneo ya utalii maalum katika Hifadhi ya Taifa Ruaha. Vilevile, Shirika litashiriki maonesho ya utalii katika masoko 19 ya nchi za India, Brazil, Argentina, Qatar, Uholanzi, Ufini, Poland, Urusi, Uswisi, Ujerumani, Israel, Ubelgiji, Marekani, Uhispania, Uingereza, Ufaransa, China, Korea ya Kusini na Italia.

168. Mheshimiwa Spika, Shirika litaendelea kuboresha miundombinu ya huduma za utalii kwa kujenga barabara mpya zenye urefu wa kilomita 2,500 katika hifadhi za Taifa Arusha, Burigi - Chato, Gombe, Katavi, Kilimanjaro, Kitulo, Mahale, Udzungwa, Manyara, Rubondo, Rumanyika - Karagwe, Ruaha, Mikumi, Nyerere na Serengeti. Aidha, Shirika

litajenga njia za utalii zenye urefu wa kilomita 251 na barabara za kutembea kwa miguu zenye urefu wa kilomita 342.5. Vilevile, Shirika litakarabati barabara zenye urefu wa kilomita 6,500; na viwanja vya ndege 17 katika hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi, Nyerere, Saadani, Tarangire, Mkomazi na Serengeti. Pia, Shirika litajenga nyumba 77 za makazi ya watumishi katika hifadhi za Taifa Kigosi, Mto Ugalla, Nyerere, Gombe, Serengeti na Ruaha. Vile vile Shirika litaanzisha Kikosi Kazi cha Ujenzi kwa ajili ya kuhudumia miundombinu ya shirika na iliyo nje ya shirika kibiashara. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa magari tisa (9), seti mbili (2) za mitambo ya kutengeneza barabara, boti moja (1), injini za boti tatu (3) na pikipiki nane (8). Katika hatua nyingine, Shirika litaanza kurusha mubashara (Live streaming) shughuli na matukio ya vivutio vilivyopo katika Hifadhi ya Taifa Serengeti.

5.3.1.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA

169. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka itaendelea kuimarisha ulinzi na usimamizi wa hifadhi kwa kufanya siku doria 284,460 katika mapori ya akiba, mapori tengefu, maeneo ya ardhioevu na Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori. Aidha, watumishi 330 watapatiwa mafunzo ya ukakamavu na utayari ya Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu. Kwa upande mwingine, Mamlaka itanunua trekta moja (1), magari 14 na pikipiki 45 kwa ajili ya doria na shughuli za utawala. Vilevile, Mamlaka itajenga madaraja matano (5) katika Pori la Akiba Lukwati/ Piti, mabwawa mawili (2) katika Pori la Akiba Swagaswaga, vibanda viwili (2) vya walinzi na ujenzi wa miundombinu maalum ya mawasiliano katika Pori la Akiba Maswa na Kanda ya Ziwa.

170. Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kutangaza zao la uwindaji wa kitalii katika maonesho mbalimbali ya kimataifa, hususan katika masoko makubwa ya Marekani, Ufaransa, Uingereza, Ubelgiji, Japan, Falme za Kiarabu na Afrika Kusini; na masoko yanayochipukia ya China na Urusi na nchi za Mashariki ya Mbali. Aidha, Mamlaka itabuni mbinu

mbalimbali za kuhakikisha vitalu vya uwindaji wa kitalii vinapata wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha vifurushi kwa bei maalum. Sambamba na hilo, Mamlaka itaendelea kutangaza maeneo ya uwekezaji mahiri (SWICA) ili kuvutia wawekezaji katika maeneo hayo.

171. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Mamlaka itaweka mifumo ya umeme wa jua kwenye miundombinu ya utalii iliyopo katika mapori ya akiba ya Mpanga/Kipengere, Wami - Mbiki, Swagaswaga na Mkungunero. Aidha, Mamlaka itaweka mifumo ya maji kwenye mapori ya akiba ya Mpanga Kipengere, Lukwati/ Piti, Wami - Mbiki, Lukwika/ Lumesule na Maswa; Eneo la Urithi wa Dunia la Kilwa; na jengo la kupumzikia watalii katika Pori la Akiba Mpanga Kipengere. Vilevile, Mamlaka itajenga makasha maalum matano (5) kwa ajili ya kutunzia wanyamapori wakubwa kwenye Pori la Akiba Pande; malango mawili (2) katika mapori ya akiba ya Pande na Ikorongo/ Grumeti; *picnic site* moja (1) katika Pori La Akiba Liparamba; uzio katika Pori la Akiba Pande, Bustani ya Wanyamapori Ruhila na Pori Tengefu la Ziwa Natron. Pia, Mamlaka itajenga kilomita 37.95 za barabara za utalii katika mapori ya akiba ya Kijreshi na Maswa.

172. Mheshimiwa Spika, katika kuvutia uwekezaji na kuimarisha uwindaji wa kitalii ikiwa ni pamoja na kuendeleza programu ya *Tanzania - The Royal Tour*, Mamlaka itaendelea kutangaza maeneo ya uwekezaji mahiri ili maeneo hayo yapate wawekezaji. Vilevile, Mamlaka itaendelea kuhamasisha ufugaji wa wanyamapori ili watu, makampuni na Mashirika binafsi waweze kuanzisha ranchi, bustani na mashamba ya wanyamapori. Sambamba na hilo, Mamlaka itaanzisha kitengo maalum kwa ajili ya kuwezesha ukamataji wa wanyamapori wa mbegu ili kufanyika kitalaam na kwa gharama nafuu.

173. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Mamlaka itaandaa mipango ya usimamizi ya jumla (GMP) ya mapori mapya ya Maswa, Moyowosi na Rungwa kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mapori hayo. Aidha, Mamlaka itakarabati kiwanja cha ndege katika Pori la Akiba Moyowosi;

ofisi ya Kanda ya Kaskazini; nyumba moja ya mtumishi Kunduchi; na ujenzi wa vimbweta vinne (4) katika Pori la Akiba Pande. Vilevile, Mamlaka itaandaa mpango wa maendeleo ya utalii; mpango wa masoko ya utalii; mwongozo wa utoaji wa *quota* za uwindaji; na viwango vya miundombinu ya utalii ndani ya mapori ya akiba. Aidha, Mamlaka itaondoa magugu maji kwenye eneo la ekari sita (6) katika Pori la Akiba Uwanda; na kusafisha kilomita 460 za barabara kwenye mapori ya akiba Maswa, Igombe, Inyonga, Moyowosi na Rungwa.

174. *Mheshimiwa Spika*, katika kuboresha mazingira ya kazi na kuongeza tija, Mamlaka itaanza ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu Jijini Dodoma; kujenga ofisi mbili (2) kwa ajili ya mapori ya akiba Msanjesi na Igombe; maghala matano (5) ya silaha; nyumba 13 za watumishi katika mapori ya akiba Mpanga/Kipengere (1), Selous (2), Maswa (2), Igombe (4) na Rukwa (4). Aidha, Mamlaka itajenga vituo vya askari vitano (5) katika mapori ya akiba ya Wami - Mbiki (2), Swagaswaga (1), Ugalla (1) na Pori Tengefu Lunda - Mkwambi (1); na karakana tatu (3) katika Kanda ya Kaskazini na mapori ya akiba ya Maswa na Rukwa.

5.3.1.4 Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro - NCAA

175. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka itaendelea kuimarisha ulinzi na uhifadhi wa maliasili na malikale kwa kufanya siku doria 36,000; operesheni maalum sita (6); kutoa mafunzo kwa watumishi 300; na kununua vitendea kazi mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika eneo la hifadhi. Katika hatua nyingine, Mamlaka itaendelea kuimarisha ushirikiano na jamii zinazopakana na Hifadhi kwa kufanya mikutano 175 ya ujirani mwema kwa lengo la kutoa elimu ya uhifadhi na kutatua migogoro. Vilevile, Mamlaka itaendelea kuwezesha miradi ya maendeleo kwa halmashauri zinazopakana na eneo la hifadhi.

176. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka itaendelea kuboresha nyanda za malisho kwa kudhibiti mimea vamizi kupitia moto mpango, kung'oa, kufyeka na kuwezesha utafiti. Zoezi hili

litafanyika katika eneo lenye ukubwa wa hekta 5,000 lilloathirika zaidi katika maeneo ya Ndotu na Kreta ya Ngorongoro. Katika hatua nyingine, Mamlaka itaotesha miche ya miti 460,000 ambayo itapandwa katika maeneo yaliyoathirika na ukataji miti na mingine itagawiwa kwa jamii inayozunguka Hifadhi. Sambamba na hilo, Mamlaka itasafisha mpaka wenye urefu wa kilomita 200 na kusimika vigingi 50 kwenye eneo hilo kwa lengo la kuzuia moto kichaa na uvamizi wa maeneo ya hifadhi. Aidha, katika eneo la Oldeani, Mamlaka itaweka uzio wa umeme rafiki kwa mazingira wenye urefu wa kilomita 30 kwa lengo la kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

177. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza na kukuza utalii, Mamlaka itajenga barabara zenye jumla ya kilomita 55.5. Kati ya hizo, kilomita 29.5 zitajengwa kutoka Loduare hadi Golini kwa kiwango cha tabaka gumu la zege, kilomita 25 kutoka Ndotu hadi Endulen kwa kiwango cha changarawe na kilomita moja (1) kutoka makutano ya Seneto na Kreta ya Ngorongoro kwa kiwango cha tabaka gumu la mawe. Katika hatua nyingine, Mamlaka itaendelea kufanya ukarabati wa mara kwa mara kwenye mtandao wa barabara zenye jumla ya kilomita 554 ndani ya hifadhi.

178. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi ya wageni na askari, Mamlaka itajenga mfumo wa maji safi katika eneo la Ngoitoktok; na kukarabati mifumo ya maji katika vituo vya askari vya Mbulumbulu, Endamagha, Lemala, Oloirobi, Seneto, Makoromba na Lerai. Vilevile, Mamlaka itaendelea na soroveya itakayowezesha uchimbaji wa visima vitano (5) vya maji katika maeneo ya Jiwe la Nasera, Olduvai, Ndotu, Laetoli na Bonde la Faru. Katika jitihada za kuvutia uwekezaji wenye tija, Mamlaka itaendelea kubainisha maeneo ya uwekezaji wa Loji zenye hadhi ya kimataifa. Mpango huu unatarajiwa kuongeza vitanda zaidi ya 480. Aidha, Mamlaka itaendelea kushiriki katika matukio na maonesho mbalimbali ya utalii na uhifadhi ndani na nje ya nchi. Vilevile, Mamlaka itaendelea kuboresha na kutumia njia za kidigitali ikiwemo

Ngorongoro *live streaming* kutangaza mubashara vivutio na matukio mbalimbali kutoka hifadhini.

179. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza thamani ya vituo vya malikale na idadi ya wageni wanaovitembelea, Mamlaka itakarabati njia za watembea kwa miguu katika vituo vya Laetoli, Amboni Tanga na Olduvai na kuboresha makumbusho katika vituo vya Olduvai, Kimondo cha Mbozi, Laetoli na Mary Leakey. Aidha, Mamlaka itaendesha mafunzo katika vyuo vitano (5), shule tano (5) za sekondari na shule tano (5) za msingi katika wilaya za Karatu, Monduli, Mbozi na Tanga Mjini ili kutoa elimu na kutangaza utalii wa miamba na malikale. Katika kuboresha huduma na maisha ya wananchi waishio ndani ya eneo la hifadhi, Mamlaka itaendelea kutekeleza programu za kuelimisha na kuhamasisha wenyeji waishio ndani ya Hifadhi kuhama kwa hiari kwenda kwenye maeneo ya nje ya Hifadhi yakiwemo maeneo maalum yaliyotengwa. Aidha, Mamlaka itaendelea na ujenzi wa ofisi za makao makuu katika eneo la Kemyn, Wilaya ya Karatu. Vilevile, Mamlaka itanunua gari maalum litakaloweza kubeba wastani wa watalii 30 wakati wa kutembelea vivutio ndani ya Hifadhi.

5.3.1.5 Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania - TAWIRI

180. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Taasisi itaendelea kuboresha miundombinu yake ikiwemo: kujenga jengo la makao makuu na nyumba tatu (3) za watumishi, kununua magari matatu (3) na vifaa vya maabara na kukarabati nyumba tatu (3) za watumishi na maabara ya Kituo cha Utafiti Serengeti. Aidha, Taasisi itaendelea kutekeleza tafiti za kimkakati zinazohusu migongano baina ya binadamu na wanyamapori, mimea vamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa, chura wa Kihansi katika eneo lake la asili, utalii na maisha ya jamii Kusini mwa Tanzania, magonjwa ya wanyamapori na yanayoambukiza wanyama na binadamu, mimea tiba pamoja na nyuki na mazao yake.

181. Mheshimiwa Spika, Taasisi itafanya sensa tatu (3) za wanyamapori katika maeneo ya Mfumo Ikojia Nyerere -

Selous - Liparamba - Mikumi, Mfumo Ikolojia Saadani - Wami Mbiki na Pori la Akiba Swagaswaga. Aidha, Taasisi itaendelea kutoa elimu na kusambaza matokeo ya tafiti zinazofanywa na Taasisi. Sambamba na hilo, Taasisi itaratibu kongamano la Kisayansi la 14 la Kimataifa, itatoa elimu ya mbinu rafiki za kukabiliiana na migongano baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu pamoja na elimu ya mbinu bora za ufugaji nyuki. Vilevile, Taasisi itachapisha matokeo ya tafiti mbalimbali katika majarida ya kisayansi.

5.3.1.6 Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - CAWM Mweka

182. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Cheti cha Msingi, Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili katika fani ya uhifadhi wanyamapori na utalii pamoja na mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Chuo kitakamilisha ujenzi wa jengo la mafunzo na kujenga nyumba mbili (2) za watumishi. Vilevile, Chuo kitakarabati nyumba 10 za watumishi, hosteli saba (7) na kuweka samani na heater za umeme 21 katika hosteli. Sambamba na hilo, Chuo kitajenga maegesho ya magari, uzio wa ukuta wenye urefu wa mita 600, vyoo, madarasa na kuweka miundombinu ya maji katika maeneo ya mafunzo kwa vitendo Kwakuchinja, Wilaya ya Babati na Arash, Wilaya ya Ngorongoro.

5.3.1.7 Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu-Sekamaganga

183. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Kituo kitaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 162 wakiwemo Askari Wanyamapori wa Vijiji (80), Waongoza Watalii (50) na Viongozi na wajumbe wa Kamati za Vijiji (32). Aidha, kitaanzisha kozi ya Astashahada ya Utalii na Waongoza Watalii (NTA 5). Vilevile, Kituo kitarabati jengo la utawala, nyumba moja (1) ya watumishi na bweni moja (1). Sambamba na hilo, Kituo kitatoa ushauri wa kitaalam kwa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori kuhusu masuala mbalimbali ya uhifadhi wa wanyamapori.

5.3.1.8 Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi

184. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Taasisi itadahili wanafunzi 400 katika fani za uhifadhi wa wanyamapori, himasheria na uongozaji wa watalii na usalama. Aidha, Taasisi itakamilisha taratibu za kuhuisha usajili wake NACTE, kuandaa mtaala kwa ajili ya uanzishwaji wa kozi ya Stashahada katika Fani ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Uongozaji Watalii na Usalama; na kuweka samani katika maktaba. Vilevile, itakamilisha ujenzi wa uzio wa chuo, kuboresha miundombinu ya TEHAMA na kuanzisha shamba la wanyamapori ili kuongeza mapato pamoja na kuimarisha utoaji mafunzo kwa vitendo.

5.3.1.9 Mfuko wa Kuhifadhi Wanyamapori Tanzania - TWPF

185. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mfuko utaendelea kuwezesha operesheni maalum za kuzuia ujangili, uhakiki na ulipaji wa kifuta machozi na kifuta jasho; utatuzi wa migogoro kati ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa na upandishwaji hadhi wa mapori tengefu matano (5) kuwa mapori ya akiba. Aidha, Mfuko utaendelea kuwezesha utoaji wa elimu na vitendea kazi kwa wilaya tano (5) zenye matukio mengi ya wanyamapori wakali na waharibifu; mapitio ya Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya wanyamapori; kujenga uwezo wa watumishi; uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori ya mwaka 2000; na kuwezesha Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu pamoja na kudhibiti ujangili.

5.3.2 Sekta ya Misitu na Nyuki

5.3.2.1 Idara ya Misitu na Nyuki

186. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara itaandaa mipango kazi ya kutekeleza Sera za Taifa za Misitu; na Ufugaji Nyuki. Aidha, Wizara itaandaa mikakati ya Taifa ya Upandaji na Uendeshaji wa Miti ya Mianzi; Kilimo Mseto; Nishati ya Mkaa; Upandaji Miti; na Uwekezaji katika Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki. Aidha, Wizara itaandaa

Mwongozo wa Usimamizi wa Misitu ya Asili na Mashamba ya Miti; na Mwongozo wa Usimamizi wa Nyuki wasiouma. Vilevile, Wizara itafanya mapitio ya mwongozo wa Uvunaji endelevu na Biashara ya Mazao ya Misitu; Sheria ya Misitu Sura 323; na Sheria ya Ufugaji Nyuki Sura 224. Kwa upande mwingine, Wizara itaendelea kufanya tathmini ya mchango wa Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki katika pato la Taifa kwa kutumia mfumo wa Uchumi wa Kijani (green accounting). Vilevile, Wizara itatafsiri kwa lugha ya Kiswahili na kusambaza miongozo mbalimbali ya Sekta ya Misitu na Ufugaji Nyuki ili kutoa uelewa mpana kwa umma kuhusu miongozo hiyo.

187. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa jamii inaendelea kushiriki kwenye uhifadhi na uendelezaji wa rasilimali za misitu na nyuki, Wizara itaandaa mkutano mmoja (1) wa wadau wa misitu na nyuki; kuwezesha uanzishaji wa hifadhi za nyuki za vijiji vitano (5); kutoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa vikundi vitano (5) vya wafugaji nyuki; kuandaa jukwaa la wataalam wa fani ya ufugaji nyuki; na kuwezesha vyama vya ushirika wa wafugaji nyuki kuandaa mikataba ya ufugaji nyuki katika maeneo ya hifadhi. Aidha, Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya misitu na nyuki inayotekelezwa na Wizara. Vilevile, Wizara itaratibu vikao vinne (4) vya Kamati ya Ushauri wa Misitu - NAFAC, vikao vitatu (3) vya Kamati ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki – NABAC na vikao vinne (4) vya Kamati Endeshi ya utekelezaji wa mpango kazi wa mazao ya misitu yaliyohandisiwa. Pia, Wizara itaratibu Siku ya Upandaji Miti Kitaifa, Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Nyuki Duniani.

5.3.2.2 Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania

188. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wakala utaandaa Mipango ya Usimamizi wa Misitu 57 yenye ukubwa wa hekta 1,703,202 na kufanya mapitio ya Mipango ya Usimamizi wa misitu ya hifadhi 111. Vilevile, Wakala utaendesha jumla ya siku doria 212,400 na operesheni maalum 355 katika maeneo ya hifadhi za misitu na nyuki. Katika hatua za kuimarisha ulinzi na kutatua migogoro katika hifadhi za misitu na nyuki, Wakala utapima mipaka ya misitu

133 na kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilomita 33,107; kusafisha mipaka yenye kilomita 5,746 na njia za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 6,000; kuweka vigingi 1,369 na mabango 2,133; na kujenga minara miwili (2) mipya ya kubaini matukio ya moto na kukarabati mingine 11. Aidha, Wakala utapandisha hadhi maeneo ya ardhi huria tisa (9) kuwa misitu ya hifadhi ya Taifa.

189. Mheshimiwa Spika, Wakala utakarabati kilomita 356.5 za njia za watalii na kilomita 157.3 za barabara za msituni; na kuandaa ramani za vivutio vya kiikolojia katika misitu ya hifadhi. Aidha, ili kuvutia utalii ikolojia, Wakala utajenga ofisi moja (1), mabanda nane (8) ya kupumzika watalii, malango matatu (3) na vyoo 15; na kukarabati barabara yenye urefu wa kilometa 210 kwa ajili ya ulinzi wa misitu na michezo ya kitalii. Aidha, Wakala utakarabati miundombinu katika vituo sita (6) ikiwemo kilometa 10.5 ya njia za kutembea kwa miguu, mageti matatu (3) na mabenchi ya kukalia 60 katika vituo vya Michoro ya Miambani Kolo - Kondo, Mji Mkongwe - Bagamoyo, Tembe la Kwihara - Tabora, Magofu ya Tongoni - Tanga na Kaole - Bagamoyo.

190. Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya malighafi ya mazao ya misitu nchini, Wakala utaongeza uzalishaji wa mbegu za miti nchini kwa kuongeza vyanzo vipya vya mbegu vitatu (3) na kuzalisha tani 24 za mbegu na miche ya miti 33,156,000. Aidha, Wakala utapanda miti katika eneo lenye ukubwa wa hekta 7,636 na kurudishia miti iliyokufa kwenye eneo la hekta 2,019. Aidha, Wakala utapalilia eneo lenye hekta 32,677, kupogolea hekta 11,421 na kupunguzia miti kwenye hekta 3,331. Katika hatua nyingine, Wakala utanzisha upandaji wa miti aina ya mpira katika Shamba la Miti Rondo na kuandaa Mipango ya Usimamizi wa mashamba ya miti 18 yenye jumla ya ukubwa wa hekta 418,119. Vilevile, katika kuhakikisha usimamizi thabiti wa mashamba ya miti ya Serikali na upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu nchini, Wakala utakamilisha maandalizi na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Usimamizi na Uendelezaji wa Mashamba ya Miti ya Serikali wa miaka 30 (2021 - 2051).

191. Mheshimiwa Spika, Wakala utatoa elimu ya kupambana na kuzuia moto kwa jamii katika vijiji 54 pamoja na kuanzisha bustani ya miti iliyo hatarini kutoweka katika eneo la Chamwino. Aidha, Wakala utaendelea kulinda hekta 158,100 za hifadhi za mikoko na kupanda miche katika eneo la hekta 83. Vilevile, Wakala utatatua migogoro ya mipaka katika hifadhi za misitu 13 na kuwezesha kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 40. Pia, Wakala utaendeleza mashamba ya nyuki mawili (2); kuanzisha shamba jipya moja (1) la ufugaji nyuki la Kipembawe katika Wilaya ya Chunya lenye ukubwa hekta 21,790; kuendeleza viwanda vitatu (3) vya nyuki; kutoa elimu kwa wafugaji nyuki 848; kuzalisha tani 49 za asali, tani 2.9 za nta na kilo 50 za chavua; na kuchonga mizinga ya nyuki 1,200.

192. Mheshimiwa Spika, Wakala utaboresha mazingira ya kazi na kuongeza ufanisi wa kazi kwa kununua magari 34, pikipiki 46, basi moja (1), malori matatu (3), boti mbili (2), mtambo mmoja (1) na kujenga majengo nane (8) ya ofisi. Aidha, Wakala utawezesha watumishi 70 kupata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 493 kupata mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Wakala utaendeleza jitihada ya kuboresha shughuli za kijeshi ambapo utatoa mafunzo ya uongozi wa kijeshi kwa watumishi 300.

5.3.2.3 Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI

193. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Taasisi itajenga jengo la Kituo cha Utafiti cha Tabora; kukarabati majengo mawili (2) ya Vituo vya Utafiti vya Kibaha na Malya; na vifaa vya maabara. Aidha, Taasisi itafanya tafiti za kimkakati sita (6) zenye lengo la kutathmini rasilimali za misitu zilizopo; kubaini mchango wa sekta ya misitu kwenye pato la Taifa kwa kutumia Uchumi wa Kijani; na kutathmini miti ya asili inayotumika kibiashara iliyo hatarini kutoweka na kubaini namna ya kuizalisha, kuipanda na kuitunza. Aidha, Taasisi itasimamia uboreshaji wa Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Misitu na Nyuki (Forest and Beekeeping Management Information System) ili kuongeza takwimu zitokanazo na miradi na programu mbalimbali za utafiti nchini.

Sambamba na hilo, Taasisi itaratibu Kongamano la Kisayansi la tatu (3) la Kimataifa na kuchapisha matokeo ya tafiti mbalimbali katika majarida ya kisayansi.

5.3.2.4 Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki

194. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Chuo cha Viwanda vya Misitu kitadahili wanafunzi 400 wa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada; na kuendesha mafunzo ya ufundi sanifu na ufundi stadi wa teknolojia ya viwanda vya misitu. Aidha, Chuo kitajenga bweni; kukarabati madarasa, ofisi na nyumba za watumishi; na kitanunua vifaa vya mafunzo na magari. Kwa upande mwingine, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kitadahili wanafunzi 450 wa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada; na kuendelea kuimarisha miundombinu ya kufundishia kwa kujenga jengo la maabara, maktaba, kununua kompyuta na kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa uzio wa Chuo. Pia, Chuo kitaanzisha Utalii wa Nyuki (Api-tourism) katika manzuki za Chuo na kuimarisha karakana kwa kununua vifaa na mashine. Katika hatua nyingine, Chuo cha Misitu Olmotonyi kitadahili wanafunzi 900 wa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kitakarabati mabweni sita (6), nyumba za wakufunzi 10; na kununua magari mawili (2) na kompyuta 50.

5.3.2.5 Mfuko wa Misitu Tanzania - TaFF

195. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Mfuko utaeendelea kuwezesha utekelezaji wa miradi 209 inayoendelea na miradi mipya 180 ya uanzishwaji wa vitalu vya miti; upandaji miti mashuleni; ufugaji nyuki; ruzuku maalum kwa ajili ya kuendeleza mashamba ya miti; na miradi ya utafiti yenye lengo la uhifadhi, usimamizi, uendelezaji na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na kuongeza thamani ya mazao ya misitu na nyuki. Vilevile, Mfuko utawezesha TAFORI kufanya na kuratibu tafiti sita (6) za kimkakati zenye lengo la kuendeleza sekta ya Misitu na Nyuki. Pia, Mfuko utawezesha ununuzi wa magari mawili (2) kwa ajili ya kuboresha ukusanyaji

wa mapato yatokanayo na mazao ya misitu na nyuki; na kuwezesha kazi ya mapitio ya sheria ya misitu kwa ajili ya kuweka vifungu vya kuimarisha Mfuko ikiwemo kuingiza suala la ufugaji nyuki. Aidha, Mfuko utawezesha kufanyika kwa vikao vya Kamati ya Ushauri wa Misitu - NAFAC; na vikao vya Kamati ya Ushauri wa Ufugaji Nyuki - NABAC.

5.3.3 Sekta ya Utalii

5.3.3.1 Idara ya Utalii

196. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka fedha 2022/2023, Wizara itakamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utalii ya Mwaka 1999; na kuandaa Programu ya Maendeleo ya Utalii nchini. Katika hatua za kuendeleza mazao ya utalii nchini, Wizara itabainisha maeneo ya fukwe katika maziwa makuu ya Viktoria, Tanganyika na Nyasa kwa ajili ya uwekezaji na uendelezaji wa shughuli za utalii. Katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora katika mikoa ya Kilimanjaro, Mbeya na Mwanza. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa wadau wa utalii kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa kupanga huduma za malazi katika daraja za ubora (AserT) pamoja na kufanya ukaguzi kwa watoa huduma za utalii nchini. Sambamba na hilo, Wizara itabaini vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji wa shughuli za utalii nchini katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Morogoro na Tanga. Aidha, Wizara itafanya mikutano mitatu (3) ya wadau yenye lengo la kuhamasisha wadau kuwekeza na kuendeleza mazao mbalimbali ya utalii. Aidha, Wizara itaratibu maadhimisho ya Siku ya Utalii Duniani pamoja na kuendelea kushiriki katika matukio mbalimbali ya utangazaji na uendelezaji utalii ndani na nje ya nchi.

5.3.3.2 Bodi ya Utalii Tanzania - TTB

197. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Bodi ya Utalii Tanzania itaandaa mkakati wa uendelezaji wa utalii wa mikutano na matukio ambao unalenga kuvutia matukio mbalimbali ya kimataifa kufanyika nchini. Aidha, Bodi

itaandaa onesho la sita (6) la *Swahili International Tourism Expo* (SITE); na kuratibu Mkutano wa 65 wa Shirika la Utalii Duniani - Kamisheni ya Kanda ya Afrika utakaofanyika tarehe 05 hadi 07 Oktoba, 2022 Jijini Arusha. Matukio hayo yatatoa fursa za kutangaza na kuendeleza utalii, kuvutia uwekezaji na kukutanisha wadau wa utalii wa ndani na nje ya nchi kupitia mikutano ya kibiashara.

198. Mheshimiwa Spika, Bodi itaratibu ziara maalum 15 za mafunzo kwa ajili ya makundi maalum ya wadau ikiwemo wakala wa biashara za utalii, waandishi wa habari, watu mashuhuri, mabalizi wa hiari wa utalii na wawekezaji katika masoko mbalimbali ya utalii. Katika juhudi za kutangaza utalii ndani na nje ya nchi, Bodi itaendelea kuandaa na kusambaza nyenzo za utangazaji utalii pamoja na kutumia mbinu za kidigitali na mitandao ya kijamii. Aidha, Bodi itaendelea programu ya utalii wa utamaduni na kutangaza mazao ya utalii ikiwemo uwindaji wa kitalii, utalii ikolojia na utalii wa malikale. Sambamba na hilo, Bodi itaendelea kushirikiana na vituo mbalimbali vya habari katika kuandaa na kurusha vipindi maalum na makala za utangazaji utalii.

199. Mheshimiwa Spika, Bodi itaendelea kutekeleza Mkakati wa Utangazaji Utalii Kimataifa wa mwaka 2020 - 2025 kwa kushiriki katika maonesho ya utalii ya kimataifa na road show za utalii. Juhudi hizo zinalenga kuitangaza Tanzania katika masoko ya utalii ya msingi, kimkakati na yale yanayoibukia kwenye mabara ya Amerika, Ulaya, Afrika, Mashariki ya Kati, Asia na Pasifiki. Aidha, Bodi itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuratibu na kushiriki katika matukio yanayohusisha utangazaji utalii ndani ya nchi. Hatua hizi zinalenga kuendeleza utangazaji wa vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi, sambamba na kuendeleza juhudi zilizoanzishwa kupitia programu ya *Tanzania – The Royal Tour*.

5.3.3.3 Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT

200. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Chuo kitadahili wanafunzi 1,537 katika ngazi ya Astashahada, Stashahada pamoja na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa

wadau 437 katika mnyororo wa utalii. Aidha, Chuo kitanunua vitendea kazi mbalimbali na kufanya ukarabati wa miundombinu ya kutolea mafunzo katika Kampasi ya Bustani, Temeke na Arusha. Vilevile, kitafanya tafiti na kutoa ushauri katika fani ya utalii, ukarimu na uratibu matukio. Katika hatua nyingine, Chuo kitajenga jengo lenye madarasa, ukumbi na jiko la kujifunzia katika Kampasi ya Arusha pamoja na kuanza ujenzi wa Kampasi Mpya ya Mwanza. Pia, Chuo kitatekeleza programu za kimkakati za kukuza ujuzi ikijumuisha uanagenzi, utarajali na urasimishaji wa ujuzi uliopatikana katika mfumo usio rasmi (recognition of prior learning). Aidha, Chuo kitaanzisha shahada ya kwanza katika fani ya Utalii na Ukarimu na kuanzisha lugha za kigeni kama Kichina, Kihispania na Kijerumani.

5.3.4 Sekta ya Mambo ya Kale

5.3.4.1 Idara ya Mambo ya Kale

201. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara itafanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Malikale ya mwaka 2008 na kuandaa mkakati wa utekelezaji; na kufanya mapitio ya Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281. Aidha, Wizara itaandaa kanuni na miongozo ya uhifadhi na utafiti wa maeneo ya malikale; vigezo vya kutambua rasilimali za Urithi wa Utamaduni kuwa Urithi wa Taifa; na mpango wa kitaifa wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za urithi wa utamaduni. Katika hatua nyingine, Wizara itafanya ufuatiliaji wa hali ya uhifadhi kwa vituo na maeneo ya malikale; na kukagua maeneo ya urithi wa utamaduni wa Taifa yaliyopo katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Morogoro, Dodoma na Kilimanjaro kwa ajili ya kuboresha orodha ya kitaifa ya maeneo ya Urithi wa Utamaduni wa Taifa.

202. Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Wizara itapima maeneo saba (7) ya malikale kwa lengo la kupata hati miliki na kupunguza migogoro ya mipaka; na kutengeneza mfumo wa maombi ya vibali vya utafiti. Aidha, itashiriki mikutano na maonesho ya Kikanda na Kimataifa

inayohusiana na uhifadhi na uendelezaji wa malikale; Vilevile, itafanya vikao vitano (5) vya wadau kuhusu uhifadhi wa malikale na urithi wa utamaduni.

5.3.4.2 Shirika la Makumbusho ya Taifa - NMT

203. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Shirika litafanya tathmini ya Uhifadhi, kuainisha thamani za kitamaduni; na kufanya ukarabati wa majenzi ya kale 22 katika maeneo ya Pangani - Tanga, Kua - Mafia, Mikindani - Mtwara na Kigamboni - Dar es Salaam. Aidha, Shirika litaweka Onesho la Kudumu la Historia katika Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni, Dar es Salaam. Vilevile, Shirika litaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba za asili kwa kufuata ramani ya Tanzania katika Kijiji cha Makumbusho, Dar es Salaam ambapo nyumba za kaya tatu (3) zitajengwa. Katika hatua nyingine, litaendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika shughuli za utafiti, uhifadhi na maonesho. Pia, Shirika litaendelea kutekeleza Mpango wa Miaka 10 wa Kuenzi na Kusherehekea Urithi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

204. *Mheshimiwa Spika*, Shirika litaendelea kutangaza vivutio vya malikale na Makumbusho kidigitali na kuhamasisha utalii wa ndani kwa kutumia maonesho tano (5) na matamasha saba (7). Sambamba na hilo, Shirika litafanya tafiti nne (4) na kukusanya na kuhifadhi mikusanyo ya asili na kiutamaduni 220. Vilevile, Shirika litaendelea kuhamasisha, kusimamia na kushauri kuhusu uanzishwaji wa makumbusho mpya za watu na taasisi binafsi. Pia, Shirika litaendelea kufanya programu mbalimbali za kujenga uelewa kwa vizazi vya sasa kuhusu uzalendo, uhifadhi na uendelezaji wa tamaduni na urithi wa Asili katika mikoa ya Mara, Simiyu na Singida.

5.3.4.3 Mfuko wa Mambo ya Kale - NAF

205. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Mfuko utawezesha ufuatiliaji wa mikusanyo na malikale ndani na nje ya nchi; kukusanya taarifa za maeneo mapya ya malikale katika mikoa ya Katavi, Simiyu, Njombe, Dodoma,

Kigoma na Lindi. Aidha, Mfuko utawezesha ufuatiliaji wa taarifa za kiutafiti katika maeneo ya malikale; uandaaji wa miongozo ya uanzishaji wa Makumbusho nchini, mpango wa uhifadhi wa mji wa kihistoria wa Bagamoyo na Pangani na mpango wa uhifadhi na usimamizi wa njia ya kati ya biashara ya utumwa na vipusa. Vilevile, Mfuko utawezesha utoaji wa elimu kwa wadau kuhusu uhifadhi na uendelezaji wa malikale.

5.4 Miradi ya Maendeleo

206. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 180,436,165,000.00** kutekeleza Miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 109,879,593,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 70,556,572,000.00** ni fedha za nje. Fedha za maendeleo **Shilingi 180,436,165,000.00** zinajumuisha **Shilingi 71,684,572,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi tisa (9) ya Idara na Vitengo viliyo chini ya Wizara; **Shilingi 108,751,593,000.00** za Miradi itakayotekelezwa na Taasisi (TANAPA, NCAA, TAWA na NCT).

207. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara itatekeleza miradi ya maendeleo kama ifuatavyo: -

i. Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW);

ii. Mradi wa Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (Public Finance Management and Reform Programm VI);

iii. Mradi wa Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya Wanyamapori (Support to Combat Poaching and Illegal Wildlife Trade in Tanzania);

iv. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi Ujangili;

v. Mradi wa Panda Miti Kibiashara (Private Plantation and Value Chain in Tanzania);

vi. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Misitua na Ufugaji Nyuki (Capacity Building in Forestry and Beekeeping);

vii. Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (Support to Beekeeping Value Chain Programme – BEVAC); na

viii. Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE Tourism Development Project).

6.0 SHUKRANI

208. *Mheshimiwa Spika*, ninapenda kutumia nafasi hii tena kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaotoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. Pia, ninawashukuru wadau wote kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kipekee, nizishukuru nchi marafiki, washirika wa maendeleo, mashirika ya kimataifa, taasisi za kiserikali pamoja na wadau wengine wakiwemo sekta binafsi kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Sekta ya Maliasili na Utalii na uchumi wa nchi kwa ujumla. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Falme za Kiarabu, Korea Kusini, Marekani, Morocco, Namibia, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi za Kimataifa ni pamoja na: AfDB, AWF, AWHF, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IMF, ITC, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, WTTC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF. Aidha, ninapenda kuwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Nitumie fursa hii kuwaomba wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

7.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/2023

209. *Mheshimiwa Spika*, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 624,142,732,000.00** kwa matumizi ya Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 443,706,567,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 180,436,165,000.00** ni za miradi ya maendeleo.

210. *Mheshimiwa Spika*, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha **Shilingi 175,884,707,000.00** za mishahara na **Shilingi 267,821,860,000.00** za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha **Shilingi 109,879,593,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 70,556,572,000.00** fedha za nje.

8.0 HITIMISHO

211. *Mheshimiwa Spika*, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: www.maliasili.go.tz

212. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Maduhuli ya Wizara kwa mwaka 2020/2021 na Makadirio kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Na.	Taasisi	Makadirio na Makusanyo kwa Mwaka 2021/2022 (hadi Aprili, 2022)				Makadirio kwa mwaka 2022/2023
		Makusanyo kwa mwaka 2020/2021	Makadirio kwa mwaka 2021/2022	Makusanyo hadi Aprili, 2022	%	
	(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)	(vi)
A: Maduhuli yaliyokusanywa kupitia Mfumo wa MMRI Portal						
1.	Wizara	22,657,242,000	22,657,242,000	6,168,830,213	27	9,507,352,000
2.	Taasisi	172,136,947,241	181,051,970,727	135,812,770,980	75	184,397,895,325
3.	Mfuko	23,752,412,851	7,622,061,000	4,461,854,701	59	7,586,918,000
	JUMLA	218,546,602,092	211,331,273,727	146,443,455,894	69	201,492,165,325
B: Maduhuli yaliyokusanywa kupitia Mfumo ya TBHAWA ya Wizara kwenda TRA						
1.	TANWAPA	363,899,596,000	253,704,221,522	140,231,422,143.61	55	257,524,745,788
2.	NCAA	162,663,179,000	162,663,179,000	73,843,062,100	45	148,000,000,000
3.	TAWA	58,063,935,590	61,647,180,000	36,910,731,830.25	60	63,839,672,808
	Jumla	584,626,710,590	478,014,580,522	0	53	469,364,418,596
JUMAKU		803,173,312,682	689,345,854,249	0	58	670,856,583,921

Jedwali Na. 2: Idadi ya Watalii Waliotembelea Hifadhi za Taifa na Mapato kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022

Na.	Mwaka	Watalii			Mapato (Shilingi)
		Nje	Ndani	Jumla	
1.	2017/2018	670,144	409,119	1,079,263	254,794,242,000
2.	2018/2019	743,248	494,254	1,237,502	282,426,174,846
3.	2019/2020	658,250	394,693	1,052,943	252,194,833,476
4.	2020/2021	153,389	358,500	511,889	56,979,796,789
5.	2021/2022*	347,040	511,860	858,900	140,231,422,143.61
	Jumla	0	0	0	0

* Hadi Aprili 2022

Jedwali Na. 3: Idadi ya Watalii Waliotembelea Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Mapato kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022

Na.	Mwaka wa Fedha	Watalii wa Nje	Watalii wa Ndani	Jumla ya Watalii	Mapato
1.	2017/2018	372,732	271,423	644,155	128,973,748,000
2.	2018/2019	430,616	270,094	700,710	143,949,144,000
3.	2019/2020	412,244	294,807	707,051	123,858,764,000
4.	2020/2021	72,632	118,982	191,614	31,426,077,258
5.	2021/2022*	184,767	162,561	347,328	73,843,062,100
	Jumla	0	0	0	0

* Hadi Aprili 2022

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Jedwali Na. 4: Mwenendo wa Uwindaji wa Kitalii na Mapato Kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022

Na.	Mwaka	Idadi ya Watalii			Mapato
		Wawindaji	Watazamaji (Observers)	Jumla	
1.	2017/2018	473	291	764	29,870,663,155
2.	2018/2019	444	360	804	25,771,163,424
3.	2019/2020	484	483	0	22,384,414,381
4.	2020/2021	355	255	610	24,945,979,320
5.	2021/2022*	494	381	875	23,657,308,675.09
Jumla		0	0	0	0

**Hadi Aprili 2022*

Jedwali Na. 5: Mwenendo wa Upandaji Miti katika Mashamba ya Miti Kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022

	Jina la Shamba	Ukubwa wa msitu	2017/2018	2018/2019	2019/2020	2020/2021	2021/2022	Jumla
1.	Buhindi	21,880	771	846	357	495	504	2,973
2.	Kawetire	5,182	263	145	47	62	78	595
3.	Kiwira	2,820	104	162	99	87	136	588
4.	Korogwe	10,276	64	215	129	108	0	516
5.	Longuza	7,067	48	117	168	133	223	689
6.	Mbizi	23,824	410	322	311	209	123	1,375
7.	Meru	8,195	291	553	357	180	258	1,639
8.	Mtibwa	16,109	653	306	125	97	166.5	1,348
9.	North Kilimanjaro	8,069	260	190	249	155	201	1,055
10.	Rondo	31,930	196	209	126	154	207	892
11.	Rubare	2,979	458	438	309		36	1,241
12.	Rubya	6,374	209	304	234	72	76	895
13.	North Ruvu	1,926	81	110	100	170	42	503
14.	Sao Hill	135,903	2,758	2,525	2,616	2,793	2,761	13,453
15.	Shume	4,863	169	120	144	174	161	768
16.	Ukaguru	3,127	270	434	303	230	210	1,447
17.	West Kilimanjaro	7,632	223	256	239	160	144	1,022
18.	Wino	39,400	883	453	420	428	509	2,693
19.	Morogoro	12,950	50	161	283	263	220	977
20.	Silayo	69,756	446	523	888	825	1200	3,882
21.	Mpepo	20,905	200	500	500	500	0	1,700
22.	Iyondo Msimwa	2,935	220	120	200	175	101	816
23.	Buhigwe	1,383	70	206	143	130	126	675
24.	Makere Kusini	65,178	N/A	N/A	N/A	173	334	507
Jumla (ha)		510,663	9,097	9,215	8,347	7,773	7,817	0*

**Hadi Aprili 2022*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Jedwali Na. 6: Mauzo ya Asali na Nta Nje ya Nchi kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi mwaka 2021/2022

Na.	Mwaka	Asali		Na	
		Tani	Thamani	Tani	Thamani
1.	2017/2018	806	8,062,842,500	338	6,598,782,597
2.	2018/2019	608	4,860,834,400	179	1,437,865,600
3.	2019/2020	2,032	13,413,721,200	251	3,865,400,000
4.	2020/2021	1,988	19,878,220,000	393	6,489,999,500
5.	2021/2022*	1,201.98	12,019,766,000	747.56	14,951,148,000
	Jumla	0	0	0	0

**Hadi Aprili 2022*

Jedwali Na. 7: Mwenendo wa Biashara ya Utalii kuanzia mwaka 2017 hadi 2021

Mwaka		2017	2018	2019	2020	2021
Idadi ya watalii wa kimataifa		1,327,143	1,505,702	1,527,230	620,867	922,692
Watalii wa Hotelini		1,163,752	1,404,672	1,353,279	563,779	848,936
Mapato (US \$ million)		2,258.96	2,595.59	2,604.46	714.5	1,310.34
Wastani wa siku za Mtalii kukaa nchini		10	10	13	10	10
Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku (US \$)	<i>Package Tour</i>	410	331	379	312	364
	<i>Non- Package Tour</i>	139	135	216	115	141

Jedwali Na. 8: Idadi ya Wanafunzi Waliidahiliwa katika Vyuo vya Wizara kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022

Chuo	Wanyamapori			Utalii	Misitu na Nyuki			Jumla
	CAWM- Mwaka	PWTI - Pasiansi	Likuyu Seka - maganga		NCT - Utalii	FITI - Moshi	BTI - Tabora	
2017/2018	551	441	97	228	133	201	672	2,323
2018/2019	600	441	140	556	180	266	803	0
2019/2020	846	300	298	550	250	400	825	3,469
2020/2021	929	343	162	1,087	224	408	867	4,020
2021/2022	834	410	204	1,082	286	378	892	0
Jumla Kuu	0	0	0	0	0	0	0	0

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Jedwali Na. 9: Idadi ya Wageni Waliotembelea Vituo vya Mambo ya Kale na Mapato kuanzia mwaka 2017/2018 hadi 2021/2022

Kituo	2017/2018		2018/2019		2019/2020		2020/2021		2021/2022 (hadi Aprili, 2022)	
	Wageni	Mapato	Wageni	Mapato	Wageni	Mapato	Wageni	Mapato	Wageni	Mapato
Magofu ya Kale	10,458	27,242,000	19,724	42,525,000	34,226	70,863,000	21,259	39,857,800	31,101	15,080,000
Zama za Mawe Isimila	1,445	8,167,000	2,634	11,469,000	2,392	10,214,000	6,823	14,866,924.5	7,490	18,972,916
Mji Mkongwe, Bagamoyo	6,798	24,324,000	11,302	32,845,200	18,392	50,793,624	9,573	21,162,000	18,848	6,113,000
Makumbusho ya Mkwawa - Kalenga	1,501	2,105,000	2,408	4,601,000	1,655	3,267,300	3,672	5,966,730	4,737	7,173,150
Magofu ya Kiwani na Songo Mhara	1,083	10,439,000	2,990	18,738,000	3,740	40,538,000	4,040	27,563,500	4,870	27,742,750
Kimondo cha Mbozi	1,368	3,039,000	3,604	6,596,000	2,705	5,061,440	3,726	11,252,480	1,692	4,211,160
Mapango ya Amboni	21,662	19,377,000	11,086	21,271,000	8,308	17,789,240	8,434	18,692,280	12,494	25,053,760
Magofu ya Tongoni	104	792,000	470	1,098,000	345	984,000	192	373,000	164	186,000
Dkt. Livingstone Ujji, Kigoma	2,606	6,224,000	3,742	8,547,180	3,198	7,786,000	3,027	6,876,475	3,551	7,793,390
Tembela Kivihara	361	902,000	407	828,000	506	919,000	392	338,000	365	600,000
Michoro ya Mambani Konda, Kolo	1,766	12,550,000	1,959	16,662,000	2,765	17,543,000	2,316	9,407,000	4,376	7,848,000
Makumbusho ya Caravan Serai, Bagamoyo	1,814	4,246,000	4,283	9,374,000	3,028	6,250,880	2,190	3,478,000	4,254	7,585,000
Nyumba Kumbukizi ya Mwl. Nyerere - Wagomeni	302	608,000	195	494,000	0**	0**	181	283,000	1,128	1,864,400
Jumla	51,268	120,015,000	64,804	175,048,380	81,260	232,009,484	0	0	0	0

**Kituo kilifungwa kwa ajili ya ukarabati mkubwa

Jedwali Na. 10: Idadi ya Wageni Waliotembelea Makumbusho ya Taifa na Mapato Kuanzia Mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022

KITUDO	TAKUMUZA WAGENI NA MAPATO											
	2019/2020			2020/2021				2021/2022 (Hadi Aprili, 2022)				
	Nje	Ndani	Jumla	Nje	Ndani	Jumla	Mapato	Nje	Ndani	Jumla	Mapato	
Nyumba ya Utamaduni	11,391	13,198	24,589	200,914,700	4,011	17,588	21,599	151,187,860	3,657	39,995	43,652	192,587,487
Kiji cha Makumbusho	2,281	5,115	7,396	74,029,200	497	234,345	234,842	125,218,267	1,061	481,254	482,315	148,258,533
Aziemia Ausha	291	4,235	4,526	14,961,400	52	2,395	2,447	8,702,950	123	3,314	3,437	17,666,300
Vita ya Majimaji	99	3,271	3,370	5,964,500	21	10,083	10,104	7,363,800	21	2,312	2,333	49,541,900
Mwalimu J. K Nyerere	62	8,809	8,871	11,231,500	15	6,285	6,300	13,633,000	15	5,353	5,368	13,192,000
Elimu Mumbwe	1,995	4,173	6,168	49,071,250	379	7,768	8,147	32,137,350	640	4,124	4,764	19,859,500
Dkt. Rashid Kawawa	-	-	-	-	-	-	-	-	4	360	364	1,005,500
Mji Mkongwe Mkindani	-	-	-	-	-	-	-	-	2	943	945	1,107,000
JUMLA	16,119	38,801	54,920	356,172,550	4,975	278,464	283,439	338,243,227	0	0	0	0

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Jedwali Na. 11: Muhtasari wa Bajeti ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2022/2023

Na	Na ya Madi	Jinala Madi	Fedha zinazotambua kwamwaka 2022/2023 (Sh)			
			Fedha za Ntari	Fedha za Nje	Jumla	Mhisani
(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)	(vi)	(vi)
1003	Sera na Mienzo					
1.	5203	Uimamizi wa Mfalasi na Kuendeleza Utalii Ukanda wa Kusini (REGROW)	141,000,000	61,184,930,496	0	WB/ CoT
2.	6251	Five year Medium Term Strategic Plan for Public Finance Management Reform Programme (PFMP)	0	145,750,000	145,750,000	Finland
Jumla Ntango			141,000,000	0	0	
2001	Wanyamapori					
3.	4810	Kujenga Uwezo wa Mbeno ya Hfachi, Mepori ya Akibara Kikosi Chidi Ujangili	188,000,000	0	188,000,000	CoT
4.	4812	Kuzua na Kupambana na Ujangili na Bishara Haramu ya Nyara	0	2,916,531,100	2,916,531,100	UNDP
Jumla Ntango			188,000,000	2,916,531,100	0	
3001	Msituna Nyuki					
5.	4647	Panda Mii Kibishara	0	3,360,500,000	3,360,500,000	Finland
6.	4648	Kujenga Uwezo wa Taasisi na Mafunzo ya Msituna Uluaji Nyuki	141,000,000	0	141,000,000	CoT
7.	4661	Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mzao ya Nyuki (BEVAC)	0	2,948,860,404	2,948,860,404	EU
Jumla Ntango			141,000,000	6,309,360,404	6,450,360,404	
4001	Utalii					
8.	4816	Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MCE)	668,000,000	0	668,000,000	CoT
Jumla Ntango			668,000,000	0	0	
Taasisi za Wiza						
9.	4813	Madi ya TANAPA	60,646,469,000	0	60,646,469,000	CoT
10.	4814	Madi ya NCA	29,340,231,000	0	29,340,231,000	CoT
11.	4817	Madi ya TAWA	15,944,893,000	0	15,944,893,000	CoT
12.		NCT	2,820,000,000	0	2,820,000,000	CoT
Jumla Ntango			0	0	108,751,593,000	
JUMAKU			109,879,930,000		70,556,572,000	

Jedwali Na. 12: Namba za Simu za kutoa Taarifa kuhusu Wanyamapori Wakali na Waharibifu

Na.	TAASISI/KANDA	FREE TOLL NUMBER	NAMBA YA TTCL
1.	Wizara - Dodoma	0800110076	0734986511
2.	Ngorongoro	0800110087	0734986512
3.	TAWA - Manyoni	0800110089	0734986513
4.	TAWA - Iringa	0800110090	0734986514
5.	TAWA - Morogoro	0800110093	0734986515
6.	TAWA - Dar es Salaam	0800110098	0734986516
7.	TANAPA - Mikumi	0800110099	0734986517
8.	TANAPA - Mbarali	0800110068	0734986518
9.	TAWA - Masasi	0800110067	0734986519
10.	TANAPA - Bunda	0800110059	0734986520
11.	TAWA - Tunduru	0800110054	0734986521
12.	TAWA - Tabora	0800110048	0734986522
13.	TANAPA - Mkomazi	0800110046	0734986523
14.	TAWA - Arusha	0800110027	0734986524

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Jedwali Na. 13: Muhtasari wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2022/2023

Na.	Bajeti	Kiasi (Shilingi)
I	Matunizi ya Kawaida	
	Mshahara	175,884,707,000
	Matunizi Mengineyo (O.C)	267,821,860,000
	Jumla Ndogo	443,706,567,000
II	Miradi ya Maendeleo	
	Fedha za Ndani	109,879,593,000
	Fedha za Nje	70,556,572,000
	Jumla Ndogo	180,436,165,000
	JUMLA FUNGU 69 (I +II)	624,142,732,000



Watalii kutoka Israel wakiwasili katika uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). Hatua hiyo ni matokeo chanya ya Filamu maarufu ya 'The Royal Tour' iliyozinduliwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



Simba jike wakiwa wamepumzika katika Hifadhi ya Taifa Serengeti



Muonekano wa Ziwa Ngosi lililopo katika hifadhi ya msitu wa asili kwenye milima ya Upoloto Wilayani Rungwe, Mbeya likiwa ni Ziwa la pili la Kreta kwa ukubwa Barani Afrika.



Muonekano wa Msikiti wa Kilwa Kisiwani ambao ni moja ya kivutio kikubwa cha watalii mkoani Lindi



Muonekano wa vitalu vya miche ya miti katika Shamba la Msitu wa Sao Hill, mkoani Iringa



Uvunaji wa asali kwa njia ya kisasa ukifanyika katika Shamba la Msitu wa Sao Hill



Muonekano wa Mlima Kilimanjaro ambao umekua kivutio kwa watalii wanaotembelea Tanzania.



Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu likiwa limesimama kikakamavu tayari kwa ukaguzi

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante, hoja imeungwa mkono. Ahsante Mheshimiwa Waziri. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati kwa niaba Mheshimia Shekilindi, Mganga Mkuu wa Dawa za Corona. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba taarifa hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard* kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022,

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu makadirio na mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawanda ya uchambuzi; katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua Fungu 69 ambalo ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kufanya ziara na kujiridhisha na hali halisi ilivyo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya fungu lililotajwa hapo juu.

Matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo makuu mawii ambayo ni taarifa ya utekelezaji wa mapato na bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa jitihada anazozifanya ambapo amekuwa akiitangaza Tanzania na vivutio vyake kupitia filamu ya *Royal Tour*. Filamu hii inaongeza na itaendelea kuongeza idadi ya watalii pamoja na kuitangaza nchi yetu kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia maoni ya Kamati kwa kuanza zoezi la kuwajengea miundombinu katika eneo la Handeni, Mkoani Tanga wananchi waliokubali kuhama kwa hiari katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ambapo sasa wananchi hawa watapata haki zao za msingi ikiwa ni pamoja na haki ya kumiliki ardhi, kufanya shughuli zao za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia vyema *forum* ya *Dubai Expro 2020* kutangaza *marketing* yaani fursa mbalimbali za kiuwekezaji zinazopatikana Tanzania. Baada ya maonesho fursa hizo zimevuta wawekezaji katika nyanja tofauti hasa utalii na mazao yake kuja kuwekeza nchini.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, huu umekuwa ni ushauri wa Kamati wa muda mrefu kuhusu utangazaji wa utalii na utekelezaji wake unaonekana kuleta matunda yanayofurahiwa karibu na wananchi wote. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itayaendeleza kwa vitendo yanayofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kuendelea kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi ili kuongeza pato la nchi pamoja na kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mpango; uchambuzi ulifanyika ili kujenga msingi wa kufanya ulinganisho na makadirio kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Maeneo yaliyochambuliwa ni ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Idara za Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Taasisi na Mifuko iliyo chini ya Wizara hiyo ilitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 211.3 kupitia mfumo wa *MNRT*. Hadi kufikia Februari, 2022, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 126.3 sawa na asilimia 60 ya malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mashirika ya Uhifadhi chini ya Wizara ambazo ni *TANAPA*, *TAWA* na *NCAA* yalitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 478 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya hifadhi zetu. Hadi kufikia Februari, 2022 makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 222.8 sawa na asilimia 47 ya malengo waliyojiwekea. Hili ni ongezeko la asilimia tano la makusanyo ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita katika kipindi kama hicho. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika kielelezo namba moja na kielelezo namba mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa kiwango cha makusanyo kimepanda kwa asilimia tano ikilinganishwa na mwaka uliopita 2020/2021, Kamati inaona kuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

mwenendo wa makusanyo kwa taasisi na mashirika haya hauridhishi kwa kuwa yalipaswa kuwa yamekusanya zaidi ya asilimia 60 ya makadirio ndani ya robo tatu ya muda wa uliotarajiwa. Kamati inaona kuwa endapo utalii utapewa kipaumbele na kuboreshwa ipasavyo Wizara itaweza kukusanya zaidi na kuchangia vizuri kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla na kwa uchambuzi huu, ni dhahiri kuwa mwenendo wa makusanyo kwa Wizara na taasisi zake sio mzuri na hautoi mwelekeo mzuri wa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa maendeleo; kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na miradi inayotekelezwa na taasisi ya *TANAPA*, *TAWA* na *NCAA*; jumla ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharamiwa miradi hiyo ni shilingi bilioni 152.8 sawa na asilimia 27 ya bajeti yote ya Wizara, ambapo shilingi bilioni 113.9 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 38.9 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea miradi minne ya Wizara katika mikoa ya Dodoma, Mwanza na Mara kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi namba 4650 kuongeza thamani ya mazao ya misitu; mradi huu ulitekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ufini (Finland). Mradi huu ulikusudiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne kutoka mwaka 2018 hadi 2022 ambapo unatarajiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 25. Lengo ilikuwa ni kuongeza faida kiuchumi, kijamii na kimazingira zinazotokana na misitu ya asili na kupunguza uharibifu wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata fursa ya kukagua utekelezaji wa mradi huu katika msitu wa asili uliopo Mpwapwa katika vijiji sita vya Ikuyu, Chiseyi, Chitemo, Lufusi, Nduga na Lwihomelo. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mradi huu ulitengewa kiasi cha shilingi milioni 208.8. Hadi kufikia

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Februari 2022 kiasi cha shilingi milioni 178.9 sawa na asilimia 86 ya fedha za mradi kilipokelewa na kutumika katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haikuridhishwa na tija ya mradi katika eneo la Mpwapwa kwa kuwa bado haujainuafisha jamii kiuchumi kama ilivyo katika maeneo mengine ambapo mradi huu unatekelezwa. Aidha, jamii haina uelewa kuhusu uwepo wa mradi huu, lakini pia miundombinu mibovu ya barabara kwenye maeneo ya mradi yanapunguza ufanisi na utekelezaji wa mradi huu. Kamati inaona kuwa Serikali irekebishe changamoto zinazopelekea mradi huo kusuasua ili kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi namba 26321247 - ujenzi wa mahema matatu; mradi huu unatekelezwa na TANAPA kwa kutumia fedha za ndani ambapo katika mwaka 2021/2022 mradi ulitengewa kiasi cha shilingi milioni 220 kulingana na makadirio na makisio ya gharama za mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati ilipotembelea mradi huu ilibaini kuwa mkandarasi amefikisha asilimia 25 ya utekelezaji ambapo ulikadiriwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2022. Aidha, Kamati ilibaini kuwa ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mradi huu ulitokana na mlipuko wa homa ya mapafu (UVIKO-19) ulisababisha kukosekana kwa fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu una lengo la kuwavutia watalii wanaopenda kupumzika maeneo tulivu na ya asili na kuongeza mapato kutokana na wageni kukaa kipindi kirefu na kuwezesha uanzishwaji wa zaoau mazao mengine ya utalii wa kutazama nyota kwa watalii watakaolala hifadhini. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuongeza mahema zaidi ili kuongeza idadi ya watalii na mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi namba 26321247 - ujenzi wa lango la Naabi (*Naabi Gate*) unatekelezwa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti; mradi huu ulianza kutekelezwa

katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa kutumia fedha za ndani. Mkataba ulianza utekelezaji mwezi Aprili, 2019 na ulipaswa kukamilika mwezi Novemba, 2019 yaani miezi nane kwa gharama ya shilingi bilioni 1.4. Mradi unahusisha ujenzi wa jengo kuu (*main building*) pamoja na maegesho ya magari. Hadi Kamati inakagua eneo la utekelezaji, mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za utekelezaji mradi ulikumbwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa fedha uliochangiwa na mlipuko wa UVIKO-19. Vilevile kutokana na changamoto za kiuendeshaji mkandarasi ameonesha kushindwa kuendelea na ujenzi, hatua iliyopelekea kusitisha mkataba kwa kufuata taratibu za kisheria na sasa taratibu za ukamilishaji mradi kwa kutumia wataalamu wa ndani na shirika zinaendelea. Ni matumaini ya Kamati kwamba mradi huu utakamilika kwa ufanisi uliokusudiwa kwa kuwa ukamilikaji utawezesha kuboresha huduma kwa watalii, miundombinu ya ukusanyaji mapato pamoja na taswira ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi; mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Korea Kusini kupitia Shirika la Misaada ya Kimataifa (*KOICA*). Gharama za mradi huu ni takribani shilingi bilioni 3.3 (dola za Kimarakeni 1,500,000) lengo likiwa ni kuongeza thamani ya hifadhi ya Serengeti, kutangaza vivutio vilivyo hifadhini, kutoa maelezo na tafsiri ya vivutio kwa watalii na kuwapa watalii uzoefu (*experience*) zaidi kuhusu hifadhi na vivutio vyake. Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha za ndani. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 113.9 lakini hadi Kamati inafanya uchambuzi Wizara ilikuwa imepokea asilimia 11 tu ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekelezaji wa miradi. Kamati haioni kwa namna gani mradi huu muhimu utaweza kutekelezeka ikiwa ndio hali ya upatikanaji wa fedha.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa maendeleo wa ustawi wa Taifa; pamoja na miradi tajwa hapo juu, ipo miradi mingine inayotekelezwa na Wizara kwa kutumia fedha za mpango wa maendeleo wa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya athari za UVIKO-19 zilizotolewa na Serikali. Wizara ya Maliasili na Utalii ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 90.2 sawa na asilimia 6.9 ya fedha yote. Mpango huu unaendelea kuisaidia Wizara kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika maeneo ya Hifadhi za Taifa, mapori ya akiba, mapori tengefu na misitu ya mazingira asili ambazo zilikuwa zimekwama kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuihuisha sekta ya utalii ambayo iliathirika kwa kiwango kikubwa na UVIKO-19 kwa kuingiza sekta hii kwenye mpango huu. Kamati inaitaka Wizara kutumia fedha hizi kwa ufanisi na kwa muda mwafaka kuboresha sekta hii. Aidha, Wizara ihakikishe kwamba inasimamia vizuri miradi iliyokwishaanza ili ikamilike kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa katika utalii na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara ya Maliasili na Utalii Fungu 69 iliidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 418.9 sawa na asilimia 73 ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2022 Wizara ilipokea shilingi bilioni 270.6 sawa na asilimia 64.6 ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika Kielelezo namba tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji huu wa kuridhisha wa fedha za matumizi ya kawaida ingefaa uendane sambamba na upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo hasa fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzingatiaji na ushauri wa Kamati; wakati wa kupitia na kuchambua mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati ilishauri masuala mbalimbali yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali. Sehemu kubwa ya ushauri wa Kamati imezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Kamati ilishauri Serikali kutenga bajeti itakayowezesha ukarabati wa barabara zilizomo ndani ya Hifadhi ya Ruaha ili kuwezesha watalii kufika eneo hilo. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara kupitia Mradi wa *REGROW* imetenga kiasi cha shilingi bilioni 16.6 kwa ajili ya utekelezaji wa ushauri huu.

(b) Kamati ilishauri Serikali iangalie uwepo wa changamoto ya mikataba ya wafanyakazi, waongoza utalii na wapagazi isiyoridhisha katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kuzingatia ushauri huu, iliandaa mikataba ya kisheria ambayo Wakala wa Biashara za Utalii (*Tour Operators*), waongoza watalii, wapagazi na wapishi wanaowaajiri wataisini kabla ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua mbalimbali, Kamati imeridhika kwamba ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara pamoja na taasisi zake katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio na mapato ya matumizi, makadirio ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara inategemea kukusanya jumla ya shilingi bilioni 670.9 kutoka katika sekta ya maliasili na utalii. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 469.4 zitakusanywa na wizara kupitia mfumo wa *TRA* kutoka vyanzo vya *TANAPA*, *NCAA* na *TAWA* na shilingi bilioni 201.5 zitakusanywa na Wizara kupitia mfumo wa *MNRT* kutoka katika Idara, Mifuko na baadhi ya Taasisi zake. Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni pungufu ya asilimia 2.7 ukilinganisha na makadirio ya mwaka wa fedha 2021/

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

2022. Mchanganuo wa makadirio hayo unaoneshwa katika Kielelezo namba nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huu, Kamati ina maoni kwamba uwekaji wa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli unaweza kuleta tija iwapo utazingatia uhalisia vinginevyo Wizara itakuwa na malengo ambayo hayatekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara Fungu 69 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 443.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Iwapo mwenendo wa upatikanaji wa fedha utabaki kama ulivyokuwa kwenye mwaka wa fedha unaoishia wa asilimia 64, ukadiriaji wa matumizi ya kawaida utaonesha kuwa na uhalisia japo tija itaonekana ikiwa utekelezaji wake mradi wa maendeleo utapatikana kwa uwiano huo. ,

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya maduhuli na matumizi kwa miradi ya maendeleo; katika mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu 69 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 180.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha inayoombwa, shilingi bilioni 70.6 ni fedha za nje, na shilingi bilioni 109.9 ni fedha za ndani. Bajeti ya maendeleo imeongezeka kwa asilimia 15 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga bajeti ya fedha za ndani za maendeleo kwa lengo la kuhakikisha miradi inatekelezeka bila kutegemea kwa kiasi kikubwa fedha za nje. Aidha, Kamati bado inahimiza utoaji wa fedha zilizotengwa kwa wakati na kwa kiasi kinachotarajiwa ili kuhakikisha kuwa hakuna mradi unaoathirika kutokana na ukosefu wa fedha kutofika kwa wakati. Kielelezo namba tano kinafafanua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tija ya fedha zilizotengwa itapatikana tu ikiwa fedha hizo zitatolewa kwa wakati, kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kiwango tarajiwa na Wizara kusimamia vema utekelezaji wa miradi iliyopo na inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati; kwa kuzingatia uchambuzi uliofanywa na Kamati naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

Moja, hali ya upatikanaji wa fedha usioridhisha hasa fedha za ndani za maendeleo, inazorotesha sekta ya maliasili na utalii ambapo uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya hifadhi na maeneo mengine muhimu ambayo yanatumika kama kichocheo cha utalii unafanyika chini ya kiwango. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha zote za maendeleo na kwa wakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ambayo pia yanaendana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 inayosisitiza katika kuongeza na kukuza wigo wa bidhaa au mazao ya utalii ili kufikia watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025 pamoja na kuongeza mapato kutoka dola za Kimarekani bilioni 2.6 mwaka 2020 hadi dola za Marekani bilioni sita mwaka 2025.

Pili, kasi ya ukusanyaji wa maduhuli; kasi ya upatikanaji wa fedha kwenye Wizara na Taasisi zake bado hairidhishi ambapo kiwango cha makusanyo kilikuwa chini ya lengo ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekelezaji. Kamati inaishauri na kusisitiza umuhimu wa Wizara kupitia Taasisi na Idara zake, kuwawekea viashiria muhimu vya kiutendaji (*KPI*) Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini yake na malengo ya makusanyo kwa kila robo mwaka na malengo hayo yawe moja ya kipimo cha utendaji kazi.

Aidha, Serikali iendeleo kuongeza ubunifu katika kutangaza na kutambulisha vivutio vya utalii nchini ili kuwavutia watalii wa nje na ndani kwa lengo la kuongeza mapato na kuboresha maisha na ustawi wa jamii.

Tatu, utambuzi na utangazaji wa vivutio; utambuzi na utangazaji wa vivutio vingine vya utalii kama utalii wa fukwe (*marine tourism*), utalii wa malikale (*traditional tourism*), utalii

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wa misitu (*forest tourism*) na utalii wa nyuki (*api tourism*) bado haujapewa kipaumbele cha kuridhisha na hivyo, Kamati inaamini kuna mapato makubwa yanapotea kwa njia hii.

Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza nguvu katika utambuzi na utangazaji wa vivutio vingine vya utalii kama ilivyoweka kwenye utalii wa wanyama ili kuhakikisha kuwa mapato katika vivutio hivyo hayapotei.

Nne, mradi wa usimamizi wa maliasili Kanda ya Kusini (*REGROW*); mradi huu umeonesha manufaa kwa kuboresha miundombinu katika hifadhi, utatuzi wa migogoro baina ya wanyamapori na binadamu, pamoja na uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi za jamii ambazo zimesaidia kuimarisha uhifadhi na kuongeza kipato. Hivyo, Serikali ifanye tathmini ya kutosha kuhusu utekelezaji wa mradi huu ili hifadhi zingine ziweze kunufaika na mradi huu katika awamu ya pili ya mradi.

Tano, migogoro ya mipaka kati ya hifadhi na vijiji; migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hifadhi inayoendelea katika maeneo mbalimbali nchini imeleta madhara makubwa kiuchumi na kijamii na kupelekea kuzorota kwa ustawi wa jamii zinazopakana na hifadhi. Hivyo, Serikali iongeze kasi katika utatuzi wa migogoro hiyo kwa wakati ili kuepusha madhara zaidi yanayoendelea kujitokeza katika sehemu hizo kote nchini.

Aidha, Serikali iweke mpango mkakati wa kujenga barabara kuzunguka hifadhi za Taifa kwa kuanzia na zile zenye migogoro ili zitumike kama mipaka, pamoja na ushirikishwaji wa wananchi katika zoezi la kuweka mipaka ili kuwa na uelewa wa pamoja na kuepusha migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, changamoto ya wanyamapori wakali na waharibifu; kwa muda mrefu sasa kumekuwa na changamoto ya muingiliano kati ya wananchi na wanyamapori wakali na waharibifu ambapo matukio ya uharibifu wa mali na kuuwa wananchi yamekithiri katika maeneo mbalimbali nchini. Hivyo Serikali ichukue hatua

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

madhubuti na ya haraka katika kukabiliana na changamoto za migongano ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu kama vile tembo, mamba, tumbili na wengineo ili kuondoa madhara yanayoendelea kujitokeza dhidi ya binadamu bila ya kuathiri uwepo wa wanyama hao.

Saba ni changamoto ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu isiyokuwa ya Serikali imeleta mgongano kwenye matumizi ya rasilimali hizo na kusababisha uharibifu unaotishia uendelevu wa misitu yetu nchini. Aidha, changamoto inaweza kuondolewa kwa kuwa na mamlaka moja inayosimamia na kuratibu shughuli zote za misitu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (*TFS*) kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania ili kuipa nguvu ya kisheria na kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria na sera katika sekta hii zilizopitwa na wakati zinasababisha changamoto katika utekelezaji wake kwa kuwa haziendani na mabadiliko ya mazingira ya sasa. Kwa mfano, Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999, Sera ya Taifa ya Misitu yam waka 1998 na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998 na Sheria ya Mambo ya kale Na. 2 ya mwaka 1964 na marekebisho yake ya mwaka 1979 zimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali iharakishe mapitio ya sera na sheria zote ambazo zimepitwa na wakati ili ziweze kukidhi azma ya kuleta maendeleo yanayoendana na mabadiliko ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (*TAWA*) mamlaka hii imeanzishwa kwa amri ya kisheria na Waziri mwenye dhamana ya Maliasili chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 ili iweze kufanya kazi ya kusimamia mapori ya akiba, mapori tengefu, jumuiya za hifadhi ya wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu. Aidha, kazi zote za mamlaka hii

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

zinasimamiwa na Bodi ya Ushauri badala ya Bodi ya Utendaji jambo linaloathiri utendaji wa mamlaka, kwa kuwa Bodi hiyo inakosa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori itakayoainisha bayana majukumu yake na kuanzisha Bodi ya Utendaji itakayoipa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt. Balozi Pindi Hazara Chana (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Mary Francis Masanja (Mb), Katibu Mkuu Dkt. Francis Kasabubu Michael pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nimshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelewa J. Mwihambi kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote. Vilevile nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein akisaidiwa na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Dickson M. Bisile, bila kuwasahau Makatibu walioandaa taarifa hii na kuhakikisha inakamilika kwa wakati, akiwemo Ndugu Ramadhan Abdallah, Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Rehema Kipera pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Mwimbe John. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lipokee taarifa hii ili lijadili na kukubali kuidhinisha Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha taarifa hii. (*Makofi*)

TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 *Maelezo ya Awali*

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ina sehemu kuu Nne (4). ambapo sehemu ya kwanza ni Utangulizi, sehemu ya pili ni Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Sehemu ya tatu ni Maoni na Ushauri wa Kamati na sehemu ya nne ni Hitimisho.

1.2 *Msingi wa Uchambuzi wa Kamati*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 6(6) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, vinaipa Kamati jukumu la kufanya

uchambuzi huu. Aidha, Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lijadili hoja ya Waziri wa Maliasili na Utalii kwa pamoja na Taarifa hii.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua **Fungu 69** ambalo ni Wizara ya Maliasili na Utalii. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kufanya ziara za kujiridhisha na hali halisi ilivyo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya fungu lililotajwa hapo juu.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo makuu mawii ambayo ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa jitihada anazozifanya ambapo mheshimiwa Rais amekuwa akiitangaza Tanzania na vivutio vyake kupitia Filamu ya 'Royal Tour'. Filamu hii inaongeza na itaendelea kuongeza idadi ya watalii pamoja na kuitangaza nchi yetu kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia maoni ya Kamati kwa kuanza zoezi la kuwajengea miundombinu katika eneo la Handeni mkoani Tanga wananchi waliokubali kuhama kwa hiari katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ambapo sasa wananchi hawa

watapata haki zao za msingi ikiwa ni pamoja na haki ya kumiliki ardhi na kufanya shughuli zao za maendeleo.

Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia vema forum ya Dubai Expro 2020 kutangaza (marketing) fursa mbalimbali za kiuwekezaji zinazopatikana Tanzania. Baada ya maonyesho, fursa hizo zimevuta wawekezaji katika Nyanja tofauti hasa utalii na mazao yake kuja kuwekeza nchini.

Mheshimiwa Spika, huu umekuwa ni ushauri wa Kamati wa muda mrefu kuhusu kutangaza utalii na utekelezaji wake unaonekana kuleta matunda yanayofurahiwa na karibu wananchi wote. Ni matumaini ya Kamati kuwa Serikali itayaendeleza kwa vitendo yanayofanywa na Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuutangaza utalii ndani na nje ya nchi ili kuongeza pato la nchi pamoja na kuboresha maisha yao.

2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, uchambuzi ulifanyika ili kujenga msingi wa kufanya ulinganisho na makadirio kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Maeneo yaliyochambuliwa ni ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa Fedha 2021/2022.

2.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Idara za Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na Taasisi na Mifuko iliyo chini ya Wizara hiyo ilitarajiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 211,331,273,727** kupitia mfumo wa MNRT Portal. Hadi kufikia Februari, 2022, Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 126,282,627,547**, sawa na **asilimia 60** ya malengo waliyojiwekea. Aidha, Mashirika ya Uhifadhi chini ya Wizara ambazo ni TANAPA, TAWA na NCAA yailitarajiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 478,014,580,522** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya hifadhi zetu. Hadi kufikia Februari, 2022 makusanyo yalikuwa **shilingi 222,829,133,431** sawa na **asilimia 47** ya malengo waliyojiwekea. Hili ni ongezeko la **asilimia 5** la

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

makusanyo ikilinganishwa na Mwaka wa fedha uliopita katika kipindi kama hicho.

Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika Kielelezo Na.1 na Kielelezo Na.2

Kielelezo Na. 1: Fungu 69 - (Wizara) Makadirio na Makusanyo Halisi katika mwaka wa fedha, 2021/2022

Idara	Makadirio 2021/2022 Tsh.	Kilichotakiwa Kukusanywa Feb, 2022 Tsh.	Kilichokusanywa Tsh.	Kilichokusanywa %
Utawala na Rasilimali Wätu, Utalii na Mfukowa Taifa wa Mambo kale	22,657,242,000	15,089,723,172	5,841,822,173	25.8
Taasisi	181,051,970,727	120,580,612,504	116,147,261,118	64
Mfuko ya Uhifadhi TAFF na TWFF	7,622,061,000	5,076,292,626	4,293,544,256	56
Jumla	211,331,273,727	140,746,628,302	126,282,627,547	60

Chanzo: Randama za Fungu 69

Kielelezo Na. 2: Fungu 69(Mashirika ya Wizara) Makadirio na Makusanyo Halisi katika mwaka wa Fedha,21/2022.

Taasisi	Makadirio na Makusanyo hadi Februari, 2022			
	Makadirio kwa Mwaka 2021/2022 Tsh	Kiasi kilichotakiwa kukusanywa hadi Februari, 2022 Tsh	Makusanyo hadi Februari, 2022 Tsh	%
(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)
TANAPA	253,704,221,522	168,967,011,533	125,233,324,726	49
NCAA	162,663,179,000	108,333,677,214	63,442,273,994	39
TAVA	61,647,180,000	41,057,021,880	34,153,534,711	55
JUMA	478,014,580,522	318,347,710,623	222,829,133,431	47

Chanzo: Randama za Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi umeonesha kwamba:-

a) Jumla ya makusanyo ya maduhuli kwa Wizara umefikia **asilimia 60** ya lengo hadi kufikia Februari, 2022 ikiwa ni ndani ya robo tatu ya muda wa utekelezaji wa majukumu;

b) Mwenendo wa makusanyo ya Taasisi za Wizara ya Maliasili na Utalii umefikia **asilimia 47** ya lengo ndani ya robo tatu ya muda wa utekelezaji wa majukumu;

c) Kwa makusanyo haya na kwa kipindi kilichobaki cha utekelezaji, ni vigumu kufikia malengo kwa kuwa tayari karibu asilimia 75 ya muda wa utekelezaji umeshapita;

d) Makusanyo ya chini ya asilimia 60 ndani ya robo tatu ya muda ni nyuma ya malengo

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuwa kiwango cha makusanyo kimepanda kwa **asilimia 5** ikilinganishwa na Mwaka uliopita 2020/2021, Kamati inaona kuwa mwenendo wa makusanyo kwa Taasisi na Mashirika haya hauridhishi kwa kuwa yalipaswa kuwa yamekusanya zaidi ya **asilimia 60** ya makadirio ndani ya robo tatu ya muda wa utekelezaji. Kamati inaona kuwa endapo utalii utapewa kipaumbele na kuboreshwa ipasavyo Wizara itaweza kukusanya zaidi na kuchangia vizuri kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla na kwa uchambuzi huu, ni dhahiri kuwa mwenendo wa makusanyo kwa Wizara na Taasisi zake sio mzuri na hautoi mwelekeo mzuri wa kufikia malengo yaliyokusudiwa.

2.2.2 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara hii inatekeleza jumla ya miradi 7 ya Fungu 69 pamoja na miradi inayotekelezwa na taasisi za TANAPA, TAWA na NCAA. Jumla ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharamiwa miradi hiyo ni **Shilingi 152,772,880,000** sawa na asilimia 27 ya Bajeti yote ya Wizara, ambapo **Shilingi 113,893,184,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 38,879,696.000** ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea miradi (4) ya Wizara katika mikoa ya Dodoma, Mwanza na Mara kama ifuatavyo: -

(a) Mradi Na.4650: Kuongeza Thamani ya Mazao ya Misitu (Forestry and Value Chain Development Programme (FORVAC))

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ufini (Finland). Mradi huu ulikusudiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne (2018-2022) ambapo unatarajiwa kutumia Jumla ya **Shilingi 25,000,000,000**. Lengo ilikuwa ni kuongeza faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira zinazotokana na misitu ya asili na kupunguza uharibifu wa misitu. Kamati ilipata fursa ya kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Msitu wa Asili uliopo **Mpwapwa** katika vijiji sita vya lkuyu, Chiseyi, Chitemo, Lufusi, Nduga na Lwihomelo. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 mradi huu ulitengewa kiasi cha **Shilingi 208,765,829**. Hadi kufikia Februari 2022, kiasi cha **Shilingi 178,889,300** sawa na **asilimia 86** ya fedha za mradi kilipokelewa na kutumika katika utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa na tija ya mradi katika eneo la Mpwapwa kwa kuwa bado haujainufaisha jamii kiuchumi kama ilivyo katika maeneo mengine ambapo mradi huu unatekelezwa. Aidha, jamii haina uelewa kuhusu uwepo wa mradi huu lakini pia miundombinu mibovu ya barabara kwenye maeneo ya mradi yanapunguza ufanisi wa utekelezaji wa mradi huu. Kamati inaona kuwa, Serikali irekebishe changamoto zinazopelekea mradi huo kusuasua ili kuleta tija iliyokusudiwa.

(b) Mradi Namba 26321247 - Ujenzi wa Mahema Matatu katika Hifadhi ya Taifa ya SAANANE

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa na TANAPA kwa kutumia fedha za ndani ambapo katika Mwaka 2021/2022 mradi ulitengewa kiasi cha **shilingi 220,000,000** kulingana na makadirio na makisio ya gharama za mradi.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ilipotembelea mradi huu ilibaini kuwa, mkandarasi amefikisha **asilimia 25** ya utekelezaji ambapo ulikadiriwa kukamilika mwishoni mwa Mwezi Aprili, 2022. Aidha, Kamati ilibaini kuwa ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mradi huu ulitokana na Mlipuko wa Homa ya

Mapafu (UVIKO 19) ulisababisha kukosekana kwa fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mradi huu una lengo la kuwavutia watalii wanaopenda kupumzika maeneo tulivu na ya asili na kuongeza mapato kutokana na wageni kukaa kipindi kirefu na kuwezesha uanzishwaji wa zao/bidhaa nyingine ya utalii wa kutazama nyota kwa watalii watakaolala hifadhini. Ni matumaini ya Kamati kuwa, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuongeza mahema zaidi ili kuongeza idadi ya watalii na mapato.

(c) Mradi Na.26321247 - Ujenzi wa lango la Naabi (Naabi Gate) unatekelezwa katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti

Mheshimiwa Spika, mradi huu ulianza kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa kutumia fedha za ndani. Mkataba ulianza kutekelezwa mwezi Aprili, 2019 na ulipaswa kukamilika mwezi Novemba, 2019 (miezi nane) kwa gharama ya **Shilingi 1,430,000,000**. Mradi unahusisha ujenzi wa jengo kuu (main building) pamoja na maegesho ya magari. Hadi Kamati inakagua eneo la utekelezaji, mradi ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 35**.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za utekelezaji, mradi ulikumbwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa fedha uliochangiwa na mlipuko wa UVIKO – 19. Vilevile, kutokana na changamoto za kiuendeshaji mkandarasi ameonesha kushindwa kuendelea na ujenzi, hatua iliyopelekea kusitisha mkataba kwa kufuata taratibu za kisheria na sasa taratibu za kukamilisha mradi kwa kutumia wataalamu wa ndani ya shirika zinaendelea. Ni matumaini ya Kamati kwamba mradi huu utakamilika kwa ufanisi uliokusudiwa kwa kuwa ukikamilika utawezesha kuboresha huduma kwa watalii, miundombinu ya ukusanyaji mapato pamoja na taswira ya hifadhi.

(d) Mradi Na. 26321247- Ujenzi wa Kituo cha Taarifa Serengeti (Serengeti Media Center)

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Korea Kusini kupitia Shirika la Misaada ya Kimataifa

(KOICA). Gharama za mradi huu ni takribani **Shilingi 3,345,000,000** (Dola za Kimarakeni 1,500,000) lengo likiwa ni kuongeza thamani ya hifadhi ya Serengeti, kutangaza vivutio vilivyo hifadhini, kutoa maelezo na tafsiri ya vivutio kwa watalii na kuwapa watalii uzoefu (experience) zaidi kuhusu hifadhi na vivutio vyake. Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi huu upo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha kutokana na upatikanaji mdogowa fedha za ndani. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wizara iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 113,893,184,000** lakini hadi Kamati inafanya uchambuzi wizara ilikuwa imepokea **asilimia 11** tu ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekelezaji wa miradi. Kamati haioni ni kwa namna gani miradi hii muhimu itaweza kutekelezeka ikiwa hii ndio hali ya upatikanaji wa fedha.

2.2.3 Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Athari za UVIKO-19

Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi tajwa hapo juu, ipo miradi mingine inayotekelezwa na Wizara kwa kutumia fedha za **Mpango wa Maendeleo wa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Athari za UVIKO-19**, zilizotolewa na Serikali. Wizara ya Maliasili na Utalii ilitengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 90.2** sawa na asilimia 6.9 ya fedha yote. Mpango huu unaendelea kuisaidia wizara kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika maeneo ya Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu na Misitu ya Mazingira Asili ambazo zilikuwa zimekwama kutokana na mlipuko wa Ugonjwa wa UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuihuisha sekta ya utalii ambayo iliathirika kwa kiwango kikubwa na UVIKO -19 kwa kuingiza sekta hii kwenye Mpango huu. Kamati inaitaka Wizara kutumia fedha hizi kwa ufanisi na kwa muda mwafaka kuboresha sekta hii. Aidha, Wizara ihakikishe kwamba inasimamia vizuri miradi iliyokwisha anza ili ikamilike kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa katika utalii na kuongeza pato la Taifa.

2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Maliasili na Utalii Fungu 69 iliidhinishwa bajeti ya **Shilingi 418,859,544,000** sawa na **asilimia 73** ya bajeti yote kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Februari, 2022 Wizara ilipokea **Shilingi 270,620,322,510** sawa na **asilimia 64.6** ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Kielelezo Na.3**

Kielelezo Na. 3: Fungu 69 - Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2021/2022

Na.	Idara/Taasisi/ Watakala	Kiasi kilichotakiwa kupokelewa hadi Februari, 2022	Fedha zilizopokelewa hadi Februari, 2022	%ya bajeti iliyoidhinishwa
i)	Matumizi Mengneyo	265,311,860,000	172,777,387,578	65
ii)	Mishahara	153,537,684,000	97,842,934,932	64
	JUMLA1	478,953,796,304	270,620,322,510	64.6

Chanzo: Randama ya Fungu 69

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni **asilimia 64.6** ya fedha iliyotengwa;

(b) Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni wa kuridhisha na unatoa mwelekeo mzuri wa ukamilishaji wa lengo.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji huu wa kuridhisha wa fedha za matumizi ya kawaida, ingefaa uende sambamba na upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo hasa fedha za ndani.

2.2.5 Uzingatiji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yaliyopaswa kuzingatwa na Serikali. Sehemu kubwa ya ushauri wa Kamati imezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Kamati ilishauri Serikali kutenga bajeti itakayowezesha ukarabati wa barabara zilizomo ndani ya hifadhi ya Ruaha ili kuwezesha watalii kufika eneo hilo. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Wizara kupitia Mradi wa REGROW imetenga kiasi cha **Shilingi Bilioni 16.6** kwa ajili ya utekelezaji wa ushauri huu.

(b) Kamati ilishauri Serikali iangalie uwepo wa changamoto ya mikataba ya wafanyakazi, waongoza utalii na wapagazi isiyoridhisha katika sekta ya utalii;

Mheshimiwa Spika, wizara kwa kuzingatia ushauri huu, iliandaa mikataba ya kisheria ambayo Wakala wa Biashara za Utalii (Tour Operators), waongoza watalii, wapagazi na wapishi anaowaajiri wataisini kabla ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Spika, katika hatua mbalimbali, Kamati imeridhika kwamba ushauri wake unaendelea kuzingatwa na Wizara pamoja na Taasisi zake katika utekelezaji wa majukumu yake.

2.3 Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2022/2023

2.3.1 Makadirio ya Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara inategemea kukusanya jumla ya **Shilingi 670,856,583,921** kutoka katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Kati ya fedha hizo **Shilingi 469,364,418,596** zitakusanywa na Wizara kupitia mfumo wa TRA kutoka vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA na **Shilingi 201,492,165,325** zitakusanywa na Wizara kupitia mfumo wa MNRT Portal kutoka katika Idara, Mifuko na baadhi ya Taasisi zake. Kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni pungufu ya **asilimia 2.7** ukilinganisha na Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mchanganuo wa makadirio hayo unaoneshwa katika **Kielelezo Na.4**

Kielelezo Na. 4: Fungu 69-Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli

Nb	Taasis/Idara	Makadirio kwa mwaka wa fedha 2021/2022	Makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023	Orgzeko/pungufu	Orgzeko/Pungufu %
1	IDARA	22,657,242,000	9,507,352,000	-13,149,890,000	-58
2	TAASSI	181,051,970,727	184,397,895,325	3,345,924,598	1.8
3	MFUKO	7,622,061,000	7,586,918,000	-35,143,000	-0.5
4	TANVPA	253,704,221,522	257,524,745,788	3,820,524,266	1.5
5	NCAA	162,663,179,000	148,000,000,000	-14,663,179,000	-9
6	TAWA	61,647,180,000	63,839,672,808	2,192,492,808	3
JMAKU		689,345,854,249	670,856,583,921	-18,489,270,328	-27

Chanzo: Randama ya Wizara Fungu 69

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi umeonesha kuwa: -

(a) Kwa ujumla makadirio ya Makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yamepungua kwa **asilimia 2.7** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

(b) Kwa kuzingatia uzoefu wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambao umefikia **asilimia 51** tu ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekelezaji, bado haitakuwa rahisi kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023; na

(c) Pamoja na kwamba makadirio ya baadhi ya vyanzo vya mapato yamepungua, bado kuna kila dalili kuwa makadirio ya makusanyo ya maduhuli hayaendani na uhalisia na kwa hali hiyo kufikia malengo ya makusanyo imekuwa vigumu.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huu, Kamati ina maoni kwamba, uwekaji wa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli unaweza kuleta tija iwapo utazingatia uhalisia vinginevyo wizara itakuwa na malengo ambayo hayatekelezeki.

2.3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara **Fungu 69** inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi**

443,706,567,000 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 175,884,707,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 267,821,860,000** inaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi, Kamati imebaini kwamba: -

(a) Bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezeka kwa **asilimia -5.6** ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Matumizi kama hayo katika mwaka wa fedha 2021/2022; na,

(b) Hali hii ililinganishwa na uzoefu wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka 2021/2022 ili kuona kama kuna uhalisia. Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, iwapo mwenendo wa upatikanaji wa fedha utabaki kama ulivyokuwa kwenye mwaka wa fedha unaoisha wa **asilimia 64**, ukadiraji wa matumizi ya kawaida unaonesha kuwa na uhalisia japo tija itaonekana ikiwa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo zinapatikana kwa uwiano huo.

2.3.3 Makadirio ya Matumizi kwa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, **Fungu 69** inaomba kuidhinishwa jumla ya **shilingi 180,436,165,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha inayoombwa, **shilingi 70,556,572,000** ni fedha za nje, na **shilingi 109,879,593,000** ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 15** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga bajeti ya fedha za ndani za maendeleo kwa lengo la kuhakikisha miradi inatekelezeka bila kutegemea kwa kiasi kikubwa fedha za nje. Aidha, Kamati bado inahimiza utoaji wa fedha zilizotengwa kwa wakati na kwa kiasi kinachotarajiwa ili kuhakikisha kuwa hakuna mradi unaoathirika kutokana na ukosefu au fedha kutofika kwa wakati. **Kielelezo Na. 5** linafafanua zaidi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kielelezo Na. 5: Fungu 69 - Ulinganisho katika Makadirio ya fedha za Maendeleo

MATUMZI	2021/2022	2022/2023	ONGEZECO/PUNGUFU	ONGEZECO/PUNGU RUP%
Maendeleo Nlani	113,893,184,000.00	109,879,593,000.00	4,013,591,000.00	-3.5
Maendeleo Nje	38,879,696,000.00	70,556,572,000.00	31,676,876,000.00	44.9
Jumla	152,772,880,000	180,436,165,000	27,663,285,000	15.3

Chanzo: Randama za Fungu 69

Mheshimiwa Spika, Katika Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2022/2023, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Bajeti ya maendeleo kwa ujumla imeongezeka kwa **asilimia 8.4**. Ongezeko hili linamaanisha kuwa idadi, thamani na ukubwa wa miradi inayotarajiwa kutekelezwa imeongezeka ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha; na

(b) Fedha za ndani za miradi zimepungua kwa **asilimia 4** wakati fedha za nje zimeongezeka kwa **asilimia 45**. Hali hii inaashiria kuwa, utekelezaji wa miradi ya maendeleo unategemea fedha za nje na hivyo kupunguza umuhimu wa kutenga fedha za ndani za miradi ya maendeleo ambazo zina uhakika wa upatikanaji wake;

Mheshimiwa Spika, tija ya fedha zilizotengwa itapatikana tu ikiwa fedha hizo zitatolewa kwa wakati, kwa kiwango tarajiwa na Wizara kusimamia vema utekelezaji wa miradi iliyopo na inayoendelea.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchambuzi uliofanywa na Kamati naomba kuwasilisha Maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:

1. Hali ya Upatikanaji wa Fedha

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa fedha usioridhisha hasa fedha za ndani za maendeleo, inazorotesha Sekta ya Maliasili na Utalii ambapo uboreshaji wa miundombinu katika maeneo ya hifadhi na maeneo mengine muhimu ambayo yanatumika kama kichocheo cha utalii unafanyika chini ya kiwango. Kamati inaishauri **Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha zote za maendeleo na kwa wakati ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ambayo pia yanaendana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 inayosisitiza katika kuongeza na kukuza wigo wa bidhaa/mazao ya utalii ili kufikia watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025 pamoja na kuongeza mapato kutoka Dola za Kimarekani bilioni 2.6 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani bilioni 6 mwaka 2025;**

2. Kasi ya Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, kasi ya upatikanaji wa fedha kwenye Wizara na Taasisi zake bado hairidhishi, ambapo kiwango cha makusanyo kilikuwa chini ya lengo ndani ya robo tatu ya kipindi cha utekelezaji. Kamati inaishauri na kusisitiza umuhimu wa wizara kupitia Taasisi na Idara zake, kuwawekea viashiria muhimu vya kiutendaji, (KPI) Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini yake na malengo ya makusanyo kwa kila robo mwaka (quarter) na malengo hayo yawe moja ya kipimo cha utendaji kazi. Aidha, Serikali iendelee kuongeza ubunifu katika kutangaza na kuvitambulisha vivutio vya utalii nchini ili kuwavutia watalii wa nje na ndani kwa lengo la kuongeza mapato na kuboresha maisha na ustawi wa jamii;

3. Utambuzi na utangazaji wa vivutio vingine vya utalii

Mheshimiwa Spika, Utambuzi na utangazaji wa vivutio vingine vya utalii kama Utalii wa Fukwe (Marine Tourism), Utalii wa malikale (Traditional Tourism), Utalii wa Misitu (Forest Tourism) na Utalii wa Nyuki (Api Tourism) bado haujapewa kipaumbele cha kuridhisha na hivyo, Kamati inaamini kuna mapato makubwa yanapotea kwa njia hii. Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza nguvu katika

utambuzi na utangazaji wa vivutio vingine vya utalii kama ilivyoweka kwenye utalii wa wanyama ili kuhakikisha kuwa mapato katika vivutio hivyo hayapotei;

4. Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini (REGROW)

Mheshimiwa Spika, mradi huu umeonesha manufaa kwa kuboresha miundombinu katika hifadhi, utatuzi wa migogoro baina ya wanyama na binadamu, pamoja na uwezeshaji wa shughuli za kiuchumi za jamii ambazo zimesaidia kuimarisha uhifadhi na kuongeza kipato. **Hivyo, Serikali ifanye tathmini ya kutosha kuhusu utekelezaji wa mradi huu ili hifadhi zingine ziweze kunufaika na mradi huu katika awamu ya pili ya mradi;**

5. Migogoro ya Mipaka kati ya Hifadhi na Vijiji

Mheshimiwa Spika, migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hifadhi inayoendelea katika maeneo mbalimbali nchini imeleta madhara makubwa kiuchumi na kijamii na kupelekea kuzorota kwa ustawi wa jamii zinazopakana na hifadhi. **Hivyo, Serikali iongeze kasi katika kutatua migogoro hiyo kwa wakati ili kuepusha madhara zaidi yanayoendelea kujitokeza katika sehemu hizo kote nchini. Aidha, Serikali iweke mpango mkakati wa kujenga barabara kuzunguka Hifadhi za Taifa kwa kuanzia na zile zenye migogoro ili zitumike kama mipaka, pamoja na ushirikishwaji wa wananchi katika zoezi la kuweka mipaka ili kuwa na uelewa wa pamoja na kuepusha migogoro isiyo ya lazima.**

6. Changamoto ya Wanyamapori Wakali na Waharibifu

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na changamoto ya muingiliano kati ya wananchi na wanyamapori wakali na waharibifu ambapo matukio ya uharibifu wa mali na kuuwa wananchi yamekithiri katika maeneo mbalimbali nchini.

Hivyo, Serikali ichukue hatua madhubuti na za haraka katika kukabiliana na changamoto za migongano ya binadamu na

wanyamapori wakali na waharibifu kama vile Tembo, Mamba, Tumbili na wengineo ili kuondoa madhara yanayoendelea kujitokeza dhidi ya binadamu bila ya kuathiri uwepo wa wanyama hao.

7. Changamoto ya Udhhibiti wa Matumizi ya Rasilimali za Misitu isiyokuwa ya Serikali Kuu

Mheshimiwa Spika, changamoto ya udhhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu isiyokuwa ya Serikali imeleta mgongano kwenye matumizi ya rasilimali hizo na kusababisha uharibifu unaotishia uendelevu wa misitu yetu nchini. Aidha, changamoto inaweza kuondolewa kwa kuwa na mamlaka moja inayosimamia na kuratibu shughuli zote za misitu nchini. **Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote nchini;**

8. Sheria na Sera Zilizopitwa na Wakati

Mheshimiwa Spika, Sheria na Sera katika sekta hii zilizopitwa na wakati zinasababisha changamoto katika utekelezaji wake kwa kuwa haziendani na mabadiliko ya mazingira ya sasa. Kwa mfano; Sera ya Taifa ya Utalii (1999), Sera ya Taifa ya Misitu (1998) na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki (1998) na Sheria ya Mambo ya kale Na. 2 ya mwaka 1964 na marekebisho yake ya mwaka 1979 zimepitwa na wakati. **Kamati inaishauri Serikali iharakishe mapitio ya Sera na Sheria zote ambazo zimepitwa na wakati ili ziweze kukidhi azma ya kuleta maendeleo yanayoendana na mabadiliko ya sasa; na**

9. Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA)

Mheshimiwa Spika, mamlaka hii imeanzishwa kwa amri ya kisheria (*establishment order*) na Waziri mwenye dhamana ya Maliasili chini ya Kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 ili iweze kufanya kazi ya kusimamia mapori ya akiba, mapori tengefufu, jumuiya za hifadhi ya wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu. Aidha, kazi zote za mamlaka hii zinasimamiwa na Bodi ya Ushauri

badala ya Bodi ya Utendaji jambo linaloathiri utendaji wa mamlaka kwa kuwa Bodi hiyo inakosa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. **Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori itakayoainisha bayana majukumu yake na kuanzisha Bodi ya Utendaji itakayoipa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake.**

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*): -

1. Mhe. Ally Juma Makoa, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Shaaban Omary Shekilindi, Mb – M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Jafari Wambura Chege, Mb
4. Mhe. Soud Mahammed Jumah, Mb
5. Mhe. Phillip Augustino Mulugo, Mb
6. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
7. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
8. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
9. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb
10. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
11. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said, Mb
12. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb
13. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb
15. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
16. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb
17. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
18. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
19. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb
20. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb
21. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb

22. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb
23. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi, Mb
24. Mhe. Dkt. Florence G. Samizi, Mb
25. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb
26. Mhe. Joseph Zakarious Kamonga, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Balozi Pindi Hazara Chana (Mb), Naibu Waziri Mhe. Mary Francis Masanja (Mb), Katibu Mkuu Dkt. Francis Kasabubu Michael pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nimshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelewa J. Mwihambi (ndc) kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote. Vilevile, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein (ndc), akisaidiwa na Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Dickson M. Bisile Bila kuwasahau Makatibu walioandaa taarifa hii na kuhakikisha inakamilika kwa wakati, akiwemo Ndg. Ramadhan Abdallah, Ndg. Elieka Saanya na Ndg. Rehema Kipera pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lipokee Taarifa hii ili lijadili na kukubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kama yalivyowasilishwa na mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ally Juma Makoa, Mb

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,
MALIASILI NA UTALII**

Juni, 2022

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Makamu Mwenyekiti kwa kusoma vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, Makamu Mwenyekiti wetu huyu Ndugu Shekilindi ni mtaalam wa dawa za asili, sasa haya makofi haya yanawezekana amewapitia baadhi yenu. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni walioingia Bungeni muda huu mgeni wa Bunge ambaye ni Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa KKKT Kijitonyama Dkt. Herioni Kimaro ambaye yuko kwenye Jukwaa la Spika nafikiri ameshashuka nchini. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wako wageni mbalimbali waliotembelea Bunge wasimame kwa pamoja wote, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo wanafunzi 118 kutoka Chuo Kikuu Mtakatifu Augustine cha Jijini Mwanza wanasoma kozi ya sheria karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 51 kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru Arusha karibuni. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Mipango cha Jiji la Dodoma karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza michango tunaanza na Mheshimiwa Mtaturu, jiandae Mheshimiwa Nehemia Gwau na ajiandae Neema Mgaya.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunifanya niwe wa kwanza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu na kwa hakika inawezekana ni baraka za Mheshimiwa Shekilindi kwa namna ambavyo amekuwa ni mtu mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutujalia uzima na afya

kukutana na leo, lakini pili nichukue nafasi hii sauti yangu sio nzuri sana, lakini nitajitahidi hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kazi nzuri anayofanya kuliongoza Taifa letu hasa kwenye sekta hii ya utalii tunamshukuru sana kwa namna alivyojitoa kimasomaso, kuhakikisha kwamba anatangaza vivutio vyetu kupitia *The Royal Tour* ambayo kwa kwell sisi tunaona ina maana kubwa sana kama nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *The Royal Tour* imeenda kuzinduliwa katika sehemu ambayo watu hawavijui vivutio vyetu, imeenda kuzinduliwa katika nchi za Ulaya. Nina amini kabisa wale ambao walishiriki na kuona vivutio vile leo tunaanza kuona matokeo yake. (*Makofi*)

Kwa hiyo, yule ambaye anaenda kupinga au ku-*criticize* suala la *Royal Tour* huyo ajuu mambo ya utalii tumuache. Kuna nchi zimefanya kazi kubwa ya kufanya *promotion* ya vivutio vyao, sisi tumefanya kwa kiasi, lakini mkuu wa nchi alivyoingia na kufanya jambo hili limetupa heshima kubwa sana duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ile filamu kila mtu akiangalia anajua kabisa anatoka Ulaya anakwenda kuona Serengeti, anakwenda kuona Mlima Kilimanjaro, anaenda kuona vivutio mbalimbali ambavyo ni vya kipekee katika nchi yetu. Kwa hiyo, sisi Watanzania tuendeleo kumuunga mkono Mheshimiwa Rais, Wizara kazi aliyofanya Mheshimiwa Rais muendeleo kui-*brand* vizuri, tusiibeze na tusiache kazi hii ni kubwa ina heshima kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiongozi wa nchi kuacha kazi zake na kuingia kufanya kazi ya sekta ni jambo kubwa na la kupigiwa mfano. Kwa hiyo mimi nilitaka nianze na hili kumpongeza sana na kuhakikisha kwamba tunafanya hivyo, matokeo tumeanza kuyaona, tumeanza kuona watu wengi wanaanza kuingia nchini kwetu kwa ajili ya kuja kuanza kuangalia vivutio vyetu, hilo nataka nisema kama la kwanza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Waziri Pindi Chana...

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa kwa nani?

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Naibu Spika, niko hapa Mheshimiwa Ramadhan.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba huu muda tunaongea mchezaji aliyekuwa wa *Manchester United* ambaye sasa hivi anacheza *PSG* ya Ufaransa Ander Herrera yuko Serengeti na matokeo ni *Royal Tour*. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Haya Mheshimiwa Mtaturu.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Naibu Spika, napokea kwa heshima kabisa hayo ndio matokeo ya *Royal Tour* ambayo tumeifanya, sasa katika hili nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri dada yangu Pindi Chana kwa kupewa heshima kubwa ya kuongoza sekta hii. Tunakujua wewe ni mtu ambaye unajua namna ya kufanya kazi hii nzuri ya kuweza kwenye eneo la diplomasia ulifanya vizuri, lakini eneo hili ninaamini utafanya vizuri zaidi ukisaidiana na mwenzako Naibu Waziri dada yangu Mary Masanja pamoja na Katibu Mkuu na wote katika wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kabisa tutaendelea kuwapa *support* kuhakikisha kwamba lengo la nchi yetu kufikisha watalii milioni tano kufika mwaka huu wa fedha tunapoenda kwa sababu ilani yetu ya uchaguzi imeeleza wazi kwamba lengo letu tufikishe watalii milioni tano, hatuwezi kufikisha milioni tano bila kutangaza vivutio ambavyo tunavyo katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nilitaka nishauri mambo machache ya kuweza kuongeza chachu katika eneo hili. La kwanza kumekuwa kweli kuna tozo mbalimbali zinatozwa, kumekuwa na kelele huko nyuma kwamba watoa huduma ambao ni wenzetu ambao walikuwa wanafanya kazi hii wamekuwa wakilalamikia baadhi ya tozo, niipongeze sana Serikali kuna baadhi ya tozo zimeondolewa, leo hii kuna baadhi ya watoa huduma wameanza kufaidika na kazi hiyo nzuri ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado tunawaomba mkae na watoa huduma hawa ambao wanafanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha inaleta na kusimamia na kuwaleta watalii. Lakini eneo hili wanaomba sana mtawanyiko wa maofisi ya kwenda kulipa tozo walipe *TARA*, waende halmashauri waende wapi imekuwa ikiwapotezea muda wanaomba wawe na dirisha moja la kuweza kulipa tozo zote wasipoteze muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo zinaweza karibia 50 ukasema siku tatu/nne unashughulikia tu kulipa mgeni mmoja inapoteza muda na itatuchelewesha sana kufikia lengo la kupata watalii wengi. *(Makofi)*

Lakini la pili ni suala la *VAT*; *VAT* kweli hamna anayekataa kulipa lakini kumekuwa na tatizo la kulipa *VAT on deposit*, anapolipa mgeni kule nje analipa moja kwa moja kwa yule mtoa huduma, mtoa huduma yule anakuwa anakatwa palepale *VAT*, ikitokea huyu mtalii ame-cancel safari yake ile *VAT* analipa huyu mwenzetu wa Tanzania, maana yake ni kwamba anaingia hasara na inatia hasara kampuni yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana hizi fedha zilipwe pale kwenye *deposit*, lakini waje kwenye maeneo ya tozo mbalimbali hiyo itakuwa umemtendea haki huyu mtoa huduma, lakini pia itakuwa ni halisia, unaweza kujikuuta unalipisha *VAT* mara mbili, mara tatu kitu wanachofanya *destination* ya Tanzania inakuwa ghali kuliko

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

eneo lolote. Hii nayo itakuwa kikwazo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hatupati watalii wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu ni suala la viza wamekuwa wakilalamika kwamba viza yetu wanapolipia *online* kumekuwa na ucheleweshaji iko *slow* sana yuko kule anataka alipie viza ili apate ruhusa ya kukata tiketi anashindwa. Kwa hiyo matokeo yake ana-*cancel* safari anashindwa na ameamua kutafuta eneo lingine, hili nalo ni kikwazo kingine naomba mkalifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la wanyama hawa wavamizi kama tembo, mimi naomba nitoe pole sana kwa wananchi wangu wa Ikungi, Singida Mashariki kwenye Kijiji cha Ntewa pale Ntuntu, juzi mtoto wa miaka miwili na nusu alikanyagwa na tembo. Eneo la Ikungi ni mbali sana na hifadhi leo hii tunaongea habari ya Ikungi sasa tunaanza kuwa na uvamizi wa tembo, lakini mnatuambia tembo wako karibu 60,000 mnasema ni tembo wachache, je, wakifika laki moja, mbili hawa tembo itakuwaje nchi hii? (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima wenzetu wataalam wa Wizara hii wakae wasiwe wanatuletea *story* iliyozeleka ya *corridor*/mapito ya tembo ya miaka, leo hii watu wengi wanaumia wanakufa mali zao zinaharibiwa kwa sababu tu tembo wanazunguka kila mahali. Inawezekana kuna mazao wanahitaji kula majani fulani, inawezekana maji hakuna maeneo ya hifadhi, basi wataalam wetu watumike kupanda hata miti au mazao yanayohitajika ndani ya hifadhi ili tembo wasitoke kuja mtaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi kama maji ni machache kule kwenye hifadhi, wachimbe mabwawa ya kutosha hiyo ndio maana ya kusema kuwepo kwa *professional* tuna wataalam wengi katika Wizara hii, tunawaamini, hebu nendeni mkakae mnapofanya utafiti fanyeni na eneo hili tusibaki kupeana *story* kwamba ohh haya ni mapito ya tembo miaka yote inapita, najiuliza kule Ntuntu mapito ni lini walikuwa wanaenda wapi hawa tembo, tembo

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wamekaa wiki nzima/wiki mbili wanafanya wananchi washindwe kufanya shughuli zao za kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutajikuta kwamba tunawahamasisha wananchi wafanye kazi, lakini hawezi kufanya kazi kwa sababu kuna tatizo la tembo wanazunguka nani hatari kwa maisha ya wananchi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nilitaka niombe sana anapokuja waziri hapa atueleze mkakati ni upi wa kitaalam, sio hoja hii ya kila siku imekuwa kama msamiati ambao haueleweki haya ni mapito, sijui ni *corridor*, sijui lugha zingine zinawasumbua wananchi hawajui.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana kazi nzuri mnayoifanya lakini eneo hili linatutia doa kama Taifa twendeni tukafanye kazi kwa pamoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Namwita Mheshimiwa Usonge Juma, jandae Mheshimiwa Neema.

MHE. MARTHA N. GWAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii niliyopata ya kuchangia Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nipongeze...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Usonge Juma Hamad.

MHE. MARTHA N. GWAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ni yule?

MHE. JUMA USONGE HAMAD: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi kunipatia fursa hii ya kuweza kusimama na kuweza kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kwanza nikupongeze sana kwa umalidadi wako wa kusimama kwenye kiti, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, dada yangu kwa kazi nzuri ambayo wanayofanya lakini pia kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya hususan kwenye filamu ambayo tayari ameizundua hivi karibuni ya *Royal Tour* ambayo imetuletea matokeo makubwa sana ambayo na faida kubwa sana kutuletea wageni katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sisi ambao tayari tunatokea upande wa pili wa Zanzibar jana napiga simu naambiwa kuna wimbi kubwa na wageni ambao wanaingia Zanzibar, kumbe faida kubwa ambayo inapatikana kupitia *Royal Tour* haipo tu kwa Tanzania Bara bali ipo mpaka Zanzibar, kwa kweli tunampongeza sana mama. Hii imetengeneza fursa kubwa sana vijana wetu kule ambao tunaita *beach boy* pamoja na waongozaji wa kitalii kufurahia matunda ya nchi yao, lakini pia matunda haya yanatokana na mama yao Mama Samia Suluhu Hassan, kwa hilo nampongeza sana Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbali na hilo sasa nijikite kwenye mchango wangu, mbali na sekta hii ya kiutalii ambayo ina umuhimu mkubwa sana kukuza uchumi wetu na maendeleo ya wananchi wetu moja kwa moja, lakini yapo maeneo ambayo bado hatujaangalia kiujumla. Ingawa Tanzania tumebarikiwa katika maeneo yasiyopungua zaidi ya saba ambayo ndio tumejikita zaidi kuleta watalii nchi kwetu likiwemo eneo la hifadhi ya wanyamapori, lakini kuna eneo la maporomoko ya maji, kuna eneo la milima, kuna

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

maeneo ya misitu, mazingira na maliasili, kuna utamaduni, utalii wa mali ya kale, lakini pia kuna utalii wa fukwe. (*Makofi*)

Mimi nataka niishauri zaidi Wizara hii mbali na kuangalia na wanyamapori lakini kwenye eneo la fukwe bado hatujawekeza zaidi. Tathmini inaonesha nchini kwetu Tanzania tuna hekari zisizopungua 1,428 kandokando ya bahari pamoja na maziwa makuu, lakini bado hatujaangalia kwenye eneo hilo. Ukweli usiopingika watalii wengi ambao tayari wanakuja kutembelea nchini kwetu Tanzania pamoja na Afrika kiujumla wanapendelea zaidi kuangalia katika maeneo ya fukwe. Leo hii mgeni anapata likizo kwenye mwaka wa miezi 12 anapata likizo ya mwezi mmoja mtalii yule ukimuuliza anakwambia maeneo ambayo nitapendelea zaidi kwenda kutembelea ni eneo la fukwe na eneo la hifadhi ya wanyamapori. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo hayo tunafanya vizuri hususani kwenye eneo la wanyamapori, lakini kwenye eneo la fukwe hasa bado hatujawekeza zaidi. Rai yangu kwa Serikali tuangalie namna gani tunaweka mpango mkakati *either* wa muda wa miaka mitano, *either* miaka kumi kwenye eneo hili la fukwe tunawekeza zaidi, inawezekana eneo la fukwe maeneo yale yanaonekana *very expensive* kwa wawekezaji kununua, lakini ninaishauri Serikali tuanzishe mfumo wa PPP (*Private Public Partnership*) hiii itatusaidia sana kama Serikali, akija mwekezaji kama Serikali inatoa asilimia 50 na asilimia 50 anatoa mwekezaji. Hii itasaidia kujenga mahotel makubwa pembezoni mwa fukwe, lakini sio fukwe tu za bahari tunayo maziwa makuu, mito na maeneo mengine mbalimbali hii itavutia sana kuleta wawekezaji na ndiyo tathmini ambayo inaonesha duniani kote huko watalii wengi ambao wanakuja wanaangali huko katika maeneo ya fukwe. Kwa hiyo, naamni tukifanya hivyo vizuri zaidi tunaenda kuongeza idadi kubwa sana ya watalii katika nchi yetu kila mwaka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbali na hilo pia kuna eneo lingine ambalo kwenye suala la chakula bado hatujawekeza vizuri zaidi. Watalii wengi ambao tayari

wanakuja nchini tunawalazimisha kuwalisha vyakula ambavyo havieleweki. Lakini miongoni mwa vitu ambavyo watalii wengi wanaokuja nchini kwetu wanavutiwa na chakula wengi wao na ndiyo maana ukifanya tathmini watalii wengi, mtalii akija mwaka huu mwakani ni nadra sana kurudi. Lakini bado hatujaangalia maeneo gani ambayo tayari tunaweza tukamvutia ili aweze kurudi miaka na miaka ni eneo la chakula tu peke yake. Na ndiyo maana ukiangalia kule kwetu Zanzibar kuna eneo la Forodhani ambalo ni eneo ambalo limeshamiri kwenye vyakula tunaita *local food* ambavyo vinatokana na bahari. Lakini bado hatujaangalia kwenye eneo hilo.

Kwa hiyo, mimi rai yangu nashauri kwamba tuanzishe hata matamatasha kila mwaka kwenye eneo la uwekezaji kwa mfano kama Dar es Salaam, Arusha, kwenye maeneo yote ambapo watalii wanakuja kwa wingi tuwawekee chakula. Chakula ni *taste* pekee ambayo inamvuta mtalii kuja nchini na kurudi mara kwa mara tofauti na wanyamapori na fukwe. Kwenye wanyamapori anaweza akaja mwaka mmoja, lakini mwakani akasema hakuna kitu kingine chochote, tembo walewale, simba walewale. Lakini kwenye chakula, tukiweka sasa chakula kizuri zaidi, tukiwawekea vyakula ambavyo tayari tumevifanyia *taste* zote naamini watalii wale watarudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri tuaangalie *Mother Africa* hapa tunayo nchi yetu ya *South Africa* wanalo zao la zabibu kwenye utalii sisi Tanzania tuko vizuri zaidi kuliko hata wao. Lakini wanalo zao la zabibu, zabibu ile ina zaidi ya vinywaji sita, saba na kuendelea. Lakini wao wamefanya kama ni tamasha kwa wao, kwa mwaka wanafanya matamasha zaidi ya 30 katika nchi yao na watalii wanakuja kwa ajili ya ku-*taste* ule mvinyo na ku-*taste* kwao inakuwa ni *free* zaidi. Hata mzungu akienda kwao basi ile *taste* ya mvinyo aliyoipata *South Africa* mwaka jana anaipata tena na watalii wengi wanarudi Afrika ya Kusini kwa ajili ya mvinyo.

Kwa hiyo, sisi kama Tanzania bado hatujawekeza tunayo *naturally*, ardhi yetu ni nzuri, hali ya hewa nzuri na

matunda pia ambayo tayari tunayozalisha ni mazuri naya na *taste* nzuri, huwezi kuyapata dunia yoyote ile. Kwa hiyo, bado hatujaangalia kwenye eneo hilo. Kwa hiyo sisi tuangalieni sisi kama Serikali. Tumsaidieni mama, mama ameonesha rai kubwa, lakini mama ameonesha nguvu kubwa kwenye sekta hii ya kiutalii haijawahi kutokea duniani, Rais kama mama amefanya kazi kubwa sana kwenye hii kwa ajili ya kuitangaza Tanzania. Kwa hiyo, lazima tuweke mipango mikakati kuweka mazingira mazuri watalii wakaanza kuja nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, jiandae Neema Mgaya, jiandae Mheshimiwa Tadayo.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, Martha au Neema.

NAIBU SPIKA: Martha Nehemia Gwau.

MHE. MARTHA N. GWAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana kwa nafasi hii uliyonipa na mimi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naomba nipongeze Wizara, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri lakini na wataalam wote katika Wizara hii kwa ajili ya jitahada zao wanazochukua kuhakikisha kwamba suala zima la utalii nchini kwetu linapewa kipaumbele, lakini pia kwa namna moja au nyingine wanajitahidi kutangaza na kuvutia watalii kuja wengi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vivutio vingi sana Tanzania ambavyo tumebarikiwa na Mungu, tuna Serengeti, Ngorongoro, Mlima Kilimanjaro na vingine vingi ambavyo sivezi kuvitaja kwa sababu ya muda, lakini tunavyo vivutio vingi ambavyo tumepewa na Mungu ila ni swali la kujjuliza ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kwa nini hatuna watalii wengi kama nchi nyingine pamoja na kuwa tuna vivutio vingi tulivyonavyo. Kwa hiyo, mimi nikaja na mambo mawili/matatu ambayo najua au nahisi yanasababisha tusipate watalii wengi, lakini pia yanasababisha hatujajitangaza vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kipekee naomba nichukue nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa *video* yake ile ya *Royal Tour* ambayo kwa kweli imeenda kuwa ni suluhisho katika Wizara hii ya utalii, lakini pia katika uchumi wa nchi yetu. Najua Mheshimiwa Rais alivua Urais akavaa uzalendo, uzalendo ndiyo uliotawala hatimaye akaamua kuwa kipaumbele na kutangaza utalii wa nchi yetu. Kwa hiyo, kwa unyenyekevu mkubwa naomba nimpongeze sana na naomba nimwambie kwamba hii mifano ni ya kuigwa kwa sisi wengine na kwa watumishi wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inaeleza ifikapo mwaka 2025 tuwe na watalii milioni tano lakini mpaka sasa tuna takribani watalii 1,500,000 na tuna miaka mitatu kufikia Ilani yetu ya uchaguzi. Kwa hiyo, mimi naamini kwamba tukiweka njia Madhubuti na tukiwa na mikakati maalum tutafikia hii idadi ya watu milioni tano kama ilivyoandikwa kwenye ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Royal Tour* ya mama imeleta mafanikio makubwa sana nchini kwetu na itaendelea kuleta, mojawapo ni kutangaza vivutio vilivyopo, lakini pia kuwasadia wawekezaji, kusaidia pato la Serikali, lakini kusaidia jamii kwa ujumla kama vile ajira nakadhalika. Kwa hiyo, jukumu langu kumpongeza mama lakini pia ni jukumu letu kumuunga mkono na sisi kuja vitu mbadala ambavyo vitasaidia kuunga juhudi zake mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa za uwekezaji pia zimefunguliwa kutokana na *Royal Tour*, ni kweli usiopingika wawekezaji watakuwa wameona fursa zilizopo Tanzania na *angle* gani waje wawekeze kwa kutumia *Royal Tour* ya

Mama. Kwa hiyo kwa hayo tu machache mama aliyotufungulia sasa ni jukumu letu la kubeba ule uzalendo wa mama na sisi kama Wabunge kuishauri Serikali, lakini pia na Wizara kuchukua yale maono ya mama na kuyaweka kwenye uhalisia ili tuweze kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita kwenye ushauri kwa Serikali kwa mambo mawili; ushauri wa kwanza ni njia za kisasa za utangazaji wa utalii, lakini wa pili utakuwa ni chombo cha ku-*regulate standards* na watoa huduma kwa ujumla. (*Makofi*)

Suala la kwanza, sasa hivi dunia iko kiganjani watu wanaita hivyo, kwa hiyo ni jukumu la Wizara au ni jukumu letu sisi sote ni kuhakikisha ni njia gani tunatangaza utalii na njia gani zinawafikia walengwa hasa tunaotaka kuwatangazia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekuwa ikijitahidi kwa namna mbalimbali kwenda labda kwenye makongamano mbalimbali, lakini labda kutoa *brochures* tofauti tofauti, ila kwa dunia ya sasa hivi lazima tujulize je, ni kweli hizi njia zinafanya kazi? Kwa sababu ni wangapi wanaosoma hizo *brochures* na hata kama Wizara wakienda kwenye maonesho wana banda la Tanzania labda vivutio vya Tanzania; je, ni kweli hilo banda linatembelewa na watu wengi? Kwa hiyo, utakuta hawapati idadi ya watu wa kutosha, lakini tukienda *digital marketing* inawafikia watu kwa haraka na kwa muda mfupi pasipo kutumia gharama kubwa sana kama sasa kusafiri sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya utafiti mdogo sana kwenye nchi jirani za Afrika, lakini na nchi za wenzetu zilizoendelea. Nimeona juzi juzi tu hapa siyo muda mrefu Kenya imeingia Mkataba na mtandao wa *TikTok*, *TikTok* ni mtandao wa vijana siyo vijana na watu wengi wanatumia kwa ajili ya ku-*post* vitu mbalimbali. Wametengeneza *short videos* ambazo zinaonesha utalii wao na hii yote ni njia ya ku-*recover* kutoka kwenye *COVID-19* ambapo sekta yetu ya utalii iliyumba sana. Kwa hiyo, kama sekta iliyumba lazima

tujifikirie ni namna gani mbadala za haraka haraka ambazo zitasababisha sisi tujitangaze kwa urahisi lakini tupate matokeo kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *digital marketing is the way forward* kwa sababu hiyo ndiyo inakupa majibu ya haraka haraka. Hata kuna *document* moja ya *World Bank* wameandika *digital platform* na *demand* kwenye *business* ya utalii, hivi ni muhimu kwa sababu siku hizi watu wakiamka asubuhi anashika simu ya mkononi kwanza tofauti na zamani ilivyokuwa. Kwa hiyo, tukitumia *digital platform* ya kuwatangazia vivutio, tuwatangazie tunatoa vitu gani Tanzania wataweza kuja kuona kwa kutumia simu ya mikononi bila ya kuwa tumeenda kutangaza, tumeenda nchi hii na nchi hii. Kwa hiyo, mimi nashauri tujikite sana kwenye *digital economy*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna nchi jirani ambazo huwa wanafanya vizuri kwenye utalii kama Morocco, wao walikuja na mkakati maalum baada ya *COVID* wakaja na mkakati maalum wa utangazaji wa utalii unaitwa *Aji and We Are Open*. Huo mkakati ulikuwa unalenga kuleta watalii tena baada ya *COVID* kuwapa *awareness* kwamba sasa tumefungua utalii wetu karibuni. Kwa hiyo, na sisi Tanzania tuje na *different* programu mbalimbali japo tunayo hii moja ya mama yetu mpendwa ya *Royal Tour*, lakini tuongeze na zingine kuonyesha kwamba sasa tumeshafungua utalii na sasa tuko tayari kupokea wageni waje kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingere cha pili katika hiyo hiyo *digital marketing* tuna watu mbalimbali mashuhuri ambao wanafuatwa na watu mbalimbali na kwa wingi mkubwa wa mamilioni na wengine wana ma-*followers* wengi. Tukiainisha *target market* yetu kama tunataka nchi ya Urusi, tunataka wa Marekani, tunataka wa London, tunataka watu wapi, ni kiasi cha kutafuta mtu mashuhuri wa hiyo sehemu akaja kutangaza utalii. Aki-*post* kwenye *platform* zake sisi tunapata watalii, nakuhakikisha msanii aki-*post* au mtu mashuhuri hata ukiwa na *viewers* watu milioni tano, milioni

10 huwezi ukakosa watu milioni moja wa kuja kutembelea Tanzania. Kwa hiyo, ni wazo langu na rai yangu kwamba Serikali mtachukua hilo suala kwa ukubwa wake kama nchi za wenzetu walivyofanya na mpaka sasa namba yao ya utalii imeanza kuwa kubwa na kurejesha kutoka kwenye ile hali ilivyokuwa ya *COVID-19*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili lilikuwa ni chombo cha ku-*regulate standards* za watoa huduma wetu na niungane na mchangiaji aliyepita, shida nyingi Tanzania kwanza zile *punctuality, standards* za watoa huduma wetu bado haziridhishi. Tunakuwa tunawatoa huduma ambao moja *whether* hawana mafunzo ya kutosha, mbili hawana uzoefu wa kutosha au walimu wao wanaowafundisha hawana *enough skills* za kuwapa hawa wanafunzi waka-*compete* au wakawa *competent* kwenye maeneo yao ya kazi.

Sasa mimi nikiangalia mfano wanasheria wana chombo chao kile *Law School* lakini wa leseni zao, watu wa *NBAA* wanatoa *CPA*; je, kama sisi tumeamua kujikita kwenye utalii na kama utalii huu ni muhimu kwa nini utisije na chombo chetu cha ku-*regulate* hawa watoa huduma, simaanishi hoteli hiyo tayari ipo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Martha kwa mchango wako.

MHE. MARTHA N. GWAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri mchango huu ni mzuri sana na naomba muuchukue na muufanyie kazi na mlete mrejesho Bungeni. Hii Filamu ya *Royal Tour* mnaweza mkaikata kwa sekunde 15, 15 kwa sababu watu kuitazama kwa kipindi kirefu hawaweze.

Kwa hiyo, sekunde 15, 15 na vitu vingine itasaidia sana kuchochea utalii nchini. Hongera sana Mheshimiwa Martha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Neema Mgaya, jiandae Mheshimiwa Tadayo.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na uhai na kuweza kusimama ndani ya Bunge hili tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake kwa utendaji mzuri katika Wizara hii. Lakini kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa programu nzuri ambayo aliizindua tarehe 22 Aprili, kule Marekani programu hii ya *Royal Tour* nina uhakika na ninaamini kwamba itakuja kuleta matunda makubwa zaidi. Nina kila sababu ya kusema hivyo kwa sababu ukitizama nchi mbalimbali ambazo zime-*practice* hii programu ya *Royal Tour* tukienda *East Africa* tu hapa Rwanda na mwigizaji alikuwa yuleyule Bwana Peter Greenberg walifanya vizuri baada ya programu hiyo na matunda yanaonekana watalii wengi Rwanda wameweza kwenda. Lakini si Rwanda tu zipo nchi mbalimbali ikiwepo Mexico, Poland, Ecuador, Israel wote hao wame-*practice* hii programu ya *Royal Tour* na matunda, matokeo chanya yameonekana kwa nchi zote hizi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sina shaka, sina hofu, nampongeza Rais wangu Mama Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi huu kwa sababu naamini Tanzania itakwenda kukuza utalii kupitia programu hii ya *Royal Tour*. Hongera sana Mama Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile hata kwenye *interview* ambayo Mama Samia Suluhu Hassan aliyofanyiwa pale *New York City* aliweza kujitanabaisha na kuainisha vivutio mbalimbali vya utalii ndani ya nchi ya Tanzania na watu wengi wakaweza kuvifahamu. Lakini tukienda mbali zaidi hata Gazeti la *New York Times* lilimuandika vizuri sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na kumpongeza na tukumbuke jamani gazeti hili siyo la udaku ni kati ya magazeti ambayo yanaheshimika Marekani. Kwa hiyo, naamini kabisa

kwa kupitia programu hii matunda makubwa yanakuja kwa kupata watalii wengi sana ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa hii iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan, ni wajibu sasa Wizara ikaangalia namna bora ya kuendelea kumuunga mkono mama na kuendelea kuchakata suala hili la utalii kuelekea Nyanda za Juu Kusini. Nyanda za Juu Kusini kama tutaweza kuchakata vizuri suala hili la utalii tutakwenda kufanya vizuri zaidi. Nyanda za Juu Kusini ukianza tu pale Mkoa wa Njombe kuna Hifadhi ya Kitulo, hifadhi ile ni bustani ya Eden, hifadhi ile hakuna inayofanana na ile ulimwenguni ni hifadhi ya kipekee ina ndege wazuri, ina maua mazuri, kama tutaweza kuipigia chapuo tutakwenda kuongeza watalii Nyanda za Juu Kusini. Lakini ukienda pale Rukwa, kuna maporomoko yale ya Kalambo, maporomoko ya Kalambo Afrika ni maporomoko ya pili yakitanguliwa na *Victoria Falls* kule Zimbabwe, bado tuna kitu kikubwa cha kuweza kukiuzua na watalii wakaja nchini kwetu kwa kupitia kule Nyanda za Juu Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tuna mbuga nzuri ya Ruaha, ni ya kipekee ina makundi makubwa ya simba ambayo *East Africa* hakuna makundi yale makubwa ya simba, tunaweza tukaweka kwenye *package* ya Nyanda za Juu Kusini na utalii ukaweza kukua na kuweza kuongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tuna utalii wa picha kwenye mashamba mazuri ya chai, mashamba mazuri miti, Mufindi kule, Njombe, Mbeya pamoja na huko Rukwa pia. Lakini vilevile tuna Kimondo kiko Songwe, hivi vitu vyote vikiwekwa kwenye *package* moja ya Nyanda za Juu Kusini tutaweza kuendelea kukuza utalii wetu na kuendelea kuongeza mapato katika sekta hii ya utalii. Tuna *beach* nzuri, kuna mzungumzaji hapa wa kutoka Zanzibar alizungumza masuala ya fukwe, tuna *beach* nzuri kule ya *Matema beach* Nyanda za Juu Kusini. Lakini vilevile unazikuta *beach* hizi na kule Ruvuma.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati sasa Wizara iangalie namna bora ya kuendeleza na kukuza utalii Nyanda za Juu Kusini ili kuweza kuendeleza watalii zaidi, lakini vilevile kuongeza kipato katika sekta hii ya utalii. Tusing'ang'anie tu Kaskazini, Kaskazini inajulikana sana, tuangalie tuna fursa nyingine za Nyanda za Juu Kusini na maeneo mengine. Bado hayajafanyiwa kazi inavyotakiwa, yakifanyiwa kazi inavyotakiwa tuna vivutio vya kipekee sana ambavyo vinaweza vikaongeza mapato ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukienda kule Ruvuma Jimbo la Mheshimiwa Jenista kuna mapitio yale ya Wakatoliki na Makanisa makubwa ambayo yamejengwa zamani, tukiweka vizuri wale wakoloni, Wajerumani ambao walijenga yale makanisa watavutiwa kuja kuona. Nafikiri kuna umuhimu sana wa Wizara kuangalia...

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nataka kumuongezea taarifa Mheshimiwa Neema kwamba kule Nyanda za Juu Kusini, lakini kwenye Jimbo la Momba tunayo pia maporomoko ambayo yako kwenye Kijiji cha Mfuto na Yala, kwa hiyo pia na yenyewe tunaomba Wizara ya Maliasili yaweze kuyatambua ili yaendeleo kuongeza watalii.

NAIBU SPIKA: Haya, Mheshimiwa Neema, taarifa.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naipokea taarifa kwa mikono yote kwa sababu nayo itaingia kwenye *package* ya utalii wa Nyanda za Juu Kusini na kuweza kuinua utalii Nyanda za Juu Kusini. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuzungumzia suala la migogoro katika hifadhi, *game reserve* na *forest reserve* ambazo zinazunguka ndani ya Mkoa wetu wa Njombe. Mpanga Kipengele upande wa Makete na upande wa Wanging'ombe kuna changamoto ya migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda upande wa Makete kuna Kijiji cha Ikovi, Kimani, Ibagu hivi vyote vina mgogoro katika *game reserve* hii ya Mpanga-Kipengere. Nilikuwa naiomba Wizara itafute namna ya kutatua mgogoro huu, umekuwa mgogoro wa miaka mingi sana, ifike namna sasa ijulikane *game reserve* mipaka yake iko wapi na vijiji viko wapi. Lakini vilevile, upande wa Wanging'ombe kule kuna vijiji kama vya Ruduga, Igando, Ihanja, Hanjawanu, Mpanga, Malangali, Wangamiko, Iyai na Mayele bado nako kuna shida ya migogoro ya mipaka kati ya vijiji na hiyo *game reserve*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vil vile ukienda Mpanga-Kipengere Forest Reserve kuna vijiji vya Masage, Wangama, Ikanga na Kipengere yenyewe bado napo kuna changamoto ya migogoro hii ya mipaka ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Wizara hii Mheshimiwa Waziri unatoka Njombe ninamatumaini makubwa mgogoro huu utakwenda kumaliza hivi punde. Vilevile Waziri wa Ardhi kipindi hicho akiwa Naibu Waziri nilishawahi kuzungumza hapa ndani ya Bunge, akaja kule Wanging'ombe, tatizo lililokuja alikuja mwenyewe, *issue* kama hizi Mheshimiwa Waziri wa Maliasili mnatakiwa mshirikiane na Waziri wa Ardhi, wote mkifika *site* kwa pamoja mkakubaliana mtaweza kumaliza matatizo haya, lakini mmoja akienda mwingine akienda siku nyingine hamuwezi kufikia muafaka. Kwa sababu, kila mtu atakuwa anaangalia upande wake ni vizuri mkafanya kazi kwa kushirikiana, ili kuweza kumaliza matatizo haya ya hifadhi na vijiji vinavyozunguka hifadhi na mapori ya akiba. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Hifadhi ya Kitulo pia bado kuna changamoto hiyo kuna changamoto kubwa sana

maana yake Hifadhi ile ya Kitulo ilianzishwa mwaka 2005 lakini migogoro ikaanza mwaka 2019 mpaka mwaka 2020; sababu ya migogoro hiyo ni kwa sababu waliweka *beacon* mpya kwa mara ya pili. Kwa hiyo, kuna vijiji kama cha Misilo, Lugoda, Igege... *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Neema kwa mchango mzuri.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ni kweli Kitulo ni sehemu nzuri sana. Mheshimiwa Tadayo, jiandae Mheshimiwa Zaytun Swai, jiandae Mheshimiwa Shally, jiandae Mheshimiwa Tarimo.

MHE. JOSEPH A. TADAYO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kupata nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Pindi Chana, Waziri pamoja na timu yake yote ikiwa ni pamoja na Naibu Waziri kwa dhamana kubwa hii ambayo Mheshimiwa Rais amewapa ya kuongoza Wizara hii ambayo kwanza inabeba uchumi wa nchi, lakini pia inabeba taswira ya nchi yetu. Mheshimiwa Pindi Chana kwa kiasi kikubwa nakufahamu tumefanya kazi pamoja kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa, mzigo huu ni *size* yako kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mary Masanja dada yangu tulikuwa wote kwenye mapambano ya tembo kule kwenye Jimbo langu yalipoanza pamoja na kwamba yanaendelea nitakueleza, lakini niliona uwezo wako, mzigo huu wa kumsaidia Mheshimiwa Pindi Chana ni *size* yako kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea maeneo mawili; moja kuhusiana na Jimbo langu lakini la pili nitazungumza juu ya habari ya *Royal Tour*. Jimbo langu linapakana na mbuga za wanyama mbili moja, ni Tsavo ya Kenya halafu na Hifadhi ya Mkomazi ya hapa kwetu Tanzania. Tumekuwa na changamoto kubwa sana ya tembo na kwa

kweli kwa juhudi ambazo Wizara imeshafanya mimi nawapongeza. Lakini mimi kwa kweli sasa hivi kilio changu kikubwa ni kwamba linapotokea janga kama hili watafiti wetu tunawasikiliza wanasema nini? Vyuu Vikuu vyetu vinasemaje juu ya janga hili ambalo limekaa muda mrefu kiasi hiki? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama basi tumefikia hapa, mimi ningeshauri Wizara kwa kweli labda mtangaze *package* kama iliyotangazwa na Wizara ya Elimu juzi kwamba, atakayeweza kutoa chapisho likaenda kwenye majarida fulani mashuhuri atapata *fifty million shillings* basi na hapa nadhani mngatangaza *boom* ili watafiti wetu waingie kazini kwa sababu hali haifurahishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda na Mheshimiwa Naibu Waziri kule hali haikuwa nzuri, lakini pia yako mambo ambayo tuliwaahidi wananchi wa Jimbo la Mwanga ambayo pia kwa namna fulani yangesaidia kupunguza kasi ya tatizo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la lango la Kaskazini la Mbuga ya Mkomazi ile ahadi mpaka leo haijaitimizwa pamoja na kwamba iliingia katika utaratibu wa bajeti ya mwaka uliopita. Tunaomba ile ahadi itimizwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na ahadi ya bweni la wavulana katika shule ya sekondari Kigonigoni, ili kuwapunguzia kutembea umbali mrefu kwa sababu ya tembo kwenye eneo lile. Pia kulikuwa na ahadi ya shule ya msingi ya Mbigili kwa sababu hiyo hiyo. Ahadi hizi bado hazijatekelezwa ninawashukuru wenzetu wa *TANAPA*, juzi juzi wamenitumia taarifa ya kuonesha kwamba zimeingia kwenye taratibu zao za bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mwakilema anatoa ushirikiano sana hasa kwenye upande wa mawasiliano namshukuru, kwa hiyo naomba sasa, ahadi zitekelezwe ili kuendelea kuwapunguzia wananchi hawa machungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna suala la kifuta machozi kwa waliopoteza maisha na fidia kwa waliopoteza mazao. Hilo pia bado halijakamilika, tunaomba hayo yatimie, ili tuendeleo kupata ushirikiano wa wananchi wa Mwanga katika janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye suala la *Royal Tour*. *Royal Tour* pamoja na yote mema yaliyozungumzwa lakini ningependa kurudi kwenye historia yake kidogo kwamba ile ni *series* ambayo huwa inafanyika ikiongozwa na yule ndugu yetu Peter Greenberg ambaye ni mtu mwenye nishani nyingi sana za kimataifa katika eneo hili na ile inatolewa kwanza kwa nchi ambayo ina vivutio mahususi vya utalii na pili nchi ambayo inakiongozi ambaye, amethibitisha kuwa na uwezo mkubwa wa kushawishi katika masuala ya kukuza uchumi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa *Royal Tour* ile kufanyika hapa ni kwamba tume-*qualify* kuwa na nchi yenye vivutio hivyo na pia kuwa na Rais ambaye amethibitika kidunia kwamba anaushawishi mkubwa katika kusukuma uchumi wa nchi yake. Kwa hilo, lazima tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa ku-*qualify* kufikia hapo na hii *Royal Tour* huwa inaongozwa na wakuu wa nchi, najaribu kusema hivyo kwa sababu kuna watu wanapata shida kwamba kwa nini tusingetumia sijui ma-*star*wa dunia? Ma-*star*wa dunia u-*star* huwa unakwisha, lakini fikiria mpaka leo kuna mahali unakwenda unauliza unatoka nchi gani? Tanzania ni *country of Nyerere*? Mpaka leo Nyerere bado wanamkumbuka. (*Makofi*)

Sasa tunajaribu kujenga *legacy* nyingine ambayo itaendeleza pale ambapo pamebaki ili kuweza kuendelea kukuza uchumi wa nchi yetu. Ilipofanyika Israel aliiongoza mwenyewe Benjamin Netanyahu - Waziri Mkuu, ilipofanyika Poland aliiongoza Waziri Mkuu - Mateus, ilipofanyika Ecuador aliiongoza Rais mwenyewe Raphael Korea, ilipofanyika Mexico aliiongoza Rais Philippe na Rwanda aliiongoza Paul Kagame mwenyewe. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni suala ambalo linaongozwa na Wakuu wa nchi sio kila mtu hapa Mbunge wa Mwanaga niende nikaongoze *Royal Tour* hilo haliwezekani. Nilikuwa najaribu kujibu hilo swali na katika nchi zote hizi ambazo *Royal Tour* hii imefanyika kwa kuongozwa na wakuu wa nchi uchumi wa nchi zile ulikua sana. Hakuna ubishi kwamba Israel pamoja na kwamba ni nchi ndogo na yenye migogoro mingi, lakini inaongoza katika uchumi na teknolojia. Rwanda hapa katika nchi za Afrika tunaingalia kabisa kwa jicho kwamba ni nchi ambayo inaongoza. Ecuador kuna programu moja imeanza pale inaitwa *Four Worlds in One Place*, ambapo waliigawanya ile nchi katika *Zone* nne tu za *climate* tu, Amazon, Andes, Coast na vile Visiwa vya Galapagos. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vinailetea watalii wengi na uchumi umekua kwa ajili hiyo tu. Sasa Tanzania tuna uwezo wa kugawa hata dunia 40 ndani ya nchi yetu. Ukienda kwenye *culture* peke yake inatosha kabisa kuvutia utalii, kuna sehemu Pwani huko, ukienda kwetu huko Kaskazini *culture* ziko tofauti ile peke yake ni kivutio. Hata chakula *for that matter*, rafiki yangu Musukuma bila ugali kwake hakuna chakula ukimletea ndizi anasema hii ni mboga. Ukienda kwa Mheshimiwa Mwigulu kule wanakula kuku wa kienyeji, lakini ukienda kwa ndugu zangu Wamasai wanasema hawa ndege sisi hatuli na kadhalika. Kwa hiyo, *diversity* peke yake ya *culture* ni kitu kikubwa sana ambacho kinauwezo wa kutuletea utalii mkubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda Zanzibar tulikwenda kule kwenye ile misitu ya Jozani, tukakuta wale nyani wekundu ambao dunia nzima unawakuta pale Zanzibar. (Makofi)

Kwa hiyo, sisi hata faru tunao wengi mpaka tuna Faru John na faru wa kila aina na sasa hivi nimeona kuna nyati weupe wamezuka. Kwa hiyo, kwa kweli kwa kutumia sasa hii *Royal Tour* ambayo imetufikisha hapo, tuna uwezo wa kuipeleka hii nchi *next level* kwa namna ambayo ni rahisi kabisa. (Makofi)

Ndugu zangu ukisoma kwenye vitabu wafalme wa zamani walitangulia wenyewe vitani, lakini wakitangulia vitani walikuwa wanakwenda pamoja na watu wao. Sasa Rais ametutangulia katika vita hii ya kufufua uchumi wetu kwa njia nyingi ambazo tumeziona hata za miundombinu na sasa ya *Royal Tour*, lakini sasa tunapaswa kwenda naye, tusiseme tu kwamba ameupiga mwingi sasa akishaupiga mwingi nani atafunga goli? Ameupiga mwingi watalii wamekuja je, Uhamiaji wako tayari pale *airport* ili kuwapitisha watalii haraka haraka tusianze kupata lawama? Ameupiga mwingi kwenye mahoteli amezungumza mchangiaji mmoja *customer service* yetu iko namna gani? Ameupiga mwingi watalii wamekuja, barabarani vizuizi vyetu hivi kilometa 100 vizuizi sita tunafikaje hapo? (*Makofi*)

Kwa hiyo, yako mambo ambayo kwa kweli tukitaka tupate faida ya hii *Royal Tour* inakuwa ni jukumu letu sisi sote, hasa sisi Wabunge ambao tunapita huko tukiwaona tuseme tupige kelele na Serikali iitokie ifanye kazi yake vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yako mambo kama hili nilizungumza la ripoti ya *CAG* ambapo imezungumzia juu ya vitalu ambavyo tayari vilishagawanywa lakini watu hawajapewa. Hiyo inaweza ikatupeleka kushtakiwa bure, tukajikuta tunalipa mamilioni kumbe tu kuna mtu mmoja ambaye baada ya mwingi kule kupigwa ameshindwa kupokea tukafunga goli. (*Makofi*)

Kwa hiyo, vitu kama hivyo na hata hivi vitalu bado ukiangalia ukilinganisha kwa kweli bei zake bado ni kubwa na muda ambao watu wanapewa mwaka mmoja ni mfupi sana. Ni vyema tungefikiria hata kumpa mtu miaka mitatu mpaka mitano wakati anapowekeza pale ajue anawekeza mahali ambapo kesho na kesho bado atakuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia utaratibu wa kuondoka na zile *trophies* kwa wale wawindaji, wakati mwingine unakuwa mgumu sana tunaona hayo malalamiko katika maeneo mengi. Kwa hiyo, mimi wito wangu ni kwamba pamoja na mama kuupiga mwingi na tukapata hii *boom* sasa

ya watalii ambayo inakuja na sekta zingine kwa sababu *Royal Tour* haikuji utalii peke yake, kwenye nchi zote ambazo ilifanyika imekuza uchumi wote kwa ujumla. Sasa ni lazima tujiandae kila sekta kuhakikisha kwamba hili linalokuja tunalipokea na kuweza kufunga yale magoli ambayo yamekusudiwa, isije ikawa timu nyingine ile ya watani wako ambayo magoli kwao kidogo inakuwa shida shida na inakuwa ya kubahatisha zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja sana na ninaomba tuunge mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana kwa mchango mzuri sana tunataka michango namna hii. Mama anaupiga, wewe unaupiga wapi? Tunataka kujua na sisi tunaupiga wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Zaytun, jiandae Mheshimiwa Shally, jiandae Mheshimiwa Tarimo. (*Makofi*)

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye bajeti ya Wizara hii ya Maliasili na Utalii. Naomba nianze kwa kumpongeza *tour guide* wetu namba moja Tanzania naye sio mwingine ni Mama yetu Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuifungua nchi yetu kiuchumi, lakini vilevile kwa kuendelea kuitangaza nchi yetu kiutalii na kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia filamu ya *Royal Tour* tumeona mafanikio yake yameanza kuonekana na mimi binafsi pamoja na wananchi wa Mkoa wa Arusha hususani wadau wa utalii ambao baadhi yao wako hapa siku ya leo tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake hizi za kuendeleza sekta hii ya utalii, lakini vilevile tunamuunga mkono na tunamshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara pamoja na taasisi zake pia basi zijitahidi kwenda na kasi ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mama Samia Suluhu Hassan ili tuweze kukuza utalii wetu hapa nchini. Mkoa wa Arusha ukiangalia uchumi wake kwa kiasi kikubwa unategemea shughuli za utalii. Sekta hii ya utalii pia ni sekta ambayo inachangia sana kulisha sekta zingine kama kilimo, ufugaji, usafirishaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mtalii akitua pale uwanja wa ndege wa KIA wanufaika ni wengi na sio tu sekta zile zilizo rasmi kama kwenye mahoteli, *tour guides* nakadhalika, lakini vile vile madereva teksi ambao wapo kwenye sekta ambazo sio rasmi wanafaidika, wakulima wa mazao mbalimbali wanafaidika, wafugaji wetu wanafaidika na vile vile wakina mama wanaouza shanga, wanaouza vinyago wanafaidika na ujio wa watalii hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sekta hii inachangia zaidi asilimia 25 ya fedha za kigeni ambazo ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Kwa kuonesha mafanikio haya ya sekta hii naiomba sana Wizara nasisitiza iendane na kasi ya jitihada kukuza sekta hii ili basi sekta hizo zingine nilizozitaja ziweze vilevile kukua kutokana na faida hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ripoti ya kidunia kwenye masuala ya utalii (*World Economic Report*) utaona Tanzania ni moja ya nchi ambazo inaongoza kwa vivutio vizuri vya utalii na vivutio vya asili vya utalii. Cha kusikitisha kidogo ni kwamba huduma zetu bado ziko chini kwenye masuala ya utalii na kwenye sekta ya utalii kikubwa kinachoangaliwa na mtalii akija hapa nchini ni jinsi gani tunaweza kumhudumia mtalii yule kwenye huduma ambazo ziko kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiongelea kuhusu huduma kikubwa kinachoongelewa hapa ni idadi ya vitanda tulivyonavyo kwa ajili ya kulaza wageni wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye tathmini mbalimbali zilizofanyika idadi ya vitanda tulivyokuwa navyo hadi mwezi Septemba, 2021 ni vitanda 560 tu, ukilinganisha na nchi jirani yetu ya Kenya ambayo ilikuwa na vitanda milioni

3.1 kwa kipindi kama hicho mwaka jana. Jumla ya vitanda vinaangaliwa kwenye mahoteli yenye hadhi za kimataifa ambazo zinaweza kulaza wageni wetu. Mahoteli mengi ukiangalia yamejengwa kipindi cha nyuma ambacho kilikuwa na msamaha wa kodi mbalimbali na hiyo iliweza kuwa-*attract* wawekezaji wetu wengi kuweza kuwekeza kwenye sekta hii ya malliasili na utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara iangalie jinsi gani itaweza kurudisha misamaha hii ya kodi (*deemed capital goods*) ili kuweza kuwezesha wawekezaji zaidi waweze kuwekeza kwenye sekta hii ya utalii kwa kujenga mahoteli yenye hadhi za kimataifa kwa kulaza wageni wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi uliopita Katibu Mkuu wa Wizara hii aliweza kukutana na wadau mbalimbali wa utalii wa Mkoa wa Arusha na vilevile waliweza kuwasilisha changamoto zao mbalimbali. Changamoto kubwa ambayo wadau hawa waliwasilisha ni kuwepo kwa gharama kubwa ya viingilio wanayotozwa wataalii wakiingia hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nimefanya tathmini mbalimbali na nimegundua kwamba kweli bei kwenye eneo moja tu la tozo, wageni wetu wanazolipa kwenye *park fees* nchi jirani ya Kenya wanatoza kati ya dola 30 mpaka dola 40 wastani, lakini sisi tunatoza wastani dola 50 hadi dola 70 na hiyo ni eneo moja tu. Kuna maeneo mengi ambayo gharama tunazowatoza watalii wetu ni kubwa na hii inapelekea watalii wetu, kuamua kwenda nchi jirani ya Kenya kwa ajili ya kutafuta unafuu wa bei hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba sana Waziri wakati anahitimisha hapa hotuba yake basi aweze kutuambia mikakati iliyonayo Serikali kwa ajili ya kupunguza gharama hizi za utalii hapa nchini ili basi tuweze kuingia vizuri kwenye soko la ushindani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ambayo wadau hawa waliwasilisha kwa Katibu Mkuu wa

Wizara hii ni waongoza utalii wanalazimika kulipa leseni zao kwa dola. Naomba sana Waziri wakati anahitimisha hapa pia aweze kutueleza basi Serikali itafanya jitihada gani ili kuwawezesha wadau hawa wa utalii, waweze kulipa leseni zao kwa fedha za kitanzania ili basi kuwapunguzia makali pale thamani ya dola inapopanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango wako mzuri Mheshimiwa Zaytun. Sasa Mheshimiwa Shally, jiandae Tarimo, jiandae Mheshimiwa Asia Halamga na Mheshimiwa Asya Mwadini. *(Makofi)*

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kipekee namshukuru Mungu sana kutuweka hapa kwenye nchi hii yenye amani tukizungumzia maendeleo ya nchi yetu. Nimpongeze sana Waziri Dkt. Pindi Chana - Balozi na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mary Masanja, Katibu Mkuu Francis na Naibu Katibu Mkuu wake pamoja na timu yote ya Maliasili na Utalii wakiwepo *TANAPA, TAWA, NCAA, TFS* na *NMT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumzia Wizara ambayo ni muhimu sana, lakini pia inaungana na Wizara nyingi sana katika kutekeleza mambo yake, lakini imempendeza Mungu leo tunazungumza bila barakoa. Natala niseme wazi ule ugonjwa wa *Covid-19* uliathiri sana Wizara hii kuliko kwingine kote na ndio maana waliishia sana wote wanaohusika na Wizara hii ya Maliasili walikwenda katika hali ngumu sana. Haijatangazwa rasmi kwamba umeisha, lakini angalau wameanza kuja watalii, lakini wamekuja watalii hao katika kipindi ambacho sasa tumeshapokea ile shilingi trilioni 1.3 ya kurekebisha mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nikwambie Maliasili na Utalii walipokea asilimia 6.9 ya hela hizo ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 90.2 na wamezifanyia kazi vizuri, japo

bado hawajamaliza, nilikuwa nawaomba sasa zitumike kwa kasi zaidi kwa sababu muda umeisha. Miezi sita ambayo aliizungumzia Mheshimiwa Rais ndio inaishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zimetumika vizuri na sina muda wa kutaja maeneo yote yaliyoguswa, lakini nitake tu kusema mimi kama nilivyosimama hapa nilitaraji elimu ifanyike zaidi kwa maeneo yote nchi nzima ambayo inagusa Wizara hii ya Maliasili na Utalii ili wote na sisi tuweze kuizungumzia kama Kiti kilivyoelekeza leo. Nataka niseme wazi haikugusa wanawake wa Kilimanjaro ili waweze kusemea vizuri na kwa nini Kilimanjaro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuung'oa ule Mlima Kilimanjaro ukaupeleka kwingine, huo ni mlima ambao unaitangaza na ni kilele kirefu kuliko vyote Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba na ninamuomba sana Mheshimiwa Balozi Pindi Chana atakaposimama aeleze kwenye elimu wanawake wa maeneo yote yenye maeneo ya utalii nchi hii kuanzia Kaskazini mpaka Kusini, Mashariki na Magharibi wamenifaikaje na ile hela ya UVIKO katika kuelimika kuendeleza utalii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumzia Wizara ya Maliasili na Utalii huwezi kuiacha Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambako ndio huko kuna hizo barabara za *TARURA*. Huwezi kuacha afya ambako ndio huko wakija watalii wanataka maeneo mazuri ya kutibiwa. Huwezi kuacha Wizara ya miundombinu ambako ndio viwanja vya ndege viko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani inagusa Wizara nyingi mno, sasa nilikuwa naomba Wizara zote hizo tajwa na nyingine ambazo sikuzitaja wakae pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii waone kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutangaza utalii duniani kwa kuwa *guide* sisi tunaipokeaje? Ametangaza na ninajua, kama inavyosema kwenye Ilani ya mwaka 2025

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

tutakuwa tumeshapokea watalii milioni tano, mimi nahisi watazidi, lakini tumejiandaa vipi sasa katika kupokea hao?
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani, Uhamiaji, wamekaa vipi na wamesaidika vipi kutoka Maliasili kuona kwamba wakifika sasa wanaingia moja kwa moja? Vibali vya kazi ambavyo labda watakuja na ma-*expatriate* wao wachache wanapewa bila vikwazo?
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi aliyofanya Mheshimiwa Rais sio ya kupuuzwa kabisa, sisi wenyewe wanawke wa Kilimanjaro tunamuomba mama aje Disemba kwetu. Disemba atakapokuwa na likizo yake ikimpendeza tunamsubiri kwa hamu tumpandishe pale juu ya Mlima Kilimanjaro, alikuja kama *guide* wakafika pale chini akafanya aliyofanya katika utaalumu wake, lakini sisi tunataka tukamwambie jambo letu la kumpongeza na mengineyo mengi. Tuna hamu kubwa ya kuja kumpongeza, lakini wanawake wote Tanzania kila aliyesimama hapa, wake kwa waume wamempongeza mama sana na mimi naungana nao. Na siwezi kurudia mambo yote aliyoyafanya ikiwa ni pamoja na hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la Wizara hii nimeona nizungumzie tu utalii, nikianza kurukaruka mambo ya fukwe, ningetamani kuona fukwe zetu zinafanana na Malindi, wanakuja kwa wingi, lakini mpaka leo hata pale Dar es Salaam, bado. Ni maeneo mengi mno ambayo tunatakiwa tuyaendeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuzungumzia utalii na kutangaza utalii yamefanyika kwenye balozi zetu. Ukitamka mambo ya nje, balozi zetu zote zilizo nje ya nchi zinatangaza utalii, lakini wakija tunafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata watu wenyewe wanaokuja wanataka vitu *organic* na sio lazima tufanye tena vile vitu vya kuweka dawa nyingi, nini, wanataka kuondoka

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wakiwa wametangaza vyakula, wametangaza kahawa nzuri, wametangaza mavazi yetu. Kila mtalii anayeondoka awe anaondoka na rubega shingoni, amemuona Mmasai kava ana yeye anataka kuondokanayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Wizara hii ya Maliasili na utalii itoe zaidi kipaumbele kuhakikisha wananchi wote sasa wanaweza kuwasikiliza na kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwanachama wa *Kilimanjaro Animal Crew*, nilikuwa naomba kuanzia wanafunzi wa shule wapende wanyama. Ni kweli, wanyama ni hatari, lakini kuna wanyama wadogo, hata paka ni mnyama, hata nyani ni mnyama, hawana madhara, hata nyoka ni mnyama. Sasa usiniulize utampendaje nyoka, wewe ukimuona nyoka kama hajakung'ata wewe unamuua wa nini? Muache nyoka apite. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndio hiyo kupenda wanyama. Inatakiwa uwaache na wenyewe waishi kwa sababu Mungu aliumba na alipoumba aliwaumba hao. Wewe usimtafute uadui, hata sisimizi usimuuwe kama hajakung'ata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba shuleni waanzishe *clubs* hizo za kuendeleza utalii wetu ili wakuenalo. Ukienda Denmark na kama hujafika Denmark unanza kusikia pale kwenye *embassy* yao aah, *have you heard the story of Hans Christian Andersen?* Wanakueleza, mimi siku hizo nilikuwa nasafiri kwenda nikasema...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Shally, mchango mzuri.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tarimo, jiandae Mheshimiwa Asia Halamga na Mheshimiwa Asya Mwadini, ajiandae Mheshimiwa Toufiq.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nishukuru kwa nafasi hii ya kuichangia Wizara hii ya Utalii, Wizara ambayo tuna *interest* nayo sana kwenye Mkoa wetu wa Kilimanjaro, lakini nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia kwa lile tukio la *Royal Tour*. Wapo watu wengi ambao bado wanabeza, lakini na mimi niungane na wale wanaomtia moyo Rais kwa sababu tayari amethubutu na amefanya na matokeo yameshaanza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi ambazo wanaendelea kufanya katika Wizara yao ambazo zinaleta matokeo chanya kwa nchi yetu. Mimi nina mambo machache ya kuchangia, nianze na jambo ambalo nilishalileta kwenye swali, la *CSR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yale yenye migodi zile halmashauri zinazozunguka ile migodi zinapata kiasi cha fedha asilimia fulani ambayo ni *CSR* kwa ajili ya maendeleo yao pale pembeni kwa wale wanaozunguka ile migodi. Sasa maeneo yanayozunguka haya mapori pamoja na vivutio vya utalii ni muhimu sana na wao waweze kupata kiasi fulani katika yale mapato ambayo yanapatikana kwenye utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano, Mkoa wa Kilimanjaro kuotesha mti ni hiyari, lakini kukata mti ni mpaka uwe na kibali cha Mkuu wa Wilaya na ni kwa nini tunafanya hivyo? Ni kwa sababu miti kule inahitajika sana kwa ajili ya kutunza uoto ule wa asili na kutunza mazingira ya ule mlima ikiwa ni pamoja na theluji yake. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amesema asilimia 85 ya nishati inayotumika nchini inatokana na mazao ya misitu ikiwa ni mkaa, kuni na vinginevyo. Sasa kule Kilimanjaro haturuhusiwi kukata hiyo miti hata kama unataka kuangukia nyumba, *process* yake ni ndefu. Sasa mkitusaidia *CSR* itawasaidia

halmashauri kuangalia namna mbadala ya ku-*subsidize* maisha ya hawa watu ili wasitumie hiyo nishauti na badala yake watumie nishati mbadala. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie maneno ambayo wameyaongelea Waheshimiwa wawili, Mheshimiwa Neema Mgaya pamoja na Mheshimiwa Swai kuhusiana na kodi nyingi na mimi hili silifunganishi tu kwa kuwaongezea faida wale wadau wa utalii, lakini zaidi ninafikiria kwamba tukiwapunguzia mzigo na biashara hii ya utalii ni *seasonal*, ina maana na wao wataongeza maslahi kwa wale watumishi wao kwa mfano wapagazi ili waweze kwa sababu, watu hawa wamekuwa wakipata mishahara kipindi ambacho ni *high season*, kipindi ambacho ni *low season* wanakuwa wanatangatanga na maisha yao yanakuwa magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili hawa wanaojihusisha na kazi hizi za utalii kama wapagazi, waongoza watalii, waweze kupata kipato hasa kipindi cha *low season* ni vizuri tuwapunguzie mzigo hawa wafanyabiashara ya utalii ili na wao waweze kuishusha hiyo faida chini na wale watu waweze kupata mafao yao bora zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na *debate* kali kwenye mitandao na mengine makongamano yamefanyika mpaka kule Moshi kuhusiana na *cable car*. Na mimi niwasilishe mawazo ya pande zote mbili, upo upande unaosema *cable car* ije na wao wanasema ni aina mpya ya utalii na inahusiana na watu ambao hawapandi mlima na nia yake sio kupeleka watu kileleni, bali ni kuwapeleka eneo ambalo wanaona mandhari nzuri na kuwarudisha. Kwa hiyo, kwao wao ni nyongeza kwenye pato la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upande wa pili wapo ambao wanasema *cable car* inatakiwa ipandishe watu mpaka kileleni, itapunguza ajira, itapunguza siku ambazo mtalii anakaa kule mlimani, itapunguza kipato cha Serikali; na mimi nasema kama ni *cable car* ya namna hiyo basi hatuna budi kuisimamisha, lakini ninaomba Wizara ifanye

tathmini nzuri, ifanye mawasiliano na makongamano pamoja na wafanyabiashara na wadau wengine tuone ni kitu chenye tija, hata ikibidi sio lazima aje mtu kutoka nje kuwekeza kwenye *cable car*, kama haidhuru mazingira yetu na kama ni kitu ambacho kitatuongezea kipato badala ya kupunguza, kitaongeza ajira badala ya kupunguza, Serikali inaweza kufanya yenyewe badala ya kuachia mtu binafsi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunaweza kujenga reli ya *SGR*, kale ka-*cable cars* sidhani kama ni kitu ambacho tunashindwa. Na mifano iko maeneo mengi duniani ambapo *calbe cars* zimekuwepo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongelee *park fees* ambazo nimeziongelea pia kidogo hapo nyuma. Inashangaza kwamba *park fees* zetu upande ambao uko *busy* kama ile *Northern Circuit* bado hazitofautiani sana nah uku *Southern Circuit*. Mimi naishauri Wizara ili kuongea idadi ya watu kule maeneo ambayo watalii hawaendi kwa wingi kule *Southern Circuit* na maeneo mengine kile kiingilio (*park fees*) kingeshushwa sana ili kuvutia watu wengine; kipandishwe pale ambapo tutaona watalii wamekuwa wengi ili kifanane nah uku kwingine. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia yale maeneo yaliyoko *busy* warekebishe kidogo, lakini maeneo ambayo hayako *busy* washushe kabisa kiingilio. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niishauri Wizara suala la *conference tourism*, inajulikana kama *MICE*, ni sekta ya *tourism* ambayo *basically* inafungamanishwa na sekta nyingine, ni utalii wa mikutano. Sasa najua wao kama Wizara hawahangaiki na suala la mikutano, lakini wanaweza wakafungamana na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano *NSSF* wanajenga majengo makubwa tu, lakini ni dhahiri wakijenga kumbi za kisasa za mikutano kwa mfano pale Moshi itaongeza idadi ya watu wanaokuja kwenye mikutano na huo ni utalii, lakini watu hao wakimaliza mikutano wanaenda kwenye vivutio vyetu kutalii. Ni sehemu ambayo inakua sana, utalii

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wa mikutano unahitaji kufungamanishwa. Ni vizuri sana Wizara ianze kuangalia namna ya kuwasiliana na Wizara nyingine kuiwekea hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili haliwahusu utalii peke yao, suala la *intellectual property* na *copyrights*. Magari haya ya utalii ambayo yamekuwa *modified* yalianzia Moshi kwenye kampuni ambayo inaitwa *Rajinda Motors* na walitaka wapewe *copyright* na *intellectual properties* za ubunifu wao, lakini Serikali imekuwa ikiwapiga chenga, sasa hivi yanakuwa *duplicated* kila mahali na sisi hatupati kitu chochote cha ziada. Nilikuwa nashauri inapotokea mtu amebuni kitu, hata kama sio kwenye utalii, lakini kwenye idara yoyote, aweze kupewa nguvu na Serikali, alinde ule ubunifu wake kama ilivyo kwa wale *Rajinda Motors* ambao walibuni haya magari ambayo ni *extended* kwa ajili ya utalii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *rescue services* kwenye Mlima Kilimanjaro. Kuna wafanyabiashara walikuwa na *helicopter* pale *Moshi Airport* na ilifanya vizuri sana kwa sababu watu wakija wanachangia, *incase* akipata shida ile *helicopter* inafanya *rescue*. Sasa hivi haipo kwa sababu, baada ya uvico mfanyabiashara yule ilibidi ashindwe ile biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nashauri Serikali, kama inaweza inaweza kuifanya hii huduma kwa kushirikiana na *NHIF* pamoja na kampuni nyingine ambazo zinaweza zikafanya ile huduma. Ni huduma muhimu inaweza ikatumika hata nje ya huo utalii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Asia.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara ya Maliasili na Utalii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kutoa pongezi kubwa kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan, kupitia filamu ya *Royal Tour* Mheshimiwa Rais ametoa muda wake, Mheshimiwa Rais ametuheshimisha Watanzania na faida nyingi tunazona zimeanza kutokea, lakini tunaamini baada ya mwaka mmoja tutaona manufaa makubwa katika nchi yetu kupitia filamu ya *Royal Tour* iliyotambulishwa na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mfupi huu tu tayari mapato yameanza kuongezeka, lakini pia imesababisha kuendelea kutambulika kitaifa na kuendelea kuongeza mahusiano kati ya Tanzania na nchi mbalimbali huko ulimwenguni, huko duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuupongeza Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (CCM), kupitia Katibu Mkuu wa Vijana kwa kuwahamasisha vijana wa Kitanzania na hivi leo tunavyoongea wameondoka Dodoma vijana kutoka mikoa mbalimbali wakielekea Ngorongoro kwa ajili ya kuendeleza muendelezo wa filamu hii ya *Royal Tour* na vijana wa Kitanzania hawa wanaenda kushuhudia maajabu ya nchi yetu ya Tanzania. Ni zaidi ya vijana 963 kwa hiyo, tumpongeze Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana, Ndugu Kenani Kihongosi, Wenyeviti wa Vijana wa Mikoa pamoja na Makatibu wao kwa kuhamasisha vijana wengine wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Pindi Chana, Naibu Waziri, lakini pia Katibu Mkuu. Ni kwa muda mfupi wameteuliwa kwenye Wizara hii, lakini tunaona namna gani ambavyo wamejipanga kuifanya kazi na kwa nini wamejipanga kuifanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto mbalimbali ambazo ziko ndani ya Wizara, lakini unaona wameendelea kuungana na Serikali kupitia timu ya Mawaziri

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

nane kuweza kutatua changamoto mbalimbali za kimipaka kati ya hifadhi pamoja na vijiji. Niendeleo kutoa rai ya kushirikisha Wenyeviti wa Serikali pamoja na viongozi wa ngazi za chini katika kutatua na kubaini mipaka kati ya vijiji na hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kuipongeza Wizara kwa kuendelea kusimamia miradi mbalimbali ndani ya Wizara ikiwemo mradi wa *REGROW* kule Iringa, mradi wa Saanane kule Mwanza, Geti la Nabi kule Serengeti na miradi mingine mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa namna ya kipekee niendeleo kukushukuru na niishukuru Wizara kwa kufungua mlango unaopita Mamire katika Hifadhi ya Tarangire njia ambayo inakuja Babati, tunawashukuruni sana kwa sababu tunauona sasa Mkoa wa Manyara utaunganika na Kanda yake ya Kaskazini kwa maana ya utalii wa kuanzia Tanga, Kilimanjaro, Arusha na sasa hivi sasa Manyara imeenda kufunguliwa kwa kufunguliwa Geti la Mamire. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuiombe Serikali kwenda kutengeneza changamoto tuliyokuwanayo kwa sasa ni barabara. Tunaomba tutengenezewe barabara ili sasa Mkoa wa Manyara uweze kufunguka na bahati nzuri Mkoa wa Manyara una vivutio vingi vipya na Mheshimiwa Waziri nichukue nafasi hii kumpongeza *RC* wetu Makongoro Nyerere pamoja na ma-*DC* wote wa Mkoa wa Manyara kwa kuendelea kuutangaza utalii na kuibua vivutio vipya vya utalii. Kufunguka kwa geti hilo kutasaidia Mlima Hanang, kule Mbulu kuna kanisa la kipekee kabisa na maeneo mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya leo katika Wilaya ya Hanang, *DC* wetu Janeth Mayanja atakuwa na shughuli ya kuitambulisha *Royal Tour* ndani ya Wilaya, lakini kwa kuwakaribisha wadau mbalimbali na kuendelea kutangaza Wilaya, lakini Mkoa, kwa ujumla wake Wizara ya Maliasili na Utalii. Nikuombe Mheshimiwa Waziri baada ya kumaliza kupitishiwa bajeti karibu sana Mkoa wa Manyara uje ujionee

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kazi wanazozifanya viongozi wa Serikali, lakini kazi wanazozifanya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kipekee niwashukuru vijana wa Mkoa wa Manyara kwa kutengeneza filamu ya *Royal Tour* ya kwetu ya Mkoa. Nimuombe Mheshimiwa Waziri, uniruhusu siku moja nikulettee vijana wale uje utambue kazi kubwa ambayo wameifanya ya kuungana na Mheshimiwa Rais ya kutangaza utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kipekee niwashukuru vijana wa mkoa wa Manyara kwa kutengeneza filamu ya *Royal Tour* ya kwetu ya mkoa nimuombe Mheshimiwa Waziri uniruhusu siku moja nikulettee vijana wale uje utambue kazi kubwa ambayo wameifanya ya kuungana na Mheshimiwa Rais ya kutangaza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye changamoto wanazozipitia vijana katika masuala ya ajira na mazingira ya kazi na leo nitaongelea vijana ma-*tour guide* pamoja na wapagazi ambao ni vijana wanaohusika na kupandisha mlima. Miaka kumi iliyopita Wizara pamoja na makampuni ya utalii pamoja na wapagazi na *tour guides* walikubaliana haya yafuatayo; kwanza, vijana kwa siku watakuwa wanalipwa dola 10 ambao ni wapagazi, lakini ma-*tour guides* watalipwa dola 20. Sasa kiwango hiki cha fedha kwa kweli kwa sasa hivi hakikidhi mahitaji ya vijana wa kitanzania tunaomba sheria ije na ibadilishwe ili vijana hawa waweze kupata maslahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, lakini sambamba na kutangaza wageni wetu kuja nchini kwetu watu namba moja ukiachana na *Migration* wanaofanyakazi kubwa ya kuwa-*handle* wageni na wanaoishi nao na kuisemea vizuri nchi yetu ni hawa vijana ambao wanaopandisha watu milimani ama wanatembea nao kuwaonesha vivutio mbalimbali vya nchi yetu. Tunaomba Wizara isimamie makampuni vijana hawa wanawapandisha watu milimani wakiwa wana masweta ya kawaida. Kwa hiyo, tuombe Wizara isimamie vijana hawa wapandishe na wafanye shughuli hizi wakiwa na vifaa

ambavyo vinastahili, lakini kwa kuzingatia maslahi ya vijana hawa.

Tatu, tuombe Wizara imefanya vikao mbalimbali na wadau wa utalii, lakini tuombe Wizara sasa ikutane na vijana hawa ili kuweza kujua changamoto mbalimbali ambazo zinawakuta kwa sababu wana kero nyingi na wanatamani Serikali yao iwasikilize ili kuweza kuboresha sasa idadi kubwa hii ya wageni wanapokuja waweze kupokelewa na picha nzuri ya vijana wa Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao watu wanaitwa *waiter* ama *waitress* kwenye mahoteli, kwa asilimia kubwa vijana hawa wa Kitanzania wanasomea na baada ya kusoma wakienda kuajiriwa hawaajiriwi wanaitwa ni *ma-trainee* anakaa *trainee* mwaka wa kwanza, mwaka wa pili miaka mitano mtu anaenda kuzeeka hapa kuna kichaka cha kuficha ajira ya Watanzania, ajira ya vijana haki stahiki zao. Kwa hiyo tuombe vijana hawa iwe kuna kikomo cha mtu awe amefuzu elimu yake na anapoenda kuajiriwa awe ni mwajiriwa na siyo ni *trainee* tena. (*Makofi*)

Tuiombe sasa Serikali kwenye ripoti ya CAG imeeleza kwamba kuna vitalu vilitangazwa na vikalipiwa, sasa tuombe tusichafue na tusijitie doa vile vitalu ambavyo vimelipiwa wale watu vitalu hivyo wapatiwa na kuendelea kuhakikisha kwamba ni kweli tumeutangaza utalii ni kweli zile fursa na faida tunazona kwa watu hawa kuondolewa usumbufu huo katika kupewa vitalu vyao. Lakini pia tukumbuke kwamba tuna kila sababu sasa ya kuweza kuongeza muda wa vitalu kwa sababu vitalu mtu anapochukua ana...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. ASIA A. HALAMGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naendelea kupongeza Serikali kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asya Mwadini, ajiandae Mheshimiwa Toufiq.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Awamu ya Tatu, unasema kwamba ifikapo 2025/2026 tunatarajia kupata wageni wapatao milioni tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tuna wageni takribani bilioni 1.5 kwa hiyo milioni moja na nusu maana yake tunatarajia kuwa na *target* ya wageni wageni 3,500 idadi hii siyo kubwa na wala siyo ndogo kama tutafanyakazi vizuri katika sekta hii ya utalii tuna uwezo wa kuifikia hata ifike mwaka huu ama ni mwakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa mdau mkubwa sana katika sekta hii ya utalii na nimekuwa nikichangia mara nyingi kuhusiana na utafutaji wa masoko ya kiutalii.

Niipongeze kabisa kwa moyo wangu wa dharti programu maalum ambayo imeanzishwa ya *Royal Tour* ambayo imekuja kwa maslahi mapana ya kutangaza utalii wetu, lakini vilevile nje tu na kutangaza kwa ajili ya kuleta wageni nchini imeamua na kujikita zaidi kuonesha mambo mengi ambayo yanapatikana kiuchumi ndani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ile *movie* ya *Royal Tour* utakuta kuna masuala mazima ya bandari, bahari, madini na vitu vingine kwa hiyo wawekezaji wanapaswa waje na watakuja kutokana na ile filamu ambayo wameiona na vitu ambavyo vimo ndani ya filamu. Lakini ni kweli tumepanga na filamu ni nzuri na ina jambo jema lakini kama Wizara nilitaka tu nijue wao wana mpango gani na wamejiandaa vipi katika utekelezaji wa programu hii? *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nazungumza haya nilikuwa nafanya mawasiliano na watu wa *tour operators* wa Zanzibar na wamesema wameipokea vizuri na filamu imeanza kuleta *impact* mpaka juzi wakati naongea wanasema kama asilimia ya hoteli 50 tayari zimekuwa *booked*. Lakini tunavyokwenda kutafuta wawekezaji tunahitaji kuleta wageni ndani ya Taifa letu ni lazima tuangalie miundombinu ambayo imetuzunguka. Je, ni rafiki na hawa wageni ambao wanakuja? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii ya utalii ni mtambuka na haitegemei tu kwamba waweze kufanyakazi peke yao lakini kuna wadau mbalimbali ni lazima wawashirikishe ili waweze kuwa wanatatua changamoto mbalimbali. Umekuwa shahidi kwenye Bunge lako zinapokuja changamoto za maji, umeme, miundombinu ya barabara Wabunge wengi huwa wanasimama kuzijadili hoja hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaona kwenye maeneo haya bado yanahitaji kufanyiwa kazi ya ziada kama tumeamua kuleta wawekezaji Wizara hizi ni lazima zishirikiane na Wizara ya Maliasili waweze kusaidiana kwa pamoja ili waweze kuleta maendeleo mapana na tuweze kuingiza pato. Barabara nyingi za kwenda kwenye hifadhi na vivutio vingine zimechakaa na ni mbovu, lakini halikadhalika kuna maeneo hata umeme hakuna yaani kunatumia *solar* na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili jambo maana yake tulipotangaza tunatarajia kupokea na kama tunapokea lazima tuwe tumejiandaa, nje na hayo nisikitike pia kwa mfano changamoto ya watu wa Uhamiaji kuhusiana na kuwapokea wageni wetu maana yake tunasema *reception* ndiyo ina *matter*. Sasa mgeni ndiyo maana kuna Mbunge hapa amechangia amesema wageni wakija huwa hawarudi, lakini mapokezi ambayo yanaanza mwanzo huwa hayana picha nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano ukienda kwenye *destination* ya Zanzibar nachukulia mfano nyumbani, pale

bandarini ukifika wageni ambao wanatoka safari pamoja na abiria wanachanganywa pamoja na wakifika pale Uhamiaji labda unaweza ukawakuta askari wapo wawili au watatu na kuna kundi la wageni na wanapofika pale yaani wageni wamening'inia kama madagaa yametandikwa kwenye mkeka yanataka kuanikwa. (Makofi)

Kwa hiyo, yaani askari anamuita mgeni njoo, wewe ni raia wa wapi, mpaka amsikie mgani anazungumza yaani nimeshuhudia mwenyewe, kiukweli nimesikitika sana. Sasa leo tuna wageni wachache tunakwenda kutangaza filamu na tumeanza kuitangaza kuna wageni watakuja kundi, makundi kwa makundi na nchi tofauti kama tunahitaji kweli kukuza utalii wetu lazima maeneo haya yakafanyiwe kazi za kimkakati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nishauri kwenye hii programu ya *Royal Tour*, kwanza kabisa kwa sababu *Royal Tour* imezungumza itakuja na *phase* ya pili na *phase* ya tatu, *phase* ya pili wajitahidi sana kushirikisha sekta binafsi ambao ndiyo wadau wakubwa wanaofanyakazi katika masuala mazima ya utalii. Lakini la pili washirikishe wazawa kama ni *royal* basi hata tuje na jina ambalo tunaweza tukasema *local tour* ambao wazawa wajue umuhimu wa kushiriki kwenye utalii na isifike hatua tukawa siku zote tunawategemea wageni kutoka nje ya nchi ndiyo ambao waweze kutuingizia pato. Sasa tuwaingize na wazawa ili tuweze kutengeneza picha na tafsiri pana ya kuweza kukuza utalii wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni la uwekezaji, tuendeleo kuhamasisha wawekezaji Mheshimiwa Waziri aliposimama hapa kwenye hotuba yake alisema kuna wawekezaji 30 tayari wameanza kutembelea Tanzania, kwa hiyo, kuna haja kuweka mazingira rafiki, tuache kuwawekea vikwazo ambavyo havina tija ili tuweze kuwasaidia waweze kuwekeza katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hii filamu ya *Royal Tour* imeandaliwa na wenzetu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo lakini kwa kuwa kuna Bodi ya Utalii

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ambayo kila siku kazi yao kukaa chini kutengeneza mipango mikakati ya kuweza kutangaza Tanzania hii ni kama hawajakabidhiwa. Niiombe Wizara ya sanaa wawakabidhi Wizara ya Maliasili kupitia Bodi ya Utalii ili waweze kwenda kufanyakazi vizuri na iweze kuwa ni nyenzo kama nyenzo zao nyingine waweze kuwa wanaitumia katika kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hifadhi zetu za Taifa, ndani ya Taifa letu tuna hifadhi 22 ambazo kwa sasa ambazo zimetangazwa, lakini ufanisi siyo wa kuridhisha na hifadhi ambazo zinafanya vizuri yaani zinaweza zikawa labda ni tano mpaka labda kuelekea 10, tano na siku zote ndiyo tunaisikia Serengeti ndiyo inafanya vizuri na imekuwa migogoro mingi, kila siku ziamkapo watu wanalalamika tembo, tembo, tembo, mazao yanapotea askari wanapigana na raia, raia wanapigana na askari hili jambo halileti afya na wala siyo sifa kwa Taifa na tuna uwezo wa kuliondoa kama tutashirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zozote duniani zilizoendelea wamewakaribisha vizuri wawekezaji wa sekta binafsi na hizi hifadhi 22 kwa Serikali bado ni mzigo mkubwa kwa hiyo kuna haja kabisa...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante kwa mchango wako kengele ya pili hiyo. Mheshimiwa Toufiq

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi

NAIBU SPIKA: Ahsante.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Nami niungane na Wabunge wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri

pamoja na Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo muda ukiruhusu nitaongelea kuhusu *Royal Tour* na pia nitazungumzia kuhusu uendelezaji wa fukwe pamoja na umuhimu wa mafunzo mara kwa mara watoa huduma wa kitalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan ambaye ni mhusika mkuu katika filamu hii ya *Royal Tour*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ana dhamira ya dhati ya kutangaza utalii wa Tanzania na vivutio vyake ili kuliongezea pato Taifa letu, pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameimarisha utalii katika Tanzania katika ile filamu ya *Royal Tour* sambamba na hilo Mheshimiwa Rais ameibeba Wizara ya Maliasili na Utalii katika nchi yetu pia Mheshimiwa Rais ameiweka Tanzania katika anga za kimataifa kwa kuitangaza hii filamu ya *Royal Tour*. (Makofi)

Mheshimiwa Rais pia amevutia wawekezaji wengi sana, ninaamini kabisa baada ya hii filamu ya *Royal Tour* watalii wengi wameanza kuja na wengine wengi sana watakuja. Halikadhalika hivi karibuni tumeona tija kwamba mwekezaji mkubwa sana kutoka Marekani ambaye ni Munir Walji amefika nchini kuhusu uwekezaji katika hoteli za kitalii. Hii ni hatua ya mwanzo na tunaamini kabisa watalii wengine wengi watakuja hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika mimi naamini watalii wataongezeka sambamba na hilo safari za ndege zitaongezeka, lakini sambamba na hilo uelewa wa Watanzania kuhusu utalii nao utaendelea kuongezeka na watalii wa ndani wa nchi yetu yaani Watanzania wengi zaidi

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

watakwenda kutalii kwa hiyo hivyo pato la Taifa litazidi kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa ujumla hii ni faida kubwa sana kwa *Royal Tour* ambayo Mheshimiwa Rais wetu ameifanya na tuendeleo kumpongeza, tumtie shime na tuendeleo kumuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema ili kusudi aweze kuliongoza Taifa letu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kuwa Wizara iendeleo kuweka juhudi katika kutangaza na kuimarisha huduma zenye hadhi ya kimataifa, lakini sambamba na hilo wanafunzi wengi waendeleo kuelimishwa umuhimu wa utalii ili kusudi wajenge tabia na wao watakapokua waweze kuwa watalii. Lakini sambamba na hilo ushauri mwingine waandishi wa habari waweze kupewa uwezo wa kuweza kuripoti habari zaidi zinazohusiana na masuala ya maliasili na utalii ili kusudi waweze kuitangaza vizuri nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo Watanzania nao pia waendeleo kuhabarishwa kuhusiana na masuala ya utalii ili kusudi na wenyewe nao pindi wanapokutana na wageni waweze kuwaelezea kuhusiana na vivutio vya nchi yetu vilivyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba pia nizungumzie kuhusiana na uendelezaji wa fukwe ili kuboresha utalii; kuna haja ya Serikali kutafuta wawekezaji watakaojenga mahoteli ili kuweza kuboresha huu utalii wa fukwe kwani hii itasaidia kwamba wale wageni watakaokuwa wametoka kwenye mapori, wametoka kwenye misitu basi wanakwenda kwenye fukwe ili kusudi nako kule waweze kufanya utalii na kupumzika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilipenda kulizungumzia ni mafunzo ya mara kwa mara kwa watoa huduma za utalii, hili nalo ni eneo muhimu sana kwa sababu watalii wanaokuja sasa hivi Tanzania yaani wanaokuja kwa kurudia kwamba wakija mara ya kwanza wakitaka kurudia tena hawazidi asilimia 20. Kwa hiyo, ipo

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

sababu ni kwamba hawa waongoza utalii waweze kupewa mafunzo zaidi ili kusudi wawe na mbinu bora zaidi za kuweza kuwavutia watalii watakaokuja mara kwa mara ili kusudi kuweza kuendeleza utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo najua kwamba wenzetu Chuo cha Mweka wameweza kutoa mafunzo haya walau kwa waongoza utalii 1,060. Kwa hiyo, naomba waongezwe wengine ili kusudi mwisho wa siku waweze kupata ujuzi na wakipata ujuzi ina maana kwamba wataweza kusaidia katika kutangaza utalii, askari wanyama pori, wale askari wa misitu na kadhalika kwa hiyo hawa wote waweze kupewa mafunzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kuzungumzia nikuhusiana na *cultural tourism*. Bado hatujalitumia sana eneo hili wenzetu kwa mfano wenzetu Ethiopia asilimia 70 ya utalii wao wanategemea kwenye *cultural tourism*, sisi tuna makabila mengi sana na tunaamini kabisa na sisi tukijikita katika *cultural tourism* naamini kabisa tunaweza tukapata watalii wengi sana zaidi.

Kwa hiyo, ushauri wangu tutume wataalam watakaoenda kujifunza kwani sisi tuna makabila mengi sana kwamba ukienda kule kwa wahehe *the way* wanavyo *dress* unajua kabisa hawa wanaonekana, ukienda labda usukumani *the way* wanavyo *dress* wanajulikana, ukienda umasaini uhayanina maeneo mengine yote. Kwa hiyo, tukiwa na ile *cultural tourism* mimi naamini kabisa watalii wengi watakuja basi na hiyo itasaidia kuongeza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda siyo rafiki baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango mizuri sana na Mheshimiwa Waziri na watu wako natumai mnayapokea na mtayafanyia kazi. Sijui kama mnazo *personal data* za watalii wanaokuja nchini kwa maana mnawasalia hata kama haji mnampelekea taarifa,

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

salamu za mwaka, *seasonal greetings*, salamu za *Christmas*, salamu za Eid ili wajue mna-*care* na ndio maana wanasema watalii hawarudi, lazima kukaa kuwabembeleza kwa sababu hii ni biashara. (*Makofi*)

Lazima muwe na kitengo maalum, tunataka kweli target ya watalii milioni tano hadi sita mpaka mwaka 2025 wakati Rais anarudi madarakani, anarudi na watalii milioni sita, ndio maana yakee. (*Makofi*)

Kwa hiyo kuna kazi kubwa ya kufanya, muwe *zero distance* na hawa watu, *customer service*, watu wa *Immigration* kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, hatutaki majambazi waje lakini wale ambao wanauadilifu wapokelewe kwa heshima na kwa tabasamu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi nafikiri upo umuhimu sana wa kutazama *data* zao na kuendelea kuwavutia kurudi. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana, hii *Royal Tour trophy of tourism diplomacyn*chini mwetu, ni zawadi ya vizazi na vizazi na vizazi. Kama ulivyosema yeye kaupiga, tujulize wewe unaupiga wapi? Sio kona apige yeye, kichwa apige yeye, *penalty* apige yeye, adake yeye, hapana, mambo mengine tufanye sisi wote, sio Mawaziri tu, bali wananchi wote ndio kazi yetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Mwita Waitara, atakuja Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mheshimiwa Mchafu, Mheshimiwa Cherehani, Mheshimiwa Mulugo, Mheshimiwa Salma Kikwete, Mheshimiwa Sitta, Mheshimiwa Gambo na wengine wataangazwa na Kiti pale ambapo kutakuwa na mamlaka ya Kiti itafaya hivyo.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA
MALIASILI NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Pallangyo Mheshimiwa Hawa Mchafu ajandae.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi nimefika na mambo mawili tu ya kuzungumza leo; jambo la kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa *Royal Tour* ambayo imefanyika Tanzania, kazi ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais ni ya kuitangaza nchi, lakini pia kuisemea, lakini amefanya kazi kubwa sana ya kuutangaza Mlima Kilimanjaro kwa sababu kuna watu waliaminishwa kwamba Mlima Kilimanjaro hauko Tanzania upo Kenya lakini kwenye kupanda mlima ule ameitangaza nchi, lakini vilevile sisi watu wa Serengeti wakati ule wa nyumbu anapokuwa anavuka Wakenya wanapanga ratiba wanasema nyumbu ni wa Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Rais alienda Serengeti na akaonesha kwamba ile ni sehemu ya Tanzania na Mbuga ya Serengeti inaendelea kushamiri. Lakini vilevile ni muhimu watu wakajua kwamba kitendo cha Mheshimiwa Rais pia kuweka wazi mikakati ya kupambana na *Covid-19* ilisaidia sana kufungua nchi, lakini pia na watalii kuongezeka. Wenzetu wanataka kujua kama kuna tatizo namna ya kuweza kuliondoa na kupambana nalo, hiyo pia ilisaidia sana. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, lakini zipo faida mbalimbali ambazo pia tumepata kama nchi na Mheshimiwa Rais amesaidia ndege nyingi za kitalii na za kimataifa kuongezeka kuja hapa Tanzania kwa mfano tarehe 4 Juni yaani kesho *Eurowings Discovering* wataanza kutoka moja kwa moja Ujerumani kuja hapa *KIA* na watabeba watalii 300 kwa wakati mmoja watakuja mara mbili kwa wiki, lakini tarehe 20 Juni, 2022 *Dutch Airlines* watatoka *direct* kule na kuja moja kwa moja *KIA* na kuongeza idadi ya watalii, kwa hiyo ni faida ambazo zinapatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, abiria wameongezeka lakini pia miruko ya ndege imeongezeka katika eneo hili, lakini vilevile mashirika mapya yameongezeka kuleta ndege zao pale, lakini mapato ya Serikali yameongezeka katika eneo hili na ajira rasmi na ambazo sio rasmi zimeongezeka, hiyo ni baadhi tu ya faida ambazo tumepata kutoka kwa hao watalii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana tunaomba aendelee nayo.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi watu wa Tarime tunamshukuru Mheshimiwa Rais ametoa fedha kujenga kilometa 89 kutoka Tarime mpaka Mugumu Serengeti, kwa hiyo hata kama kuna watalii kutoka Kenya kule watawuka pale wataenda pale Kibaso na Marariet na kuweza kutoa huduma na fedha itaongezeka na uchumi utaongezeka katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba katika eneo hilo la *Royal Tour* Wizara iongeze *package* ya Kiswahili kama sehemu ya utalii, kama inawezekana wale wenzetu wakija hapa kwetu tu wapate *crash program* ya kufundishwa Kiswahili ili wakienda wajue kwamba Kiswahili kipo Tanzania na sisi ndio wataalam wa Kiswahili, kwa sasa ilivyo katika somo huko duniani Wakenya wanapata ajira kubwa sana ya Kiswahili kana kwamba wanakijua kuliko Watanzania, kwa hiyo tutumie fursa hiyo kutangaza Kiswahili chetu, vijana wapate ajira lakini pia ipatikane ajira ya ukalimani. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo kwa kweli mambo yote mazuri hayo ya *Royal Tour* yanaharibiwa na migogoro iliyopo katika maeneo yetu. Kule kwangu Tarime Vijijini Mheshimiwa Rais alikuta Tume ambayo ilikuwa imeundwa na mtangulizi wake Mheshimiwa Magufuli akafanya maamuzi akaelekeza Mawaziri nane waende kwenye maeneo yetu kutatua changamoto. Nasikitika kusema mpaka leo tangu nimezungumza hapa hotuba ya Waziri Mkuu, Wizara hatujawasiliana wala wahusika na kule katika eneo la mgogoro hawajafika kwa hiyo, watu wangu wanalalamika, lakini vilevile kuna vijiji 975 ambavyo vinahusika katika maeneo mbalimbali zaidi ya mikoa 10 na kitu ambayo ina mgogoro wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni jambo kubwa ambalo Wizara lazima ilibebe na ilifanye, kama Mheshimiwa Rais amesimamia *Royal Tour* imeanza inafanya kazi, watalii wanakuja, ndege zinaongezeka, lazima tutatue migogoro ya wananchi wetu, itakuwa haina maana sana kama tunapata faida ya watalii kuongezeka halafu migogoro ipo katika maeneo yetu, inatia doa katika kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Rais amefanya, hivyo Mheshimiwa Waziri unayo kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ningechangia tofauti sana kama mwenzako mtangulizi angekuwa amekaa hapo, nilimuomba mara kadhaa tangu mwaka 2020 aende pale Tarime aende pale Nyanungu, aende Gorong'a aende Kwihancha, hawajawahi kwenda kuwasilikiza wananchi wangu na wanalalamika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tarime ina kata tatu ambazo zina mgogoro na Hifadhi ya Serengeti na tuna vijiji saba, huu mgogoro pia unagusa watu wa Bunda, inagusa watu wa Serengeti, inagusa watu wa Butiama inaenda mpaka Rorya utaona ni sehemu kubwa sana ambapo tungepanga haya mambo...., ukienda Kijiji cha Masanga, Kenyamosabi, Kegonga, Nyandage, Karekatonga, Kibaso, Nyabirungo huku kote kuna migogoro mikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hawaishii hapo, nataka niseme tu kwamba yapo mambo ambayo yamefanyika katika eneo la Tarime yametesa sana watu wangu, kwa mfano kuna maeneo ambayo watu wameuawa, unashangaa mtu analishwa mizoga, watu wanalishwa pilipili mpaka wengine wamekuwa vipofu, lakini pia wanachoma nyumba wa watu, wanaharibu mazao ya watu. Hili jambo sio jambo zuri. Kwa mfano ukienda Kata ya Gorong'a kuna watu 10 wameuawa, Wanene Masyaga, Chacha Nyahiyo, Nchakwa Chacha Mahanga, Chacha Mwita Magori, Lucas Gasaya Marwa, Manga Wankyo, Wambura Chacha Mwaisori, Mwita Ryoki, Woryo na Manga Karumanga hii ni kata moja tu watu 10 wameshauawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kata ya Nyanungu kuna watu watano; Nyang'anyi Chacha, Mwita Nyangaya, John Sensema, Marwa Sasi, Mwita Chacha Mugesu hii miili mingine ilipotea ili kupoteza ushahidi, na Tume zimeundwa nyingi sana hapa sio sawa waliokufa, waliopigwa risasi, tunao watu hapa saba Chacha Magalya, Woryo, Seerya Magaiwa, Matiko Gesabo, Emaru Moseti, Boke Waisiko, Chacha Mwiniko hawa wamepigwa risasi wapo ni walemavu.

Mheshimiwa Spika, Tume zimeundwa nyingi, bahati mbaya katika eneo hilli unaunda Tume ambayo gari lenyewe tunawalalamikia watu wa TANAPA Serengeti wanatoa gari, wanatoa posho, wanatoa hoteli, wanaandaa chakula, ripoti zote hazijawahi kutoka, nikisema hayo mambo utafikiri natunga. Ningeomba Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili aende katika Jimbo la Tarime Vijijini aone kwamba mambo haya ni ya uongo au ni ya ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ninayoyazungumza yapo na nimewaandikia barua wahusika wa Wizara hii kwamba nendeni mkawasikilize, ukienda kwenye mipaka ya hifadhi nililalamika kwamba mmechukua greda, mmelima barabara katikati ya mashamba ya watu, lakini mashamba yale...

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Mwita kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

T A A R I F A

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nimshukuru mchangiaji anayechangia, naomba tuweke kumbukumbu sawa, nampa taarifa kwamba anaposema Mawaziri hawajafika katika mikoa iliyotembelewa mara mbili kwa ile timu ya Mawaziri Wanane mkoa wake ni mmojawapo ambao tumeenda mara mbili, timu ya kwanza ilienda ikiongozwa na Mheshimiwa Lukuvi walienda mpaka vijijini, ile ya pili tumeenda tumeongea na ule uongozi wa mkoa na maelekezo yote yametoka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, anaposema hawajaenda aweke kumbukumbu vizuri kwa sababu tunaweza tukapotosha kwa kitu ambacho sio sahihi sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara unaipokea taarifa hiyo?

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sina nia ya kutaka kubishana na Mheshimiwa Waziri dada yangu Dkt. Mabula, ninachosema kwamba walienda Musoma wakaishia Musoma Mjini hawakwenda Nyanungu, hawakwenda Gorong'a, hawakwenda kwa wananchi, na mgogoro uliopo ni kwamba *beacon* ambazo zinatangazwa *GN 235* ya mwaka 1968 wananchi wanabishania kwamba siyo kweli. Kwihanja walipokwenda wataalam wakakutana na viongozi wa wananchi wale wazee, wakawaonesha na *beacon*, leo mgogoro umekwisha pale Kwihancha, hapa sehemu ya Gorong'a na Nyanungu ni kwamba *beacon* wanasema ni za kwao, ni eneo la hifadhi, wananchi wanasema hapana tunakaa hapa, watu wamezaliwa pale miaka 80 unaishi hapo, ukienda ukakaa nao watakuonesha *document* zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri eneo hili kuna watu ambao wamezaliwa wameongoza miaka 20 Udiwani wapo hadi leo. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri na wenzake wa Maliasili na Utalii watume watu waende waongee na wale wazee au niwalete hapa uwasikilize ndio hoja iliyopo.

Mheshimiwa Spika, lakini ipo mifugo imekamatwa, kwa mfano Nyangage watu 20 wameathirika na kukamatwa mifugo yao...

SPIKA: Mheshimiwa Waitara ngoja, kabla haujahamia kwenye mifugo unajua nilikuwa naiskiliza hoja yako ili nielewe unaelekea wapi, umetaja hapo watu waliouawa, umetaja hapo watu waliopigwa risasi kwa maana ya kwamba wameumizwa. Huyo anayeyafanya hayo ni nani maana hayo mambo ni mazito sana, anayeyafanya hayo ni nani?

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, mambo yote hayo ya risasi na mauaji watuhumiwa wanaolalamikiwa ni wa Hifadhi ya Serengeti kwa sababu watu wanapotea kwamba wameenda kuchunga halafu hawaonekani na ilikuwa ng'ombe wamekamatwa, lakini mtu haonekani, kwa hiyo wanaotuhumiwa hapa ni Hifadhi ya Serengeti, sasa nani *specific* kwa maana ya majina...

SPIKA: Ngoja, ngoja, kama hizo ni tuhuma mbona wewe umezisema kana kwamba inajulikana kabisa kwamba ni nani aliyefanya hayo mauaji na ni nani aliyepiga hizo risasi.

Kwa sababu hili ni Bunge, ukisema mambo mazito kama hayo na kwamba kuna Tume hazijawahi kufanya chochote na hayo mambo hayajatokea jana wala leo, sasa hebu liweke vizuri ili mimi nijue nini cha kuiagiza Serikali hapa.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sijataja majina ya watu hapa, ninachoomba hapa ni kwamba haya ni malalamiko ya wananchi na majina yapo na Tume zimeundwa kwa mfano huyo Manga Kahurumanga ni mwaka jana, Mkuu wa Mkoa aliunda Tume na mimi nilikuwepo, ripoti mpaka leo hayajatoka. Kwa hiyo,

hayo yote yamefanyiwa kazi majibu kwa wananchi pale hakuna.

Kwa hiyo, nitaomba utusaidie kwamba viongozi wa Serikali na hasa wa Hifadhi ya Serengeti haya malalamiko wayafanyie kazi yakome yasiendeleo, yaani watu wasipotee katika mazingira ya kutatanisha, ndio ombi langu.

Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: Ngoja, ngoja.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu tuhuma hizo ni nzito sana na tuhuma zinaelekezwa kwa chombo cha Serikali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, tuhuma anazozitoa Mheshimiwa Mbunge katika kuchangia ni nzito kwa kweli na mimi nakuelewa kwa nini unataka upate angalau nini ambacho Serikali inasema.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ni kiongozi tena wa muda mrefu na uwakilishi wetu sisi kama Wabunge sio kusema tu ndani ya Bunge, ipo mifumo mbalimbali ambayo tunakutana na Wabunge na Serikali. Sasa kulileta hapa jambo zito kwa maelezo ya namna hiyo mauaji, risasi, hakuna kinachofanyika ni tuhuma nzito ambazo kwa kweli pengine zinahitaji tafakari, lakini pia kwa nafasi ya humu niseme tu kama anazo tuhuma mahsusi si vizuri kuzisema kwenye chombo hiki kikubwa badala ya kuwa tumekutana na tukapata hizi *information* na utafiti ukafanyika, tukajua kweli ni vipi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mtu akipotea haina maana mtu ameuwawa kuna watu chungu mzima hapa wana ndugu zao wamepotea. Hata mimi mwenyewe kwetu kuna watu wamepotea, sasa sio akipotea ameuwawa na mtu fulani au na watu fulani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nadhani ama atuhakikishe hilo analolisema na kama anaweza kuonesha ushirikiano na Serikali katika kueleza hayo yote anayoyasema au afute maelezo haya yasiwe sehemu ya mchango wake. *(Makofi)*

SPIKA: Sawa, sasa Mheshimiwa Mbunge yeye ameeleza kwa kirefu na mimi nilikuwa ninamskiliza ili nielewe hoja yake inaelekea wapi na kabla hajahamia kwenye mifugo kuna hoja nzito ya watu waliopigwa risasi ambao maana yake kwa maelezo yake yeye na amewasoma hapo majina maana yake wapo waliopigwa hizo risasi kwa maelezo aliyoyatoa yeye, lakini pia amesoma hapo majina akisema hawa watu wameuawa. Maana yake kwa maelezo yake yeye anao ushahidi kwamba wameuawa kwa sababu hauwezi kusema mtu ameuawa kama amefariki, wanaofariki wapo wengi watu wanaumwa malaria na nini ukisema mtu ameuawa maana yake lazima kuna ushahidi unaoashiria kwamba kuna mtu amemua mtu mwingine.

Sasa kwa sababu hili jambo ni zito kwa kweli na tupo kwenye Wizara hapa wakiwa wameleta hoja hapa ili tuwapitishie jambo lao, sasa Mheshimiwa Waitara huo ushahidi ulionao kuhusu mambo haya, wewe niletee mimi huo ushahidi ulionao, halafu huo ushahidi ulionao ukishaniletea mimi nitaiagiza Serikali kwa sababu siko nao huo ushahidi hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niletee ushahidi ili mimi niagize Serikali kuhusu jambo hili kwa sababu tuhuma hizi ni nzito sana ulizozitoa hapa ndani. Malizia mchango wako. *(Makofi)*

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na nitafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninasema kuna mifugo ya watu inakamatwa kwa mfano nimesema Kata ya Nyandege watu wameathirika mifugo yao, Tyegonga watu 18; Korong' a watu 17; na hayo yote ya mifugo kuna malalamiko makubwa sana, jambo baya lililofanyika pale ni kwamba wanakamata

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

mifugo ya watu hawa ni jamii moja; mjomba, shangazi, sisi ni wale wale, halafu wanapeleka pale Kibaso kwenye uwanja wa wazi wanapiga mnada ng'ombe za watu.

Mheshimiwa Spika, unajua katika maisha yetu kama mtu alikuwa analimia ng'ombe zake halafu wamekamatwa wakaenda wakauzwa, mwenzake akachukua unatangaza watu waanze kuuwana.

Mheshimiwa Spika, ningepia pia hata kama ni faini au hata kama ni kuuza wasiuzie pale pale katika maeneo yale yale ya jirani wapeleke sehemu nyingine kama ni lazima wauze mifugo ya watu. Nitaomba sana hapa kwamba watu wa Hifadhi ya Serengeti wanatakiwa watoe huduma na ushirikiano kwa watu wale wanaokaa karibu na Hifadhi ya Serengeti, waliahidi CSR lakini maeneo haya hakuna maji, hakuna malambo hakuna zahanati...

(Hapa kengele ililia kuahsiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Mwita Waitara kengele ya pili imegonga, nakupa dakika mbili umalizie mchango wako.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kwamba kwa kuwa hawa watu wa hifadhi wanafanya shughuli pale, ugomvi ulipo kwenye kata yangu na ni ugomvi mkubwa ni kwamba pale wakati wa kiangazi hakuna malambo, yamekauka, hakuna mito tofauti na Mto Mara, hawa wa hifadhi waliahidi kwamba wangepachika malambo katika eneo lile ili wakati wa kiangazi mifugo ipate maji, wasiende kwenye Mto Mara, katika hali ya kawaida kama hakuna *alternative* wakati wa kiangazi watu wataenda kwenye Mto Mara, wataenda kulisha ng'ombe na kuchota maji, ugomvi unaanzia pale, wanakamatwa. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ningeomba kwamba yapo mambo mengi katika Hifadhi ya Serengeti, tunapenda kuunga mkono Serikali kwa kazi nzuri, lakini naomba Mheshimiwa Waziri kwa dhati kabisa ni mpya kwenye Wizara hii, lakini ningeomba jambo la kwanza twende pale mambo ninayozungumza hapa siyo kwa kwangu, wanipe nafasi ya kwenda kukaa na wananchi, awasikilize, aone hata hizo familia azitembelee, utagundua kwamba kuna shida kubwa pale Tarime na kwa kweli naomba msaada wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba ulibebe jambo hili kama mzazi. Kule kuna kilio kikubwa sana, migogoro ya ardhi hapa ni karibu kila Mkoa, Waziri lazima ajiipange. Kazi nzuri ya utalii ili ifanyike vizuri lazima migogoro kwenye majimbo itatuliwe, twende tuwasikilize watu, kama ni kusogeza mipaka bahati nzuri Mheshimiwa Rais ameonesha njia jambo hili siyo jema, tunataka mapato ya utalii, lakini watu wetu pia waendeleo kuishi kwa amani na kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Mwita, leo ni siku ya Ijumaa nitakupa nafasi mpaka siku ya Jumanne niwe nimepata ushahidi wa hayo yote uliyoyasema hapa.

Mheshimiwa Dkt. Pallangyo atafutaiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu, Mheshimiwa Cherehani ajiandae.

MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi nichangie kwenye hotuba hii ya bajeti ya Maliasili na Utalii na moja kwa moja niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais Mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anawafanyia Watanzania hakika tumeshuhudia akihangaika huku na kule akituhangaikia sisi kama mama anavyohangaikia familia yake tunampongeza sana. Lakini amekwenda mbali zaidi akaamua kutengeneza filamu ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Royal Tour ambayo kimsingi imekuja kufungua nchi yetu kwenye biashara ya utalii na tunaamini kabisa kwamba sasa hivi tutapata watalii wengi na nimedodosa kule Arusha kuna makampuni mengi ya utalii wanasema *booking* zipo nyingi sana ni juu yetu sasa kujipanga kwa ajili ya kupokea wageni wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kumpa nafasi ya juu kwenye Wizara hii kama Waziri. Lakini pia nimpongeze Naibu Waziri Mheshimiwa Mary Masanja kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais akambakiza kwenye nafasi yake ya Unaibu Waziri kwenye Wizara hii, hawa wote viongozi wetu hawa wanafanya kazi nzuri wanatosha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kumpongeza sasa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu watendaji wote pale Wizarani kwa kazi nzuri ambayo wanafanya hakika tunawaona tunashuhudia, hata ukisoma hotuba ya Waziri mapato yatokanayo na maliasili nyuki wenyewe tu inachangia *percent 3.3* kwenye pato la Taifa, si hivyo tu inachangia *percent 5.9* kwa biashara ya nje ya nchi hii lakini biashara ya utalii inatupatia kwenye pato la Taifa *percent 17* lakini pia *percent 25* ya fedha kutoka nje. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni kazi nzuri nilibahatika nilipata neema ya kutembelea Hifadhi ya Ngorongoro mwezi wa tatu nikiwa na Kamati yangu pamoja na Hifadhi ya Mkomazi kwenye mradi wa faru kazi zinazofanyika kule zinafurahisha tunaamini kabisa kwamba uhifadhi na utalii unakwenda kukua kwa kiwango kikubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naendelea kupongeza Wizara, lakini pia niseme kwamba kwa jinsi utalii unavyokua nchini mwenzangu asubuhi alizungumzia kuhusu *cable cars*, hakika milima yetu kuna milima miwili Mlima Kilimanjaro na Mlima Meru ni vivutio vikubwa sana kwa utalii nchini hapa. Nilipata neema ya kwenda *South Africa* nikashuhudia jinsi ambavyo *cable cars* zinafanya kazi naamini kabisa kama huku

tunakokwenda tutajenga hizo *cable cars* kwenye Mlima Kilimanjaro na Mlima Meru tutasomba watu wengi kule mjini ambao watakwenda kupanda mlima na kushuhudia vivutio vya utalii, lakini pia kuingiza na kuongeza pato la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na salamu zangu hizi za pongezi, kule kwenye jimbo langu kuna changamoto ya mpaka wa Kijiji cha *Olkung'wado* na Hifadhi ya Arusha. Changamoto hii ilisababishwa na *TANAPA* kununua mashamba mawili yaliyopo kwenye Kitongoji cha Momella na inavyoelekea ni kwamba Serikali ya Kijiji na wananchi hawakuhusishwa vizuri matunda yake ni kwamba sasa hivi kuna sheria mbili zinafanya wananchi wanapata shida, wanateseka kidogo. Sheria ya Uhifadhi inawafanya wananchi pamoja na kwamba kile kijiji yale mashamba walikuwa wanaishi pale, wamezaliwa pale wanaonekana kwamba wamevamia.

Kwa hiyo, wahifadhi wakiwaona wakiwa palepale kwenye mashamba yale wanawaona kama wameingilia hifadhi. Pia Sheria ya Ardhi inaona kama wame *trespass*, wamevamia sehemu ambayo si ya kwao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi nishauri Sheria ya Ardhi ina sehemu ambayo inasema kwamba yaani inatoa mwanya kwamba kama mwananchi amekuwa kwenye ardhi kwa zaidi ya miaka 12 anaweza akapewa kwa kutumia kipengele cha *address possession*.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba Wizara hizi mbili Maliasili na Wizara ya Ardhi wakae chini, waangalie ni wapi makosa yalifanyika kwa sababu kile kijiji kina Mwenyekiti wakati mashamba haya yananutuliwa alikuwepo Mwenyekiti na Mwenyekiti ardhi ipo chini yake sijui kama aliridhia hayo manunuzi. Kwa hiyo, kwa kweli nashauri kwamba Waziri wa Maliasili na Waziri wa Ardhi wakutane waone ukweli wa hili jambo kwa sababu ukifuatilia mgogoro huu wananchi wanavurugwa mara kwa mara, wanapigwa mabomu wakati mwingine, wanafukuzwa, mifugo yao

inafukuzwa, lakini pia mashamba yao yanaharibiwa na jambo hilo si sawa ni tofauti na ni kinyume kabisa na azma ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo inazungumzia maisha bora kwa Watanzania wote, hilo ni ombi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matukio yaliyotokea mwaka 2017/2018 hayafurahishi hata kidogo na ndiyo maana nilisema niliseme hili kwa sababu wahifadhi wana *element* ya kupenda wanyama na misitu yao kulliko binadamu na hilo si kosa ndiyo kazi waliyopewa, lakini pia tukubali kwamba na binadamu wana *value* yao na tunataka wananchi wafurahie maisha yao katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, Mheshimiwa Phillip Mulugo, ajjandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Awali yayote nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dada yangu Pindi Chana pamoja na Naibu wake Waziri Mary Masanja, Katibu Mkuu wa Wizara hii Dkt. Francis Michael na Naibu wake Juma Mkomi kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nitapenda kuanza mchango wangu kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan juu ya suala zima la *Royal Tour*. *Royal Tour* imefungua na kuitangaza zaidi nchi yetu, vivutio vya utalii vilivyopo hapa nchini lakini pia sambamba na hilo *Royal Tour* imeweza kuongeza fursa za uwekezaji na utalii hapa nchini kwetu. Hivyo ni muhimu sana *Royal Tour* ifanyike kwa kasi kubwa sana. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, matokeo ya *Royal Tour* leo tumeweza kuongeza watalii wengi zaidi, tunaambiwa Mkoa wa Dar es Salaam, Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Kilimanjaro kwa miezi mitatu ijayo hoteli zipo *full booked* kwa ajili ya kupokea watalii kuingia nchini. Lakini kwa upande wa ndege wameongeza *flight* mfano, *Emirates* kutoka tatu kwa wiki mpaka saba kwa wiki, *Qatar* kutoka saba kwa wiki mpaka 15 kwa wiki. Hii ni hatua kubwa sana ama ni matokeo makubwa sana ya *Royal Tour*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ingawa lengo la *Royal Tour* si kuongeza tu watalii pia tunahitaji *investment* pamoja na biashara ili kukidhi mahitaji ya watalii wetu hapa nchini. Kama hivyo ndivyo watalii wetu hapa nchini watahitaji hoteli nzuri, *rest house*, vivutio vya huduma muhimu, barabara nzuri, usafiri wa ndege wa uhakika, wahudumu wazuri *interns of customer care*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni vema Bunge lako likafahamu utalii ama Wizara hii ya Utalii *can't stand alone* ili kuweza kufikia mkakati sawasawa wa masuala mazima ya utalii hapa nchini. Hivyo basi Wizara kama Miundombinu, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Mawasiliano na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni lazima zizungumze lugha moja ili tuweze kufikia malengo tarajiwa ya sekta nzima ya utalii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa na kazi nzuri sana ya kuhakikisha milango ya utalii inafunguka na imefunguka kwelikweli. Tumeona kwenye filamu ya *Royal Tour* kupitia hapo kisiwa chetu cha Zanzibar kimeweza kupata watalii wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, *alternative* ya utalii hapa nchini ukiacha Kisiwa cha Zanzibar ni Kisiwa cha Mafia Mkoani Pwani, Kisiwa cha Mafia *Mashallah* Mwenyezi Mungu amekijalia kina *beach* ama fukwe nzuri sana, lakini pia kuna samaki yule wa ajabu mwenye madoido anaitwa *whale shark* ama papa potwe ambaye wazungu wanampenda sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna *sport fishing*, nikisema nielezee vivutio vilivyopo katika kisiwa chetu cha Mafia nitapoteza ama nitachukua muda mwingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, isipokuwa kwa masikitiko makubwa kabisa *as we are speaking here over 90 percent* ya ardhi ya Kisiwa cha Mafia hakijapimwa. Leo tunazungumzia suala la uwekezaji, tunazungumzia suala la biashara; ni mfanyabiashara gani, ni mwekezaji gani atakuja kuwekeza kwenye ardhi ambayo haijapimwa. Tunajua wazi hakuna mwekezaji wa namna hiyo, wenzetu wanavyotaka kuwekeza wanahitaji wawe na *title*, sasa kama hatuna *title*, kama eneo hatujapima tusifikiri kama tunaweza kupata hao wawekezaji.

Kwa hiyo, mimi nataka niwaombe sana Serikali hususani Wizara ya Ardhi iangalie namna ya kupima maeneo haya mahususi kama vile Kisiwa cha Mafia ili tuweze kukifungua kwa upande wa utalii. Hakuna biashara ya utalii isiyoendana na hoteli, migahawa pamoja na fukwe nzuri za *beach*. Sasa kama hatujapima ardhi yetu itakuwa tunapoteza wakati na ndiyo maana nikasema ni vema Wizara hizi zikazungumza lugha moja ili tuweze kuufungua utalii pamoja kisiwa chetu cha Mafia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukizungumza habari ama biashara ya utalii mimi nitaomba Serikali ikija inieleze mipango na mkakati wa kuhakikisha inakipanua kiwanja cha ndege cha Mafia. Kiwanja cha ndege cha Mafia ni kidogo chenye *runway* ya mita 800 kimsingi ndege kubwa haziwezi kutua pale na tunafahamu watalii wanapotoka eneo la utalii wanataka waende *straight* kwenye *destination* na wakitoka hapo waongoze moja kwa moja kwenda eneo wanalotaka kwenda kutalii. Wazungu hawapendi mambo ya *transit*, kwa msingi huo tunaweza tukapoteza baadhi ya watalii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nataka niombe sana Serikali ije na mipango ya kuhakikisha kwamba inapanua kiwanja hiki cha ndege, lakini pia tuweze kujenga

barabara ya lami iliyokuwa kule Mafia ya Ras Mkumbi kilometa 55. Mtalii anapoingia, ametua kwenye ndege anapoingia kwenye gari kuelekea hotelini barabarani vumbi tupu.

Kwa hiyo, lazima tujenge miundombinu yetu ili tuweze kuifungua sekta hii ya utalii. Lakini kisiwa cha Mafia kina visiwa vidogo vidogo kama Chole, Jibondo na vinginevyo, kwa hiyo, mtalii kutoka kisiwa kimoja mpaka kwenda kisiwa kingine tunahitaji tupate vyombo vya kuwachukua kama *speed boat*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwahiyo, nitaomba sana Serikali ije na majibu ya kujibu hizi changamoto ya namna gani tunakifungua kisiwa cha Mafia kwa ajili ya kuchochea utalii. Niombe sana kwamba *Royal Tour* inaendelea, *episode* ya pili ama *season* ya pili, nataka kuomba sana ipige jicho lake kwenye kisiwa chetu cha Mafia ili na yenyewe iweze ku-*appear* kwenye hii filamu ya *Royal Tour*.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi mwisho nimalizie na ombi ama ushauri kwa Serikali. *Royal Tour* kwa ushauri wangu mimi ni vema ikakabidhiwa ama ikawa chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii na si kule Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo licha ya kwamba Serikali ni moja tunakubali, lakini ili iweze kusimama vizuri ni vema ikawa mikononi mwa Wizara ya Maliasili na Utalii na si kwenye michezo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (Makofi)

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, atafuatiwa na Mheshimiwa Phillip Mulugo, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, ajiandae.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Spika, ahsante, nikushukuru sana wewe, lakini pia tumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kibali cha pekee cha kutufanya leo tuendeleo kukutana hapa. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, cha kwanza niendeleo kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nafasi ya pekee hasa tukio la jana ambalo mimi naona limevunja rekodi kwa mara ya kwanza kuweza kukutana na Makatibu Mahsusi, ni mwanamke ambaye anajua uhitaji wa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niendeleo kumshukuru sana Waziri wa Maliasili na Utalii Dkt. Pindi Chana pamoja na dada yangu Naibu Waziri Mary Masanja na Katibu Mkuu Dkt. Francis Michael kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika nchi hii wanamsaidia ipasavyo Mheshimiwa Rais, wanaisaidia na wanaitendea haki Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye mada hasa kwenye maslahi ya hawa ndugu zetu wa maliasili, hawa Jeshi la wenzetu Jeshi la Maliasili, Jeshi la Uhifadhi Wanyamapori, hawa watu ningemuomba Mheshimiwa Waziri waangaliwe sana ni askari ambao iwe mvua ya kwao, liwe jua la kwao, wanyama wakali porini ni wa kwao, majangili ni wa kwao. Kwa hiyo, ningeuomba Serikali iwaangalie kwa mapana sana hasa suala la marupurupu na namna gani ya kuweza kukaa nao karibu, wanafanyakazi ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia kwenye taarifa kwenye ripoti ya Mheshimiwa Waziri eneo la uhifadhi lipo zaidi ya kilometa 307,800 ni zaidi ya asilimia 32 ya eneo la nchi lakini wanaolinda na kuzungukia hili eneo ni maaskari wa uhifadhi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningemuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na mambo mengine mazuri wanayoyafanya hawa watu lazima waangaliwe sana kwenye suala la marupurupu. Ninajua sana hata watakapoangaliwa suala la marupurupu hawa ni askari ambao wanalinda rasilimali za nchi. Kwa hiyo, mimi ningeuomba Mheshimiwa Waziri hili liangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri nilikuwa na suala la watu wa *TFS* sijajua hawa watu wanaochoma mkaa wanakosea wapi. Ukiona mwananchi amepakia gunia lake la mkaa

anasafirisha kwenda kuuza, ukifuatilia wakati mwingine, aidha, ana mgonjwa au mke wake anaumwa au kafanyiwa *operation* hospitalini. Anataka akatafute fedha ya dharura aidha ya kwenda kulipia matitabu au kwenda kumkomboa mke wake hospitalini aweze kurudi nyumbani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ningeomba anakutana na wenzetu hawa maaskari ambao ni watanzania wenzetu anakamatwa ananyang'anywa hata baiskeli ananyang'anywa hata gunia lake la mkaa na ametembea labda kilometa 20, anarudi kwa mguu. Ningeomba wizara iangalie utaratibu rafiki wa kuweza kuwaelimisha hawa watu, wawaelimishe hawa watu namna nzuri ya kuvuna mkaa wao. Wakati mwingine hata hajakata mti, amechimba mizizi kule kwenye shamba lake, akaikausha vizuri ili angalau aweze kuhudumia. Aidha, ameondoka kabisa nyumbani, ameacha hakuna hata unga hamna hata chakula angalau akauze gunia lake la mkaa au debe lake la mkaa aweze kurudi na unga, aweze kurudi angalau na mahindi kwa ajili ya kuhudumia watoto wake lakini madhara yake anakumbana na hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba tuwabadilishe wenzetu askari hasa *TFS* wawe angalau na muda wa kuwapa elimu hawa watu tusiendeele ku-*copy* toka zamani, mimi nikiangalia hata asilimia kubwa ya Wabunge humu tunatumia mkaa huwezi kula tu na hata huyu aliyeenda kumkamata nyumbani kaacha gunia la mkaa, ugali aliokula umepikwa kutumia mkaa, sasa inakuwaje tena anageuka kuwa mwiba kwa wenzetu hawa. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ni kweli.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Spika, ningeomba sasa huyu mwenye gunia moja hawezi kwenda Wilayani akatafute kibali. Mfano, nikiongelea Jimbo la Ushetu kutoka kule ukapate kibali zaidi ya kilometa 40 aende akatafute kibali cha gunia moja halafu arudi kwa ajili ya kusafirisha, huku ana tatizo nyumbani, huku hana chakula, mimi ningeomba wenzetu wa *TFS* wajikite kwenye kutoa elimu, lakini wajikite kwenye kuwafundisha hawa vijana

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

waweze kuwa na mashamba yao ya miti kwa ajili ya kwamba sasa pandeni miti yetu hapa na utaratibu unakuwa ni bora zaidi kuliko wanavyofanya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee eneo la Ushetu, tuna mgogoro ambao naona umedumu kwa muda mrefu, mgogoro wa pori letu la halmashauri, *Usungwa Forest Reserve* pamoja na Kigozi – Muyoyozi ambao toka tarehe 31 Disemba, 2019 kuna timu ilikuja kwa ajili ya kutatua huu mgogoro, lakini haikutoka na matokeo wala haikutoa jibu na mbaya zaidi haikukutana na Madiwani wala Mwenyekiti wa Halmashauri hata Mkurugenzi wa Halmashauri haikukutana naye.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha aje anisaidie ni lini tutaenda kushughulikia mgogoro wa wananchi hawa wa Ushetu ambao wanaoteseka hasa wananchi waliopo katika Kata ya Nyankende, Kata ya Ulewe, Kata ya Idahina, Kata ya Ulowa, Kata ya Ubagwe na Kata ya Sabasabini ni maeneo ambayo wananchi wake wanateseka na mgogoro huu ambao umedumu kwa muda mrefu. Niombe sana ndugu zangu waziri kwa sababu uwezo wako wa kazi ni mkubwa, tuje tukashughulikie huu mgogoro ili tuondoe kati ya *Usungwa Forest Reserve* ambayo ilikuwa ni bonde la Halmashauri ya Ushetu lenye *GN number 442* ya mwaka 1959 lakini kwenye mgao wa mwaka 2020 wakati Kigozi inapanda kuwa *TANAPA* ukaingizwa huko sasa ni mgogoro ambao unawatesa sana wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningekuomba Mheshimiwa Waziri kwasababu uwezo wako wa kazi ni mzuri na Naibu Waziri na Katibu Mkuu mje sasa mtuambie ni lini tutaambatana pamoja kwenda kukaa na wananchi na wazee wa eneo hili maeneo yote haya ambao ni wazaliwa wa eneo hili ili tuone namna gani tunatatua. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Sawa.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa nashauri ndugu zangu wa maliasili, tunajua

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

tunachangamoto nyingi, lakini kubwa sana ninawaomba Mheshimiwa Waziri fanya ziara kwenye maeneo haya ukifanya ziara kwenye maeneo haya kutana na wazee, kutana na Madiwani kwenye haya maeneo yote ya migogoro watakusaidia sana nakumbuka hata hawa mawaziri wanane ambao waliteuliwa kwa ajili ya kuzungukia kutatua hii migogoro hawajawahi kukanyaga Ushetu, hatujawahi kuona Ushetu wanakuja kututatulia hii migogoro. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba ndugu zangu mnapokuja kushughulikia hii migogoro mje na Ushetu mkutane na Madiwani na maeneo mengine mkikutana mkakaa na Madiwani, Madiwani wa maeneo husika na Wenyeviti wa Vitongoji wana mambo mengi ambayo wanaweza wakawaelezea na namna nzuri ya kuweza kusimamia sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri utakapokuja unisaidie sana ili wananchi wangu wasiendelee kuteseka na suala la mkaa tuje na utaratibu mzuri ambao tutawasaidia wananchi wetu namna nzuri ya kuboresha na namna nzuri ambayo itafanya sasa wawe wapandaji wazuri wa miti na kujenga uoto mzuri wa asili wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye nchi hii. Ninajua kila Mbunge kwenye eneo lake barabara zinajengwa, hospitali zinajengwa, kila kitu kinafanyika. Mheshimiwa Rais anafanya kazi, hata kwenye gharama ya mafuta katoa shilingi bilioni 100. Shilingi bilioni 100 ukiziweka humu tunaweza tukakosa hata mahali pa kukanyaga. Mama anaupiga mwingi, kwa kweli tumshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Phillipo Mulugo atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete. Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ajiandae.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara hii ya Maliasili. Nina vipengele vitatu, pongezi, malalamiko na hatimaye ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa heshima kubwa kabla sijaanza kuchangia naomba niamini kwamba mimi ni Mkristo, ni-*quote* kifungu cha Biblia, Kitabu cha Mwanzo, mstari wa 24 hadi wa 30 kinasema hivi na naomba Maliasili mnisikilize; "Mungu akasema, nchi na ijae kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa kufugwa, nacho kitaambacho na wanyama wa mwituni kwa jinsi zake, ikawa hivyo. Mungu akamfanya mnyama wa mwitu kwa jinsi zake na mnyama wa kufugwa kwa jinsi zake na kila kitu kitaambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake, Mungu akaona kuwa ni vyema. Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wake, kwa sura yake, wakatawale samaki...", naomba mnielewe, huyo mtu aliyembwa huyo, akatawale samaki wa baharini, ndege wa angani na wanyama wote wa nchi yote pia na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi, huyo mwanadamu akavitawale. (*Makofi*)

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba mwanamume na mwanamke. Mungu akawabariki wote, akawaambia zaeni mkaongezeke, mkaijaze nchi na kuitiisha, mkawatawale samaki wa baharini, mkawatawale ndege wa angani na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi mkakitawale." (*Makofi*)

"Mungu akasema tazama nimewapa kila mche utoao mbegu anampa binadamu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia na kila mti ambao matunda yake yana mbegu vitakuwa ndivyo chakula chenu. Mungu akasema na chakula cha kila mnyama wa nchi na kila ndege wa angani na cha kila kitu kitambaacho juu yake chenye uhai, majani ya miche yote ndiyo chakula chenu ikawa hivyo. Mungu akaona kila

kitu ni chema alichokifanya, ikawa asubuhi, ikawa usiku, siku ya sita." (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimeyasema haya nikiwa na maana kwamba yawezekana miaka hii ambayo nimekaa Bungeni huu mwaka wa kumi na mbili sijawahi kuona kabisa Wizara ya Maliasili na Utalii ikileta sheria za kubadilisha kwa haya mambo tunayoyasema, kwa sababu kila siku ni manung'uniko ya Wabunge. Wenyeviti wa Vijiji wanalalamika, watu wanauliwa na mamba na tembo na simba, lakini *no reaction* na fidia yenyewe ni ndogo sana, hakuna hata sheria yakuja kubadilisha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye fidia hapa, nilikuwa naandika hapa, mtu aliyejeruhiwa na tembo analipwa shilingi 200,000 majeruhi wa kawaida, lakini aliyejeruhiwa jeraha la kudumu yaani maana yake amekatwa mkono, amekatwa mguu yaani hajafa analipwa shilingi 500,000 maskini ya Mungu; toka mwaka 1980 sheria haijabadilika. Mtu aliyekufa anapewa shilingi milioni moja basi na inawezekana wengine hata wazazi walishafariki hata hii milioni moja hatujawahi kuona.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maghembe amesema hajawahi kunipa, Mheshimiwa Kigangwalla amesema hajawahi kunipa, huyu Bwana Ndumbaro hajawahi kunipa, Mheshimiwa Pindi Chana naye miezi mingapi sijui kama atanipa. Lakini ninachotaka kusema ni nini? Wizara ya Maliasili tufumue sheria zote. Wizara ya Maliasili tutawaonea bure hata wale maafisa kwa sababu ni sheria zimekuwa za hovy hovy. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, miaka ya 1980 wakati sheria zinaundwa hizi za maliasili, vijiji sasa hivi vimepanuka. Ukienda pale Mkwajuni makao makuu ya Wilaya ya Songwe kilikuwa ni kijiji na vitongoji viwili, leo ndiyo makao makuu ya Wilaya na ndiyo mji mkubwa wa Mkwajuni. Ukitembea mita 500 wanakwambia hii ni *TFS*, ukitembea upande mwingine mita 200 huwezi kukusanya kuni, huwezi kuvuna mkaa yaani ni shida tupu. (Makofi)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Mkwajuni, mdogo wangu Shaibati anafanya kazi nzuri pale, haki ya Mungu tena bila yeye sijui mimi ingekuwaje, kwa sababu anaunganisha watu, wanakwenda wanaomba hata *TFS* angalau wakatiwe kaeneo kadogo wanatafuta kuni, lakini imeshindikana. Nao *TFS* wanakuja na sheria.

Sasa jamani ndio maana nimesoma hata neno la Mungu hapo; Mungu amemuumba binadamu akaitawale dunia, akaitawale na nchi na vitu vyote vilivyoubwa tuvitatwale sisi. Leo hii eneo la mapori tengefu Tanzania nzima yako maeneo 26. (*Makofi*)

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Mulugo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, nani huyo tena?

T A A R I F A

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, kataarifa kadogo tu kwa ajili ya kizuri unachozungumza Mheshimiwa Mbunge. Hata Nusu Maili iliyokuwa imewekwa kwenye hifadhi ya Mlima Kilimanjaro na mkoloni toka mwaka 1923 hawa wameiua. (*Makofi*)

SPIKA: Haya Mheshimiwa Mulugo unaipokea taarifa hiyo?

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, lakini Wabunge hebu mniache niongee vitu vya maana, leo nalihutubia Taifa hapa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe hii elimu, nimesema eneo la mapori tengefu Tanzania idadi ni maeneo 26 yanatawaliwa na *TAWA*; Mapori ya Akiba Tanzania yako 27

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

yako chini ya TAWA; Mapori ya Hifadhi ya TANAPA ni maeneo 22; Mapori ya Hifadhi ya Misitū (TFS) yako 419. Nchi yetu ni eneo kubwa sana *square kilometer* 946,000. Lakini *square meter* 307,800 zote ni maeneo ya hifadhi, asilimia 32.5 ni maeneo ya hifadhi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa Mungu amesema nendeni mkazae, mkaongezeke, tunaongezeka kila siku. Mwaka 1970 anaosema Mheshimiwa pale mwaka 1980, mwaka 1990, 2000, 2010, 2020 vizazi na vizazi vimeongezeka. Ninaposema Mkwajuni ilikuwa ni kijiji leo ni Wilaya, sasa wananchi waende wapi? yaani kule kwetu sisi maeneo yote ya Kapalala, maeneo ya Udinde, maeneo ya Gua, maeneo ya Kanga, maeneo ya Ngwala ni shida tupu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, maana ukienda kwa wachimbaji wadogo kila wakitaka kuziona dhahabu, wameziona nina dhahabu zile pale, TFS anakuja, anasema ondokeni, wanawafukuza, wanawapiga, ni shida tupu. Hii nchi jamani ni ya kwetu sisi, Mungu alitumba tuitawale. Hata neno la Mungu linasema, zaeni mkaongezeke, tutawale. Mama wa watu anakwenda kukusanya kuni, anafukuzwa, anakwenda kukusanya mkaa anafukuzwa. Sasa wakinamama ambao hawana umeme maskini ya Mungu, hata gesi hamna kwenye vitongoji. Mheshimiwa Waziri wa Umeme juzi ananiambia kwamba vitongoji tutaanza kupeleka umeme, lakini unaweza kushangaa ikachukua hata miaka 10, ni maneno tu tunayopewa kama sera. Lakini leo wananchi wanaishije jamani? Hali ni ngumu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Wabunge, toka tumeanza kuchangia hii Wizara, mimi ni mwanakamati pale, nani ameipongeza Wizara ya Maliasili hapa? Tunapongeza *Royal Tour* tu, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kutuletea *Royal Tour*. Hakuna mtu yeyote anayeweza kusema kwamba labda hongereni, TAWA mmefanya hivi, TANAPA mmefanya hivi, TFS mmefanya hivi. Bila *Royal Tour* hapa hii Wizara haiwezi hata kupongezwa, ni hatari, ni malalamiko tu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa kila siku Wabunge wanalalamika, sasa kwa nini Serikali isichukue hatua? Ni kweli wale wanatumia sheria, sasa sheria ni sisi Wabunge tuzibadilishe, hali ni mbaya sana huko, maeneo ni yetu sisi wenyewe. Ukienda kuvuna mbaao hupati kibali. Juzi Mkuu wa Mkoa kule kwetu ameenda kule Kapalala, ameenda kule Buha, maana yake sasa hivi wananchi wa Kapalala hawawezi kulima. Mheshimiwa Bashe ametupa mpaka na zile mbegu za korosho, hawawezi kulima kwa sababu hakuna maeneo ya kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Mkwajuni Mji umetapakaa, umeenea, huku wanaweka sekondari za kata, huku sijui wanajenga majengo ya Serikali, wanaingia kwenye hifadhi, jamani hii hali tuibadilishe. Ukienda kwenye tembo huko ndiyo nisiseme, Kata ya Buha, Kata ya Kapalala, tembo wanaua watu, tembo wanakanyaga watu, mazao ya wananchi, hapa nina *list* ya majina karibuni 84 ningeweza kuyasoma, nitakuandikia, nitakuletea. Watu 84 mazao hakuna na mwaka huu kuna njaa sana. Tembo ni nani? Tembo ni nani mpaka atuzidi sisi wakati Mungu ametupa kibali cha kuwatawala hawa wanyama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mungu ametupa kibali cha kutawala wanyama. Tutawale na wanyama na kwenye maji kule. Ndugu zangu...

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Mulugo umesema unalihutubia Taifa, lakini tuongozane vizuri hapa. Umetaja hapo watu 84, umeanza kwa kusema watu wanauawa, watu wanakanyagwa na tembo, mazao. Sijajua hao 84 wako kundi gani? Maana unasema na wewe una majina hapo.

Waheshimiwa Wabunge, lazima ukisema jambo humu ndani tuwe na uhakika nalo. Kwa hiyo, tutarejea kule kwa Mheshimiwa Waitara. Hebu tuweke vizuri kwenye hao watu 84 hapo.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, ukiona mtu kama Mulugo anasema haya Bungeni nina ushahidi. Hii

taarifa nimetoa kwenye Halmashauri ya Wilaya yangu ya Songwe kwamba kuna watu hapa wamekufa kwa mamba ni wengi. Nimekusanya taarifa za miaka mitano iliyopita. Nimekusanya taarifa za miaka mitano za watu walioharibiwa na tembo mazao yao. Kwa hiyo, kama ni hivyo nitakupa, wako watu 84 wameathirika na mamba pamoja na tembo. Kwa hiyo, ni kitu ambacho nina uhakika. (*Makofi*)

SPIKA: Sawa. Ngoja, ngoja twende vizuri, twende vizuri.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

SPIKA: Kwa sababu unao huo ushahidi na unasema Halmashauri yako ndiyo iliyoleta hizo taarifa.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, yes. Ndio, ndio.

SPIKA: Na wewe hizo taarifa Jumanne nitaomba nizipate.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, nitakuletea, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine ni masuala ya mipaka, hizi GN za hawa watu wa hifadhi, Maliasili. Kijiji cha Ngwala na Kijiji cha Buha hali ni mbaya, wakati Mheshimiwa Waziri anachangia hapa, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi namheshimu sana, alisimama akasema Tume ilikuja. Nasema kwa ushahidi nilionao, Tume ya Mawaziri haijawahi kufika Songwe kwenye vijiji vyangu vya migogoro. Mimi ndiyo Mbunge kule na kila nikifika wanasema hawajawahi kuona, hawajawahi kufika Ngwala, hawajawahi kufika Kapalala, hawajawahi kufika Udinde, hawajawahi kufika Mkwajuni, hawajawahi kufika Patamela, hawajawahi kufika Saza, hawajawahi kufika Ngwala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapana tusidangaye hapa, kama walienda maeneo mengine lakini siyo maeneo yetu wengine,

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ni migogoro mitupu. Jamani alisema Mheshimiwa Silaa siku ile pale, tunakwenda kwenye uchaguzi 2025, tupeni raha na sisi huko tukaseme vizuri kwa wananchi. Naomba taarifa ambazo Wabunge tunatoa ndani ya Bunge humu tunakuwa tumezikusanya kwenye vijiji, kwenye kata, kutoka kwa Madiwani, zinakuwa ni taarifa rasmi. Naomba Serikali itusikilize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda maeneo kama ya Guha pale, sasa watu walime nini sasa?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Sekunde 30, muda wako umeisha. Sekunde 30 malizia.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo inasema tulime, lakini Wizara ya Maliasili tuvune mbao, tuvune na mkaa, maeneo hakuna.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba, ombi langu la mwisho tufumue Wizara ya Maliasili yote, tubadilishe sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete atafuatiwa na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta. Mheshimiwa Riziki Lulida ajiandae.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, hatimaye niungane na wachangiaji wote ambao wamechangia katika Wizara ya Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee zimuendee Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya

kuipaisha nchi yetu ya Tanzania si katika Afrika bali duniani kwa ujumla wake na hasa kupitia suala zima la utalii la *Royal Tour*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, kutokana na hivyo, Mama anatambulika duniani. Hivi karibuni Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amepata tuzo ya aina yake kuhusiana na masuala mazima ya miundombinu ya barabara. Hongera sana Mama yetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan, fanya kazi Watanzania tuko nyuma yako na dunia inakuona. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, naomba niwatambue viongozi katika Wizara hii ya Maliasili na Utalii ambayo Wizara hii inaongozwa na Mheshimiwa Pindi Chana pamoja na Naibu Waziri wake, bila kusahau Katibu Mkuu wa Wizara hii. Wamewasilisha taarifa yao vizuri na taarifa ina mambo mengi na ndio maana tumepata fursa ya kuchangia Wizara hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kwenye Wizara hii wameeleza mafanikio yaliyopatikana na mafanikio haya ni kupunguza kwa ujangili kwa asilimia 90. Sasa mimi nataka nianzie hapo katika kupunguza ujangili kwa asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, kweli nakubaliana nao, ujangili umepungua kwa asilimia 90; kupungua kwa ujangili kwa asilimia 90 ndiyo kumeweza kuleta madhara. Tembo wameongezeka, tena wameongezeka kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa tembo hawa kumeleta madhara makubwa katika nchi yetu. Na hili ninalizungumza kila mtu hapa ambaye kwenye eneo lake anapitiwa na tembo. Unakuta tembo hao kama hawajaua watu, tembo hao kama hawajakanyaga mazao, kama hawajavunja nyumba, tembo hao kama hawajaharibu miundombinu ya barabara, si tembo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachotaka hawa tembo watengenezewe mazingira ya kimkakati, tunajua tembo wanamanufaa, tembo anasaidia watalii wanapoingia kutafuta tembo alipo, pesa za kigeni zinaingia,

lakini pamoja na kuingia pesa za kigeni madhara tunayoyapata kama wananchi ni makubwa. Akikanyaga mazao watu watapewa fidia, *either* ya chakula na vitu vingine. Chakula kitatolewa, lakini mtu huyu anapouawa *compensation* yake ni kitu gani, uhai hakuna kitu kingine? Kwa hiyo, hili ni lazima tuliangalie kwa umakini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nizungumzie tu kwenye Jimbo langu la Mchinga. Jimbo la Mchinga hili lina shida kubwa sana sana ya tembo, tembo ni wengi. Kila kukicha unapata adha ya tembo. Ukienda Kata ya Kiwawa tembo ndiko wanakolala, ukienda Kata ya Milola usiseme, ukienda Rukanda tembo wamejaa, ukienda Nangaru kutwa watu wanahangaika na tembo. Lakini tembo hawa tunaambiwa watu walime mazao ya chakula na biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa kama tembo huyu akija kwenye eneo kazi yake kubwa ni kutingisha *either* mikorosho au minazi, mtu ataweza kulima? Na tembo anatingisha mnazi, nazi zikianguka kazi yake huyu tembo kula hizo nazi, anakula nazi. Kwa hiyo, matokeo yake hakuna mashamba hata kwenye mazingira yale ambayo wanalima mazao ya kawaida ya bustani, akija kwenye shamba bustani ya tikitimaji, matikitimaji yale yote yanaliwa hakuna hata moja linalobaki. Hao ndiyo nani hao, ndiyo tembo hao. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, upande ule wa kwetu kule kuna njaa kwa ajili ya hawa wanyama tembo hawa. Tembo si rafiki, tena ilifikia hatua tulipokwenda kule mchinga wanasema sasa tuambieni sisi binadamu na tembo nyie mnamtaka nani? Basi kama mnamtaka tembo nendeni kachagueni tembo sisi hatutaki. Wananchi wanafikia kusema hivyo tuchague tembo... (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa hebu weka hicho kisemea chako vizuri.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, yaani watu wamechoka na tembo, ikafikia hatua mama unatuambiaje au tuwauwe hawa tembo? Nikawaambia hapana hiyo sio sheria msiwauwe hawa tembo waacheni sheria zinatekelezwa, sasa kwa muhktadha huo tuliomba na Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Milola tukafanya mkutano, kuangalia hali halisi ya tembo na akakuta kuna mtu ameuwawa na Mheshimiwa Naibu Waziri akaenda kumpa pole, nilikuwa naye mimi mwenyewe na baada ya hapa wakasema watatoa kifuta machozi mpaka leo kifuta machozi hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wale wanadai kifuta machozi, kwa hiyo hali ya tembo sio nzuri kwa sababu watu wengi wamezungumza kuhusu tembo nafikiri nimeeleweka lakini kubwa tuna hitaji kituo cha askari wa wanyamapori, lakini wakasema tutawapa kituo hivi unatupaje kituo, polisi wawili na tembo wako 30 hivi polisi huyo wataweza! *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, hawawezi.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, polisi hawezi matokeo yake kituo hakijajengwa, polisi wawili, polisi hawana usafiri hawana chochote, hata pikipiki hawana. Sasa tunafanyaje?

Mheshimiwa Waziri ukija hapa unihakikishie kwamba kile kituo tutajenga na polisi mtatupa na polisi wenye silaha, sasa hivi ukienda Jimbo la Mchinga mengine haya hayazungumzwi yanazungumzwa masuala ya tembo, niishie hapo kwenye tembo.

Mheshimiwa Spika, tunakuja kwenye eneo la utalii; eneo la utalii kuna sehemu inaitwa Tendaguru, Tendaguru ndio sehemu ambako ametoka huyu mjusi mkizungumzia mjusi anafikiria kama kimo chake kama mimi, mjusi huyu ni zaidi ya hili jengo mara mbili, huyo *Dinosaur* asili yake ni Lindi kwenye Manispaa ya Lindi kwenye Jimbo la Mchinga eneo linaloitwa Tandagulu na Tandagulu hii iko katika Kata ya Mipingo. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali leo hii wameanza kujenga *information center*, watu wakitoka watakuja pale kupata habari kwenda huko Tendaguru, lakini Tendaguru huko wanafikaje? Barabara ni mbovu mbovu ajabu, sasa wakati *information center* inajengwa tunaomba na barabara ile ijengwe. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja pale, Mnyangara daraja lile linakaribia kwisha, kwa hiyo, daraja likiisha na ile barabara ya kuelekea kwenye eneo ambako huyu mjuji amezaliwa watalii wanataka wajue Ujerumani ndiko aliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa watu wakitoka Ujerumani wajue wapi ametoka kila mtu ana asili yake na ndio maana watu duniani wanatafuta vinasaba, kinasaba cha yule ni kule.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo yote niwashukuru wale ambao wametupa ardhi, kuna akina mama na akina baba wametoa ardhi heka nane.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Jonas Van Zeeland ajiandae.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mezani. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi, lakini nawashukuru wananchi wa Urambo pamoja na familia yangu kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Pindi Chana, Naibu wake Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na watendaji wote walioko katika Wizara hii kwa kweli kazi yao ni kubwa cha maana ni kwamba tuwape mawazo mengi na jinsi ambavyo wanaweza kuhakikisha kwamba kazi inaendelea vizuri zaidi ya kile kinachondelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza mama yetu Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anajitahidi kupata njia mbalimbali za kuongezea mapato ikiwa ni pamoja na *Royal Tour*. Mimi nina kata nne ambazo zinaingia ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugara, Urambo. Niishukuru Serikali kwa kutupa hifadhi hiyo walivyopitisha kama azimio tulishukuru, lakini yako mambo ambayo pamoja na shukrani inabidi yafanyiwe kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tulipoambiwa kwamba tumepata hifadhi pamoja na kushukuru mimi nilikwenda kuonana na Kamati inayohusika nikawaambia kwamba panapotokea kitu kikubwa kama hiki watu wamepata hifadhi kwa mara ya kwanza, ni vizuri ingekuwa inatolewa elimu kukutana na wananchi wanaohusika, kuwaambia hifadhi maana yake nini, wajibu wao kama wananchi, wajibu wa Serikali ili wajue kwamba kweli hiki tumekipata lakini utaratibu wake wa kushughulika nacho ni moja, mbili, tatu, nne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikwenda kuwaomba Kamati husika kwamba waongee na Wizara ili waje waongee na wananchi wanaopakana na hifadhi ikiwemo ni kata nne zifuatazo; kuna Nsenda, Ukondamoyo, Ugara na Uyumbu; na kulikuwa na umuhimu wa kukutana na watu hawa kwa sababu katika mwaka 2013/2014 wananchi hawa walilima mazao yao, wakaruhusiwa kwamba mkivuna msirudie tena, lakini kabla hawajavuna yakachomwa moto mazao yao, kwa hiyo ikaleta uhasama kati ya Serikali na wananchi kwa sababu waliwachomea mazao yao wakati waliwaahidi kwamba hawatayachoma mpaka wamalize kuvuna ila wasirudie tena.

Mheshimiwa Spika, na ndio maana nikaona kwamba kumbe kitu kikubwa sana ni ilikuwa ni elimu na kukutana na wananchi ili kuweka mahusiano yawe mazuri, na wao wananchi wa kata hizo nne walikuwa na sababu zao wanasema wakati wa kuunda vijiji mipaka ilikuwepo, lakini maliasili ilipokuja kuweka mipaka yake ikawarudisha nyuma wakati kama walivyoongea wenzangu watu wanaongezeka

idadi na wao wale wazee tulikwenda nao Mheshimiwa Hasunga alikuja kama Naibu Waziri, Mheshimiwa Ramo Makani alikuja kama Naibu Waziri, Mheshimiwa Mabula kama Naibu Waziri wa Ardhi kuja kuona mgogoro na tuliandika barua rasmi kwamba wao wanaona kwamba eneo lao la asili wamesogezwa nyuma, kwa hiyo, wana uhaba ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ndio nikaona kwa kweli kulikuwa na haja ya kukaa nao kuwekana sawa kabla haijawa hifadhi, lakini bado tunashukuru hifadhi imepatikana, lakini kuna haja ya kufanya yafuatayo; na huu mgogoro unajulikana tulileta hapa rasmi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi langu mimi kwa niaba ya hizo kata nne ni kama ifuatavyo; la kwanza pamoja na shukrani ya kupata hifadhi bado wakakae na wananchi waongee nao waone jinsi ambavyo watashirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, la pili na ambalo pia nimeongea Mheshimiwa Rais alipokuja Tabora nimeliongelea kwamba pamoja na kushukuru kupata hifadhi wananchi kwa sababu wameongeza tunaomba eneo tupate angalau kilometa 5.5 hata ikiwezekana Serikali itupe kilometa 6 ili wananchi waliozoea kufunga nyuki na njia mojawapo ya kupatia mapato waweze kuweka mizinga yao.

Kwa hiyo, bado narudia kuomba tena ndani ya Bunge hili tukufu kwamba Serikali ione umuhimu wa kuwarudishia angalau kilometa tano au sita waweze kupata mahali pa kuweka mizinga yao na kuvuna asali na pia mifugo yao iweze kupata eneo, hilo ni ombi la pili.

Mheshimiwa Spika, ombi la tatu; sasa hivi awaruhusiwi kuingia kwenye Hifadhi yetu ya Taifa kwa sababu wanasema hawawezi kwenda kuvuna asali yao, asali inavunwa kuanzia mwezi huu wa sita na mwezi wa saba, naiomba Wizara iwaruhusu watu wanaofuga nyuki waende wakavune asali zao tayari sasa hivi mwezi wa sita na mwezi wa saba. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, lakini pia sisi kama Urambo tuna asali yetu ina kaweusi hivi, sasa tulivyoipata nyingi tukatafuta wamarekani wanaitwa *Follow the Honey* wakaja kuomba wakasema ile asali yetu sisi inafaa sana kutengeneza *chocolate*, kwa hiyo tukaandika barua rasmi Wizara ya Maliasili na Utalii kuomba mashine na tukawaonesha eneo ambalo tumeliandaa kwa ajili ya kukusanya asali. Nawashukuru Wizara walimtuma mwakilishi wao mkurugenzi akaja akaahidi kwamba Urambo tutapata mashine ya kuchenjuwa asali na sisi Urambo tupeleke asali Amerika na kwingineko wakatengeneza *chocolate*, lakini mpaka sasa hivi hatujapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi naamini kama Wizara ilituma Mkurugenzi tunaomba ile ahadi iendelee kwa sababu Serikali yetu ni sikivu watupe mashine ya kuchanjua asali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na la mwisho, kengele?

MBUGE FULANI: Mheshimiwa Spika, bado.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ya kwanza.

Kwa hiyo tunategemea kupata mashine kwa sababu ahadi ni deni tunaiomba Serikali ituletee mashine na sisi tuchenjeu asali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na lingine ni suala la Serikali kama kuna tatizo mimi ningeomba liwe linaisha, fikiria sisi tangu mwaka 2014 Mawaziri wote wamekuja hao akina Hasunga, wamekuja akina Makani, wamekuja mama Mabula suala linaendelea. Mimi ningeomba Serikali kama kuna changamoto imetokea ifuatiliwe iishe, kuliko wazo moja tatizo linaendelea miaka na miaka mimi naona sio kitu kizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wameongelea sana kuhusu tembo na mimi pia kuna tembo kwangu tarehe 21

mei, Mzee Damian Lukaka, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi ameuawa na tembo katika Kata ya Ukondamoyo Kijiji cha Kamalenge na mimi mwenyewe nikapeleka pole. Naomba kweli suala la tembo liangaliwe kwa njia nzuri, kweli tunahitaji tembo, lakini pia tunahitaji usalama wa wananchi wetu kwa hiyo naomba suala la tembo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba tu nirudie kwa mara ya mwisho kabla kengele ya mwisho haijaliala, kwanza tupate elimu, tushirikishe wananchi; pili tunaomba tutengewe eneo; tatu tunaomba wafuga nyuki waruhusiwe kwenda kuvuna asali yao; na nne kama nilivyosema mashine ya kuchenjua asali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Lulida atafuatiwa na Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo ajiandae.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia sisi wote kuwa na afya njema kuwepo hapa. Mimi ni balozi wa utalii, lakini mimi ni Mwenyekiti wa *Caucus* ya Bunge ya kusimamia ulinzi wa wanyamapori akiwemo tembo na wanyama wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile mimi ni mama mjusi, nalizungumzia suala la mjusi kwa miaka, lakini leo nitazungumzia sana suala la Selous. Nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana aliyofanya ya kuitangaza Tanzania ulimwenguni kote kwa kupitia *Royal Tour* na nilizungumza miaka nyuma Tanzania inahitaji kutangazwa na utangazaji wake wa namna hii, tunahitaji kutangaza katika mitandao mbalimbali ikiwemo hii aliyofanya kwenda Marekani kuitangaza *Royal Tour* na kwa kweli dunia kwa ujumla wake umemtambua kama Tanzania ina vivutio vingi. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina vivutio vingi na hasa ukiangalia katika kanda, kuna kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kule tunakwenda Katavi kuna Rukwa Lukwati hili ni eneo la wanyamapori ambao wanatokea Zambia kila mwaka wakija Tanzania wakifika mpaka katika mbuga za Katavi na kuendelea sehemu mbalimbali iwe Gombe na baadhi ya *game reserve*. Ni hasa *Selous corridor* hii *corridor* ni maalum Mwenyezi Mungu aliumba ile *corridor* na *corridor* ile ni kwa ajili ya tembo, nyati, simba, mbwamwitu wale wanatoka katika hifadhi ya Nyasa wanavuka Mto Ruvuma kwa makundi kama ile ile kwa Serengeti Masai Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania tukubali tunahitaji uchumi, tunahitaji maendeleo, lakini tunahitaji wananchi wetu. Hawa wananchi wengine wasijiingize katika migogoro ya wanyamapori, mimi mwaka 2014 nilipewa nafasi ya kuzunguka na Wabunge na ndio maana nasema elimu kwa Wabunge inabidi iletwe hapa ndani watambue haki za wanyamapori na haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro ambayo inaitwa *wildlife and human being conflict*, tukifanya hivyo wanadamu wataacha kuziharibu njia za wanyamapori, ukitoka Nyasa unataka kuingia Namtumbo, binadamu wame- *intervein* njia za tembo, tembo anashindwa pakupita anaingia katika mashamba ya watu, hivyo anashindwa kuingia Selous mle ndani ya Selous binadamu amejigiza mle ndani anafanya uwindaji haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nilipewa *fund* na *GIZ* kuzunguka na waandishi wa habari, tumevumbua mambo mengi sana ya binadamu. Nilikuwa na mama Mary Masanja tukaenda Tendaguru wamevamia wafugaji wako ndani ya Tendaguru wanyama wote wanakimbia na wanapokimbia hawana mahali pa kwenda wanakwenda kwa binadamu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Mama Masanja ni shahidi, sasa akatoa tamko kuwa atakapokwenda tena wale watu watakuwa wameondoka wote na alitoa taarifa kwa Mkuu

wa Wilaya wavamizi wote waliovamia katika eneo la Tendaguru waondolee nataka nipate majibu akitoka hapa je maagizo yale yametokeleza?

Mheshimiwa Spika, leo unamkuta tembo anataka kutulia Tendaguru tena msitu mkubwa sana, lakini binadamu mle amekaa analima katika hifadhi ambayo imeshatunzwa iko chini ya *TFS* sasa unasema migogoro mingine ni binadamu anasababisha migogoro hiyo kwa ajili ya kupitia njia ya wanyamapori. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitaizungumzia Selous ambayo ni mbuga ya kwanza katika Afrika, lakini ni mbunga ya pili duniani kwa ukubwa, na Selous inazunguka katika mikoa sita Mkoa wa kwanza naanza Morogoro, Iringa, Ruvuma, Pwani Lindi na Mtwara katika hiyo mbunga ndio inazunguka humo ndani kuna wanyama wa kutisha, lakini sasa nenda ndani ya Selous utaona ni vurugu tupu binadamu anavamia anachimba humo ndani, lakini maendeleo yote hayapeleki Selous, maendeleo yanapeleki Kaskazini tu.

Mheshimiwa Spika, sasa tujiulize kama huko hamkuangalii mtategemea migogoro haitakwisha? Nimesikiliza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri humo ndani kote wamepanga *fund* lakini siioni *fund* ambayo itakweda Selous haipo, lakini jiulize kama mbuga kubwa kama hii inaachwa tunategemea kuna maendeleo makubwa ya kimkakati? Mikoa hii kwa mfano Mkoa wa Lindi, Ruvuma na Mtwara tuna mradi mkubwa wa *LNG* unakwenda katika miaka mitano kama mkipanga watalii na watu mbalimbali watakaotembelea Selous tulitegemea.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, tulitegemea itakuwa na miundombinu, lakini kama hamjatengeza miundombinu msitegemee mafanikio katika Selous.

SPIKA: Mheshimiwa Riziki Lulida kutoka kwa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

T A A R I F A

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi, nataka nimpe taarifa mama yangu anayechangia, kuna fedha zilitoka kwa ajili...

SPIKA: Ngoja, ngoja anaitwa Mheshimiwa Riziki Lulida.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, sawa Mama Lulida.

SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, nilitaka nimuongozee taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Kuchauka anaitwa Mheshimiwa Riziki Lulida.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Riziki Lulida. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa mchangiaji kwamba anavyosema ni sahihi kabisa kwamba kuna fedha zilitoka kwa ajili ya utalii Kusini zile fedha ziliishia Mikumi. Kwa hiyo kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Maliasili wao Kusini maana yao ni Mikumi na Iringa sio Lindi na Mtwara. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hizi taarifa hizi tunazosisema humu ndani hizi tuwe makini kidogo. Mheshimiwa Riziki Lulida.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, taarifa naipokea hizo fedha zilitolewa na *World Bank* kwa ajili ya maendeleo ya kutengeneza barabara katika maeneo mbalimbali katika mbuga zetu, lakini nililizungumza mwaka juzi kuwa Lindi na Mtwara hela zile hazikupelekwa hasa kwa Selous na hii naizungumzia kwa vile Jimbo la Liwale ndio tunategemea kupata barabara na kuna viwanja vya ndege, lakini hazikupangiwa bajeti hata kidogo katika maeneo hayo.

Hivyo matokeo yake mtalii anavyotaka kwenda kuwinda Liwale inamuia vigumu sana kwa vile hakuna njia ya kupita kumfikisha Liwale na wala barabara ya kutoka Dar es Salaam au kutoka Nangulukuru kwenda Liwale inapitika kwa msimu, hivyo taarifa yake naipokea.

Mheshimiwa Spika, tunataka kuisaidia Serikali katika kuendeleza utalii ni lazima tuunganishe na *private sector* na hii itatusaidia katika maendeleo. Nataka nitoe mfano wa *private sector* ilivyosaidia sekta ya utalii, *Bakhresa Group of Companies* ameleta meli ambazo zinakwenda Zanzibar, amefungua mahoteli makubwa Zanzibar, matokeo yake ameliletea urahisi Zanzibar kwa ajili ya watalii kwa vile watapata mahali pa kukaa, usafiri wa uhakikia kwa kutumia boti mbalimbali za Zanzibar, tulitamani sisi mkishirikisha *private sector* katika masulala ya maendeleo ya utalii nina imani Visiwa vya Mafia nao wataibuka katika utalii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimeona mapato ya utalii yameingia kwa asilimia tano tu, lakini kama mtafungua maeneo mbalimbali kwa mfano Kanda ya Ziwa, mkaifungulia mawasiliano makubwa kati ya Burundi, Rwanda na maeneo ya Burigi tutapata utalii mkubwa mpaka Kigoma. Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Zambia - Tanzania mkifanya mashirikiano katika masuala ya utalii tutavuta katika masuala ya utalii. Lakini Mozambique - Tanzania tukiisimamia katika hilo suala tutafika mbali katika suala la maendeleo, lakini je, tuna mahoteli? Mahoteli maana yake leo tukitangaza tunategemea tupate na mahoteli ya kuwapokea wageni wetu, tunahitaji mawasiliano ya barabara na miundombinu, leo tunahitaji *fund* kubwa ili hii sekta iweze kufanya kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru watu wa *TANAPA* wanafanya kazi kubwa sana, siyo kazi ndogo kushindana na binadamu, binadamu anataka kumuwinda tembo ili amue na tembo na yeye vilevile ni mnyama mwenye akili kuliko binadamu anakuwa hakubali vilevile kuuana. Hivyo hapa ni lazima tuungane nao watu wa *TANAPA*, watu wa Ngorongoro na watu wa *TAWA* hii kazi ni kubwa binadamu anategemea

kufanya ujangili apate maslahi yake. Nina mfano hai sasa hivi ujangili umerudi tena, sasa tuseme vizuri kuwa hapa ni binadamu na wanyama wako katika mgongano. Serikali simamieni tunahitaji mapato makubwa na wananchi wapate faraja kwa kupitia sekta ya utalii. Tanzania tunategemea utalii kwa ajili ya wanyama watano; simba, tembo, nyati, chui na faru. Ivory Coast walikuwa na wanyama kama Tanzania kwa fujo za binadamu sasa hivi ni historia.

Naiomba Serikali yangu na wananchi kwa pamoja tushirikiane katika ulinzi huu, siyo ulinzi wa kuiachia peke yake Maliasili, ni jambo letu na maendeleo yetu, Mama anatangaza utalii na sisi tuwe wadau wa kusimamia utalii huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema ahsanteni sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zainab Athman Katimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mheshimiwa Amsabi Mrimi Jeremiah, ajiandae.

MHE. ZAINAB A. KATIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza na mimi nianze kwa kutanguliza pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuendelea kuaminiwa katika Wizara hii, lakini niwapongeze pia watendaji wote katika Wizara hii na niwaambie tu waendeleo kufanya kazi kwa bidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nipongeze pia jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais ambazo tumeona kwenye *Royal Tour*, tumeona Rais ameweza kuifungua Tanzania, kuitangaza, kuweza kuwavutia wawekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo utalii na haya mambo yote yanaenda kuleta tija kubwa sana katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi ningependa kwanza kuzungumzia migogoro mikubwa ambayo inatokea kati ya maeneo ya Hifadhi pamoja na Vijiji; na ukisikiliza hata katika michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia migogoro hii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kwa hiyo, pamoja na mambo mengine mimi ninadhani kwamba kuna haja ya kuangalia sheria zetu zinazungumzaje masuala haya ya changamoto au migogoro ya ardhi ambayo inatokana na hifadhi zetu pamoja na vijiji. Kwa mfano ukiangalia Sheria ya *Wildlife Conservation Act* ya mwaka 2009, kifungu cha 16(4) ambacho labda naweza nikakisoma, ambacho kinasema; *"The Minister shall, within twelve months after coming into to operation of this Act and after consultation with the relevant authorities, review the list of game controlled areas for purposes of ascertaining potentiality justifying continuation of control of any of such area."*

Halafu kifungu kidogo cha (5) ambacho ndio cha msingi hapa kinasema; *"For the purposes of subsection (4), the Minister shall ensure that no land falling under the village land is included in the game controlled areas."* (Makofi)

Sasa hapa sheria inatambua maeneo ya mapori tengefu, lakini sheria inasisitiza kwamba Waziri baada ya kuanza kwa hii sheria, baada ya kutungwa hii sheria ikianza kutumika ndani ya miezi 12, Waziri apitie orodha ya mapori haya tengefu na katika mapitio hayo ahakikishe kwamba maeneo ya vijiji hayatowekwa ndani ya mapori tengefu. Kwa hiyo, vijiji viachwe, maeneo ya vijiji yaendeleo kuwa vijiji yasiwe ndani ya orodha ya mapori tengefu. Kwa hiyo, ukisimamia sheria hii inaweza ikandoa baadhi ya hii migogoro tuliyokuwa nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini hatuishii hapo tu unajua sheria kwa mfano Sheria ya Ardhi ya Vijiji yaani *Village Land Act* inatambua kwamba kijiji kinaweza kuwa kile ambacho watu wameishi kwenye eneo hilo kwa zaidi ya miaka 12 kabla ya kuanzishwa kwa sheria hii. Kwa hiyo wamekuwa wakiishi kwa miaka kwa tamaduni zao, wameweka makazi na wameishi kwenye eneo hilo linatambulika kama kijiji. Kwa hiyo, leo hii unavyokuja kutengeneza mazingira ya kumfukuza mtu kwenye eneo ambalo ameishi tangu uhai wake unanza mpaka anafikia umri huu, unamfukuza, yeye anafahamu eneo lile ni nyumbani kwa hiyo ukimtoa kwenye eneo kama hilo kidogo inakuwa ni changamoto. Lakini mwisho wa siku

pamoja na kuwepo sheria hizi zote lengo letu pia ni kuzingatia uhifadhi, kwa sababu maliasili zote tulizokuwa nazo hapa Tanzania kuna haja ya kuhakikisha bado zinaendelea kuwepo zirithiwe, tuwarithishe vizazi na vizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri na ninafahamu haya mambo ni yanaenda kwenye Wizara tofauti tofauti, Wizara ya Ardhi inahusika na Wizara hii inahusika. Kwa hiyo, waangaalie nafahamu kuna timu ambayo inatutua hii migogoro, lakini waharakishe kwa sababu migogoro imeendelea kuwepo kwa muda mrefu sana na inaleta changamoto kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naweza kuishauri Serikali kuhusiana na migogoro hii ambayo inatokana na mwingiliano wa maeneo ya uhifadhi na maeneo ya makazi ya watu kwa maana vijiji ni kuhakikisha kwamba hivi vijiji na maeneo yake mipaka yake inakuwa inatambulika. Kwa sababu mipaka ya vijiji ikijulikana na vijiji hivi vikipimwa vizuri mimi ninaamini kwa kiwango kikubwa ule mwingiliano wa kati ya vijiji na hifadhi utapungua kwa asilimia kubwa. Kwa hiyo, naomba sana Serikali izingatie hayo kwa sababu migogoro hii haina tija kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ni kubwa sana na hili litalisisitiza sana nikiwa kama Mbunge kijana, lakini nikiwa kama mama ni uhifadhi. Wananchi inabidi waelimishwe hasa hawa wananchi wanaokuwa wanaishi kwenye vijiji vinavyopakana na maeneo haya ya hifadhi, waelimishwe umuhimu wa wa kuhifadhi maeneo haya ambayo sisi tumeyarithi kutoka kwa mababu zetu, waelewe umuhimu wa utunzaji wa maeneo haya na mchango wake na athari zake katika mazingira kwa ujumla. Kwa sababu wakifahamu na wenyewe watakuwa ni sehemu ya kuhakikisha wanayalinda maeneo haya ya Hifadhi, wanayatunza ili tuweze kuyarithisha kwa vizazi vijavyo. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kwa hiyo, naomba sana na hili suala ukiangalia kwenye ukurasa namba 114 wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kwenye kifungu cha 69(d) kimezungumzia mambo ya kuimarisha mahusiano kati ya wananchi wanaopakana na maeneo haya ya hifadhi ili kuwafanya wananchi na wenyewe waelewe kwa upana wake umuhimu wa hifadhi na waweze kulinda maeneo yetu ambayo tunayahifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kule kwetu Kigoma tuna hifadhi yetu ambayo inaitwa Gombe na Mahale. Gombe na Mahale wewe mwenyewe ni shahidi kwa sababu nafahamu umeshawahi kufika. Ulitembelea kule na Mheshimiwa Assa Makanika, Mbunge wa Jimbo. *(Makofi)*

Sasa hifadhi ile ni hifadhi ambayo wanapatikana viumbe ambao wana upekee sana, kule kuna sokwe mtu na duniani kote sokwe mtu hawa wamekuwa wana umaarufu mkubwa sana. Lakini sasa kuna uhitaji mkubwa wa kufungua njia kwa ajili ya utalii katika eneo hili.

Kwa hiyo, naomba, kwa sababu Serikali ni moja waboreshe miundombinu ya kufika katika hifadhi hii na miundombinu ya kule mikubwa zaidi ni uwanja wa ndege. Sasa kwenye bajeti ya masuala ya uchukuzi kila mwaka huwa inatengwa fedha kwa ajili ya kupanua kiwanja chetu cha ndege cha pale Kigoma, mwaka wa fedha uliopita shilingi bilioni nane, mwaka huu imetengwa shilingi bilioni saba.

Kwa hiyo, tunaomba mboreshe miundombinu kwa sababu na yenyewe itakuwa kuchochea kwenye masuala ya Utalii na kwa sababu Serikali ni moja ndiyo maana nasema hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Amsabi Mrimi Jeremiah, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, nami nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kupata nafasi hii niweze kutoa mchango wangu kwenye sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nami niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na kazi nzuri sana ambayo ameifanya ya kuutangaza utalii wetu duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba napingana na wenzangu, sisi watu wa Arusha ndiyo wanufaika wakuu wa utalii na ndiyo maana utaona leo watu wakizungumza kuhusiana na mateso ya tembo, sisi tunazungumza kuhusiana na ajira ambazo zinameongezeka kwenye mahoteli yetu, tunazungumza mapato ambayo yanapatikana kwenye nchi yetu, tunazungumza faida nyingi, tunazungumza mama ambaye analima mbogamboga anaweza akauza bidhaa zake kwenye hoteli, tunazungumza mfugaji kutoka Ngorongoro ambaye anafuga anaweza akauza maziwa kwenye mahoteli. Kwa hiyo, sisi watu wa Arusha tukiwaambia kwamba ni wanufaika wakubwa wa masuala ya utalii ni vizuri wakataelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kwenye upande wa usalama; tunauza bidhaa nyingi sana, tunauza wanyamapori, tunauza *big five* na vivutio vingine, lakini lazima tukubali kwamba *component* ya usalama ni *component* kubwa sana ndiyo maana sisi katika Jiji la Arusha kwa kushirikiana na Serikali katika ngazi ya Mkoa, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa usimamizi mzuri wa *IGP* Simon Sirro pamoja na *RPC* wa Arusha vimewezwa kujengwa vituo vya kisasa maalum kwa ajili ya kuwahudumia watalii. Tuna kituo kikubwa pale *Central*, tuna kituo pale Kikatiti kama unatoka *airport*, tuna kituo kule Engikaret kama unatoka Namanga kwa maana ya Kenya, tuna kituo Makuyuni na tuna kituo Karatu maalum kuhakikisha kwamba watalii hawasumbuliwi barabarani. Wanakuwa na kituo kimoja wanasimama, wanakaguliwa na maisha yanaendelea. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwenye hoja hii, tunawaomba wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii watusaidie kuwaunga mkono Jeshi la Polisi kwenye masuala ya usalama kwa sababu usalama ndiyo bidhaa namba moja kwenye utalii, kama hakuna usalama hakuna utalii. Wana shida ya magari kwa ajili ya *patrol*, tunataka wazungu/wageni wakija kwenye nchi yetu wanapokelewa kwa *escort* kuanzia *airport* wanapewa *red carpet*, wanakwenda kwenye mahoteli ili wakirudi wakaongee hadithi nzuri ya namna watu wa Tanzania tulivyo wakarimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tunaomba pia Wizara ya Maliasili itusaidie, wenzetu wa *TATO* hawa wa masuala ya utalii, *private sector*, wao wamejenga kile kituo kilichopo pale Arumeru, wenzetu wa *TATO* wamejenga kituo kilichopo pale *Central*, wametoa gari *brand new Land Cruiser* na Wizara ya Maliasili kwa sababu wao ndiyo wanufaika wakuu watusaidie kwa kuwaunga mkono kwa kutusaidia hayo magari kwa ajili ya polisi, lakini pia na kuboresha na kituo kilichobaki cha Makuyuni na kile kituo cha Engikaret.

Mheshimiwa Spika, pia niwashukuru wenzetu wa *CRDB* kwa sababu wameahidi kutuchangia pikipiki kumi kwa ajili ya kuimarisha usalama na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kwenye programu nzima ya *Royal Tour*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo langu la tatu; kuna leseni ya biashara kwa ajili ya *mountain guide*. Kipindi kilichopita tulizungumza kuhusiana na *tour guide*, hawa *tour operators* ambao walikuwa hawana kampuni wana gari moja moja walikuwa wanalazimika kujichomeka kwenye makampuni mengine ili wafanye biashara. Serikali ikashauriwa ipunguze tozo ili iweze kuwashawishi watu wengi zaidi kuweza kujisajili na kufanya biashara, wakaweza kupunguza ile *TAA license* gharama yake kutoka kwenye dola 2,000 hadi kufika dola 500 mpaka ninavyoongea sasa hivi wale wafanyabiashara wadogo wadogo zaidi ya 270 wameweza kujiandikisha na Serikali inaweza kuwatambua, inaweza ikapata mapato na masuala yanaendelea. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Tunaomba pia kwenye jambo kama hilo tulifanye wale *mountain guides* ambao wanatakiwa walipe dola 2,000 kila mmoja. Hebu niambie mtu leo ametoka pale Mweka kusoma au ametoka chuo chochote cha utalii anataka kuanza kazi ya kupeleka wageni mlimani, anaambiwa bila kuwa na dola 2,000 ya leseni huwezi kuanza kazi, matokeo yake sasa wanatafuta wale wenye biashara za utalii wanawapa dola 10, 10 kwa kila mgeni ili wapate vocha na waweze kupeleka watu kwenye utalii.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri Serikali ikaliangalie suala hilo, mkawapa nafasi, mkapunguza angalau kutoka mtu anayepandisha Mtalii mmoja mpaka 100 mkampa dola 500, wanaopandisha watalii 100 na kuendelea mkawapa dola 2,000 na kuendelea na mkifanya hivyo watakuwa wamewatambua wale watu wa wadogo, wameingiza kwenye mfumo rasmi, watafanya shughuli zao, lakini baadae pia itakuwa rahisi kuweza kulipa kodi pamoja na masuala mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna changamoto kwenye upande *land base rent*. Unajua kule Serengeti kuna tozo nyingi sana, kuna mtu analipa *park fee*, kuna ambao wanalipa *concession fee*, mtu akilala tu kwenye hoteli yoyote kwenye *park* kama siku kama ni *high season* dola 60, kama ni *low season* dola 50 bila *VAT*. Lakini bado hawa Maliasili wamekuja kuleta kitu kinaitwa *land base rent*. Sisi ushauri wetu kwa sababu ukileta hii tozo inaonekana kwa makadirio watapata dola milioni 3.2, ni bora wangeongeza *fee* kidogo angalau dola tano au dola 10 ili waweze kupata ile kodi na ni kodi ambayo italipwa na mgeni kutoka nje, haitalipwa na yule mwekezaji itaweza kupunguza changamoto na maisha pale yataweza kuendelea.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusiana na tozo mchanganyiko; ukienda kwenye ma-*gate* yetu, leo mtalii mfano kutoka Arusha akitaka kwenda *Lake Natron* anakutana na vijiji kama vitatu kila kijiji analipa dola 10, kingine dola 10, kingine dola 10, baadae anakwenda *TAWA* analipa dola 25. Sasa unashindwa kuelewa Serikali ni moja

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kwa nini kila mtu akusanye tozo kana kwamba Serikali hii haina usimamizi? Ni vizuri Serikali iratibu tozo zote, kama zinalipwa *TAWA* zilipwe *TAWA*, kama ni Halmashauri walipe Halmashauri, halafu wao ndani ya Serikali watagawana kidogo kidogo ili kuondoa usumbufu na siku hizi fedha zote zinaenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali sasa kuna haja gani ya kila mtu kulipa moja moja.

Mimi nilikuwa naomba Serikali yetu izungumze Lugha moja kwa maana ya TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Fedha wakae chini waje na utaratibu mmoja ili kuondoa usumbufu kwa watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pale Arusha tuna eneo linaitwa *Clock Tower*; *Clock Tower* ndiyo *centerya* Afrika kati ya Cairo kule Misri na Cape Town kule Afrika ya Kusini. Pale *Clock Tower* tunaambiwa kwa sababu ni *center* sisi tunataka tuitumie kama kivuko...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Sekunde 30 malizia sentesi.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Spika, tunataka tuitumie kama ni kivutio cha utalii. Tumeongea na Balozi wa India yuko tayari kushirikiana na Wizara ya Maliasili pamoja na Serikali ngazi ya Mkoa ili tutengeneze *tower* pale ambayo mwisho wa siku watalii wakija watafika pale, watapanda kwenye ile *tower* watalipa tozo, tutaitangaza Arusha yetu, wataangalia Mlima Meru ulioko jirani pale, mapato yatapatikana. (*Makofi*)

SPIKA: Haya, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni ambao wameingia katika kipindi chetu hiki cha pili cha kukutana leo; yupo mgeni wa Bunge ambaye ni Bi. Sharon Mo - Balozi wa Utalii Afrika Mashariki ambaye ameambatana na familia yake, karibu sana, sana. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Waheshimiwa Wabunge, nazani mmemuona Balozi amefanana na Balozi kwa hiyo mmeweza kutofautisha Balozi, hebu simama tena, eeh yule ndiyo Balozi. Watu wasije kuwa wamechanganya mambo, ahsante sana, karibu sana *(Makofi)*

Lakini pia wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao na wenyewe wameingia mchana huu, karibuni sana, tusimame wote wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao mmeingia mchana huu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 150 na walimu 12, kutoka Shule ya Sekondari Ritaliza iliyopo Rombo, Mkoani Kilimanjaro, haya karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni wetu nimelazimika kuwatangaza ili kama wanataka kuendelea na ratiba zingine wawe huru kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Amsabi Mrimi Jeremiah, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi ajiandae.

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Maliasili na Utalii. Awali ya yote nimpongeze sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya ya kutangaza nchi yetu hasa hasa kupitia filamu ya *Royal Tour*, tunamshukuru sana. Lakini pia niipongeze sana Wizara hii ya Maliasili na Utalii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo na kipekee kabisa tunawapongeza, pale Serengeti wanaendelea na uratibu wa miradi mikubwa ya kijamii inayofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani ya *KfW*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua Wizara hii ya Maliasili *co-business* yake ni kuhakikisha wanahifadhi maliasili zetu zote pamoja na kuliwezesha Taifa kupata mapato. Sasa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

yako mambo kama matatu hivi ningependa kuyachangia ili kuona kuwa wanaweza kufanya kazi hii vizuri.

Jambo la kwanza naishauri Wizara hii sasa iharakishe ujenzi wa uwanja wa ndege wa Serengeti. Uwanja wa ndege wa Serengeti unaweza kutusaidia sana kuongeza uhifadhi, ukienda ndani ya Hifadhi ya Serengeti kuna viwanja vingi sana, kuna utitiri wa viwanja na viwanja vile vinaathiri sana uhifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna ndege nyingi zinatua, ni makelele mengi, sasa mambo haya huwa yanakwenda taratibu taratibu, yanafukuza wanyama kuna hali ya utulivu kukosekana, wiwanja vimekuwa vingi sana. Sasa sisi katika Halmashauri ya Serengeti tumetenga eneo tayari na ninaishukuru Wizara inaendelea na michakato ya ujenzi wa uwanja. Sasa tunawaomba waongeze kasi ya ujenzi wa uwanja ule na ujenzi wa ule pia utasaidia sana wananchi kuona sasa manufaa makubwa ya uwepo wa Hifadhi ya Serengeti katika maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna habari ya ushindani wenzetu wa upande ule ambao tuna *-share* nao *ecosystem* na wao sasa wanakimbizana, kuona namna ambayo wangepanya wapate watalii wengi sana na watalii hao ni wale wale wanaokuja Serengeti. Sasa niwaombe sana waongeze kasi ya ujenzi wa uwanja huu itatusaidia sana kuongeza mapato kwa sababu pia hata watalii hawa itawapunguzia *cost* kwa sababu hawatasafiri umbali mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kuna mikataba ambayo Wizara ya Maliasili inaingia na mahoteli ambayo yanajengwa katika hifadhi. Mikataba hii tunaomba sana Wizara, Wabunge wengi wamelalamika habari ya *CSR* haieleweki, habari ya *service levy* haieleweki katika mahoteli. Lakini ukiangalia kwa kiasi kikubwa ni kwa sababu ya mikataba. Mikataba hii tungeiomba Wizara inaposainiwa iweze kubainisha kabisa wazi kwamba wahusika watalipa

service levy pamoja na *CSR* katika halmashauri ambazo hoteli hizi zipo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaiomba sana Wizara izingatie hili leo ni aibu sana unakwenda katika Wilaya kama za Serengeti zenye hifadhi kubwa halmashauri hazina mapato. Kwa nini hazina mapato ya kutosha na mahoteli? Ni kwa sababu hoteli zile, hazioni zinawajibika *direct* kulipa *CSR* pamoja na *service levy* katika halmashauri hizi. Kwa hiyo, tunaomba sana Wizara hii ijitahidi kuhakikisha jambo hili sasa linaondolewa utata. Pale Serengeti tumehangaika muda mrefu tunazo hoteli nyingi ndani ya hifadhi zaidi ya hoteli 200 pamoja na *camp sites*, lakini malipo yao ya *service levy* imekuwa ni shida malipo yao ya *CSR* yamekuwa ni shida, tunaomba sasa kwa mwaka huu unaoanza Wizara hii itusaidie kumaliza tatizo hili. (Makofi)

Jambo lingine la tatu, ningeiomba sana Wizara hii ya Maliasili na Utalii ipitie upya, Wabunge wengi wamelalamika kuhusiana na tembo pamoja na wanyama wakali. Tembo na wanyama wakali wameendelea kuwepo karibu kila mahali. Sasa tunaiomba Wizara kwa sababu uhifadhi umekuwa ni mzuri sana na wanyama wameongezeka na wanyama hawa ndio ambao watalii wanawafuata. Sisi hatuna lengo la kusema wanyama hawa sasa waondolewe wasiwepo, sasa tunaomba tupitie vizuri zile taratibu zetu za uhifadhi. Kuna haja sasa ya kujenga *fence* ya umeme ambayo haina madhara tunahaja hiyo na ukiangalia wenzetu kule wanafanya. Kuna wakati nimepita Masai Mara nimeona pembeni wao wamejenga *fence* na hakuna namna ambayo tutazuia wanyama hawa wasiweze kuwadhuru wananchi...

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Spika, sasa tutalia hapa tutapiga kelele tutaonekana kwamba hatuna mapenzi mema na hawa wanyama hapana, tunawahitaji.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Amsabi kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

TAARIFA

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampa taarifa Mheshimiwa Amsabi kwamba ni kweli kuna haja ya kuweka *fence*, lakini *fence* hiyo ikijengwa isije ikajengwa kuziba mito iliyozunguka wananchi. Kwa hiyo, ijengwe kuelekea mapori ya wanyamapori, sio kule kwa wananchi. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, taarifa imetolewa lakini nilishawakumbusha hapa ndani, sio kazi yako wewe kusema kama Mbunge anachokisema ni halali sio halali; kweli au si kweli labda kama umesimama Kuhusu Utaratibu. Kwa hiyo, huwezi kusema anachokisema ni kweli yeye anajua ni kweli ndio maana kasema.

Mheshimiwa Amsabi unapokea taarifa hiyo?

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Spika, ahsante napokea taarifa hii na nipende kuhimiza sana kwamba kuna maeneo ya vijiji ambavyo sasa ile *buffer zone* haipo, kwa mfano, kule kwenye Jimbo langu ukianza Kijiji cha Mbilikili ukienda hapa Bisalala, Tamkeli, Mbalibali, Machochwe mpaka Merenga kule wamemaliza kabisa eneo la *buffer zone* halipo. Sasa maeneo kama haya ndio ambayo naona kwa sasa ni lazima *fence* iwekwe, kwa sababu kwa namna yoyote ile wale wanyama hakuna namna ya *kuwa-control*, lile eneo la kinga halipo tena. Kwa hiyo, katika maeneo kama haya yapewe kipaumbele cha kwanza katika kuangalia kwamba sasa yawekewe *buffer zone*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa nini wanyama hawa wanapowaua wananchi na wanapoharibu mazao fidia imekuwa ni changamoto sana. Kwa hiyo, niiombe Wizara hii

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wanayo taasisi ya *TAWA* ambayo tunajua kwa utaratibu wao ndio wanaoratibu kutoa fidia kwa wananchi. Lakini pia wapo Maafisa Wanyamapori hawa *DGO's* hawa Maafisa Wanyamapori pamoja na *TAWA process* ile inakwenda kwa taratibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, Mheshimiwa Emmanuel Kishoni Ole-Shangai ajjandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya Maliasili. Kama ilivyo ada nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama jioni hii ya leo niseme mawili matatu. Lakini vilevile, kama ilivyo ada nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa maono makubwa ya filamu yetu ya *Royal Tour*.

Mheshimiwa Spika, manufaa yanayopatikana kwenye filamu hii sina haja ya kuyarejea ni mengi sana na mimi naunga mkono. Wapo waliobeza nimewasikia mahali wamebeza wamesema kwamba walionufaika zaidi ni wale washiriki wa filamu hii wakimtaja yule mzungu ambaye alikuwa anashirikiana na mama kwamba ndio wamenufaika zaidi wao kuliko sisi, sio kweli. Sisi Watanzania tumenufaika sana na tutaendelea kunufaika leo, kesho na kesho kutwa vizazi mpaka vizazi vijavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeomba hii nafasi mahususi nizungumzie suala la Hifadhi ya Selous. Kwa asilimia kubwa Hifadhi ya Selous iko kwenye Wilaya ya Liwale, lakini manufaa makubwa ambayo tungeyapata sisi kule hatuyaoni. Nimeshasimama hapa mara nyingi nikiomba Wizara hii watufikirie na sisi kutuwekea lango la kuingilia watalii kule angalau na sisi tunufaika.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kwanza kabisa zamani kulikuwa na utalii wa uwindaji ambao sasa nguvu yake imepungua, sasa hivi ni utalii wa picha. Lakini ukiangalia miundombinu ya Wilaya ya Liwale, Wilaya ya Tunduru kule Kusini kwa ujumla wake, hakuna miundombinu yoyote ya kuweza kuingia kule Selous na kufanya utalii wa namna hiyo. Kwa hiyo, naendelea kuiomba Serikali kama nilivyotangulia kusema hapo awali kwamba mnapozungumzia utalii Kanda ya Kusini msiishie Mbeya, Iringa na Mikumi mjue kwamba Kusini Selous ipo Liwale, Kilwa na Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *point* ya pili inahusiana na wanyamapori, nisipo nilizungumza hili sitoelweka. Sisi Liwale ni waathirika wakubwa sana wa wanyama wanaoitwa tembo na mara ya mwisho hapa nilitoa ushauri, nilisema basi Wizara ione umuhimu wa kutusaidia kutuwekea angalau askari hata mmoja kwenye kila kata. Kwa sababu, mimi nina vijiji kuna kijiji kinaitwa Ngumbu, Mkutano, Nangegeja, Nahoro, Mtawatawa, Mtawango, Lilombe, Ndapata sisi kule kwetu mwezi wa sita ndio mwezi wa mavuno kuanzia mwezi wa tano kuja mwezi wa sita, lakini tayari wakulima walisharudi kutoka mashambani tangu mwezi wa nne mazao yote yamemalizwa na tembo kwa hiyo wamerudi wako kijijini.

Mheshimiwa Spika, tembo wamemaliza kila kitu na hakuna msaada wowote na nikawaambia kutoka Liwale Mjini mpaka vijijini huko hakuna kijiji ambacho kiko karibu zaidi ni kilometa 30, lakini vijiji vilivyo vingi ni kuanzia kilometa 70, 80 mpaka 90, nikasema basi tunaomba mtuongezee maaskari, jambo lile halikuwa sawa na halikutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo naleta ombi lingine kambi ya watu wa Selous kwa Wilaya ya Liwale iko Liwale Mjini. Mheshimiwa Waziri naomba kambi ile ihamishwe irudishwe kule ambako ilikuwa *proposed* kujengwa katika Kata ya Barikiwa au ikajengwe Mkutano. Haina maana yoyote watu watoke vijijini waje mjini waitafute Selous waje kutoa taarifa, wakija pale mjini kutoa taarifa wanakuta Selous hawana magari, hawana usafiri na masika barabara hazipitiki.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mimi naomba sana, naomba sana, naomba sana, leo ni ombi la pili hili nasema kambi ya Selous Liwale ihamishwe iwekwe kijijini kama ilivyo ile ya Miguruwe, ipelekwe vijijini.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwa sababu nilishaomba askari kwenye kila kata jambo hili haliwezekani, sasa mwaka huu naomba ombi la pili, naomba ifikapo mwezi wa saba muanze kutuletea chakula, watu wa Liwale hawana chakula wamesharudi mashambani sasa naomba muwalettee chakula hatutoelewana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikifika mwezi wa saba wale watu wanaanza kupata shida ya njaa kwa sababu nimeshakuambia wamerudi tangu mwezi wa nne mazao yameliwa wamerudi. Naomba sana hilo jambo lizingatiwe.

Jambo la tatu, nilishasema hapa kwenye vikao mbalimbali kuhusu fedha zilizokuja kwa ajili ya kuimarisha utalii Kanda ya Kusini. Zile fedha mimi naomba nizione zikiingia Tunduru, nizione zikiingia Liwale, nizione zikiingia Kilwa, kwa sababu kama jiografia ya Wizara ya Utalii Kanda ya Kusini maana yake ni Kanda ya Nyanda za Juu Kusini watuambie hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nizungumzie kadhia ya wachimbaji wadogo wadogo ambao mimi nakubaliana na Wizara kwamba walivamia Selous wakaenda kuchimba dhahabu na haya machimbo ni mapya, lakini mimi nataka niwaambie walioitangaza hii kambi ya kuchimba madini ni askari wa wanyamapori, hii kambi iko zaidi ya kilometa 90 kutoka Liwale Mjini wananchi walijuwaje kama kuna madini huko kwenye hiyo Selous? Lakini ni askari wenyewe wa wanyamapori waliwapeleka watu kule, wakawaeleza kule kuna madini, matokeo yake wote wamekwenda kule wamekuwa wengi wanaanza kuwapiga. Nguvu inayotumika kuwahamisha watu hifadhini ni kubwa kuliko. Mtu amekwenda kule ana sururu, ana jembe anachimba madini unakwenda na silaha kubwa kubwa, mnajeruhi watu, mnatimua watu, kwa *resistance* gani ambayo wanaipata

askari wa wanyamapori wanaanza kuwahangaisha watu kwa namna hiyo? *(Makofi)*

Mimi naomba Mheshimiwa Waziri nguvu inayotumika kuwahamisha watu kwenye hifadhi zilingane na ubinadamu kwa watu hao au nguvu wanayotumia watu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine wamekwenda kule wenyewe *Selous* ndio waliowapeleka, kwa hiyo, mimi naomba sana. Maana sitaki kusema hapa kwamba kuna watu wameuawa na nini nisije nikaambiwa nilete taarifa, sina taarifa rasmi za watu kuuawa, lakini nguvu inayotumika kuwaondoa watu *Selous* ni kubwa mno, mimi nawaombeni sana...

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

SPIKA: Haya ahsante sana. Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Lekishoni Ole-Shangai, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mary Masanja ajiandae.

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Spika, ahsante naomba nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara yetu ya Maliasili na Utalii. Lakini awali ya yote nianze kwa kuwapongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa taasisi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwashukuru kwa sababu Kaliua ni miongoni mwa maeneo ambayo yamepakana na Hifadhi kubwa mbili, kwanza tuna *Ugara National Park*, lakini pia tunayo Kigosi, lakini tuna *TFS* na tuna *TAWA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ile timu ya Mawaziri nane ilipita katika Wilaya yetu ya Kaliua na tumenufaika kwa sababu

sehemu kubwa ya changamoto imeweza kutupunguzia. Wilaya yetu takribani vijiji 26 vilikuwa kwenye hifadhi, lakini kwa kazi nzuri iliyofanywa na timu hiyo, sasa wananchi wale wako huru na tunajipanga kwenda kwenye matumizi bora ya ardhi katika vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mimi nina machache ambayo ningeweza kuyashauri, kwanza kwenye Hifadhi ya Ugara; Hifadhi ya Ugara ni Hifadhi mpya, lakini hifadhi hiyo mpya mimi nimekwenda kutembea na timu mbalimbali ya uongozi wetu wote wa wilaya tumekuta hifadhi ile ni nzuri sana na inavivutio vizuri sana. Mimi nilikuwa napenda niishauri Wizara kuwekeza nguvu nyingi kwenye ukarabati wa miundombinu na miundombinu ambayo tunaomba kwa Hifadhi ya Ugara ni barabara nzuri ifike *Ugara National Park*, lakini miundombinu ya mawasiliano, miundombinu ya *internet* na miundombinu ya hoteli na *camp*s mbalimbali. Nalisema hili sio kwa maana ya Ugara peke yake, lakini ukienda Kigosi miundombinu ya kuingia Kigosi ni shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado ukienda Katavi miundombinu ya kuingia Katavi ni shida, ukienda Biharamulo pale Burigi Chato hiyo yote miundombinu ni shida. Lakini ukiangalia ukanda wote ambao nimeutaja unaweza ukafanya vizuri kama inavyofanya vizuri ukanda wa Kaskazini, lakini tunaendelea kuangalia tukiwekeza fedha nyingi ukanda ule wote umepakana na nchi mbalimbali, Uganda jirani zetu, Congo jirani zetu, Burundi jirani zetu. Sasa nchi hizi zote zingeweza kutuletea tija kwa sababu vivutio tulivyonyavyo huko ni vizuri na tukivihamasisha vizuri tukavitangaza vizuri nina uhakika ule ukanda wote utafunguka vizuri sana. Kwa sababu unakuta kutoka Burundi mpaka unaingia Hifadhi kilometa 30, sasa kwa nini hatujatangaza kwa kiwango ambacho ni kizuri na kiwango kikubwa zaidi? Nilikuwa nashauri miundombinu ile kwenye hifadhi zote ambazo nimetaja iboreshwe na twende kwa kasi zaidi kama Mheshimiwa Rais anavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine nilikuwa naliomba ni kwenye marekebisho ya mipaka, ni kweli

tumepita, vijiji viko huru, lakini baadhi ya maeneo bado urekebishaji wa mipaka bado migogoro haijaisha. Kwa mfano, Igagala Namba Nne hicho ni kijiji, Ugansa bado, Usinge bado, Luganjo Mtoni bado, Kombe bado; nilikuwa naomba maeneo haya wayape kipaumbele, ili kuhakikisha sasa wananchi tunaishi kwa furaha kwa amani tukiendelea kulinda hifadhi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tabora ni miongoni mwa mikoa ambayo inazalisha asali na uzalishaji mkubwa umepakana na hizo hifadhi. Sasa nilikuwa nawashauri kwanza naomba tupewe muda kwa sababu kuna eneo ambalo limeongezeka la *TFS* likaenda Ugara sisi kule kuna mizinga. Tunaomba tupatiwe angalau miezi miwili wale wananchi wavune na waweze kutoa mizinga yao, hilo ndilo ombi ambalo ningependa mliangalie kwa ukanda mzima wa Urambo, ukanda mzima wa Kaliua na ukanda mzima wa kuelekea njia ya Ushetu pote humo ni wafugaji wa nyuki. *(Makofi)*

Ushauri wangu mwingine ni kuhusiana na utalii wa ndani; Mheshimiwa Rais ametusaidia kwenye *Royal Tour* kwa maana ya kutusaidia kufungua huko, lakini tunapopata janga sisi wa ndani tunakwama kwa sababu miradi mikubwa inategemea wafadhili. Ni kwa nini sisi tusijenge utamaduni wa kuhamasisha utalii wa ndani tukajengeka kifikra kuwa tayari kutembelea hifadhi zetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri utalii wa ndani tuupe hamasa kubwa sana na mimi niwaombe Wizara watoe nguvu pale Kaliua ile hifadhi ukifika kule kwa kweli, kuna kivutio kikubwa, nilimuona *Mr. Shelutete* alikuja kama mara mbili, lakini nilipokuja kuangalia sikuamini, ile ni Kaliua kweli? Kwa sababu, ilikuwa ni vivutio vizuri kweli kweli, sasa sasahivi wananchi wamehamasika, lakini miundombinu bado nis shida. Niombe zaidi tuweke hiyo miundombinu ili tuweze kufikika kwa hali ambayo ni nzuri na hali ambayo itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nashauri pia kuhusiana na askari wa maliasili. Natambua kabisa na

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wenyewe wanapata changamoto wapo askari wanauawa kabisa, lakini nilichokuwa nashauri mimi hebu tuwape mafunzo askari wetu namna gani bora ya kukabiliana na wale ambao hasa zile vurugu za kawaida za mipakani kwa sababu nguvu ikitumika kubwa malalamiko yanakuwa ni makubwa sana. Nashauri tuboreshe mahusiano zaidi kwa maana ya kuwapa mafunzo ambayo sio lazima watumie silaha peke yake, lakini hata kuelimisha kwa maana ya kutujengea mahusiano mazuri na hifadhi zetu zitakuwa ni endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja, nimalizie; Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Kaliua, Kaliua tulikamata magogo pale tukauza shilingi bilioni moja na nusu, Waziri Mkuu aliahidi kile kijiji...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Sekunde 30 malizia sentensi.

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Spika, ahsante, Kijiji cha Wachawaseme wapewe zahanati yao. Mkurugenzi wangu ameshaleta ile *bill* ya zahanati pale, mpaka leo tumepata shilingi bilioni moja na nusu, zahanati karibu shilingi milioni 70 bado hamjatuletea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Lekshone Ole-Shangai, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Mtoa Hoja ajiandae.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuwa mchangiaji wa mwisho wa hotuba ya Waziri wa Maliasili na Utalii. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa filamu yake ya *Royal Tour* ambayo Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Naibu Spika alisema asubuhi kwamba, mama ameupiga mwingi na sisi tunaupiga wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi niwashauri Wizara kwamba Mheshimiwa Rais ametutangaza vya kutosha, sisi tunatakiwa kuweka miundombinu wezeshi kwa ajili ya kuwapata watalii. *(Makofi)*

Kwanza ukijaribu kuangalia barabara zetu zinazokwenda kwenye hifadhi zetu nikitolea mfano barabara kutoka Lodoare kwenda *Nabi Gate* ni barabara ambayo yanapita magari yanayokwenda Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na Serengeti, kwa hiyo, tunatakiwa kuhakikisha kwamba, tunaboresha miundombinu yetu. Lakini pia barabara inayotoka Mto wa Mbu kuelekea Loliondo ni barabara muhimu pia ambayo Wizara hii inatakiwa kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi kuangalia namna ya kuboresha ili watalii waweze kupita katika njia zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kipengele cha idara ya wanyamapori, nimeona mapendekezo yao ya kuweza kupandisha baadhi ya mapori tengefu kuwa mapori ya akiba. Mapori hayo yaliyotajwa, kipengele namba 5.3.1.1 *Lake Natron*, Kilombero, Loliondo, Lolkisale, Longido, Mto wa Mbu na Simanjiro. Mimi naomba niwaambie kwa upande wa pori tengefu la Loliondo wananchi wa Loliondo wameleta mapendekezo yao na wameshakabidhi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Niishauri Wizara mkapitie taarifa zile za Loliondo pamoja na Ngorongoro ili angalau zikafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini leo huku tunalia Loliondo, mmeshaenda *Lake Natron*. Wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro pande zote mnapiga Mashariki, Kusini, Kaskazini, wananchi wanalia kote. *Lake Natron* ni Wilaya ya Ngorongoro pia, Loliondo ni Wilaya ya Ngorongoro, ukienda Ngorongoro tarafa ya Ngorongoro eneo la *Ngorongoro Conservation Area* ni Wilaya ya Ngorongoro. Sasa hao wananchi kwa nini hamtaki wapumue? Kila upande mnawapiga, kwa nini? Leo

mnakuja kusema mnapandisha pori tengefu la Mto wa Mbu, hivi pori tengefu la Mto wa Mbu liko wapi? Liko wapi?

Mheshimiwa Spika, kote kumekuwa ni mji, sasa maana yake tunaendelea tena kwenda kuongeza taharuki kwa wananchi wa Wilaya ya Monduli. Bado hatujamaliza Monduli, Wamasai wa Longido watalia kwa sababu mmeandika hapa, bado hawajapumzika hao tunaenda Lolkisale watalia kule, bado hatujanyamaza tunaenda Simanjiro. Hao wananchi tunawatakia nini? Huu uhifadhi tunaouhifadhi ni kwa manufaa ya nani?

Mheshimiwa Spika, kama uhifadhi sasa imekuwa kilio kwa wananchi haina haja ya kuwa na uhifadhi huu. Ni lazima tuwe na uhifadhi ambao unawaletea wananchi maendeleo, lakini uhifadhi ambao unaleta kilio kila siku kwa Watanzania hauna manufaa kwa sababu leo wakilia wananchi wa Kilombero, watakimbia Loliondo, wakilia wa Loliondo wataenda *Lake Natron*, wataenda Simanjiro, wataenda Lolkisale, sasa sijui hawa wananchi tunawatakia nini?

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani kinachotakiwa sasa ni lazima tuamue mgogoro wa eneo la Loliondo umedumu kwa zaidi ya miaka 31 sasa, Serikali ni lazima tufikirie namna wale wananchi waachwe waendeleo na maisha yao, tumewarudisha nyuma kimaendeleo, kiuchumi na lile eneo ndipo wanapochungia mifugo yao.

Kwa hiyo, mimi nishauri Wizara kuna maeneo mengi tumeshahifadhi, *square kilometer* 307,800 za Tanzania nzima ambayo ni asilimia 32.5 mpaka 40 ya ardhi yote tuliyonayo Tanzania. Maeneo mengine tuwaache wananchi waendeleo na maisha yao.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine Wizara hii, kama alivyosema Mheshimiwa Mulugo, wanyamapori wanaingia kwenye mashamba ya wananchi, tunasema tunatoa fidia, lakini miaka yote tumeshindwa kutoa fidia kabisa. Kama alivyosema Mheshimiwa Kuchauka hata wananchi wangu wa Kata za Oloipiri, Soitisambu, Ololosokwan na kata nyingine

mashamba yao yote yameliwa na tembo. Sasa tutafute namna ya kuwapelekea chakula kwa sababu tembo wanaingia kwenye mashamba wanamaliza moja kwa moja, lakini hakuna fidia yoyote inayotolewa na Wizara ya Maliasili, lakini pia kuna wananchi wanauawa na tembo na wanyama wengine wakali...

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Ole-Shangai, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Londo.

T A A R I F A

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, sio tembo tu, hivi tunavyozungumza kwa wiki nne ndege wanashambulia mashamba ya wakulima katika Kata ya Kilangali, Wilaya ya Kilosa, lakini ndege hawa wanahifadhi ndani ya Hifadhi ya Mikumi na tumeomba zaidi ya mara tatu/mara nne tupate kibali cha Wizara ya Kilimo kwenda kuuwa ndege hawa, hatujapata mpaka sasa. Kwa hiyo, sio tembo tu wanakula mazao ya wakulima, hata ndege pia. *(Makoff)*

SPIKA: Mheshimiwa Ole-Shangai.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru na ninapokea Taarifa ya Mheshimiwa Londo, lakini kikubwa...

SPIKA: Ngoja, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, ili upokee au ukatae Taarifa, lazima Kiti kiwe kimekuuliza unaipokea au unaikataa? Kwa hiyo, mimi sijakuuliza swali hilo, nimekuita tu ili uendelee kuzungumza.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru, niendelee kwa sababu, jamaa ameamua kula muda wangu, lakini mimi nishauri Wizara hii wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro wameleta maoni yao, wamekabidhi

kwa Waziri Mkuu, mkaisome, hayo ndio maoni ya wananchi na ndio msimamo wao.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kukaa, ili badae Waziri atakapokuja atuambie *fine* kwa ajili ya mifugo wanaoingia hifadhini ni shilingi ngapi? Kwa sababu kumekuwa na *varieties*, leo unakuta ni 10,000; 50,000; mpaka laki moja; kwa hiyo, baadae Waziri atuambie ni kiasi gani kinatakiwa mifugo wanapoingia hifadhini? Ahsante nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza kwa hotuba ya bajeti ambayo itafungua fursa zaidi. Hata hivyo nina ushauri na hoja kadhaa ambazo nisipopata majibu ya kuridhisha nitashika shilingi kwa nia njema ya kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Mradi wa *REGROW*; mradi huu ulizinduliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tarehe 12 Desemba, 2018 wakati huo akiwa Makamu wa Rais. Hata hivyo kumekuwa na kusuasua sana katika kutekeleza mradi huu ambao ni mkopo wa Benki ya Dunia wa kiasi cha dola milioni 150 za Kimarekani.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya mradi huu pamoja na mambo mengine ni kuboresha mazingira ya shughuli za utalii ikiwa ni pamoja na ku-*upgrade existing roads, airstrips* lakini pia kujenga kituo kikubwa cha habari kwa maana ya *information centre* pale Kihesa, Kilolo. Aidha, mradi huu unatarajiwa kuboresha ushiriki wa wananchi wanaozunguka hifadhi ama kwa mafunzo ya uhifadhi au kwa kupata ajira ndani ya sekta.

Mheshimiwa Spika, mradi huu ambao narudia kusema kuwa utekelezaji wake ni wa mwendo wa kinyonga

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ungeweza kunufaisha kaya zaidi ya 20,000 na wakulima wanaozunguka Hifadhi ya Ruaha.

Mheshimiwa Spika, mradi huu kwa mujibu wa maelezo ulipaswa kwa mtiririko uwe umeanza na kukamilika mwaka 2024 ambapo ilipaswa mpaka kufikia mwaka huu wa 2022 kiasi cha fedha dola milioni 111 ziwe zimeshatumika kutekeleza hayo niliyoyataja hapo juu. Kwa mtiririko ilipaswa baada ya uzinduzi *by 2020* kiasi cha dola milioni 41 kilipaswa kiwe kimetumika; *by 2021* kiasi cha dola milioni 76 kiwe kimetumika; *by 2022* kama nilivyosema kiasi cha dola milioni 111 kilipaswa kiwe kimetumika; *by 2023* kiasi cha dola milioni 141 kilipaswa kiwe kimetumika; na *by 2024* kiasi chote cha dola milioni 150 kiwe kimetumika, na hapa tuelewane hoja sio tu kutumika bali kutumika katika shughuli zilizopangwa kwa lengo la kuboresha mazingira ya utalii na ushiriki wa wananchi katika uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anafanya jitihada kubwa kufungua milango kwa kushiriki mikutano ya Kimataifa ikiwemo *Royal Tour* ambako anaitangaza nchi na utalii wetu, kwa kufanya hivi watalii watakuja, je, kama tumekuwa na mwendo wa kinyonga kutekeleza mradi wa *REGROW* hatuoni kuwa tunajikwamisha na kumkwamisha Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Spika, pili, fedha hizi sio *grant*, ni mkopo ambao inafaa matunda yake yaanze kuonekana, lakini sasa tunajivuta, mara ilikuwa sijui *GN* kutoka ardhi ili kufidia na eneo, sijui muda wa mradi tumeongeza, *for whose interest*. Kwa hiyo, kama mtu ninayejali utalii kama sehemu ya kuongeza mapato ya Taifa na wananchi, jambo hili sio sahihi, ndio maana pasipo majibu ya kutekelezeka nitashika shilingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu misitu; tunashukuru sana sekta imetulia sana, nawapongeza sana *TFS* kwa ushirikiano na pia kwa kupokea mawazo ya wadau. Nawashukuru pia kwa *CSR*, wanatupa *support* kubwa sana watu wa Mafinga na Mufindi, nawashukuru mno.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, nina ushauri katika mambo mawili; kwanza ni kuhusu tozo; ninashauri baadhi ya tozo sasa umefika wakati tuziondoe, kwa mfano *LMDA*, tayari sasa maeneo mengi yamepandwa miti, tozo hii ambayo ililenga kuirudisha shambani kupanda miti, ni wakati sasa tukaiondoa sambamba na kuangalia suala la bei na tozo nyingine ili kusisimua biashara.

Pili, Kituo cha Panda Miti Kibiashara chini ya ufadhili wa Serikali ya Finland; sisi Halmashauri ya Mafinga Mji kwa kushirikiana na Seikali tunaomba tufanye jitihada za pamoja ili baada ya *phase* ya sasa kumalizika, Finland watusaidie kwa *phase* nyingine zaidi ili kuendana na muda wa uvunaji wa miti toka mradi ulipoanza. Hii itasaidia kufanya tathmini ya uhakika na kupima matokeo ya mradi umekuwa na msaada kwa kiasi gani katika Taifa na jamii. Hata hivyo ili jambo hili lifanikiwe ni muhimu sana sote kwa pamoja tukashirikiana kushawishi *GRL* kutuachia lile eneo na baadae mradi ukiwa umemalizika kwa ukamilifu kituo kirithiwe na Halmashauri ya Mafinga Mji.

Mheshimiwa Spika, *CSR* kwa makampuni; jambo hili ni la hiyari lakini makampuni makubwa yaliyowekeza katika maeneo yetu yanao wajibu wa kutoa *CSR*, kwa sababu sisi tumewapa maeneo lakini moto ukitokea wananchi wanashiriki kuuzima, ikiwa *TFS* kupitia Shamba la *Sao Hill* wanatoa *CSR*, *why not* haya makampuni? Ushauri, naomba tuwe na *forum* nao na ikibidi watoe taarifa zao za *CSR*.

Mheshimiwa Spika, mimi ndio *champion* wa kushauri na kusukuma ajenda ya kwamba kama tunataka kujenga uchumi wa viwanda tuzuie kusafirisha *veneer*, na mimi ndiye pia nilishauri kuwa kwa kuwa kiwanda sio kama kwenda kununua nyanya sokoni ambapo utazikuta tu, basi tuwape muda, hata hivyo imethibitika kuwa muda huo ni mfupi na ndio maana kama mshika au mtoa hoja ninashauri, pafanyike *extension* hata ya miaka miwili ili watu hawa wajipange.

Mheshimiwa Spika, ni mjinga tu ndiye ambaye huwa habadilishi mawazo, jambo hili limeathiri pia mapato ya mtu

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

mmoja mmoja, lakini pia *own source* kwa Halmashauri zetu ikiwemo Mafinga Mjini. Ni kwa muktadha huo nashauri kuwa tufaye *extension* pasipo masharti na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri pamoja na ugeni wake katika Wizara nilimueleza kwa kina jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba ushauri huu wa kufanya *extension* ya *ban* uwe huru pasipo masharti kwa sababu kwa msisitizo kabisa wapo watu walitumia mwanya huu kujineemesha jambo ambalo sio sawa.

Mheshimiwa Spika, tunachosisitiza mara zote ni *welfare* ya wafanyakazi katika viwanda na pia ulipaji wa kodi na tozo za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utomvu maarufu kama gundi, imethibitika kuwa hakuna athari hasa kwa miti iliyokaribia kuvunwa, ushari wangu makampuni yanayovuna ambayo hayazidi mawili, moja linavuna katika shamba la Serikali na moja katika mashamba ya *GRL*, wapewe miti ya kutosha ili kusudi wananchi wapate ajira, Halmashauri ipate *cess* na Serikali iongeze mapato. Suala hili lina faida sana hasa katika ulinzi shirikishi dhidi ya majanga ya moto. Kazi ya kuvuna gundi ilikuwa inaajiri zaidi ya watu 1000 na wengi wao wanawake, na ni kazi ambayo mtu anaweza kufanya sanbamba na kazi zingine, kwa mfano mtu akitoka shamba anajiongezea kipato kwa kwenda kuvuna gundi, analipwa kulingana na kiwango alichovuna, mimi kama mtu niliyekulia kwenye misitu, nawapa ushauri ambao ni *genuine* sana ambao tija yake ni kubwa kwa ustawi wa misitu na jamii zetu.

Mheshimiwa Spika, bei elekezi ya vigogo; katika vikao tulivyokaa tumejadili sana suala la bei elekezi ya vigogo kwa Wachina, ninashauri tufikie mwisho, nakambuka Kamati ya Profesa Felister ilikuwa tayari na ripoti ya nini kifanyike ili kuwa na *win win situation*, kwa hiyo pamoja na kuwa biashara ni huria lakini lazima tuwe na *mechanism* za kuona kuwa wananchi wetu wananufaika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana, Mbunge na Waziri wa Maliasili na Utalii pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Mary Masanja, Mbunge. Vilevile nimpongeze Dkt. Francis - Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mkome.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhamasisha na kuutangaza utalii wetu. Nasi Wilaya ya Nyasa tunamuunga mkono.

Mheshimiwa Spika, maombi, kwanza kumaliza mgogoro wa Lipalamba na wanakijiji wa Kijiji cha Mseto; kusaidia kutengeneza barabara zinazopita kwenye hifadhi ya Lipalamba ambazo zinahitaji kifusi kutoka mbali; tunaomba shilingi 5,000,000 kwa ajili ya kukamilisha zahanati ya kijiji cha Mipotopoto kinachopakana na Hifadhi ya Lipalamba na huo mkakati wa utalii kwenye maziwa makuu ikiwemo Nyasa umetajwa kwa kifupi sana. Naomba ufafanuzi ni kitu gani kitafanyika?

Mheshimiwa Spika, niliomba kujenga hosteli ndogo kwenye hifadhi hiyo ili kuanzisha utalii wa eneo hilo. Hadi leo sikujibiwa; je, Wizara yenu haina utamaduni wa kujibu barua?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wa maandishi kufuatia kuwasilishwa kwa bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni mchango kwa Wizara hii; kwanza ili kuboresha utalii na kuvutia watalii wengi nchini Wizara haina budi kushirikiana na Wizara nyingine kwa ajili ya kuboresha miundombinu mbalimbali ya barabara hasa barabara ya kutoka Loduare mpaka *Nabi Gate* kwani ni barabara muhimu sana kwa watalii wanaotembelea Hifadhi

ya Ngorongoro na Serengeti na barabara ya lami kutoka Mto wa Mbu mpaka Loliondo kwani nayo ni muhimu kwa watalii kufika Oldonyo Lengai.

Mheshimiwa Spika, Wizara ipitie na kufanyia kazi maoni ya wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro, Sale na Loliondo kwani ndiyo mwarobaini wa changamoto za muda mrefu za maeneo hayo. Ni muhimu sana Serikali ione kuwa eneo la pori tengefu la Loliondo ni ardhi ya vijiji, hivyo vijiji husika ziruhusiwe kutumia ardhi yao bila usumbufu na wananchi waondokane na mgogoro wa ardhi iliyodumu kwa miaka 31 sasa, kimsingi mgogoro huu umewarudisha wananchi nyuma kiuchumi na wengine kupoteza maisha pamoja na mali zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara itafakari upya namna ya kufanya kazi na Baraza la Wafugaji ili kurejesha mahusiano na wananchi wanaoishi kwenye eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, pamoja na kutekeleza jukumu lake la kuwapatia wananchi wenyeji maendeleo kama ilivyo kwenye sheria iliyoanzisha eneo hilo bila kuwawekea vikwazo vya kimaendeleo kama ilivyo sasa.

Pia Wizara itekeleze *MoU* iliyoingwiwa kati ya Wizara, Baraza la Wafugaji, *NCAA* na Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro na kuwaajiri watumishi wa Baraza la Wafugaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu kuboresha huduma za waongoza watalii na *quality za magazine*.

MHE. HAMIS M. MWINJUMA: Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kuhusu biashara ya viumbe pori hai, *specifically* inayohusisha wadudu wadogo yaani vipepeo, mijusi, jongoo, ndege na vinavyofanana na hivyo ifunguliwe.

Mheshimiwa Spika, biashara hii ilikuwa inafanyika kwa miaka kadhaa kabla ya kupigwa marufuku na kusitishwa tarehe 17 Machi, 2016 kwa agizo la Serikali. Watanzania waliokuwa wanashiriki biashara hii wameingia hasara kubwa na kurudishwa nyuma sana kiuchumi, na mfano halisi ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wananchi na wafanyabiashara waliokuwa wanashiriki biashara ya vipepeo jimboni kwetu Muheza, Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, ninazo hoja kadhaa za kwa nini Serikali inatakiwa kuirudisha biashara hii. Kwanza, miradi ya kufuga na kusafirisha vipepeo kibiashara haina madhara yoyote ya kimazingira, haipunguzi idadi ya vipepeo na kinyume chake inawaongeza. Kwa kawaida muda wa kuishi wa vipepeo ni majuma mawili na vipepeo hutaga mpaka mayai 400 na kwa njia zao za kawaida hutotoa mawili ama matatu tu, ila wakitotoleshwa kwa njia za kibinadamu zilizokuwa zikifanyika mayai yote hutoa vipepeo.

Pili, inasaidia sana kwenye uchumi wa wananchi mmoja mmoja. Wananchi wa vijiji vyetu walikuwa wana uwezo wa kupata mpaka shilingi milioni moja kwa mwezi ambazo ni fedha nyingi mno kwa mazingira yetu. Kwa kusitisha biashara ile, wananchi wetu wamerudi kwenye ufukara wa kabla haijaanza kufanyika na kwa vile wanaishi pembeni ya hifadhi tunahatarisha mno kwao kuvutiwa na kufanya shughuli za kihalifu kwa misitu yetu. Kwa hiyo, biashara ile ilikuwa inasaidia ulinzi pia kwa misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika biashara ile ilisaidia miradi ya kijamii yenye faida kubwa. Tuliweza kujenga madarasa kadhaa, miradi ya maji ya bomba na fedha taslimu zilizolipwa kwa Serikali za Vijiji. Yote hayo yamepotea kwa kusitishwa kwa biashara ile. Kwa kifupi ni kuwa zuiu lile lilikosa macho kama lilivyokosa mashiko. Halina faida yoyote iwe ya kimazingira ama kiuchumi na ni wakati sasa wa Serikali kuliondoa. Serikali kama ilivyo kwa wananchi wa maeneno husika Wilayani Muheza, inapoteza fedha nyingi kwa kuendelea kuizua. Serikali kuruhusu tena usafirishwaji wa vipepeo nje ya nchi kuna mantiki kubwa kwa ustawi wa wananchi wale na pato la Taifa pia kiujumla.

Kwa kuongezea, Kamati ya Bunge ya Uwekezaji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jerry Silaa ambayo ilitembelea maeneo ya Tarafa ya Amani, Wilayani Muheza kunakofanyika ufugaji wa vipepeo iliishauri Serikali kuondoa

zuio na kuifungulia biashara ile. Faida ni nyingi na hakuna hasara yoyote kwa kufanya hivyo.

Niiombe tena Serikali kupitia Bunge lako tukufu, iondoe zuio lile ili kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwanza kwenye nia yake ya kuwarahisishia maisha wananchi wa Tanzania, lakini pia kuendelea kuitangaza Tanzania kama alivyofanya kwenye filamu ya *Royal Tour* kwani vipepeo hawa wanakwenda kutumika kwenye maonesho ya vipepeo nje ya nchi na sifa za uzuri wao zinaipamba nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake ya kiubunifu na hatimaye kubuni filamu ya *Royal Tour*, filamu hii sio tu imeitangaza nchi yetu kimataifa lakini pia imefungua ajira nchi kwa kuleta watalii wengi. Filamu ya *Royal Tour* itaongeza pato la Taifa letu na kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja na hatimaye nchi mzima. Viko vivutio vingi nchini ambavyo hapo awali havikujulikana kama viko nchini, wapo waliodhani viko nchi za jirani vivutio kama vile Mlima Kilimanjaro, Mbuga ya Serengeti, na kadhalika. Leo dunia nzima inatambua vivutio vyote vilivyo nchini na hivyo kukuza utalii nchini.

Suala la pili ni kuhusu uwepo wa wanyama pori jamii ya tembo na mamba. Wanyama hawa wanaongezeka kwa kasi huku ardhi ikibakia ile ile, lakini pia binadamu tunaongezeka kila kukicha. Madhara ya ongezeko la wanyama pori kwa jamii zetu ni makubwa sana ikiwa na watu kupoteza maisha, mazao ya biashara na chakula. Jambo linalokwenda kuchangia kwa kiasi kikubwa ukosefu wa chakula hapa nchini na kuongeza umasikini kwa watu wetu. Kwa mfano katika Wilaya ya Liwale kwenye Kata za Miruwi, Nangano, Mlembwe, Mkutano, Lilombe na Liwale B. Wakulima kwenye kata hizo wamesharudi kutoka mashambani bila ya chakula baada ya mazao yao kuliwa

na tembo, tayari watu hawa wanahitaji msaada wa chakula. Hivyo naiomba Serikali kulitambua jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kushauri huko nyuma kutuongezea askari wa wanyama pori, ushauri ambao haukutiliwa maanani na matokeo yake ndio haya. Sasa nazidi kuishauri Serikali ione ni jambo gani bora kuwa na wanyama wengi nchini, huku wananchi wengi wakitaabika na umasikini wa kukosa chakula na mahitaji mengine au kuajiri maaskari wengi zaidi na kusambaza kwenye kata zetu wakasaidia kuwadhhibiti wanyama hawa waharibifu.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba mambo mawili yafanyike kwa haraka; kwanza, viwango vya kifuta mchozi viboreshwe ili vibebe uhalisia wa maisha ya leo, baada ya kuviboresha basi vitolewe kwa wakati kulingana na majira ya mwaka ya kilimo nchini. Si vyema mkulima akasubiri miaka miwili kwa mazao yaliyo liwa kwa miaka miwili nyuma, jambo linaloongeza si tu chuki kwa wakulima wetu kwa Serikali yao, pia linaongeza umasikini kwa jamii husika.

MHE. ABEID M. IGHONDO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa mchango wangu wa maandishi katika Wizara hii muhimu ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza mawaziri wa wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na zaidi nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa mstari wa mbele kuitangaza nchi yetu na vivutio tulivyonavyo hususan kupitia *Royal Tour*.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo langu kuna msitu wa Mgori ambao unamilikiwa na wananchi kupitia Serikali za Vijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Singida, hata hivyo wananchi hawa wapo tayari kuukabidhi msitu huu kwa Wizara ili uwe ni msitu wa Hifadhi ya Taifa ambapo hatua kadhaa zimeshanyika kukamilisha mchakato huo.

Ningependa wakati Waziri anafanya majumuisho aniambie ni hatua gani iliyofikiwa maana ni muda sasa tangu jambo hili limeanza kufanyiwa kazi. Ningependa kuona jambo

hili linafikia mwisho ili msitu huu uweze kulinufaisha Taifa letu na pia wananchi wetu waweze kunufaika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kuishauri Wizara kuvitangaza vivutio vyetu ipasavyo na kuiboresha safari *Channel TV* inayotumika kutangaza vivutio vyetu. Ninashauri wawepo watangazaji bobezi katika *channel* hiyo, pia Balozi zetu zitumike ipasavyo kutangaza vivutio vyetu na kuhamasisha watalii wengi kuja nchini ili nchi yetu ipate watalii wengi.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusisitiza Mheshimiwa Waziri anipatie mrejesho kuhusu umiliki wa msitu wa Mgori mchakato wa Serikali kuuchukua mmefikia wapi? Kwa nini unachukua muda mrefu namna hii?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Naibu Waziri Mheshimiwa Mary F. Masanja na wataalamu wa Wizara na wadau wa maendeleo kwa mchango mkubwa sana kwenye sekta ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, Mlima Kilimanjaro na viunga vyake ni moja ya vivutio muhimu vya utalii ambavyo vimeipatia Tanzania heshima kubwa kimataifa. Ndani ya Mlima Kilimanjaro na maeneo yanayozunguka mlima kuna vivutio vya aina mbalimbali vya kitalii.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni, Rais wetu alishiriki kikamilifu kwenye filamu ya *Royal Tour* iliyokuwa na kipengele cha kutangaza utalii ukiwepo Mlima Kilimanjaro. Kutokana na hili, ni vyema tukachukua tahadhari mapema ili watalii watakapoanza kumiminika kuja kutalii Kilimanjaro wakutane na mazingira mazuri. Tusipofanya hivyo, watalii wakija wakikumbana na changamoto watapeleka sifa mbaya

kuhusiana na eneo letu na kuathiri idadi ya wageni watakaotembelea Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kwenye suala la vivutio vya Mlima Kilimanjaro na umuhimu wa kutatua changamoto za vivutio hivyo ili kuwezesha watalii kufika maeneo hayo kirahisi na kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni imegundulika kwamba mti mrefu kuliko yote Barani Afrika umepatikana katika Kijiji cha Tema, Kata ya Mbokomu, Jimbo la Moshi Vijijini, Mkoani Kilimanjaro. Mti huo ambao una urefu wa mita 81.5 upo ndani ya eneo la Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (*KINAPA*). Ugunduzi huo umeonesha pia huu ni mti wenye miaka mingi zaidi duniani kwani una miaka 600. Mti huu umeupa heshima Mkoa wa Kilimanjaro na Tanzania kwa jumla. Kugundulika kwa mti huo kumeongeza chachu ya watalii kupanda Mlima Kilimanjaro na wengine kwenda kushuhudia mti huo.

Mheshimiwa Spika, licha ya mti huu kuwa kivutio ambacho kinaweza kuiingizia Serikali fedha za kigeni, lakini changamoto iliopo ni ugumu wa kuufikia mti huo. Ili kufika katika eneo la Mrusungu ambapo ndipo ulipo mti huo mrefu zaidi, ni safari ya kutembea kwa mguu kwa takribani muda wa saa nne kwenda na kurudi kwa kupita katika milima, mabonde, mito na makorongo.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto hii, ninaishauri Serikali iboreshe miundombinu ya barabara ili kuweza kuufikia mti huo iwapo watalii watataka kwenda kuuona. Barabara ya kufika kwenye mti huu ni mbaya sana na hii ni changamoto inayowafanya watalii wasitembelee eneo hili.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ihakikishe kuwa eneo hili linaendelezwa ili liwe na hadhi ya kuwa sehemu ya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro. Vilivile ninaishauri Serikali itengeneze utaratibu wa kuhakikisha wanaokwenda kuuona mti wanalipa ada.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili utahusu maporomoko ya maji Materuni. Maporomoko haya ni moja ya maporomoko ya maji katika Mto Mware, Kata ya Uru Mashariki, Jimbo la Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro. Maporomoko haya yanapatikana katika Kijiji cha Materuni pembezoni mwa Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Maporomoko haya yana urefu wa zaidi ya mita 100. Pamoja na kivutio cha maporomoko ya maji, eneo hili la utalii limekuwa maarufu kwani watalii wanaokwenda kuona maporomoko hupata fursa ya kutembelea shamba la kahawa na kujifunza jinsi kahawa inakuzwa, kuvunwa na kusindikwa. Watalii hupata fursa ya kujaribu kwa mkono yao kuchoma na kuandaa kikombe cha kahawa kwa kutumia njia asili ya Wachaga.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa inayokabili eneo hili ni ubovu wa miundombinu ya barabara yenye urefu wa kilometa 15 kutoka mjini Moshi. Kutokana na ubovu wa barabara, watalii hupata shida kufika katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, changamoto za barabara katika maeneo yanayopeleka watalii kwenye vivutio vya Mlima Kilimanjaro zinatakiwa zipewe kipaumbele cha pekee na Wizara ya Maliasili na Utalii kwani wao ni wanufaika wakuu. Ninaishauri Serikali iachane na kuzitegemea *TARURA* na *TANROADS* kwani mitandao yao ya barabara ni mingi, na hawajatoa kipaumbele kikubwa kwa barabara za jimbo langu kama zile za kupeleka watalii kupitia *Umbwe Gate*, *Kidia VIP Route*, *Materuni Waterfalls*, Mti Mrefu Kijiji cha Tema huko Mbokomu, Kanisa la Kibosho Singa na maeneo mengine muhimu.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali, huu ni wakati wa kutumia michango ya *Corporate Social Responsibility (CSR)* unaotokana na mapato ya Mlima Kilimanjaro kutengeneza miundombinu ya barabara katika jimbo langu la Moshi Vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya michango yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa hotuba nzuri iliojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa (*national competitiveness*). Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambayo ni *Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na programu ya kutunza maliasili zetu, Serikali iweke usimamizi wa msitu hasa ya asili ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya nishati. Katika kupangilia matumizi mazuri ya ardhi, ihusishe Wizara zote zinazosimamia Maliasili, Ardhi, Kilimo, Wizara za Maji na pia Wizara inayosimamia Mazingira. Kwa vile binadamu tunaongezeka ni muhimu kuhakikisha ulinzi kwa kuhifadhi mazingira yetu na kuwepo msukumo zaidi kwenye kuboresha mazingira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali kurejesha mahusiano mazuri kati ya *TANAPA* (Hifadhi ya Kitulo) na wananchi wa Kata za Ilungu, Igoma, Ulenje na Inyala, bado suluhu haijapatikana. Kuna mgogoro wa miaka mingi wa mpaka kati ya *TFS* na wananchi wa Kijiji cha Mwashoma. Pia kuna mgogoro wa *TANAPA*

(Hifadhi ya Kitulo) na wananchi wa Kijiji cha Kikondo ambao eneo lao lilichukuliwa na TANAPA bila kulipa fidia. Pamoja na changamoto hiyo ya GN za Hifadhi ya Kitulo, pia kuna utata wa mpaka wa Wilaya ya Mbeya na Wilaya ya Makete na inahitajika Wizara ya Ardhi kupitia upya mipaka na kurekebisha. Kutokana na mgogoro huu kuchukua muda mrefu na kusabisha uvunjifu wa amani, kuna ahadi ya mwaka 2015 alitoa Mheshimiwa Hayati Magufuli na kumwelekeza Waziri wa Ardhi na pia Waziri wa Maliasili na Utalii wa wakati huo kupitia upya mipaka, ili wananchi wa Kata za Ilungu na Inyala, hususani Kijiji cha Kikondo na Mwashoma waachiwe maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwa kukushukuru kwa nafasi ya kuchangia kwa njia wa maandishi.

Pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya katika kukuza sekta ya utalii, tumeona kazi yake nzuri ya filamu ya *Royal Tour*.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie hoja nilizotumwa na wananchi wa Jimbo la Kwela kwenye Wizara hii muhimu. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais, wewe na Naibu wako. Ni imani yangu na wananchi wa Jimbo la Kwela kuwa mtamsaidia vema Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako tukufu, niwasilishe kwako mgogoro wa muda mrefu sana kati ya wavuvi wa forodha ya Ilanga, Nankanga na Legeza dhidi ya mapori ya akiba ya Lwafi na Uwanda. Lakini pia Hifadhi ya Uwanda na Vijiji 16 vilivyopo kata ya Nankanga, Kapenta, Kipeta na Kilangawana.

Mheshimiwa Spika, utangulizi; Hifadhi ya Uwanda *Game Reserve* iliyoanzisha mwaka 1959 na wakoloni. Mwaka 1974 ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali na ikawa chini ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Halmashauri hadi mwaka 2013 walikabidhiwa *TAWA*. Mwaka 2014 *TAWA* walianza kazi rasmi kwenye Pori la Akiba la *Uwanda Game Reserve*. Pori la *Uwanda Game Reserve* linazungukwa na vijiji 16 na wakazi zaidi ya 50,000 wa vijiji hivyo ni wakulima, wafugaji na wavuvi.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya *Uwanda Game Reserve* wakati inaanzishwa eneo hilo lilikuwa ardhi kavu na baadae kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, maji ya Ziwa Rukwa yaliingia na kuungana na nchi kavu na kuwa ziwa kwa asilimia 80 ambapo eneo hilo ni ziwa kwa sasa. Hivyo eneo la nchi kavu la pori limebaki asilimia 20 tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mabadiliko hayo, Hifadhi ya *Uwanda Game Reserve* imebaki inatumia mipaka ile iliyoukwa na wakoloni haijabadilishwa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali halisi kwa sasa; baada ya *TAWA* kukabidhiwa Hifadhi ya *Uwanda Game Reserve* wakulima, wafugaji na wavuvi wanaishi kwa manyanyaso makubwa kwa maslahi ya askari mmoja mmoja wa *TAWA*.

Mheshimiwa Spika, wavuvi wanaishi kwa shida na kupoteza mali zao na maisha yao. Kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 wavuvi waliokufa wamefikia 40 na chanzo cha wavuvi hao kufa ni askari wa *TAWA*. Wapo waliojitosa majini kwa kuogopa kipigo kutoka kwa askari. Mvuvi anaona bora ajitose majini kuliko kukamatwa na askari. Pia wapo wavuvi waliokamatwa na waliopigwa sana na wengine kupata ulemavu wa kudumu. Wapo wavuvi waliopigwa risasi na kufa kwa sababu ya kunyang'anywa samaki wao walipojaribu kuzuia samaki wao wasinyang'anywe wakiwa hawana hata silaha yoyote.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matukio ya kikatili kwa wavuvi kuna wengine walijeruhiwa na kuwa walemavu wa kudumu. Mfano mwaka 2020 Ndugu Jeko wa Kata ya Kilangawana alijeruhiwa na risasi mpaka leo ni mlemavu wa mkono na shingo. Wakati huo Ndugu Mwakilima alipigwa risasi mpaka kupoteza maisha na askari wa *TAWA* anayeitwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Manyama akiwa na askari mwenzake. Pamoja na tukio hilo kuripotiwa Kituo cha Polisi Laela bado hamna hatua zozote zilizochukuliwa na askari huyo yupo bado kazini. Kitendo hiki cha kinyama, kimeleta chuki kubwa sana kati ya wahifadhi na wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa vibali vya uvuvi; baada ya wavuvi wengi kufa na kuwapo kwa msugvano mkali kati ya wananchi na wahifadhi, *TAWA* walikuja na mpango wa vibali maalumu kwa kila mvuvi anayetaka kuingia kuvua ndani ya Ziwa Rukwa. Kuanzishwa kwa mfumo wa vibali vilivyotengenezwa na *TAWA*, badala kuwa suluhu ya tatizo, imekuwa sasa kama nyezo ya kumkomoa mvuvi. Kwa sababu mtindo wa kibali umeleta adha nyingi sana tena za kinyonyaji kama ifuatavyo:-

Kwanza, mvuvi anatakiwa awe na kibali toka *TAWA* kinachomruhusu kuingia ndani ya ziwa na kuvua kwa miezi sita wanalipa shilingi 15,000. Mvuvi anatakiwa awe analipa kibali cha ngalawa toka *TAWA* kinachomruhusu kuingia ndani ya ziwa na ngalawa na kuvua kwa miezi sita wanalipa shilingi 15,000.

Pili, mvuvi anatakiwa kulipa kila siku anapoingia ziwani kuvua shilingi 5,000; tatu, mvuvi anatakiwa kulipia ngalawa ya kuvulia kwa kila siku anapoingia ziwani shilingi 2,000; na nne, mvuvi anayetumia boti anatakiwa kulipia *engine* ya boti kila siku anapoingia ziwani kuvua shilingi 20,000 na boti yenyewe analipia shilingi 2,000.

Mheshimiwa Spika, tano, mnunuzi wa samaki hata kama ananunua samaki mmoja anatakiwa kulipa kila siku anpoingia ziwani kwenda kununua samaki analipa shilingi 4,000; na mwisho akina mama wachakataji kwa maana kuparua samaki nao wanalazimika kulipa kila siku anpoingia ziwani kufanya kibarua hicho analipa shilingi 4,000. Pamoja na ukweli kwamba kipato chao ni cha chini sana kwa kazi hiyo ambapo akipata kiasi kikubwa kwa siku ni shilingi 6,000 na mara nyingine wanaweza wasipate chochote kutokana na upatikanaji wa samaki siku hiyo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kwa hiyo, TAWA kwa kipindi cha miezi sita inatoza wastani wa shilingi 4,890,000 ambayo ni sawa na shilingi 815,000 kwa mwezi mmoja ambayo ni fedha nyingi sana kwa mvuvi wa hali ya chini. Wakati huo huo mvuvi ana tozo nyingine kwenye taasisi nyingine za Serikali ambazo anawajibika kulipa kama ifuatavyo; leseni ya mvuvi ya Halmashauri analipa kwa mwaka shilingi 20,000; leseni ya ngalawa ya Halmashauri analipa kwa mwaka shilingi 20,000; na leseni ya TASAC mvuvi analipia ngalawa kwa mwaka shilingi 50,000.

Mheshimiwa Spika, kutokana na tozo kuwa nyingi tena kandamizi kwa wavuvi wamelalamika sana kwenye uongozi wa *Uwanda Game Reserve*, lakini majibu yao kwamba wao hawana mamlaka yoyote isipokuwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii ya Maliasili na Utalii japo nao wanakiri kuwa tozo hizo ni nyingi mno na kandamizi sana kwa wavuvi ila zipo juu ya uwezo wao.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu kwanza *Uwanda Game Reserve* ambayo kwa sasa ni ziwa kwa asilimia 80, tunaomba eneo la hifadhi kwenye ziwa liwe mita 500 kama ilivyo kwenye hifadhi zingine zinazopakana na ziwa.

Pili, kipindi tunasubiri kurekebisha kwa mipaka ya hifadhi kama Serikali itaridhia; tozo zile za kila siku kwa mvuvi kuingia ziwani kuvua zipunguzwe walau ziwe hata shilingi 500 na tozo ya ngalawa nayo iwe shilingi 500 kwa kila siku ambapo kwa mwezi mvuvi atalipa jumla ya shilingi 30,000. Hapo tutakuwa tumemsaidia mvuvi kujikwamua kutoka kwenye umaskini. Kwani ilivyo sasa ni kama kumkomoa mvuvi.

Tatu, kipindi tunasubiri kurekebisha kwa mipaka ya hifadhi kama Serikali itaridhia; tozo zile za kila siku kwa wanunuzi na akina mama wachakataji wa samaki kuingia ziwani kufanya shughuli zao zipunguzwe walau ziwe hata shilingi 500 kwa siku.

Nne, tozo za miezi sita kwa mvuvi kuingia ziwani kuvua zenyewe zibaki; tano, kipindi tunasubiri kurekebisha kwa

mipaka ya hifadhi kama Serikali itaridhia hasa kwa wavuvi; tunaomba alama ya mipaka iweke ili kuepusha migongano kati ya wahifadhi na wavuvi na sita, kwenye forodha ya Ilanga Muze inayopakana na Hifadhi ya Lwafi, ziwekwe upya alama zilizoonesha maeneo ya kuvua kulingana na makubaliano ya awali kati ya wavuvi na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Mlele Mpimbwe kabla ya TAWA kuja kwani utaratibu wa mwanzo ulikua mzuri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko haya kujirudia mara nyingi na wavuvi kuathiriwa sana tunaomba zoezi la kuwakamata wavuvi wakiwa ziwani kusubiri mpaka hapo alama za utambuzi zitakapowekwa. Kwani wavuvi wanashindwa kujua mipaka ya eneo la hifadhi na eneo lisilo hifadhi. Wavuvi waliahidiwa kwa muda mrefu kuwekewa alama mpaka sasa hamna kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, wavuvi wanaokamatwa hasa kwenye forodha ya Ilanga iliyopo Halmashauri ya Sumbawanga, wasipelekwe Halmashauri ya Mlele Mkoa wa Katavi kwani ni mbali sana. Hii inapelekea wao kukosa haki zao kwa sababu wanakuwa hawana hata mtu wa kuwadhamini na inapokuwa kesi imeenda mahakamani inakuwa shida kupata dhamana.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kuwepo na vikao au mkutano ya pamoja kati ya askari wako wanapoingia ili kuweka mahusiano mazuri kati ya wavuvi na askari wanyama pori. Pia tunaomba jambo lolote linalowahusu wavuvi au taarifa yoyote ile ya wavuvi itolewe kupitia vyama vyao, Wenyeviti wa Makambini siyo mtu binafsi ili kuondoa makanganyiko na habari za uzushi kusambaa.

Kuhusu taarifa ya Mawaziri Wanane wanaotatua migogoro itoke mapema ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao. Kwani kwenye Jimbo langu la Kwela tuna vijiji 16 wenye mgogoro na hifadhi ya Uwanda na mwaka huu ndio hali ni mbaya kabisa, wananchi wameshindwa hata kufanya shughuli za kilimo kutokana na mgogoro huo, kwani walizuliwa na wahifadhi kulima hata maeneo ambayo

wamekuwa wanalima miaka ya yote ya nyuma. Sababu ya wahifadhi kwa wananchi ni kwamba wasubiri ripoti ya Mawaziri Wanane ambayo waliahidiwa ingetoka mwaka jana mwezi wa nane, lakini mpaka leo kimya.

Mheshimiwa Spika, kama itakupendeza Mheshimiwa Waziri upange ziara uje kujionea mwenyewe hali halisi juu ya mgogoro huu ulloathiri wakulima, wavuvi na wafugaji kwa kipindi kirefu sana. Kwa mfano ndani ya Jimbo langu la Kwela zaidi ya kata nane zipo kwenye mgogoro huu, hii ni hatari. Alikuwa mwaka jana Katibu Mkuu wa CCM Taifa na Naibu Waziri wako waliona hali ya malalamiko kwa wananchi yalivyokuwa makubwa.

Mheshimiwa Spika, wahifadhi waache kutumia nguvu kubwa kupita kiasi wanapokabiliana na wananchi hasa wavuvi, kwani vifo vilivyotokea na watu kupata ulemavu vimezidisha chuki kati wananchi na Serikali. Hatua kali zichukuliwe hasa kwa askari wanaofanya vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu, mfano yule anayetuhumiwa kufanya mauaji ya mvuvi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana.

MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na amani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake uliotukuka kheri na baraka ziwe kwake.

Mheshimiwa Spika, aidha natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Dkt. Francis.

Mheshimiwa Spika, binafsi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, nimejionea na kupata taarifa za

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

utekelezaji wa Wizara katika kipindi cha Kamati hivyo basi nina ushauri tu kwa maslahi ya Taifa letu.

Kwanza, Wizara hii sio Wizara inayoshughulikia masuala ya Muungano wa Tanzania, lakini ushirikiano kati ya baadhi ya taasisi za SMZ na SMT zitasaidia kuongeza idadi ya watalii wa ndani na wakimataifa. Mfano, Mamlaka ya Hifadhi na Urithi wa Mji Mkongwe Zanzibar, Idara ya Mambo ya Kale, Idara ya Utamaduni na Sanaa, Mamlaka ya Mazingira na kadhalika, hivyo basi nashauri Wizara ya Maliasili na Utalii ishirikiane na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ya Zanzibar kwa lengo la kuongeza idadi na namba ya watalii.

Mheshimiwa Spika, pili, Wizara kuongeza kasi ya utangazaji wa vivutio sambamba na kubuni *activities* tofauti katika vivutio vyetu. Mfano, kuweka michezo ndani ya maeneo wanayozuru/sehemu za utalii. Hii itasaidia wageni kushawishika kuja mara kwa mara nchini.

Tatu, kuboresha miundombinu katika maeneo yanayotumika kwa wageni kutembelea, mfano barabara; nne kuboresha huduma ya mawasiliano katika hifadhi zetu. Kukosa mawasiliano ni changamoto kwa watalii kwani zipo sehemu bado mawasiliano ya simu hakuna.

Tano, kufikisha huduma za kifedha kwa baadhi ya maeneo yanayotumika kwa kazi za kitalii. Mfano ATM, WAKALA na kadhalika ili mtalii aweze kutumia akiwa ndani ya hifadhi kununua huduma tofauti na hii zaidi inawalenga watalii wa ndani; sita, kumaliza miradi yenye kuongeza idadi ya watalii lakini pia yenye kuongeza fursa za ujio wa watalii nchini, mfano, meli kwa ajili ya utalii wa majini, malango katika hifadhi zetu, Mradi wa *REGROW*, Mradi wa Nyuki na kadhalika.

Saba, kuitumia filamu ya *Royal Tour* katika matamasha ya kimataifa. kwani filamu ya royal tour imeitangaza sana nchi yetu; nane, Wizara kutumia historia na uasilia wa maeneo yanayotumika kwa shughuli za kitalii. mfano; Mikindani (biashara ya Utumwa), machifu na historia zao (Chifu Mkwawa Nyika wa Iringa) na kadhalika; tisa kuipa nguvu

Idara ya Malikale na Makumbusho na kumi, kuboresha mahusiano mema na Mataifa tofauti.

Mheshimiwa Spika, kumi na moja, Wizara ifikirie kuweka kumbukumbu ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipa nguvu ya kifedha na maarifa Wizara hii na wananchi wa Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, nampongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutusaidia na kuisaidia sekta ya utalii kifedha kwa kuamini kuwa sekta hii ina mchango mkubwa sana kuinua uchumi wa Tanzania. Ninawatakia kila la kheri katika kutimiza majukumu mliokabidhiwa na Mheshimiwa Rais. Mimi Mjumbe wa Kamati naunga mkono hoja asilimia mia. Ahsante sana.

MHE. AMINA DAUD HASSAN: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia makadirio na mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa Taifa letu kwa kutuletea utalii kupitia *Royal Tour*. Pia nampongeza Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, tuzidi kuitangaza Tanzania kupitia watalii wanaokuja Zanzibar wanaokwenda Jozani kuna wanyama adimu kama kima punju vilevile kuna utalii wa kuzamia mbizi upo Paje na utalii wa *culture* na mila na desturi na utamaduni wetu. Mfano mapishi, ustaarabu wa mapokezi mazuri ya wageni pia tuishukuru Serikali kwa watalii wanakwenda kutembelea mikoa ya Tanzania Bara wanamalizia kuja Zanzibar ili kuweza kuona vivutio vizuri ambavyo vinapatikana Zanzibar kama hoteli iliyopo baharini Pemba, na hoteli mbalimbali kubwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa *private sector*, tunamshukuru Bakhresa kwa kuleta meli zake ili kuweza kuwapatia na kuwasafirisha watalii kwa urahisi na kuweza kufika Tanzania Bara kwenda kuona Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na kadhalika na kwenda visiwani bila ya shida yoyote.

Mheshimiwa Spika, natoa wito na kuishauri Serikali iweze kuiongezea bajeti Wizara hii ili iweze kuongeza miundombinu rafiki kwa watalii wetu ambao wanatarajiwa kuja kwa wingi sana. Kwa mfano, barabara, kuongeza hoteli ya nyota tano, kuongeza usafiri wa anga na baharini ili kuweza kumudu ongezeko la utalii, na hata watalii wanapokuja kwetu waone raha kama wapo nyumbani kwao, lakini vilevile nchi yetu itaimarika na kuongezeka kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kupitia njia hii ya mchango wa maandishi kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye maeneo mawili yanayoambatana pamoja na utalii wa tiba (*medical tourism*) na utalii wa kibiashara (*business tourism*).

Mheshimiwa Spika, maeneo haya mawili ya sekta ya utalii yanategemea sana jitihada kutoka kwenye sekta nyingine kama vile sekta za afya, sekta ya ujenzi, sekta ya ulinzi, na sekta ya biashara. Hivyo Wizara ni lazima iwe na mashirikiano na Wizara za Ujenzi, Afya, Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mambo ya Nje, Ulinzi na Mambo ya Ndani. Lengo ni kuona jinsi gani mipaka inatumika kama fursa, badala ya kuichukulia kama zao la laana na uadui.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka miundombinu ya Hospitali za Rufaa za Mikoa na Kanda kuwezesha utekelezaji wa utalii wa tiba (*medical tourism*), lakini pia nchi yetu ina mipaka, mkakati inayozalisha majirani ambao ni soko kubwa

kuwezesha utekelezaji wa utalii wa biashara (*business tourism*). Mipaka inaleta wateja wa maeneo hayo mawili ya utalii wa tiba na utalii wa biashara.

Mheshimiwa Spika, nchi kama vile Malawi, Mauritius, Mozambique, Comoro, Seychelles, Zambia, Congo, Rwanda, Burundi, Somalia, Uganda, Sudan, Somalia na Kenya ni muhimu katika utekelezaji wa utalii wa biashara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. MAIMUNA S. MTANDA: Mheshimiwa Spika, maeneo ya utalii katika Wilaya ya Newala nikianza na utalii; Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba mtume tume ya wataalamu waje Jimbo la Newala Vijijini kuona maeneo mazuri ya utalii yaliyopo Jimbo la Newala Vijijini katika Kata ya Chilangala ambako kuna maporomoko mazuri sana ya utalii katika Mlima Miyuyu.

Aidha kwenye Jimbo la Newala Mjini lipo Shimo la Mungu eneo zuri kabisa la utalii. Tunaomba mje muwekeze katika Wilaya ya Newala kwenye masuala ya utalii.

Pia Wilaya ya Newala kuna kivutio kizuri sana cha utalii wa utamaduni wa Kimakonde kuanzia ngoma na vyakula. Katika Jimbo la Newala Vijijini katika Kata ya Mchemo huwa kuna maadhimisho ya siku ya utamaduni wa Kimakonde, tunaomba Wizara yako ituwezeshe kuimarisha sherehe hizo, pia mje mjionee siku hiyo maalum. Kama Wana-Newala tupo tayari kushirikiana nanyi katika kila hatua.

Mheshimiwa Spika, changamoto kati ya *TFS* na wananchi wa Kata ya Chilangala; naomba kuuwasilisha kwenu mgogoro unaofukuta kati ya wananchi wa Kata ya Chilangala na *TFS* ambapo mwezi Aprili mwananchi mmoja amefariki katika harakati zitokanazo na mgogoro wao kutotatuliwa hali iyoleta kadhia hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Masanja. Mtoa hoja ajiandae. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa kibali cha kuweza kujadili bajeti yetu ya Wizara ya Maliasili na Utalii katika siku hii ya leo, lakini kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini nimpongeze sana kwa kuipa kipaumbele sekta hii ya maliasili na utalii ambapo hivi karibuni ameweza kuzindua filamu ya *Royal Tour* na kwa kiasi kikubwa na kiwango kikubwa ameweza kuhamasisha utalii wa ndani na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyoongea sasa ndani ya miezi minne ya Januari mpaka Aprili tumekuwa na ongezeko la watalii wengi sana na kuanzia mwezi Mei mpaka Disemba hoteli nyingi hifadhini zimejaa kwa maana ya *booking*. Hivyo ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuipa kipaumbele sekta hii ya muhimu ambayo kiukweli sisi tukishindwa kutekeleza majukumu haya basi tulaumiwe sisi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tumhakikishie tu Mheshimiwa Rais kwamba tutaendelea kutangaza utalii, tutaendelea kuhabarisha habari njema za vivutio vyetu tulivyonavyo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru Wabunge wote kwa michango yao mizuri sana na mingi imekuwa ni ya kutuelekeza, lakini pia kutuonesha namna ambavyo tunataka kwenda, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu hii ya Maliasili na Utalii ina changamoto nyingi sana na sisi tunatambua hilo na tumeyapokea mengi ambayo mmetuonesha njia na sisi tunawaahidi kwamba tutaenda kuyatekeleza na yale magumu ambayo tutaona yanatushinda sana basi tutashirikiana na ninyi kuhakikisha kwamba sekta ya utalii inapaa na zaidi tunamsaidia Mheshimiwa Rais kuendeleza sekta hii. *(Makofi)*

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Mheshimiwa Spika, nipende tu kusema machache ili niunge hoja; kwanza kabisa nipende tu kusema kwamba jukumu la Wizara ya Maliasili na Utalii ni kulinda, kutunza, kuhifadhi, lakini pia na kuendeleza utalii. Sisi kama Wizara tumepewa jukumu hili la kuangalia maeneo yote yaliyohifadhiwa, tunayatunza, tunayalinda, tunayahifadhi, lakini yanapoleta kivutio kizuri basi tunahamasisha utalii ili watu waone maeneo haya kwamba tumeyatunza kwa namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo ndani ya maeneo haya tunatunza vyanzo vya maji, lakini tunatunza misitu, lakini tunadhibiti mabadiliko ya tabianchi, sambamba na hilo tunatunza mazingira. Sekta nyingi zinaitegemea sana sekta hii ya maliasili; nikianza na sekta ya nishati, bila kuwa na vyanzo vizuri vya maji hatuna umeme, kwa hiyo, uchumi wan chi unategemea sana katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ninapoenda kwenye misitu pia, misitu yetu tukiimaliza tukashindwa kuitunza vizuri hatutaweza kuishi. Tunasema misitu ni uhai, lakini sambamba na hilo tunapata maji kutoka kwenye maeneo yale kwa hiyo, ningependa kuliweka wazi hili tutambue kwamba tunapoyahifadhi haya maeneo tuna lengo zuri kabisa la kuhakikisha kwamba sisi tunaishi na Mungu aliyaweka haya maeneo ili yaweze kutufanya tuishi vizuri. Tunapata hewa nzuri kutoka kwenye maeneo haya. Wizara ya Muungano na Mazingira wanatutegemea sisi, tukisema leo maliasili tutelekeze haya maeneo hizi sekta nyingine zote haziwezi kuendelea. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niendeleo kuwaomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuwa na changamoto nyingi katika sekta hii, lakini bado tuone na upande wa pili wa umuhimu wa sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta hii unategemewa sana na sekta mbalimbali. Nikienda kwenye sekta ya mifugo, tunapoleta mtalii hapa ndani lazima mtalii atakula, nikisema uvuvi atakula samaki, nikienda kwenye

usafirishaji pia tutasafirisha abiria, nikienda kwenye kilimo pia tutauza mazao yetu kwa huyu mtalii anayekuja, lakini tutauza maji, lakini kwa wakati huohuo sekta hii inatuletea watalii wengi ambao wanatuongezea uchumi wetu katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaenda moja kwa moja kwenye eneo la migogoro ya mipaka; sekta hii ni kweli tumekuwa na changamoto nyingi sana za mipaka, migongano kati ya hifadhi na wananchi na inaleta hatari kubwa na pengine wananchi wanapoteza maisha.

Kwanza nitoe pole sana kwa wananchi ambao wanakumbana na kadhia hii, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais alianzisha Kamati ya Mawaziri Nane na sambamba na hilo tumeendelea kuhabarisha umma, pale ambapo kuna migogoro mipya wailete tuitatue na changamoto hizi tumeshaanza kuzipokea na Serikali ya Awamu ya Sita imeweza kuachia vijiji 920 ambavyo vilikuwa ndani ya hifadhi, lakini kwa huruma ya Mheshimiwa Rais amevirudisha kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo migogoro mipya bado tunaipitia ili tuhakikishe kwamba mwananchi kwanza, hifadhi tunaingalia baadae. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba ndio maana kuna Kamati hii ambayo inazunguka nchi nzima, lengo ni kutokuwepo na taharuki kwa wananchi. Na haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais na tunayatekelea kwa sababu alisema sitaki kusikia taharuki yoyote. *(Makofi)*

Niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, tunaenda kutatua matatizo haya kwa mashirikiano baina ya wananchi na wahifadhi, ili kuleta amani nzuri na wahifadhi wawe na amani ya kuyasimamia yale maeneo ambayo yatakuwa yameachiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuendeleo kuipongeza Serikali na tuendeleo kuwa-*support* Maliasili na Utalii ili tuweze

kufikia mahali ambapo jamii zitambue uhifadhi ni sehemu ya maisha yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitapenda pia niongelee eneo la tozo. Waheshimiwa Wabunge baadhi wameongelea kuhusu tozo; ni kweli sisi tuna tozo, lakini tunaangalia hizi tozo tukijilinganisha na washindani wenzetu. Tuna washindani wa nchi jirani ambao tunapopanga hizi tozo tunaangalia na wenzetu wana tozo za aina gani.

Mheshimiwa Spika, mfano nitapenda kuongelea katika hifadhi zetu nne ambazo mwaka jana tulipandisha kiwango cha kiingilio kutoka dola 60 kwenda dola 70, tuliongeza dola 10. Ukilinganisha na washindani wetu mpaka sasa nikisema hata Masai Mara sisi tunapotoza Serengeti kwa dola 70 wenzetu wako dola 80. Serengeti ni hifadhi bora Barani Afrika, unapoiongelea Serengeti huilinganishi na Masai Mara, lakini bado Serengeti iko chini ya Masai Mara, kwa hiyo, tunapoongelea hizi tozo lazima tujilinganishe na wenzetu wana kiwango gani na sisi tuna kiwango gani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo tulipandisha kwenye maeneo ya Tarangire, Arusha pamoja na Ziwa Manyara ambapo tulitoka dola 45 kwenda dola 50, tumeongeza dola tano. Kwa hiyo, tuangalie tozo zetu hizi ziko na ni kipindi cha *peak*, kipindi cha *high season*. Tunapoenda kwenye *low season* tunaenda kwenye tozo ya kawaida ambayo ilikuwa ni ya miaka ya nyuma. (Makofi)

Kwa hiyo, bado ukilinganisha na vivutio vyetu vilivyo bora tuko kwenye *standard* nzuri na watalii wanaendelea kuongezeka. Niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwenye eneo hili tumejipanga vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nataka niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kuhusu miundombinu katika maeneo ya hifadhi. Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais amweweza kutupatia fedha shilingi bilioni 90.2 za kujenga miundombinu ya barabara katika maeneo

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

ya hifadhi. Fedha hizi tumezielekeza kununua miundombinu ya mitambo, lakini pia na ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba utekelezaji wa fedha hizi utakapokamilika tutaondokana na kero ya uharibifu wa barabara wa mara kwa mara ndani ya hifadhi kwa sababu tutakuwa na mitambo ambayo hii mitambo itakuwa inatengeneza hizi barabara mara kwa mara na wakati huo huo *Royal Tour* imeshatufungulia utalii, tunaamini utalii utakuwa juu na barabara zitakuwa zinatengenezwa kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine ambalo wameweza kuliongelea...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, muda wako umekwisha. Dakika moja malizia.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nilitaka tu niongelee kidogo kwenye eneo la *REGROW* kwamba, eneo la *REGROW* lime-*cover* hifadhi nne ya Ruaha, Mikumi, *Nyerere National Park* pamoja na Udzungwa, sio Mikumi tu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mary Masanja, sasa kwa sababu umetaja hapo majina ya hifadhi na kumbukumbu zetu ili zikae sawa sawa hii inayoitwa Selous, hii inayoitwa Nyerere watu wamesema Selous humu ndani wewe umeita Nyerere sasa sema jambo hapo ili Wabunge wajue inaitwa nini sasa hivi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kabla ya *Nyerere National Park* kupandishwa hadhi kuwa *national park* lilikuwa ni pori la akiba ambalo lilikuwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

linaitwa Selous. Baada ya *Nyerere National Park* kupandishwa hadhi lilimegwa pori la Selous likabaki sehemu kuwa pori la akiba na *Nyerere National Park* ikapandishwa kuwa Hifadhi ya Taifa, kwa hiyo tuna *Game Reserve* ya Selous na wakati huo huo tuna *Nyerere National Park*. (Makofi)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maelezo ya muhimu sana hayo kwa sababu michango imetokea hapa mwingine anaweza kuwa anazungumzia lile eneo la *Nyerere National Park* akawa anasema ni Selous na mwingine atakuwa anazungumzia Selous atasema Nyerere. Kwa hiyo nafiki ni muhimu sana tujielimishe ile mipaka ili tuwe tunajua tunalizungumzia eneo lipi kati ya hayo mawili.

Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake. (Makofi)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kupata nafasi hii ya kutoa ufafanuzi wa baadhi ya maeneo. Nianze pia kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa kutuongoza vema, lakini pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kuchambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa bajeti yetu vizuri na ushauri waliotupa kwa kweli tutaendelea kuuzingatia.

Mheshimiwa Spika, tumepata wachangiaji takribani 36 na kati yao waliochangia kwa kuongea ni takribani 26 na pia waliochangia kwa maneno takribani wachangiaji 10.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na Waheshimiwa wengine wote na Mheshimiwa Naibu Waziri kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Rais ametuonesha dira, ametuonesha njia juu ya suala zima la uhifadhi na masuala mazima ya utalii hususan suala zima la *Royal Tour*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nichukue nafasi hii kumshukuru sana sana Mheshimiwa Rais wetu kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kutuongoza vema katika kutukumbusha kwamba masuala haya ya utalii tujue na kutambua kwamba yanachangia pato la Taifa lisilopungua asilimia 17 na tuna maelekezo kwamba ifikapo mwaka 2025 tuendelee kuongeza pato la Taifa hadi kufikia dola za Kimarekani zisizopungua bilioni sita na watalii takribani milioni tano. Hivyo ni jukumu letu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuona ni namna gani eneo hili tunaliboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile nishukuru sana kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge wote Waheshimiwa Wabunge wamechangia michango mbalimbali na sisi Wizara tuseme tu kwamba michango hiyo tunaichukua tunaifanyia kazi na tutaleta majibu hayo kwa maandishi kwa michango yote tutaleta kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda haraka haraka katika eneo la udhibiti wa wanyama pori wakali na waharibifu nianze kwa kutoa pole kwa changamoto hii kwa wananchi kutokana na adha ya wanyama pori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua za muda mrefu na muda mfupi kukabiliana na changamoto hii. Suala la wanyama hawa limekuwa ni changamoto iwe ni tembo na wanyama wengine na tumelizungumzia sana na kwa kweli tunaafiki kwamba eneo hili tuone namna gani ya kuboresha na tukiboresha ndipo sasa tutaweza kuwalinda wananchi wetu wasipate madhara na maumivu yoyote, lakini pia tukizidi kuboresha tutaona jinsi gani ya kulinda hata hifadhi zetu.

Mheshimiwa Spika, hatua za muda mfupi zinajumuisha kuanzisha ujenzi wa vituo 19 vya kudumu kwa ajili ya askari wa Jeshi ya Uhifadhi na kizimba kimoja kwenye maeneo yafuatayo; Wilaya ya Meatu - Kijiji cha Malwilo kutakuwa na kituo; Rufiji katika Kijiji cha Ngarambe; Busega katika Kijiji cha Kigereshi; Lindi katika Kijiji cha Milola; Tunduru katika Kijiji cha Milonde; Mwanga katika Kijiji cha Kwakoa; Iringa katika Kijiji cha Itunundu; Songwe katika Kijiji cha Udinge; Nzega katika Kijiji cha Ndala; Mvomero katika Kijiji cha Lubungo; Chamwino

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

katika Kijiji cha Ilangali; Mpwapwa kutakuwepo na kituo pale Mtera; Nachingwea tutaweka kituo pale Nditi; Liwale Ng'ungu kutakuwa na kituo; Kondo katika Kijiji cha Mkungunero; Malinyi kutakuwepo na kituo pale Kwa Kilosa Mpepo na Karatu kutakuwepo na vijiji vya Kambi ya Nyoka, Oldeani na Kambi ya Simba na kujenga kizimba kimoja cha mamba katika Jimbo la Buchosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vituo hivi 19 vitajengwa kwa bajeti ya mwaka huu 2021/2022 ambapo ndani ya mwezi Juni, 2022 ujenzi utaanza rasmi. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2022/2023 Wizara itajielekeza kujenga vituo vingine hivi ni vya mwanzo kutakuwa na vituo vingine tena 13 kwenye maeneo mengine yenye changamoto. *(Makofi)*

Vilevile hatua za muda mrefu ambazo zinajumuisha kuwa na mpango bora wa matumizi ya ardhi kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta nazo zitakuwepo kutoa elimu za uhifadhi kwa jamii zinazoathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu; kuendelea kuwadhibiti tembo, mamba, viboko, fisi na wanyamapori wengine ambao ni hatarishi kwa njia tofauti kwa lengo la kumaliza madhara haya; kutumia njia mbadala za kielektroniki kwa mfano kuwafunga wanyama *GPS Collar* na kuona ni namna gani tunaendelea kudhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo niendeleo kutoa rai kwa wananchi kuona namna gani tunaweza tukajiepusha na kuvamia maeneo ya hifadhi kwa shughuli za kibinadamu ambayo hupelekea wanyamapori kusababisha migongano baina ya wanyama na binadamu. Kwa hiyo, tuendeleo kushukuru sana kwa maoni ambayo tumepata namna ya kuendelea kuboresha maeneo haya ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni suala zima la *Royal Tour* na eneo hili ambalo linachangia sana pato la Taifa tumepata ushauri wa aina mbalimbali hapa umetokea ushauri wa jinsi ya kuratibu ziara za mafunzo kwa wakala wa utalii na hilo tatalizingatia na kuendelea kutumia watu maarufu na waandishi wa habari kwa ajili ya kutangaza

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

vivutio vyetu. Wizara imeendelea kutumia watu maarufu na Wizara imetumia watu maarufu mfano mchezaji wa timu ya Taifa ya Ufaransa Mamodou Sakho; msanii maarufu wa filamu ya *Nolly Wood* kutoka Nigeria Gimy Aik; msanii maafuru wa filamu Will Smith wa Marekani pia amewahi kufika katika hifadhi zetu; mchezaji wa Klabu ya Real Madrid Vallejo Jesús; na mchezaji maarufu wa timu ya *PSG* Andrea Herrera, hii yote ni mikakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mnamo mwezi wa 10 tutaendelea kuwa na mkutano mkubwa sana pale Arusha hii yote ni katika kutangaza masuala ya utalii, huu ni Mkutano wa 65 wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia utalii duniani Kamisheni ya Afrika utafanyika nchini mwezi Oktoba, 2022 Jijini Arusha na utakuwa na takribani washiriki wasiopungua 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii ukiwa na watalii tuseme 1,000 wamelala Tanzania chukua mfano watalii wote hawa 1,000 kila siku asubuhi wanakula mayai mawili maana yake utalii huu unaongeza tija na sekta mbalimbali za uchumi maana yake yule mjasiriamali ambaye anafuga kuku, analima mchicha na mazao mengine ataongeza kipato na ndiyo maana tunasema suala hili la utalii tuone namna gani ya kuendelea kuliimarisha. Lakini pia tunaendelea kushirikiana na ofisi zetu za ubalozi kote duniani kuendelea kutangaza vivutio hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tumeona kwamba upo umuhimu wa kutumia digitali katika kutangaza utalii, kwa hiyo, tunaimarisha utangazaji wa utalii kupitia vituo maalum vya kidigital cha kutolea taarifa mbalimbali za vivutio vya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu idadi ya vitanda kwa mwaka 2021 Wizara ilifanya utambuzi na uhakiki wa huduma za malazi katika mikoa 26 nchini ambapo jumla ya huduma za malazi 10,432 zilipatikana zenye jumla ya vitanda 122,532 na vitanda 132,684. Hata hivyo tunaendelea kuhamasisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wadau mbalimbali waendeleo kuwekeza katika huduma za malazi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya sheria na kanuni; Wizara inafanya mapitio na sheria mbalimbali na kanuni na kuona kama kuna umuhimu wa kufanya maboresho ya tozo zilizopo. Sambamba na hatua hizi Wizara inaendelea kuboresha miundombinu ya utalii nchini ili kuimarisha kufikika kwa vituo vya utalii mbalimbali.

Aidha, Wizara inatoa elimu kwa wadau mbalimbali wa utalii ili kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa watalii ambao wanatarajia kuongezeka kutokana na programu hii lazima tuwaandae watu wetu tutoe elimu na vyo vyetu vya utalii vinaendelea kutoa elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia inaendelea kuimarisha ulinzi na kuendeleza rasilimali wanyamapori, misitu, nyuki na malikale kwa kufanya masuala mbalimbali ikiwa ni kuendeleza, kuimarisha kwa mfano Jeshi la Uhifadhi la Wanyamapori na Misitu na kuongeza vitendea kazi na idadi ya watumishi na kuwajengea uwezo kwenye nyanja mbalimbali. Hivi sasa tumeomba kibali cha kuweka askari 600 ambao askari hawa watasaidia pia kudhibiti wanyama wakali katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nikushukuru sana kwa nafasi hii naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja imetolewa lamuliwe)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri sasa tutaendelea na ratiba yetu, Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI: Kamati ya matumizi.

SPIKA: Kamati ya Matumizi.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae, Katibu.

KITABU CHA PILI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifungu 1001 – *Administration & Human*

Resources Management.....4,284,769,280

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na ninalo jina moja hapa la Mbunge anayetaka ufafanuzi kuhusu jambo mahsusi la kisera, Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; mnajua sera ya utalii ni kukuza utalii kwa kushirikiana na wananchi, lakini vilevile kuhakikisha wanaleta maendeleo kwa wananchi. Sasa na nitangulize kabisa nisiporidhika nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi sana katika hifadhi zetu hasa wananchi wanapolima wanyama wakali wanapotoka na kwenda kuharibu mashamba yao, na tumekuwa tukizungumza mara nyingi Serikali ifanye marekebisho ya sheria ili iendane na mazingira ya sasa kuhusiana na kifuta jasho. Leo mtu anaandaa shamba lake zaidi ya milioni tano anatomia au milioni kumi, anakuja analipwa kifuta jasho shilingi 100,000; leo mtu anadhuriwa na tembo analipwa laki mbili, laki tano mtu anayekufa yamkini familia yake inalipwa milioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo nyeti tumekuwa tumelizungumza sana lakini Serikali inapata kigugumizi gani

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

kufanya marekebisho na mwanasheria Zainab Katimba ametusaidia vizuri? Tunahitaji *commitment* ya Serikali wananchi wanalalamika. Nisiporidhika nitashika shilingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati na-*wind up* nimesema kuhusu mapitio ya sheria na kanuni Wizara itaifanyia mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali kuona kama inakidhi wakati wa sasa, ili kuona kama kuna haja za kuzifanyia maboresho. Kwa hiyo hoja aliyoisema Mheshimiwa ni ya msingi na ipo katika mazingatio ya Wizara. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya naona bado umesimama.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa *commitment* ya dada yangu na Mheshimiwa Mary Masanja na unajua mwanamke anapotoa *commitment* anaifanyia kazi na natoa *doubt* nawapa muda, ahsanteni. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa muda uliobaki tunaingia kupitisha mafungu kwa pamoja, Katibu.

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifungu 1002 – Finance and Account Unit.....	Sh. 1,220,252,000
Kifungu 1003 – Policy and Planning Unit.....	Sh. 1,521,685,479
Kifungu 1004 – Government Communication Unit.....	Sh. 399,476,000
Kifungu 1005 – Internal Audit Unit	Sh. 560,700,000
Kifungu 1006 – Procurement Management Unit.....	Sh. 745,344,899
Kifungu 1007 - Legal Services Unit	Sh. 557,798,240
Kifungu 1008 – Management Information System.....	Sh. 1,046,949,000
Kifungu 1009 – Research and Training Unit.....	Sh. 16,712,839,000

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kifungu 2001 – <i>Wildlife</i>	Sh. 355,198,896,192
Kifungu 3001 – <i>Forestry and Beekeeping</i>	Sh. 36,198,789,000
Kifungu 4001 – <i>Tourism</i>	Sh. 15,384,039,000
Kifungu 4002 – <i>Antiquities Unit</i>	Sh. 9,875,029,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

KITABU CHA NNE

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 69 – Wizara ya Maliasili na Utalii

Kifungu 1002 – <i>Finance and Account Unit</i>	Sh. 145,750,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i>	Sh. 61,325,930,496
Kifungu 1008 – <i>Management Information System</i>	Sh. 0
Kifungu 1009 – <i>Research and Training Unit</i>	Sh. 0
Kifungu 2001 – <i>Wildlife</i>	Sh. 109,036,124,100
Kifungu 3001 – <i>Forestry and Beekeeping</i>	Sh. 6,450,360,404
Kifungu 4001 – <i>Tourism</i>	Sh. 3,478,000,000
Kifungu 4002 – <i>Antiquities Unit</i>	Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa tukae, mtoa hoja taarifa

T A A R I F A

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha

kazi zake sasa naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:
Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono ahsanteni sana na sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na watendaji wote wa Wizara hii kwa pongezi hizo zinatokana na kwamba Bunge limepitisha Makadirio yenu ya Mapato na Matumizi kwa hivyo nawapongeza sana. *(Makofi)*

Lakini pia nawapongeza kwamba mnafanyakazi nzuri pamoja na changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezisema hapa. Wizara hii sote tunafahamu kwamba kufikia hapa tulipofika imepiga hatua kubwa sana. Kwa hiyo, juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali zimeonekana na kwa kweli kwa taarifa iliyoletwa pia na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii nayo inaashiria kwamba Serikali inasikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na mengi wameshayafanyia kazi na wanaendelea kuyafanyiakazi na wanaendelea kuyafanyia kazi mambo mengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawapongeza sana pia kwa kuwa wasikivu kwa mawazo yanayotolewa na Waheshimiwa Wabunge na hapa pia hata kwa yale ambayo hamjapata fursa ya kujibu tunafahamu mtayaleta kwa maandishi ila kwa yale mliyofanikiwa kuyajibu hapa yameashiria kwamba mnao utayari wa kufanyiakazi changamoto za wananchi ambazo

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

wawakilishi wao wamezisema hapa ndani, kwa hiyo nawapongeza sana kwa hilo pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge Wizara hii pengine imekuwa ya kipekee kwa sababu Mheshimiwa Rais kwenye Wizara zote anafanyakazi nzuri, wanasema anaupiga mwingi kwenye Wizara zote lakini Wizara hii ameingiza miguu yote miwili mpaka amewasaidia kufanya hii kazi ya kuonesha vivutio tulivyonyavyo na sasa Waheshimiwa Wabunge baadhi ya michango yenu iliashiria kwamba pengine huko baadaye ifanyike tena nyingine, halafu pengine yatembelewe maeneo tofauti yale ambayo ameenda. *(Makofi)*

Nadhani kwa hapa tulipofika kwanza na sisi tujiongeze kwenye maeneo yetu kila mtu afanye kile ambacho Mheshimiwa Asia alichangia hapa asubuhi kwamba Manyara kule wamefanya mambo wao wametengeneza ya kwao ila nadhani pengine inabidi iitwe jina lingine badala ya kuitwa *Royal Tour*. Kwa hiyo, kila mtu kwenye maeneo yake wajaribu kuona kitu wanachoweza kufanya. Kwa mfano huu mzuri ambao ameonesha Mheshimiwa Rais killa mmoja wetu achukue hatua ya kufanya jambo katika eneo lake na hivyo tunawatakiwa kila la kheri kwenye utekelezaji wa yale ambayo mmeahidi kwamba mtayafanyia kazi ambayo wamesema Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili
na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023
Yalipitishwa na Bunge)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujamaliza kuna tangazo hapa na kuna mambo mawili ya ufafanuzi.

Moja; leo kuna Wabunge wawili ambao wameagizwa kuleta ushahidi lengo ni jema kabisa kwa sababu

Waheshimiwa Wabunge ninyi ni wawakilishi wa wananchi na kama wawakilishi wa wananchi mkileta hoja zao hapa ndani lazima Bunge lizichukue kwa uzito unaostahili na kuweza kutoa maagizo mahususi kwa Serikali ili iweze kuchukua hatua mbalimbali. Kwa sababu huwezi kuja Mbunge hapa ukasema mambo mazito kutoka kwenye Jimbo lako halafu mambo yakapita tu kwamba jamani lakini si mlisikia nimesema hapana. Lazima Bunge lichukue hatua stahiki na Serikali pia ichukue hatua stahiki.

Kwa hivyo ushahidi utaletwa hiyo siku ya Jumanne hatua zitachukuliwa baada ya hapo kwa sababu hatutaki wananchi waendeleo kupata kadhia kama wameshapata kadhia tunataka tuchukue hatua ili zile kadhia zisendelee kutokea huku. Kwa hiyo, tutakapopata huo ushahidi tutatoa maagizo mahususi.

Waheshimiwa Wabunge hili ni pia ni kwa sababu ilitokea siku si nyingi nadhani mbili, tatu zilizopita zilitolewa tuhuma humu ndani za kuhusu mauaji Lushoto sijui kama wote mnakumbuka lilikuja jambo hilo zito sana hapa ndani na likawa limechangiwa kwa namna ile iliyoashiria pengine kuna ukweli kwa hiyo kiti hapa hakikuweza kusema jambo lolote kwa sababu lilichangiwa kama vile ni la uhakika ama uhalisia kwamba ni jambo linalotokea huko. Lakini siku hiyo hiyo tukaona taarifa Jeshi la Polisi likitoa ufafanuzi juu ya jambo hilo.

Sasa lazima sisi Wabunge tunapotoa michango yetu hapa Bungeni tujitahidi kutafuta taarifa zilizo za uhakika kwa sababu sisi tukituma ujumbe huko nje ukazua taharuki inakuwa changamoto ni kubwa sana. Kwa hiyo, lazima sisi kama viongozi kila mmoja wetu aone ni jukumu lake anaposimama kusema hapa taarifa ile anayoisema awe na uhakika nayo ili kutokuleta taharuki kwa wananchi.

Kwa hiyo, hili la kudai ushahidi leo pamoja na mambo mengine kwamba Bunge tutataka kuchukua hatua kama wako wananchi ambao wanapata kadhia za namna hii ambazo Wabunge wameshazisema, lakini pia hatutaki kuleta

NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

taharuki huko nje kwa mambo yanayozungumzwa hapa ndani. Kwa hiyo tutakuwa tukichukua hizo hatua ili tusilite taharuki kwa wananchi, lakini pia kwa wananchi ambao wanapata kadhia Bunge lazima lichukue hatua.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo hapa mbele kutoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inawaalika Wabunge wote kushiriki katika kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Duniani. Maadhimisho hayo yatafanyika siku ya Jumapili tarehe 5 Juni, 2022 kuanzia saa 2.30 asubuhi katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete hapa Dodoma.

Zoezi hili nirudie muda saa 2.30 asubuhi, Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

Waheshimiwa Wabunge, wote tunaalikwa na tunaombwa pia tuhudhurie sherehe hizo sote tutakuwa tukiongozwa na Kamati yetu ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwenye hili zoezi lakini Waheshimiwa Wabunge wote tunatarajiwa kuhudhuria wiki hii ya muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirishwa shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 1.50 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 6 Juni 2022 Saa Tatu Asubuhi)